# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 13 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA- KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

Na. 310

### Ajira na Mikopo kwa Vijana

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE K.n.y. MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS** aliuliza: -

Je, Serikali ina kauli gani kuhusu utekelezaji wa wito wake kwa vijana kujiajiri au kujiunga katika vikundi ili kutambuliwa na kukopesheka kisheria?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI inasimamia utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye

ulemavu kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 Kifungu cha 37A na Kanuni za utoaji na usimamizi wa mikopo za mwaka 2019 na Kanuni za Marekebisho za mwaka 2021. Mikopo hii imewezesha makundi ya vijana kupata mitaji kwa ajili ya kuanzisha na kuboresha shughuli zao za uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutoa wito kwa vijana kutumia fursa zinazowalenga, zikiwemo za elimu ya vikundi, mafunzo na ushauri wa kitaalam kwa shughuli zinazofanywa na vikundi vya vijana, mikopo na fursa ya mikopo inayotolewa katika mamlaka za Serikali za mitaa ili waweze kijikwamua kiuchumi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, wapo vijana ambao tayari walishajiunga kwenye vikundi maeneo mbalimbali lakini hawajapata mikopo. Je, Serikali iko tayari kuwasaidia vijana hao ili waweze kupata mikopo?

Swali la pili, kwa kuwa Serikali imeridhia tena mikopo ya asilimia 10 kurejeshwa, katika Halmashauri zote za Mkoa wa Kigoma ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji wako vijana na wanawake ambao tayari walishaanzisha vikundi na kujiunga kwenye vikundi na wamekidhi vigezo.

Je, Serikali ipo tayari kuwapatia kipaumbele vijana hawa na wanawake ambao tayari walishaanzisha vikundi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge naomba kumtaarifu kwamba Mheshimiwa Rais, Daktari Samia Suluhu Hassan ameridhia kuanza kutolewa kwa mikopo ile ya asilimia 10

ya mapato ya ndani ya Halmashauri na kuanzia tarehe 01 Julai, 2024 mikopo hii itaanza kutolewa. Kwa hiyo sasa hivi maandalizi yanaendelea na niwahakikishie vijana wote Tanzania wanawake na watu wenye ulemavu wakae mkao wa kula, kuanzia tarehe 01 Julai, 2024 mikopo hii itaanza kutolewa kwa makundi hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kipindi hichi chote ambacho mikopo hii ilikuwa imesitishwa fedha zimekuwa zikitengwa pia marejesho katika vile vikundi ambavyo vinadaiwa yamekuwa yakikusanywa. Kwa hiyo, mpaka muda huu fedha ziko za kutosha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu wakiwa kwenye vikundi vyao wajiandae, fedha ziko za kutosha na ikiwemo vijana, wanawake na watu wenye elemavu wa kutokea Mkoa wa Kigoma watapata mikopo hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma Mbunge wa Geita sasa aulize swali lake.

Na. 311

**Watumishi *Housing* na *NHC* Kujenga Nyumba za Watumishi Geita *DC***

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itawezesha ujenzi wa nyumba za Watumishi wa Geita DC kupitia Watumishi *Housing* na *NHC* kisha Halmashauri kulipa kwa awamu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi huzingatia taratibu za kibajeti na mipango ya maendeleo ya Serikali. Kwa misingi hiyo, Serikali itaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia

utaratibu bora wa jinsi ya kutumia fursa zilizopo kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizopo ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeshapewa utaratibu wa uingiaji wa mikataba na mashirika yanayojihusisha na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita iandae maombi maalum kwa Watumishi *Housing*, *NHC* na *TBA* ili ijumuishwe kwenye miradi ya ujenzi wa nyumba za watumishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 31 ikiwemo Halmashauri ya Geita zilianzishwa nadhani mwaka 2019 hazina nyumba hata moja. Sasa upatikanaji wa fedha za kibajeti unaenda kulingana na Halmashauri zote zinakuwa zinapewa mgao. Serikali haioni umuhimu wa kutenga bajeti maalum kwenye zile Halmashauri 31 ikiwemo Geita ambazo zimeanza miaka miwili iliyoisha hazina hata nyumba moja? Nashukuru.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa bajeti 2023/2024 Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 37.18 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunatarajia Halmashauri ziweze kutenga bajeti zake zinazotokana na mapato ya ndani kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, pia tunataka Halmashauri ziweze kuwa bunifu katika kuongeza mapato yake ili ziweze kumudu majukumu yake ikiwemo ya ujenzi wa miundombinu muhimu hii ya nyumba za watumishi. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba Serikali Kuu inakuwa inatenga bajeti pia

niendelee kusisitiza na kuzihamasisha Halmashauri kuweza na zenyewe kutenga bajeti kwa ajili ya kuhakikisha inajenga miundombinu hii muhimu kwa ajili ya watumishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na mimi nasimama kuzungumzia mpango mkakati wa watumishi *housing investment* ambao tunakwenda kutekeleza utaratibu wa kujenga nyumba za watumishi katika Halmashauri zote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe kwa sababu Bunge lako lilitupitishia bajeti na kwa kuanza tutaanza na nyumba 51 katika Halmashauri sita zikiwemo Halmashauri ya Dodoma, Halmashauri nyingine ambazo zimetajwa katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na jambo la Geita naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutakapotoka hapa tutakutana kwa ajili ya kumweleza juu ya mkakati huo na nyumba ngapi ambazo tumetenga katika Halmashauri hiyo ili wafanyakazi au watumishi wa umma waliopo katika Halmashauri ya Geita nao pia wawe sehemu ya wanaofaidika na mpango huo wa utekelezaji wa majukumu ya Awamu ya Sita, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga Mbunge wa Vwawa sasa aulize swali lake.

Na. 312

**Ujenzi wa Vituo vya Afya vya Msia na Ihanda – Vwawa**

**MHE. JAPHET N. HASUNGA** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali imechelewa kuanza ujenzi wa Vituo vya Afya vya Msia na Ihanda – Vwawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa Vituo vya Afya nchini. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya nchini kwa kadri fedha zinavyopatikana, ambapo Vituo vya Afya vya Msia na Ihanda – Vwawa navyo vitapatiwa fedha kwa ajili ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa Fedha 2024/2025 kipaumbele cha Serikali kimewekwa kwenye kukamilisha miradi viporo ya hospitali za Halmashauri na kununua vifaatiba kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ili kukabiliana na upungufu huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu hayo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hili swali nimekuwa nikiuliza mara nyingi sana hapa Bungeni na mara nyingi nimepata majibu yanayokaribia kufanana. Nataka nipate *commitment* ya Serikali, ni lini hasa mtaanza kupeleka fedha kwa ajili ya vituo hivyo vya Msia na Ihanda kwa sababu mlituambia tuandike, tulishaandikia hivyo vituo kwa muda mrefu?*(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa kituo cha Hezya kimeshakamilika na majengo yalishakamilika muda umepita kidogo. Ni lini Serikali itapeleka vifaatiba ili kituo hicho kifunguliwe na kianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ahsante kuhusiana na swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge

nimhakikishie kwamba Serikali inakusudia kujenga vituo vya afya, lakini kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2024/2025 kipaumbele cha Serikali ni kuhakikisha kwamba inakamilisha ile miradi viporo ya hospitali za Halmashauri pia kununua vifaatiba. Kwa sababu katika kipindi cha muda mfupi vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi vimeongezeka, vimekuwa ni vingi, hospitali zimetoka kuanzia 77 sasa hivi tuna hospitali 177. Vituo vya afya tulikuwa navyo 535 sasa hivi tunavyo vituo vya 896, tulikuwa tuna zahanati 4,554 sasa hivi tuna zahanati 6,160.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kipamumbele cha Serikali ni kuhakikisha vituo hivi vya kutolea huduma za afya vinakuwa na huduma bora kwa kupeleka vifaatiba pia kuajiri watumishi wa kada ya afya. Kwa hiyo, nikuhaikikishie Mheshimiwa Mbunge naomba uiachie Serikali, imelipokea na tunaamini kwamba tutakuja kujenga vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali la pili la Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na kituo chake cha Hezya anahoji kwamba ni lini tutapeleka vifaatiba? Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka 2024/2025 Serikali imetenga jumla ya bilioni 66.7 kwa ajili ya vifaatiba. Kwa hiyo, nikuhakikishie tutakipa kipaumbe kituo hiki cha Hezya ili kiweze kutoa huduma kwa wananchi wake.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yawe mafupi moja kwa moja bila historia wala maneno mengi ya ziada. Mheshimiwa Miraji Mtaturu swali la nyongeza.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali italeta fedha za kujenga Kituo cha Afya cha Misughaa katika Jimbo la Singida Mashariki ambacho tayari tulishaambiwa kitajengwa hivi karibuni? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba Serikali inakusudia na inatambua umuhimu wa ujenzi wa vituo hivi vya afya. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kituo hichi cha afya kitajengwa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha lakini kwa sasa kipaumbele kikiwa ni kuboresha huduma katika vituo vya kutolea huduma ya afya msingi vilivyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata ya Mpambala Wilaya ya Mkalama haina zahanati wala kituo cha afya, Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kujenga kituo cha afya katika Kata hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kwa kadri ya upatikanaji wa fedha itahakikisha kwamba inajenga zahanati na kituo cha afya alichokiomba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itapeleka milioni 250 katika Kituo cha Afya Ngwelo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa kadri ya upatikanaji wa fedha Serikali itahakikisha kwamba inapeleka fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha kituo cha afya alichokitaja Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu Serikali inatambua umuhimu wa kusogeza huduma za afya kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha afya Kata ya Iwondo Mpwapwa ili wananchi wa Kata hiyo waweze kupata huduma za afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kusogeza huduma za afya msingi kwa wananchi na Serikali tayari imeshaanza ujenzi wa vituo vya afya mbalimbali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali itakuja kujenga kituo cha afya kwenye Jimbo lake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru Kituo cha Afya Kabwe ni miongoni mwa vituo viporo kwa kuwa ndiyo kipaumbele cha Serikali lini mtaenda kukamilisha kituo hichi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha Serikali kukamilisha miradi viporo vya hospitali za Halmashauri, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kuwepo kwa kituo cha afya alichokitaja. Serikali kwa kadri ya upatikanaji wa fedha itahakikisha inakuja kujenga kituo hichi ili iweze kusogeza huduma za afya msingi kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini sasa ulize swali lake.

Na. 313

**Upungufu wa Maafisa Ugani – Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaajiri idadi ya Maafisa Kilimo na Mifugo 34 wanaohitajika katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uhitaji wa Maafisa Kilimo na Mifugo katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu ili kutoa huduma kwa wakulima na wafugaji. Serikali kwa kutambua uhitaji huo, imeendelea kutoa ajira za watalaam hao kila mwaka ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali iliajiri afisa kilimo mmoja. Aidha kwa mwaka wa fedha 2024/25, Halmashauri ya Mji wa Mbulu katika mpango na bajeti imepanga kuajiri Afisa Kilimo mmoja, Afisa Mifugo mmoja, Maafisa Mifugo Wasaidizi watano na Afisa Uvuvi mmoja.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuajiri wataalam wa sekta za kilimo, mifugo na zingine katika Halmashauri ya Mbulu Mji na Halmashauri nyingine nchini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa masikitiko sikutarajia haya majibu. Upungufu huu ulikuwa una miaka karibu 10 na ajira ya 2022/2023 ni Afisa mmoja. Sasa hivi mwaka huu wa fedha hatuna nafasi yoyote ya ajira kwa ajira zinazokuja mwaka wa fedha unaoisha Juni. Mimi naomba swali hili lipate majibu kwa wakati mwingine. Serikali ije na majibu ambayo yatawaridhisha wananchi wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, majibu ya Naibu Waziri hapa ama majibu ya Serikali yanasema, "Aidha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Halmashauri ya Mji Mbulu katika mpango wa bajeti imepanga kuajiri afisa kilimo mmoja na afisa mifugo." Kama

ndiyo hayo na wewe unayo, mbona unasema kwenye bajeti ijayo hampo kabisa?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru; upungufu huu umetokana na mgawanyo wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Halmashauri Mama ya Wilaya. Wakati wa mgawanyo, Halmashauri ya Mji wa Mbulu ilipokea 40%. Tatizo kubwa ni pale ambapo kila aliyestaafu hatujapata ajira mbadala. Kwa sababu hiyo kata 10 na vijiji 34 havina maafisa hao. Sasa, nilitegemea katika ajira inayokuja hivi punde tungepata wachache, ili kupunguza idadi hii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii ninaona kwamba…

**SPIKA:** Sasa, ngoja kwanza. Wachache si ndio hawa waliotajwa hapa?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, moja ameajiriwa, saba wanasema halmashauri imepanga kwenye bajeti yake. Halmashauri haina mamlaka ya kuajiri. *Commitment* ya Serikali kupunguza upungufu huu kwa Halmashauri ya Mji wa Mbulu haujaniridhisha mimi.

**SPIKA:** Sawa, sasa wewe kutokuridhika haimaanishi kwamba, haya siyo majibu sahihi kwa swali lako; ndiyo ninachokitafuta hapo. Kwamba hujaridhika lakini kilichojibiwa na Serikali ndiyo hiki kilichopo hapa; yaani Serikali imekujibu lakini wewe ungetamani majibu mazuri zaidi ya haya si ndiyo, nimekuelewa vizuri?

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Basi sawa, keti.

Hoja ya swali kuja kujibiwa upya labda wewe utaliuliza vingine, ili Serikali ilete majibu tofauti lakini kwa maana ya swali ulilouliza na jibu lililojibiwa hapa lipo sawasawa. Ndio majibu ya Serikali kwa swali lako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Bunge halijaamua kama swali lako litajibiwa upya, ndio umeshajibiwa, ila uliulize vingine ili uje ujibiwe hayo majibu pengine unayoyatafuta. Haya yaliyojibiwa hapa yapo sawa sawa kwa hiyo Serikali haitakuja kujibu upya swali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa umesimama unataka swali la nyongeza kwenye majibu ambayo mwenyewe hajaridhika nayo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo ni sekta ambazo tunazihitaji sana kwa ajili ya uzalishaji lakini kuna upungufu mkubwa wa watumishi, siyo huko Mbulu tu, ni karibu nchi nzima. Ni kwa sababu gani Serikali kwa maana ya hizi Wizara tatu hazijakaa pamoja zikaandaa *cabinet paper* ili kuwe na ajira nyingi, sawa sawa na tunavyoajiri walimu na watu wa afya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa, tunavyoajiri walimu kwani Mheshimiwa George walimu wametosha? Si na wenyewe bado tuna upungufu? Haya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mbunge ametoa pendekezo kwamba Wizara tatu zikae pamoja. Kwa hiyo, ni pendekezo kwenu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, naweza kusema kwamba, tumechukua mawazo yake. Nimhakikishie kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa watumishi hawa (maafisa kilimo na maafisa mifugo). Katika mikakati ya Serikali, mkakati wa kwanza ni kuhakikisha kwamba inaajiri maafisa hawa kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, pia mkakati mwingine, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amenunua pikipiki kwa ajili ya maafisa ugani Tanzania nzima na amewakabidhi. Kwa hiyo, sasa niwakumbushe Wakurugenzi waweze kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mafuta kwenye pikipiki hizi, ili hawa maafisa ugani wachche waliopo waweze kuhudumia na kata za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia huduma za maafisa ugani zimeenda kidijiti. Sasa hivi tuna mfumo wa M- Kilimo ambapo, mkulima anaweza kutumia simu yake kumuuliza maswali afisa ugani na akapata majibu kielektroniki (kidijiti). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huo pia ni mkakati madhubuti wa kujaribu kupunguza ukali wa upungufu wa maafisa hawa. Pia, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali ambao na wenyewe wanatoa huduma hizi za maafisa ugani. Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa maafisa hawa na ina mikakati. Mkakati mojawapo ni kutengeneza ajira na kuajiri maafisa hawa ili waweze kuja kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 314

**Kuhimiza wananchi juu ya utunzaji wa mazingira**

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipangaje juu ya kuhimiza wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira ikiwemo na upandaji miti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza Khamis, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa utunzaji, uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa njia mbalimbali ikiwemo vipindi vya redio, runinga, magazeti, Hotuba za Viongozi, Machapisho ya Ofisi ya Makamu wa Rais na

mitandao ya kijamii. Aidha, elimu ya utunzaji wa mazingira itaendelea kutolewa kupitia maadhimisho mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Siku ya Wakulima, Siku ya Mazingira Duniani, Siku ya Ozoni Duniani, Siku ya Jangwa na Ukame Duniani na Siku ya Misitu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 - 2032 ambapo, pamoja na mambo mengine itaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti nchini hususani katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Katavi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, swali la nyongeza.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, Serikali imejipangaje kuweka ruzuku kwa nishati ya gesi ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Serikali haijaweka bado mkazo kwenye kila nyumba moja kupanda mti wa matunda au kivuli. Ningeomba kupata majibu kwenye hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, najibu maswali mawili ya Mheshimiwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ruzuku kwenye matumisi ya nishati. Tayari tulishakaa pamoja na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Ofisi wa Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ili kuona namna ya kupunguza sasa gharama hasa za uingizaji wa vifaa vya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuweza kuona namna ambavyo wananchi wanaweza wakahimili kuweza kutumia hiyo nishati.

Mheshimiwa Spika, pia hata juzi wakati unaziduliwa ule mpango ama mkakati maalum wa nishati safi ya kupikia. Tayari kwenye mpango ule imeshapendekezwa kwamba, sasa Wizara zinazohusika zione namna ya kupunguza gharama za uingizaji wa vifaa vya matumizi ya nishati safi ya kupikia. Lengo na madhumuni wananchi pia waweze kuhudumu ama waweze ku-*afford* matumzi ya nishati safi.

Mheshimiwa Spika, kingine pia mpango ule wa wananchi kuendelea kupanda miti nyumba kwa nyumba, ikiwemo miti ya kivuli, miti ya matunda na miti ya dawa unaendelea. Tayari tumeshatoa wito kwa Viongozi wote wa Dini, Viongozi wa Chama na Serikali wauendeleze mpango ule katika mikoa yote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nimuombe Mheshimiwa Mbunge sasa na yeye kwa kushirikiana na wadau katika Mkoa wake, aendeleze ili na sisi Ofisi ya Makmu wa Rais Mazingira, tupo tayari kwenda kumuunga mkono kupanda miti katika Mkoa wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali ya nyongeza yawe mafupi. Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mvua kubwa za mwaka huu zimesababisha mafuriko hadi kuua watu kule Moshi. Je, Waziri yupo tayari kufuatana na Wabunge wa Moshi na wale wa Viti Maalum, kwenda kuona jinsi gani Mto Rau umeathirika kwenye kingo zake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, juzi tu nilikuwa katika Wilaya ya Moshi na nimeona athari kubwa iliyojitokeza kutokana na mvua kubwa ikiwemo kuharibika kwa makazi pia kuharibika kwa mazingira kwa ufupi na miundombinu iliyoharibika.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote wa Wilaya ya Moshi na wa Tanzania nzima. Nipo tayari kufuatana nao kwenda kwenye mikoa yao kuona hali na namna ya kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa bado miti inaendelea kukatwa na inayopandwa si kwa kasi kubwa. Je, ni lini Serikali itakuja na sheria ya kuthibiti hasa wale watu wa chini chini kidogo ambao wanaendelea kukata miti na kuharibu mazingira, sheria italetwa lini humu ndani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Asha. Sheria ipo na tayari tumeshaanza kuchukua hatua. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba, wale wote ambao wanavunja Sheria ama utaratibu katika kuharibu, kukata miti, kuchoma misitu na kufanya uchafuzi mwingine wa mazingira. Sheria zipo na tutaendelea kuwachukulia hatua, kama ambavyo Sheria zimeelekeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina mkakati gani wa kupanda miti kandokando ya mito pamoja na barabara zote za *TANROADS* nchini ili kulinda miundombinu ya barabara pamoja na mito isiendelee kuharibika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, miongoni mwa

sababu zinazopelekea kuathirika na hata kupotea kwa badhi ya mito hasa ile mikubwa ya asili na kuharibika kwa misitu mingi ni suala zima la ukatwaji na kutokupandwa miti kwenye maeneo haya, hasa maeneo ya barabara na maeneo mengine. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge tayari tumeshaanza kufanya hiyo kazi. Tayari kuna mito mingi tumeshaanza kuipandia miti.

Mheshimiwa Spika, pia, tayari maeneo mengi katika nchi yetu hasa katika Mkoa huu wa Dodoma, tayari tumeanza jitihada ya kupanda miti maeneo ya barabarani ili lengo na madhumuni kuanza kurejesha miti ya asili, pia kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 315

**Ujenzi wa Kituo cha Kusambaza Umeme Nkangamo – Momba**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha kusambaza Umeme Nkangamo – Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa niaba ya Waziri wa Nishati.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO) K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Serikali kupitia Mradi wa *TAZA* unaotekelezwa na *TANESCO* upo katika hatua za awali za ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme kilichopo katika Kijiji cha Nkangamo, Kata ya Nkangamo, Halmashauri ya Wilaya ya

Momba. Pia kipo kilometa 20 kutoka Halmashauri ya Mji wa Tunduma katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo hiki unatarajia kuanza hivi karibuni ambapo kwa sasa hatua ya kusaini mkataba kati ya *TANESCO* na mkandarasi atakayejenga Kituo hiki, tayari umekamilika. Kukamilika kwa kituo hicho kutawezesha upatikanaji wa umeme wa uhakika katika Mkoa wa Songwe ikiwemo Halmashauri ya Momba, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Baada ya majibu hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Pamoja na hatua hizo ambazo tunaendelea kusubiri, tuna changamoto ya kuwa na umeme usiokuwa na nguvu *(low voltage)*. Serikali imejipangaje kutusaidia kutatua changamoto hiyo ili wananchi waweze kufanya shughuli zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Tuna changamoto ya uhaba wa mita hivyo, kuvunja moyo wananchi ambao huduma ya umeme imeshawafikia. Ni lini mtatusaidia kupata mita Jimboni Momba?

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (MHE. STEPHEN L. BYABATO) K.n.y. NAIBU WAZIRI MKUU NA WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nikianza na la kwanza; tatizo la *low voltage* hasa linasababishwa na wateja kuwa wengi kuzidi miundombinu ambayo awali ilipelekwa katika eneo hilo. Kwa

hiyo, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge baada ya hapa atawaelekeza wenzetu wa *TANESCO* wakaangalie ni maeneo gani ambayo yamepungukiwa nguvu ya umeme, ili katika kipindi hiki ambacho bado kituo kikuu hakijajengwa cha kwenda kuongeza umeme mkubwa, waweze kuongeza nguvu za umeme katika maeneo hayo hasa kwa kupeleka *transformer* kubwa zenye uwezo wa kuhudumia wateja waliopo kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la pili la mita. Ni manunuzi ya kawaida na tutahakikisha kwamba, mita na vifaa vingine vyote vinavyotakiwa kupatikana kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi vinapatikana na si Momba peke yake hata katika ameneo mengine ili wananchi waweze kupata huduma kwa sababu mwamko wao umekuwa ni mkubwa sana, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe sasa aulize swali lake.

Na. 316

**Mkakati wa kuifanya Wilaya ya Ukerewe kujitosheleza kwa chakula**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kuifanya Wilaya ya Ukerewe kujitosheleza kwa chakula kwa kutumia rasilimali zilizopo ikiwemo maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji iliyopo Ukerewe ambayo ni Skimu ya Bugolora na

Bwawa la Miyogwezi inayotumia *pump* kutoa maji Ziwa Victoria. Ukarabati utakapokamilika jumla ya hekta 320 zitaweza kumwagiliwa na wakulima wa Ukerewe kufaidika na kilimo hicho.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeainisha skimu za Kiozu, Busegena na Mibungo zenye jumla ya hekta 3,809 zilizopo Wilayani Ukerewe kwa ajili ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, kabla ya kuanza ujenzi wa skimu hizo, ili kuimarisha uzalishaji wa mazao ya chakula. Aidha, ushauri wa wataalamu na matumizi ya ardhi na maji katika kilimo cha umwagiliaji yatawezesha kuongeza tija na uzalishaji na hivyo kuchangia kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa mbolea ya ruzuku kwa wakulima wote nchini, ili kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula. Kwa upande wa Ukerewe, jumla ya tani 29.15 za mbolea zimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza. Pamoja na Serikali kugawa *soil kits* (vipimia udongo) mwaka jana, Ukerewe ni moja kati ya wilaya ambazo hazikupata vifaa hivi. Nataka kujua ni lini Serikali itapeleka vipimia udongo kwenye Wilaya ya Ukerewe?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Pamoja na kuonesha kwamba Ukerewe imepata mbolea ya ruzuku lakini wakulima wa Ukerewe wamekuwa wanapata shida sana kupata mbolea hii kwa sababu hakuna wakala wa uhakika kwenye eneo lile. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba, wanapeleka wakala au anapatikana wakala atakaye-*station* pale kwa ajili ya kusaidia Wakulima wa Ukerewe kupata mbolea?

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nikiri kwamba ni kweli Halmashauri ya Ukerewe ni moja ya halmashauri ambazo hazijapata *soil kits*, kwa sababu mwaka jana tuligawa katika halmashauri 142 kati ya 184 zilizopo nchini. Kwa hiyo, hizi halmashauri 142 zilizobakia zitapata katika mwaka huu wa fedha kwa sababu tayari tumeshafanya manunuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mbolea nikiri kwamba, bado tumekuwa na changamoto ya wasambazaji. Pale Ukerewe tuliweka msambazaji ambaye anaitwa *OMAP* pamoja na Kampuni ya Minjingu. Katika mwaka unaokuja msimu wa kilimo tutamuongeza wakala wa *TFC* (Kampuni ya Uzalishaji Mbolea), ili aende pale kuongeza nguvu katika usambazaji wa mbolea kwa wananchi wa Ukerewe, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ina mkakati gani wa kuongeza skimu za umwagiliaji katika Wilaya ya Ileje ili wananchi waweze kunufaika na maji yaliyopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Wananchi wa Ileje wawe na uhakika kwamba, tunafanya upembuzi yakinifu wa skimu saba kwa wakati mmoja ili kuhakikisha kwamba tunaongeza shughuli za umwagiliaji katika eneo hilo. Kwa hiyo, ni jamnbo ambalo ni endelevu na linafanyika katika wakati uliopo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini sasa Serikali itaifanya Halmashauri ya Msalala kujitosheleza kwa chakula kwa kutumia rasilimali ya Bwawa lililopo Kijiji cha Igundu, Kata ya Mwalugulu kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kwamba Bwawa hilo lipo katika mipango yetu, tunachotaka ni kulijenga na liwe bora, ili liweze kutumika katika kipindi chote. Kwa hiyo, jambo hilo lipo katika mipango ya Wizara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha wananchi wa Mji wa Iringa wanaendelea kupata mbogamboga na matunda kwa kukarabati Skimu ya Umwagiliaji ya Mkoga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ni kwamba moja ya maelekezo ambayo sisi Wizara ya Kilimo tunayo kutoka kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kuhakikisha tunapitia zile skimu zote za zamani za asili, kujaribu kujenga skimu mpya pamoja na kuhakikisha tunajenga mabwawa ili kuhakikisha kilimo cha umwagiliaji kinakuwepo

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika eneo la Mkoga ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliainisha, lipo katika mipango yetu na tunalifanyia kazi. Kwa hiyo, nimuondoe shaka tu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, jambo hilo litafanyika ili kuhamasisha kilimo cha mbogamboga kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 317

**Kutenga eneo la ukaguzi wa magari kwa Polisi Dar es Salaam**

**MHE. MARIAM N. KISANGI** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuwatengea Polisi Mkoa wa Dar es Salaam maeneo ya kufanyia ukaguzi wa magari kupunguza msongamano barabarani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kushirikisha Halmashauri ya Jiji na Manispaa zake pamoja na *TANROADS* ili kubaini na kutenga maeneo kwa ajili ya ukaguzi wa magari unaofanywa na Jeshi la Polisi, ili kupunguza msongamano katika jiji la Dar es Salaam, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mafupi ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyingeza.

Kwa kuwa nyakati za asubuhi askari wa usalama wa barabarani hufanya ukaguzi wa kushtukiza ambao unasababisha msongamano na hasa katika maeneo ya Gerezani, kwenye Daraja la *SGR*, Ilala Boma, Magomeni Mapipa, kwenye Njia Panda ya Kanisani, Kunduchi Mtongaji, Buguruni, Amana, Jirani na Mkuu wa Mkoa na meneo mengi ya Mkoa wa Dar es Salaam ukaguzi huo hufanyika: -

Je, Serikali haioni haja ya kuharakisha mchakato huo ili kuondoa kero ya kusimamaisha magari na ongezeko la foleni katika Jiji la Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa changamoto hiyo hiyo ya ukaguzi inaikumba pia barabara ya Dar es Salaam kuja Dodoma, utakuta kuna vizuizi usiku vimewekwa vyuma ambavyo havina alama yoyote au viashiria na askari ambaye hana mavazi maalumu, hali ambayo inasababisha hatari kwa askari wenyewe lakini pia kwa waendesha magari.

Je, Serikali imejipanga vipi sasa katika kuhakikisha wanatengeneza vifaa vya kisasa vya ukaguzi badala ya kuweka vyuma barabarani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mariam Kisangi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, kwa kutambua msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato huo utakwenda haraka ili kukamilisha maeneo haya na yatengwe tayari kwa ajili ya ukaguzi na hivyo kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili kuhusu askari wanaoweka vizuizi barabarani, ninaomba nilielekeze Jeshi la Polisi kupitia kwa *IGP* kuhakikisha kwamba askari wote wanaoweka vizuizi kwanza wavae zile nguo mahasusi ambazo zinaonesha kwamba wapo lakini pia wawe na taa ili kuhakikisha kwamba wao wenyewe wawe salama lakini pia watumiaji wengine wa barabara pia wawe salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri kabisa ambayo

yamejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba kuongezea swali la Mheshimiwa Mariam Kisangi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia kumtaarifu Mheshimiwa Mariam Kisangi kwamba katika mwaka huu wa fedha tunatarajia kuanza utaratibu wa ukaguzi wa magari wa lazima kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa utaratibu wa *EPP*. Mchakato huo upo katika hatua nzuri na pale utakapokuwa umekamilika changaoto hii itakuwa imepata ufumbuzi wa kudumu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe sasa aulize swali lake.

Na. 318

**Kugawa eneo la Hifadhi ya Mkweni kwa wananchi Mbogwe**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itagawa eneo la Hifadhi ya Mkweni kwa wakulima na wafugaji Mbogwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kupitia Kamati ya Mawaziri wa Wizara nane wanaoshughulikia utatuzi wa migogoro ya vijiji 975, Hifadhi ya Msitu wa Vilima vya Mkweni haikuwa kwenye orodha ya misitu yenye migogoro hivyo hapakuwa na mapendekezo yoyote ya kumegwa kwa hifadhi hii. Aidha, ilibainika kuwa hakuna uhaba wa ardhi katika vijiji vya jirani na msitu bali kulikuwa na uelewa mdogo wa masuala ya uhifadhi na hasa mipaka ya msitu huo. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ameelekezwa kuimarisha mipaka na kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mazingira hayo, pamoja na umuhimu wa hifadhi hii kwa jamii inayozunguka msitu husika, tunashauri kuwa wananchi wa maeneo hayo wazingatie mipango ya matumizi bora ya ardhi iliyoandaliwa mwaka 2020/2021. Kwa kufanya hivyo watatumia ardhi yao kwa manufaa zaidi bila kuwepo migogoro yoyote, kwa kuzingatia mahitaji yao mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kwenye majibu imeonekana wale Mawaziri nane hawakufika Mbogwe lakini huu mgogoro upo na wananchi wanaihitaji ardhi hiyo: -

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana na mimi sasa ili twende tukaone kiuhalisia kusudi tuweze kuwasaidia wananchi hao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kumekuwa na changamoto kwenye Wilaya ya Mbogwe kwa vile Wilaya ya Mbogwe imekaa katikati ya mapori. Huku upande wa Geita kuna Kijiji cha Nyashinge; wananchi wakiwa wanasafiri kuingia Mbogwe wanakamatwa na kupigwa na askari wa hifadhi.

Je, huo ni utaratibu au ni kinyume cha sheria? Naomba utoe ufafanuzi ili askari walioko kule kwenye *site* waelewe kwamba wajibu wao ni nini wanapomkamata mwananchi anapita kwenye pori. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Vilima vya Mkweni yenye ukubwa wa hekta 15,000 na zaidi ni muhimu sana kwa uhifadhi. Vilevile tunafahamu kwamba ni muhimu kwa maisha ya wananchi kwa sababu hifadhi hii

inazungukwa na vijiji vitano ambavyo vinategemea sana shughuli za umwagiliaji wa maji yanayotoka kwenye hifadhi hii. Kwa umuhimu huo niko tayari kwenda Mbogwe ili tuweze kupata muafaka wa jinsi ya kusimamia vizuri hifadhi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, nitumie fursa hii kuwakumbusha wahifadhi wetu kwamba, wanapofanya shughuli zao za uhifadhi wahakikishe wanazingatia sheria na kanuni zilizopo bila kuwaonea wananchi na kwamba Serikali haitafumbia macho askari yeyote atakayekwenda kinyume na taratibu zilizopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 319

**Umuhimu wa Kudhibiti Tembo**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatenga maeneo ya kikanda yatakayorahisisha udhibiti wa tembo wasihatarishe maisha ya watu na mali zao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TAWA* imetenga kanda saba za kiutendaji ambazo zinatumika katika kusimamia shughuli za uhifadhi ikiwemo udhibiti wa wanyamapori wakali na waharibifu kama vile tembo, ili wasihatarishe maisha ya watu na mali zao. Kanda hizo za kiutendaji ni Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kusini Mashariki, Kanda ya Kati, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Magharibi na Kanda Maalumu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kupitia kanda hizo za kiutendaji jumla ya vikosi 47 vya askari vimeanzishwa katika maeneo mbalimbali nchini vikiwa na jumla ya askari wahifadhi 133 na askari wanyamapori wa vijiji 184.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninaomba kusema kwamba, kwa kuwa tembo wanapoharibu mazao ya wakulima na hata kuua wananchi, hakuna fedha ya kulipa katika muda mfupi na kwa kiwango kinachotakiwa: -

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka kuanzisha mfuko wa fidia chini ya Wizara hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa tembo wakiua binadamu fidia yake ni shilingi milioni tano na kwa kuwa bnadamu ana thamani kuliko tembo: -

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa wa kuleta mapendekezo ili sheria hii ibadilishwe, kwamba binadamu alipwe fedha zaidi kuliko tembo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa tuko kwenye majadiliano kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii na wenzetu wa Wizara ya Fedha kuhusu viwango vipya vinavyopendekezwa ili tuweze kuja na mfumo mpya wa malipo. Kwa hiyo ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, wakati wa kulifanyia kazi jambo hili, basi tutaweza kuchukua mawazo yake yale ya kwanza na haya ya kuwa na mfuko maalumu ili tuone jinsi ambavyo tunaweza kutekeleza jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 320

**Changamoto ya Maji Kata ya Lihimalyao – Kilwa**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza: -

Je, ni nini mpango wa Serikali kutatua changamoto ya ukosefu wa maji Kata ya Lihimalyao – Kilwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha tena kwamba msizungumze na simu Bungeni. Msizungumze na simu Bungeni. Humu Bungeni kuna wageni wanakuja kujifunza namna tunavyoendesha shughuli za Bunge. Ninyi mnafikiri mnatoa ujumbe gani kwao kwa kupokea simu kwenye Mkutano wa muhimu sana kama huu? *(Makofi)*

Simu zenu ni za muhimu mnazungumza na wapiga kura, nenda nje. Ukizungumza na simu humu ndani utatajwa ili ukazungumze nje na hiyo simu na usijisikie vibaya. Kwa sababu tangazo hili nimeshalirudia mara nyingi na ninadhani mpaka sasa kama ni mwalimu mmemwelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kata ya Lihimalyao ina jumla ya vijiji sita vya Lihimalyao Kaskazini, Lihimalyao Kusini, Rushungi, Kisongo, Ruyaya na Namakongoro. Kati ya vijij hivyo, Kijiji cha Ruyaya kinapata huduma ya maji safi. Aidha, vijiji vya Kisongo na Rushungi vitapata huduma ya maji kupitia programu ya visima 900 ambapo shughuli za utafiti wa maji chini ya ardhi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 inatekeleza mradi wa maji Lihimalyao kupitia kisima kirefu cha Pandeploti utakonufaisha vijiji vilivyobaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, mradi wa Pandeploti ambao unakusudia kunufaisha vijiji vilivyobaki, ningependa kupata majibu ya Serikali: -

Je, ni lini mradi huu utakamilika kwa ajili ya vijiji vilivyobaki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa mara ya mwisho Kata ya Lihimalyao ilitembelewa na Waziri wa Maji mwaka 2009 na kulikuwa na changamoto kadhaa alizozibaini ili kutatua changamoto hizo.

Je, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri yuko tayari sasa kuambatana nami kwenda Jimbo la Kilwa Kusini Kata ya Limalyao ili kujiona changamoto ya tatizo la maji katika kata hii na hatimaye tuzitatue kwa pamoja? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto zilizopo katika jimbo hilo na katika huu mradi wa Pandeploti kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, Serikali inaendelea na kufanya tathmini ya mwisho ili waweze kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika katika vijiji vilivyobaki.

Mheshimiwa Spika, katika ombi la pili, Serikali kupitia Sekata ya Maji – Wizara ya Maji, sisi tuko tayari kuandamana na Mheshimiwa Mbunge kwenda katika eneo hilo ili kujionea hali halisi ya changamoto ili tuweze kuchukua hatua stahiki na wananchi wa pale waweze kupata maji safi na salama.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bilakwate, swali kwa kifupi.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji kwenye Kata ya Songambele? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Innocent Bilakwate kwa kufuatilia sana mradi huu na kwa uhalisia ni kwamba mradi huu unaunganisha vijiji viwili na katika kijiji cha kwanza kibali kilishatoka na mkandarasi ameshapatikana na ataanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, katika kijiji cha pili ambacho ni cha Songambele ambapo mradi wa *P4R* ambao tunatarajia kabla ya Julai 2024 kibali kitatoka na baadaye mkandarasi atapatikana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafikisha huduma ya maji katika eneo hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ashante kwa kunipa fursa aya kuuliza swali dogo la nyongeza: -

Je, ni lini mradi wa vijiji 11, Tarafa ya Mlimba utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninatumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Godwin Kunambi kwa kazi kubwa aliyoifanya kuupambania mradi huu. Ninakumbuka kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu alienda kwenye ziara katika Jimbo la

Mlimba na akiambatana na Waziri wa Maji Mheshimiwa Jumaa Aweso, na alitoa maelekezo ya madai ambayo mkandarasi alikuwa anadai. Wiki mbili zilizopita mkandarasi huyo ameshalipwa shilingi bilioni moja. Tunafahamu kwamba bado kuna madai mengine lakini tunamtaka mkandarasi huyu awepo *site* na kazi iendelee na kuhakikisha kwamba hata anapoleta madai na sisi Serikali tutahakikisha kwamba tunamlipa kulingana na *certificates* ambazo atakuwa ana-*raise,* ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 321

**Mradi wa Maji Nangombo – Nyasa**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza: -

Je, lini mradi wa maji Nangombo – Nyasa utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kusitisha mkataba na mkandarasi aliyetekeleza Mradi wa Maji Nangombo – Kilosa, uliopo Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma kutokana na kasi ndogo ya utekelezaji. Mradi huo umefikia wastani wa 8%, huku muda wa mkataba ukiwa umefikia kikomo kwa zaidi ya miezi sita. Baada ya mkataba huo kusitishwa, mradi huo utaanza kutekelezwa kupitia wataalam wa ndani ambapo kazi zinazotarajiwa kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji *(intake)*, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 45.5, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 1,000,000 na ujenzi wa vituo 10 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, mradi huo utatekelezwa ndani ya miezi nane kuanzia Juni 2024 na kunufaisha wananchi 14,323 waishio katika vijiji vinne vya Nangombo, Kilosa, Likwilu pamoja na Ruhekei.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza ninaomba niweke mezani masikitiko yangu makubwa pamoja na wananchi wa Nangombo na Kilosa kwa kucheleweshwa na kuteswa kwa muda mrefu bila kupata maji kutokana na ucheleweshaji wa mradi huu. Swali langu la nyongeza: -

Je, ni lini Kijiji cha Chiulu na Malini ambao nao pia walitegemea kunufaika baada ya kukamilika kwa mradi huu wataweza kupatiwa maji?

Je, ni kwa nini mradi wa Songambele, Puulu na Ngehe unasuasua mpaka leo kwa tabia hizi hizi za mradi wa Nangombo, na ni lini utakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ninafahamu na Serikali inatambua changamoto ya maji katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja. Sisi kama Serikali tumekwishaanza kuchukua hatua. Kwa Vijiji vya Malini pamoja na Chuulu Serikali imeshakamilisha usanifu wa miradi hiyo na kibali cha kutangaza kumpata mkandarasi tayari kimeshatoka.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mradi huu utaanza katika bajeti ya mwaka 2024/2025. Tunaamini kabisa kwamba utekelezaji wake utaenda kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa eneo la Songambele ni kweli kabisa kwamba Mradi wa eneo hili umechelewa; na hapa hatuwezi kuzunguka. Ni kweli kabisa umechelewa, lakini tayari sasa Serikali imeshachukua hatua. Kuna mabomba ambayo yalikuwa yanahitajika, Serikali tayari imeshanunua na kuna bomba lile kubwa kwa ajili ya mradi, tayari nalo limeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba utekelezaji wake na yeye basi au-*own* ule mradi na apate muda wa kuwa anatembelea kuona kile ambacho tayari Serikali imeshaelekeza na wakandarasi wanatekeleza, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ni lini mradi wa Mtangimbole, Ngadinda, Lutukila na Ndelenyuma katika Halmashauri ya Madaba utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tumewataka wakandarasi wote nchi nzima, wale ambao wanadai na wale ambao hawadai. Kazi ambayo wanatakiwa kuifanya ni kuhakikisha kwamba miradi iendelee wakati Serikali ikiwa inaendelea kufanyia kazi madai yao.

Kwani tunaamini kwamba wakishafanya hivyo basi itakuwa ni rahisi zaidi Serikali kuwa inalipa kulingana na *certificate* ambazo watakuwa wameziwasilisha Serikalini. Tunaamini baada ya kukamilisha hilo na mradi huu utaweza kukamilika kwa wakati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa wabunge.

Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mbunge wa Bahi, sasa aulize swali lake.

Na. 322

**Balozi Mbalimbali Kuhamia Dodoma**

**MH. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini Balozi mbalimbali zitahamia Dodoma kuunga mkono juhudi za Serikali kuhamia Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. MBAROUK NASSOR MBAROUK)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kufanya jitihada za kushawishi balozi zote zinazowakilisha nchi zao hapa nchini kuhamia Makao Makuu ya Nchi Dodoma. Tayari, Serikali imetenga eneo maalum la kujenga ofisi za kibalozi na makazi ya waheshimiwa mabalozi na tayari hati za viwanja hivyo zimeanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea pia kuzihamasisha balozi kwa kuwafahamisha juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali za kuboresha miundombinu katika jiji la Dodoma ambayo ni muhimu kwa mabalozi hawa katika utekelezaji wa majukumu yao pindi watakapohamia. Kutokana na juhudi hizo zipo balozi kadhaa ambazo zimeishaleta wataalamu wake ili kukagua viwanja hivyo na sasa wanaandaa michoro ya majengo watakayojenga. Aidha, hadi sasa nchi nne tayari zimeshafungua

ofisi za ubalozi jijini Dodoma na Nchi hizo ni China, Ufaransa, Uingereza na Ujerumani lakini pia na pamoja na Ofisi ya Uratibu wa Umoja wa Mataifa *(UN)*. Wizara inaendelea kuzishawishi nchi nyingine kufungua ofisi zao ndogo hapa jijini Dodoma. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali; nina maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza, kwanza nishukuru kwa hizi balozi ambazo zimefungua ofisi ndogo. lakini je, nilitaka kujua ni kwa ajili ya hizi ofisi kupokea tu barua kuzipeleka makao makuu ya *embassy* zilizopo Dar es Salaam au na huduma zingine zitaanza kutolewa kama *VISA* na mambo mengine?

Mheshimiwa Spika, swali jingine la nyongeza ni kwamba kwa mujibu wa *international customs* kuhusu *embassy* hizi…

**SPIKA:** Mheshimiwa mtazame mtu anayezungumza yupo upande gani. Endelea nilikuwa namwambia Mbunge aliyekatiza mbele yako.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Swali langu la pili, ni kwamba kwa mujibu wa *international customs* kuhusu balozi alipo Mkuu wa nchi na balozi zinatakiwa ziwe katika eneo lile na kwa majibu ya Serikali ni kwamba bado zitaendelea kushawishi. Sasa nilitaka nipate majibu ya Serikali, je, makadirio ni miaka mingapi balozi zote zitakuwa *full operating* Dodoma na tukichukua mifano kama nchi zingine wamefanya hivyo kama ilivyo Nigeria, Ujerumani na pale Kuala Lumpur na maeneo mengine, je, lini hasa tunategemea?

**SPIKA:** Umeshauliza maswali mamwili Mheshimiwa.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. MBAROUK NASSOR MBAROUK):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kufunguliwa kwa ofisi hizi kutarahisisha kupatikana kwa huduma mbalimbali kutoka katika ofisi hizo. Huduma hizo ni kama vile uratibu wa kupatikana kwa *VISA* katika nchi hizo, lakini pia utarahisisha mawasiliano baina ya balozi hizi na Serikali. Mwisho ni kufanikisha miadi mbalimbali kati ya balozi hizi na wale ambao wanataka hizo huduma katika hizo balozi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na lini hasa balozi hizi zitaamia Dodoma au zitakamilisha kuhamia Dodoma, hakuna muda maalum uliyowekwa kwa sababu hii pia inategemea na mipango ya nchi husika katika kuhamia hapa Dodoma, kwa sababu kila nchi inautaraibu wake na tunafahamu kwamba kuna baadhi ya nchi zimekamilisha kujenga majengo yao mapya ya ubalozi katika Mji wa Dar es salaam hii miaka ya karibuni tu. Kwa kuchukulia mfano, nchi ambazo hivi miaka ya karibuni zilihamisha makao makuu yao ni kama vile nchi ya Shirikisho la Uman ambalo lilihamisha makao makuu yake mwaka 2000 na ilichukua takribani kama miaka mitano mpaka balozi zote kuhamia katika mji mkuu.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine ni Nigeria ambayo wao walihamisha makao makuu yao mwaka 1991 na ilichukua takribani kama miaka 12 mpaka balozi zote kuhamia katika makao makuu ya mji huo au ya nini, nchi hiyo Mji wa Abuja. Kwa hiyo, sisi ni imani yetu kwamba kwa jitihada kubwa ambazo Serikali inachukua katika kuimarisha miundombinu katika Jiji la Dodoma haitachukua muda mrefu balozi zote zitahamia Dodoma. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umesema nchi ya Lagos, natumai ulikusudia kusema Nigeria, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 323

**Kuboresha Utendaji wa Mamlaka ya Hali ya Hewa**

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha utendaji wa Mamlaka ya Hali ya Hewa ili waweze kutoa utabiri sahihi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, swali la nyongeza. Aah! Majibu, samahani.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha Mamalaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* nchini kufikia lengo la kutoa utabiri sahihi wa hali ya hewa nchini, Serikali kupitia Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2023/2024 imetenga jumla ya shilingi bilioni 13 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa rada, vifaa na miundombinu ya hali ya hewa ambapo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali ikiwemo, ufungaji wa rada mbili za hali ya hewa unaofanyika katika mikoa ya Mbeya na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, aidha, *TMA* imeingia mkataba wa kununua rada nyingine mbili za hali ya hewa zitakazofungwa katika mkoa wa Dodoma na Kilimanjaro na hivyo kufikisha lengo la muda mrefu la kuwa na rada saba za hali ya hewa nchi nzima. Pia *TMA* imeingia mkataba wa kununua mtambo wa kisasa ya kuandaa utabiri wa hali ya hewa *(Complete forecasting system)* ambayo itaimarisha uwezo wa kupokea *data* za hali ya hewa, picha za *satellite*, kuchakata na kuchapisha kidijiti matokeo ya utabiri wa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, *TMA* imenunua mitambo mitatu ya uangalizi wa hali ya hewa katika bahari ya Hindi ambayo itafungwa katika pwani ya Zanzibar, Dar es Salaam na Bagamoyo na hivyo kuongeza mchango wa huduma za hali ya hewa katika uchumi wa bluu. Aidha, mitambo 15 ya kupima hali ya hewa

mahususi kwa sekta ya Kilimo imeshanunuliwa na itafungwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Jumla ya mitambo 10 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe imepokelewa ambapo mitambo mitatu imeshafungwa katika vituo vya hali ya hewa vilivyopo Mtwara, Songea na Arusha, maandalizi ya ufungaji wa mitambo saba iliyobaki inaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha utendaji wa *TMA* Serikali imeajiri watumishi wapya 31 wa Kada tofauti tofuati na kuwapangia katika vituo mbalimbali vya hali ya hewa nchini na hivyo kuimarisha uwezo wa *TMA* katika kuendelea kutoa huduma bora za hali ya hewa nchini. Aidha, Serikali imeendelea kuimarisha shughuli za Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kujenga Ofisi ya hali ya hewa ya Kanda ya Mashariki na kituo cha Tahadhari za Tsunami Jijini Dar es Salaam, ambapo kazi hiyo ya ujenzi imefikia asilimia 39.

**SPIKA :** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka watumishi wa mamlaka katika ngazi za kanda, mkoa na wilaya ili kuboresha huduma za mamlaka na huduma kwa wananchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kutumia simu za mikononi ili kuwapelekea wananchi taarifa muhimu za hali ya hewa pale inapotokea kwamba kuna hali tete katika maeneo mbalimbali husika? *(Makofi)*

**SPIKA :** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza mpaka ninapozungumza Mamlaka ya Hali ya Hewa inawatumishi 537 na imekwisha ajiri watumishi wengine 31 na mwaka wa fedha ujao tunategemea kuajiri watumishi 64. Kwa hiyo, tutaendelea kupeleka watumishi hatua kwa hatua ili kuhakikisha kwamba tunaifikia nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, pili kwa upande wa mfumo waliyouzungumza wa *SMS*, mpaka ninapozungumza Mamlaka ya Hali ya Hewa lazima tuipongeze kwa sababu ikitoa taarifa za utabiri sasa hivi karibu nchi nzima inajua kwamba kuna utabiri wa hali ya hewa, kutakuwa na Tsunami na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wake aliyoutoa ni mzuri, tumeshaanza mchakato, tumeanza na mfumo wa *farm SMS* ambao tunapeleka kwanza zile *SMS* kwa wakulima. Tutakuwa na makundi mengine mengine na hatimaye tutafikia jamii nzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa wabunge. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 324

**Idadi ya Walimu wa Elimu Maalum Nchini**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Walimu wa Elimu Maalum nchini ni wangapi na upungufu ni kiasi gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Januari 2024 walimu wa Elimu maalum waliopo katika ngazi ya Elimu ya awali, msingi, sekondari, vyuo vya Ualimu, vyuo vya *FDC*, *VETA* na Vyuo Vikuu wapo 4,341 wakiwemo wanaume 2,489 na wanawake 1,852. Aidha, hadi kufikia Januari 2024 bado kuna upungufu wa walimu wapatao 2,754.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua katika kuongeza idadi ya walimu wenye taaluma ya Elimu

maalum kwa lengo la kukabiliana na upungufu uliopo ili kukidhi mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kuweka kipaumbele kwa walimu waliosomea Elimu maalum katika ajira mpya za walimu na kuongeza udahili wa walimu tarajali katika vyuo vya ualimu vinavyotoa taaluma ya Elimu maalum nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri na kwa hatua ambazo zimeendelea kuchukuliwa. Ili kuondoa changamoto ya upungufu wa walimu hawa na ili kuwawezesha wanafunzi wenye ulemavu kusoma kwenye maeneo yao. Serikali imefikia hatua gani kuwafanya walimu wote wasome Elimu maalum nchini, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwisha jibu kwenye swali la msingi, kwamba Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali ikiwemo na kuajiri lakini nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako Tukufu, Serikali imepanga au inaendelea na mikakati ifuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuongeza vyuo vya Ualimu ambavyo vinavyotoa Elimu maalum. Mwanzoni nadhani tulikuwa na chuo kimoja, tulikuwa na chuo kimoja mwanzoni lakini hivi sasa tuna vyuo vitatu vya Ualimu ambavyo vinatoa Elimu maalum, ambavyo ni Patandi, Mpwapwa pamoja na Kabanga.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa Elimu ya juu, vyuo vikuu ambavyo kwa sasa vinatoa Elimu maalum, kipo Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma pamoja na Chuo Kikuu Huria Tanzania. Nimuondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, kwenye mitaala iliyoboreshwa, somo la lugha ya alama ya Tanzania pamoja na somo la Elimu jumuishi katika mtaala huu mpya sasa ni somo la lazima, litasomwa katika hivi vyuo vyote vya Ualimu nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo katika vyuo vikuu, somo hili la Elimu jumuishi katika maboresho ya mitaala tunaendelea katika vyuo vikuu kupitia mradi wetu wa *HEET*. Somo hili la Elimu jumuishi nalo vile vile litakuwa la lazima kwa walimu wote wanaosoma Ualimu katika vyuo vikuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya waheshimiwa wabunge. Waheshimiwa wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Nitaleta matangazo niliyonayo hapa mbele, kwanza ni tangazo la wageni na tutaanza na wageni waliyopo jukwaa la Spika.

Tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ambaye ni Waziri wa Afya na wapo katika jukwaa la Spika, yupo Dkt. John Jingu ambaye ni Katibu Mkuu na yupo Dkt. Grace Magembe Naibu Katibu Mkuu, yupo Profesa Tumaini Nagu, Mganga Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mary Chatanda, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania wa Chama Cha Mapinduzi, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu Riziki Kingwande, Naibu Katibu Mkuu Umoja wa Wanawake Tanzania Bara. *(Makofi)*

Yupo Dkt. Phidelis Mafumiko, Mkemia Mkuu wa Serikali, yupo Profesa Abel Makubi, Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Mifupa *(MOI), y*upo Dkt. Peter Kisenge, Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Dkt. Alphonce Chandika, Mkurugenzi Mtendaji Hospitali ya Benjamini Mkapa, ahsante sana, Dkt. Mwaiselagi Julius, Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Kansa *Ocean Road*, Ndugu Benard Konga ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF),* Dkt. Adam Fimbo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TMDA)* NA Ndugu Mathew Cogan, Mwenyekiti wa Wadau wa Maendeleo. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Anna Hoffman, Mkurugenzi Mkuu *USAID*, Ndugu Mark Bryan Schreiner ambaye ni Mwakilishi Mkazi *UNFPA*,

yupo Ndugu Florence Temu, Mkurugenzi Mtendaji *AMREF* Africa, yupo Profesa Said Aboud, Mkurugenzi Mkuu *NIMR* na Dkt. George Mgomella, Mkurugenzi Mkuu Kituo cha Uthibiti wa Magonjwa *(CDC)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sijui kama ni uthibiti au udhibiti lakini imeitwa uthibiti hapa, Kiswahili ni kigumu kidogo, najua ni udhibiti sasa kumbe ni uthibiti.

Haya yupo pia Dkt. Godlove Mbwanji, Mkurugenzi Hospitali ya Kanda Mbeya, Profesa Gileard Masenga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda *KCMC,* Dkt. Fabian Masaga, Mkurugenzi wa Hospitali ya Kanda Bugando na Ndugu Brenda Msangi, Afisa Mtendaji Mkuu *CCBRT. (Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mwanaali Makwaya, Dada wa Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Neema Mwalimu, mdogo wake Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza ambaye alipata kuwa Mbunge na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Nimetumia maneno alipata kuwa Mbunge kwa sababu nimejifunza hivi karibuni kwamba siasa huwa hamna kustaafu, kwa hiyo nisije nikamuita Mbunge Mstaafu kumbe anakusudia kugombea, kwa hiyo, aliyekuwa Mbunge. *(Makofi/Kicheko)*

Yupo Ndugu Idrisa Sekiboko, mjukuu wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, sasa sijajua kati ya wale mabinti zake ni yupi aliyezaa huyu, lakini mjukuu wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu. *(Makofi/Kicheko)*

Haya wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Ummy Mwalimu ambaye ni Waziri wa Afya na hawa ni Kamati ya Siasa Wilaya ya Tanga Mjini wakiongozwa na Ndugu Sophia Mhina, Kaimu Katibu wa CCM Wilaya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 19 wa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na hawa ni Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania,

wakiongozwa na Rais wa chama hicho, Ndugu Amaddius Shayo, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine, nitaanza kuwasoma kama ifuatavyo:-

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Zainab Katimba, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye ni Katibu Uhamasishaji na Chipukizi Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni saba wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hawa ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Jimbo la Uzini, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, ambaye ni Naibu Waziri wa Madini na hawa ni wapiga kura wake kutoka Longido, Mkoa wa Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja, ambaye ni mpiga kura wake kutoka Tabora. *(Makofi)*

Vilevile yupo mgeni wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ambaye ni rafiki yake kutoka Kyerwa. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Mheshimiwa Deus Sangu na hawa ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni Wenyeviti wa Jumuiya za Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla ambao ni Mkurugenzi Mtendaji na Wafanyakazi wa *Ebony FM* kutoka Iringa. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi na hawa ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni watoto wake kutoka Sikonge. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa *Engineer* Isack Kamwelwe, ambaye ni mtoto wake halafu kuna Daktari wa *DCMC* na msaidizi binafsi kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Aziza Sleyum ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Sikonge, Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Neema Lugangira, ambao ni Viongozi wa Chama cha Wakunga Tanzania *(TAMA)* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 37 wa Mheshimiwa Regina Qwaray ambao ni Kikundi cha Muungano kutoka Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wapo wageni 50 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq ambao ni wanafunzi wa Shule ya Awali na Msingi ya *St. Mark's* kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wafanyakazi watano kutoka *Nzota Company Limited* ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 35 na walimu wanne wa *Canon Andrea Mwaka International School* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 65 wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 17 wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, kutoka Jijini Dodoma. Nadhani ni makundi mawili tofauti. Haya hapa kuna 65 na wale 17, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ndio wageni tulionao hapa Bungeni.

Tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge; Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge, anapenda kuwataarifu kwamba, tumemaliza kazi ya kuandaa chumba maalum kwa ajili ya kutoa huduma ya awali ya afya kwa Waheshimiwa Wabunge, watakaopata uhitaji wakati Shughuli za Bunge zikiendelea. Chumba hicho kipo kati ya Lango A na B, kwenye Ukumbi wa Bunge. Kwa hiyo, ukitoka hapo nje ulizia kipo wapi, ili uelezwe Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ambao wanakuwa wanahitaji huduma hiyo ama wanajihisi vibaya wakiwa hapa ndani wapate huo ukaribu kuliko kule Kituo cha Afya, kinakuwa kipo mbali kidogo. Kwa hiyo, tumeshaweka huo utaratibu ndani ya Ukumbi huu wa Bunge. Kwa hiyo, ukitoka tu hapo nje unaweza kupata hiyo huduma. Kama hujui hicho chumba kipo sehemu gani unaweza kuelekezwa na wahudumu ukishatoka hapo nje.

Baada ya matangazo hayo Waheshimwa Wabunge, tunaendelea na ratiba yetu. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 76. Kwa sababu ya muda ninaomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, tarehe 12 Mei, 2024 katika Kijiji cha Mkomalilo, kuna watu wangu watatu wamepigwa mishale na Walinzi binafsi wa mfugaji. Eneo hili limekuwa na mvurugano wa muda mrefu na kati ya wale wagonjwa watatu waliopigwa mishale mmoja yupo Bugando na hali yake ni mbaya sana. Kwa bahati mbaya, nasikia, toka alipoingia hospitali jana usiku mpaka sasa hata huo mshale haujatoka.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Mkomalilo, kina asilimia 90 ya wafugaji, kimetenga eneo maalumu kwa ajili ya wafugaji. Huko nyuma kulikuwa na migogoro ya mipaka, Wakuu wa Wilaya ya Serengeti na Bunda kwa kushirikiana na Mkuu wa Mkoa wa Mara, wakaamua mipaka.

Mheshimiwa Spika, yupo mfugaji mmoja aliyeonekana kwamba, anatoka Serengeti akawa ameingia kwenye mpaka wa Mkomalilo na amekaa kwenye eneo la malisho ya wafugaji. Wale Wafugaji wanasema atoke, lakini yeye hatoki, yupo mule ndani na analindwa na Polisi na ana taa kwa hiyo, watu wanapoenda kuchunga inakuwa mvurugano. Kumekuwa na mgongano, watu wamekuwa wakiuwana kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako, hususan kwa Serikali, ni watu wangapi watauawa kwenye eneo hili, ili Serikali iweze kutatau tatizo hilo? Ninaomba Mwongozo wako.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Getere hapa kwa Kanuni yetu ya 76, akitaka Mwongozo wa Spika. Kanuni ya 76, inaweka Masharti ya Mwongozo unaoweza kuombwa hapa ndani. Ni lazima jambo liwe limetokea hapa Bungeni mapema. Sasa jambo alilolieleza hapa Mheshimiwa Getere, kuhusu hicho Kijiji cha Mkomalilo kwamba, kuna wananchi wamepigwa mishale na wapo hospitali wakipata

matibabu na kwamba, ni ugomvi unaohusu mipaka, maana yake huyo ni Mwekezaji kwa hiyo, ni kati ya Mwekezaji na Wanakijiji. *(Kicheko)*

Sasa Mheshimiwa Getere, hoja yake kwa kupitia Kanuni hii ya 76, inataka jambo liwe limetokea hapa Bungeni, lakini kwamba, wananchi wamepata athari, Mheshimiwa Mbunge ametaarifiwa. Mimi sasa sina taarifa za ziada kuhusu hicho ambacho kimetokea huko na kwamba, mishale ni nani amempiga nani na hiyo mipaka mimi sijui iko sehemu gani ambako kuna hiyo changamoto.

Waheshimiwa Wabunge, ninachoweza kusema sasa hivi kwa sababu, ni hoja ambayo inahusu mipaka. Kwa hiyo kuna hoja ya ardhi hapo, lakini ardhi kwa maana ya Halmashauri ndio wamesaidia kupima hiyo mipaka. Sasa ili tujiridhishe kwamba, walikuwa sehemu gani na hiyo mishale imepigwa ikitokea wapi ni lazima kufanyike uchunguzi fulani.

Kwa hatua hii Bunge haliwezi kusema chochote hata kuiagiza Serikali kwamba, ifanye nini zaidi ya kufanya uchunguzi juu ya jambo hili, ili wale watakaobainika kwamba, wamefanya uhalifu huu wachukuliwe hatua zile za kisheria. Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere, utafuatilia kwa sura hiyo. Bunge linaweza kusema hivyo, kwa sababu watu wameumia na kweli wapo hospitali, maana yake ni wameumizwa. *(Makofi)*

Sasa kama wameumizwa na mwekezaji maana yake ni hatua zitachukuliwa dhidi ya huyo Mwekezaji, lakini kama ni wananchi wao wenyewe pia, yeyote aliyempiga mwenzake mshale maana yake ni kuwa ni mhalifu. Kwa hiyo, kwa sura hiyo, Wizara ya Mambo ya Ndani nayo inahusika hapa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hili nadhani mlichukue kwamba, Mheshimiwa Mbunge, amelisema hapa na muweze kulifanyia kazi kwa utaratibu wenu wa kawaida kwa sababu, Bunge halina taarifa za ziada. Kwa hivyo, hakuna tunachoweza kutoa Mwongozo juu ya jambo hili.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na ratiba yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namuita sasa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, aje awasilishe hoja ya Wizara yake.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge na Afya na Masuala ya UKIMWI, ambayo imepitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara ya Afya. Ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali, kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024 na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uzima na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee ninaomba kutumia fursa hii kwa dhati kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Afya, ambayo ndio inasimamia pia Sekta ya Afya. Sekta inayogusa maisha ya kila siku ya kila mtu mwanamke au mwanamume, kijana au mzee, tajiri au masikini, sababu mtu ni afya, afya ni mtaji.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta ya Afya kwa kutoa miongozo, maagizo na maelekezo mbalimbali yaliyolenga kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mhesimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Afya imepata mafanikio makubwa na tunapenda kutambua mapinduzi makubwa yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya utawala wake.

Mheshimiwa Spika, moja, ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutoa huduma za afya, umewezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuongezeka kutoka 8,549 Mwaka 2021 hadi vituo 9,693 Mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuongezeka kwa vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ikiwemo *MRI,* kutoka saba hadi 13, *CT scan* kutoka 12 hadi 45, *Digital X-Ray* kutoka 147 hadi 346, *Ultrasound* kutoka 476 hadi 668, *Eco* kutoka 95 hadi 102 na *Cath Lab,* ambao ni mtambo wa kufanya uchunguzi na kufanya upasuaji wa moyo bila kufungua kifua kutoka moja hadi nne. Vilevile tuna *Petty Scan Machine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu kubwa alilotekeleza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, ni kuongezeka kwa idadi ya vitanda vya kulaza wagonjwa kutoka vitanda 86,131 Mwaka 2021 hadi vitanda 145,374 Machi, 2024. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, pia, anaandika historia kwa kuongeza idadi ya vitanda, kwa ajili ya wagonjwa mahututi katika vituo vya umma kutoka vitanda 258 Mwaka 2021 hadi vitanda 1,362 Mwaka 2024. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, upatikanaji wa dawa umeimarika hadi kufikia asilimia 79 Machi, 2024 kutoka asilimia 58.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia, pia ameongeza idadi ya hospitali zinazotoa huduma ya magonjwa ya dharura *EMD* kutoka saba Mwaka 2020 hadi kufikia 116 Mwaka 2024. Sasa hivi *EMD* tunaziona mpaka ngazi ya Hospitali za Halmashauri, huyu ndiye Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la saba ni, kuimarika kwa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi, ambapo wananchi wanapata huduma hizi ndani ya nchi, lakini pia tumevutia wagonjwa kutoka nje ya nchi kutoka wagonjwa 5,705 hadi wagonjwa 7,845.

Mheshimiwa Spika, jambo la nane ni, kuongezeka kwa vituo vya kutoa huduma za afya vyenye uwezo wa kutoa huduma za uzazi wa dharura *(CEmONC)* kutoka 338 hadi vituo 523.

Mheshimiwa Spika, jingine, kubwa ni kupungua kwa vifo vya wajawazito kutoka vifo 556, kwa kila vizazi hai 100,000 hadi vifo 104. Pia, kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kutoka vifo 67 hadi vifo 43 katika kila vizazi hai 100,000.

Mheshimiwa Spika, jingine kubwa la Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka yake mitatu ni kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kutoka vifo 29,000 Mwaka 2022 hadi vifo 22,000 Machi, 2024 na kupungua kwa vifo vitokanavyo na kifua kikuu kutoka vifo 25,800 Mwaka 2022 hadi vifo 18,100 Mwaka 2024. Namba zinaongea, tumesikia, tumeona na kudhibitisha wenyewe mambo makubwa ambayo yamefanyika ndani ya Sekta ya Afya, chini ya Mheshimiwa Rais, wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, na wananchi wote tuendelee kumuunga mkono Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ili maono yake ya kuboresha sekta ya afya na wananchi kuendelea kupata huduma bora za afya yatimie. Kupitia mafanikio haya ni dhahiri kuwa, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, ni kinara wa mageuzi chanya ndani ya Sekta ya Afya nchini Tanzania na Barani Afrika.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia na Mheshimiwa Rais, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Wanafamilia kwa kumpoteza Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi, ambaye naye alichangia kwa kiasi kikubwa kuleta matokeo chanya katika Sekta ya Afya, ikiwemo kuhamasisha watu kufanya mazoezi, ili kujikinga na magonjwa

yasiyo ya kuambukiza. Tunamuomba mwenyezi Mungu aipe roho ya Mzee wetu Ali Hassan Mwinyi, pumziko la milele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatoa pole pia, kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia, kwa kumpoteza Mwanasiasa nguli na mahiri, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu, aipe roho yake pumziko la milele.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye naye amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunatimiza wajibu wetu wa kuboresha huduma za afya hususani, afya mazingira kwa wananchi wa Mijini na Vijijini.

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii pia, kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa Uongozi wake mahiri katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya. Kipekee, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuhamasisha wanaume kupima Virusi vya UKIMWI na pia kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambikiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake aliyoitoa kwenye Bunge lako Tukufu, Tarehe 3 Aprili, 2024, ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika kipindi cha Mwaka 2024/2025. Tunampongeza Mhesimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kuteuliwa kuwa, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchanguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* na Baraza, ambacho ni Chombo Kikuu cha kufanya maamuzi kinachojumuisha Wabunge kutoka Duniani kote. Umetunyanyua wanawake wa Tanzania, umeinyanyua Tanzania. Tunakushukuru na kukupongeza na ninaamini wanawake, vijana na wasichana wanajifunza mengi kutoka kwako. Tunakuombea

kila la heri, Sekta ya Afya tutakuunga mkono, ili uweze pia kuibeba agenda ya *Universal Health Coverage* ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, tunampongeza Naibu Spika, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, kwa kukusaidia katika kuliongoza Bunge lako Tukufu. Tunawashukuru pia Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wa Kamati za Bunge pamoja na Waheshimwa Wabunge wote, tunawashukuru kwa mchango wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tunapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI chini ya Mwenyekiti wake mahiri Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo na Makamu wake Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara ya Afya, hususani katika kipindi cha maandalizi ya Bajeti hii. Tunamtakia Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kila la heri katika kinyang'anyiro cha kushika nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, ninawaahidi pia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara yangu itazingatia maoni na ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo ya awali ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2023/2024, mpango na makadirio ya mapato na matumizi pamoja na vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, katika hatua hii ninaomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* kuanzia ukurasa wa kwanza hadi ukurasa wa mwisho ambapo hotuba ina kurasa 326.

Mheshimiwa Spika, niruhusu nifanye mapitio kwa ufupi kuhusu utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2023/2024. Tulikuja mbele ya Bunge lako Tukufu na vipaumbele 13 ambapo tumeviainisha katika ukurasa wa 10 hadi ukurasa wa 13 wa Hotuba yangu. Kwa upande wa makusanyo Wizara ya Afya

inakusanya fedha kutoka kwenye tozo pamoja na uchangiaji wa huduma katika taasisi, hospitali na ada za vyuo. Bunge lako lilitukadiria kukusanya shilingi bilioni 677.6. Hadi Machi 2024 Wizara na taasisi zilizo chini yake imekusanya shilingi bilioni 528. 7 sawa na 78% ya makadirio.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, Bunge lako lilituidhinishia kutumia jumla ya 1,235,316,516,000. Kati ya fedha hizo, fedha za matumizi ya kawaida ilikuwa ni shilingi bilioni 502.9 na fedha za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 732.3. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 838.4 kimepokelewa sawa na 68% ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, pia tumepokea fedha kutoka vyanzo vya nje kiasi cha shilingi bilioni 96.9 kupitia Mfumo wa D-Fund kwa ajili ya utekelezaji wa miradi misonge ya UKIMWI, kifua kikuu na malaria. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 73.7 tumepokea kutoka Mfuko wa Dunia kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria. Shilingi Bilioni 17 tumepokea kutoka Benki ya Dunia na shilingi bilioni 6.1 tumepokea kutoka Taasisi ya *Suzan Thompson Buffet Foundation Account* kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Afya ya Mama na Mtoto. Maelezo zaidi yapo kwenye ukurasa wa 13 hadi ukurasa 17 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, afua ambazo tumezitekeleza ni nyingi lakini nitapita katika maeneo machache. Kwa upande wa huduma za kinga naomba nijikite katika huduma za chanjo kwa watoto ili kuwalinda na kupata magonjwa. Katika kipindi hiki Wizara iliweka lengo la kuwachanja watoto wadogo milioni 2.1 chanjo za kuwakinga na magojwa 11 ikiwemo Ugonjwa wa Pepopunda, Surua, Polio, Nimonia na Homa ya Ini. Hadi kufikia Machi 2024 tumewafikia watoto 2,245,722 sawa na 103% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa chanjo, *WHO* inapima ufanisi wa kufikia lengo kwa kutumia chanjo inaitwa *Penta3* ambapo sisi tumeweza kufikia kiwango cha 103%. Pia tumeendelea kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka 14 dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi ambapo tumenunua

chanjo ya *Human Papilloma Virus (HPV)Vaccine* ambapo hadi Juni tumeweza kuwafikia watoto 663,949 kulinganisha na 535,703 waliopata chanjo katika kipindi kama hiki mwaka 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari zaidi tumeona kwamba ipo haja ya kuanza kutoa chanjo ya kuwakinga wasichana dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kuanzia umri wa miaka tisa kabla hawajaanza kujiingiza katika masuala mengine. Hivyo tuliendesha Kampeni ya Chanjo ya *HPV* kwa wasichana na kutokana na tafiti kuonesha kwamba *dose* moja inatosha kumkinga msichana dhidi ya kirusi kinachosababisha saratani ya mlango wa kizazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu ndani ya wiki tatu tumewafikia wasichana milioni 4.8 ambao wameweza kupata chanjo hii ya kuwakinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi. Nitumie fursa hii tena kuwahimiza wananchi hususani wazazi na walezi wenye watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kuendelea kuhakikisha wanawapeleka wataalamu wao kupata chanjo. Pia naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwahakikishia wazazi na walezi wenzangu chanjo ya *HPV* ni salama tuwapeleke mabinti wetu wenye umri wa miaka tisa hadi 14 kupata chanjo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za lishe tumeendelea na afua mbalimbali ikiwemo kutoa matone ya Vitamini *A* kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano, ambapo tuliwafikia watoto 9,456,430 kulinganisha na watoto 9,052,340.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya mazingira tumeendelea kuhimiza wananchi kuchukuwa hatua ikiwemo kuzingatia Kanuni za Afya za Usafi na Mazingira ambapo tumeona idadi ya kaya zenye vyoo bora zimeongezeka kufikia kaya 7,775,181 kulinganisha na kaya 7,087,523. Maelezo zaidi yapo katika ukurasa wa 32 hadi 40 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko kwa kutumia Mfumo wa Kielekroniki wa

*Integrated Disease Surveillance and Response* katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya. Katika kipindi hiki tumeona mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu ambao ndiyo ulioripotiwa zaidi katika Mikoa 16 ya Mara, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Kagera, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Ruvuma, Mwanza, Dodoma, Geita, Manyara, Morogoro na Katavi. Kwa hiyo tumeona kipindupindu ndiyo lilikuwa suala kubwa kwa upande wa magonjwa ya mlipuko. Pia tumeendelea kutoa elimu ya afya kwa umma na huduma za afya kwa ngazi ya jamii kupitia vyombo mbalimbali, lengo ni kuchochea mabadiliko chanya ya tabia na mitindo bora ya maisha kwa kuhamasisha jamii kuzingatia Kanuni za Usafi, huduma za lishe, afya ya vijana, afya ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo tumelitekeleza ni kuzindua na kuanza utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii *(Integrated and Coordinated Community Health Workers Program)* ambapo tutautekeleza katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kupitia mpango huu kila kitongoji na kila mtaa kwa maeneo ya mijini watakuwa na wahudumu wawili wa afya ngazi ya jamii ambao ni wakazi wa kijiji au kitongoji husika au mtaa husika na tutawapa mafunzo ya miezi sita pamoja katika masuala ya lishe, afya uzazi, mtoto na vijana, afya na usafi mazingira, magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyo ya kuambukiza na magonjwa ya mlipuko na athari za mabadiliko ya tabianchi. Tunaamini kabisa wahudumu wa afya ngazi ya jamii watakuwa ni daraja kati ya vituo vya kutoa huduma za afya na jamii na kupitia kaulimbiu yetu "Afya ya jamii nyumba kwa nyumba hatumwachi mtu", tunaamini tutamfikia kila Mtanzania aliyepo mjini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma ya afya ya uzazi kwa mama na mtoto tumeendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto ili tuweze kufikia malengo ya maendeleo endelevu. Kama nilivyosema awali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia tumefanya vizuri sana katika kupunguza vifo vya wajawazito kwa zaidi ya 80%. Tumefanya vizuri pia kupunguza vifo vya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano kutoka 67 hadi 43. Tumeangalia takwimu za nchi

jirani kwa mfano Uganda, vifo vya wajawazito ni 189, Burundi ni 494, Kenya 530, Malawi 381, Msumbiji 127, Somalia 621, Sudani Kusini 1,223, Zambia 135, Tanzania ni 104 katika kila vizazi hai 100,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipaumbele chetu kupunguza ni vifo vya watoto wachanga. Leo ninafurahi kwamba tunaye Mwenyekiti wa UWT Taifa Mama yangu Mary Chatanda amenihakikishia kwamba, UWT wanaibeba *agenda* ya vifo vya watoto wachanga kuanzia Jumuiya ya UWT katika matawi, kata, wilaya, mikoa na Taifa na Mama Chatanda amesema atapita kwenye kila zahanati, kila kituo cha afya, kila hospitali kuangalia vifaa vya kuhudumia watoto wachanga ikiwemo vifaa vya kusaidia watoto wachanga kupumua, ataangalia dawa, ataangalia upatikanaji wa watumishi. Nakushukuru sana Mwenyekiti wa UWT Taifa kwa kuonesha mwongozo mzuri wa kuisaidia Serikali katika kupambana na vifo vya watoto wachanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumelifanya, tume-*print* vitabu vipya kwa ajili ya wakina mama wajawazito na watoto. Zamani tulikuwa tunatumia kadi moja tu ya *clinic* lakini tumebaini kuwa makuzi na ukuaji wa mtoto wa kike na mtoto wa kiume yanatofautiana. Kwa hiyo tumetengeneza kitabu kwa ajili ya ufuatiliaji wa afya ya mtoto, hiki ni kitabu cha mtoto wa kiume lakini pia tumetengeneza kitabu kwa ajili ya mtoto wa kike. Pia tumetengeneza kitabu kwa ajili ya mama mjamzito.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie kuwataka watoa huduma za afya wa Serikali, kadi za *clinic* vitabu hivi haviuzwi. Vinapaswa kutolewa bure kwa wanawake wote nchini na tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia ametupa fedha tumetengeneza vitabu hivi ambavyo sasa vinakwenda kuweka mbadala wa kadi hizi za *clinic*. Narudia tena kuwataka wataalamu wetu kuhakikisha vitabu hivi, *MSD* isiuze kwa vituo na vituo visiwauzie wananchi wanaopaswa kupata vitabu hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya ya watoto, tumeendelea pia kuhakikisha upatikanaji wa dawa za watoto ikiwemo dawa hii kwa ajili ya kutibu homa ya mapafu

*(pneumonia)*, tumenunua vidonge milioni 38 kulinganisha na vidonge milioni 30. Tumenunua dawa za kutibu kuharisha, pakti za *zinc* na *ORS*. Narudia tena, hii dawa inaitwa *Amoxicillin DT,* dawa hii inatibu watoto wanaopata changamoto za nimonia, wengi karibu 70%. Dawa hii inapaswa kutolewa bure, haipaswi kuuzwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, 70% ya watoto wanaoumwa chini ya miaka mitano wanapata maambukizi katika mfumo wa hewa. Kwa hiyo inamaana tukisimamia matumizi ya dawa hii vizuri tutapunguza 70% ya malalamiko ya watoto kuhusu ukosefu wa dawa lakini tumejipanga kwa sababu kuna baadhi ya wataalamu wetu siyo waaminifu. Tunaichapa kuanzia Julai itaandikwa haiuzwi, halafu tuikute kwenye duka inauzwa, ili tuweze kupunguza malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuongeza huduma za wodi za watoto wachanga zimeongezeka 66 katika kipindi hiki na hivyo kufikia 241 kutoka 175. Tumeendelea pia kutekeleza afua za kupambana na kifua kikuu, malaria, UKIMWI pamoja na homa ya ini na magojwa ya ngono. Kubwa ambalo tumelifanya ni kuanzisha *program* jumuishi ya mapambano dhidi ya Virusi vya UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono. Tumeweka katika ukurasa wa 68 hadi 85 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dawa tumepokea shilingi bilioni 103.3 na tumepeleka *MSD*. Kama nilivyosema, hali ya upatikanaji wa dawa muhimu imeboreka kutoka 75% hadi 79% Pia tumeangalia kwenye zahanati tumeona upatikanaji wa dawa ni 63%, vituo vya afya 66%, hospitali za wilaya 72%, hospitali za rufaa za mikoa 94%, kanda maalum na Taifa ni 89%. Kwa hiyo msisitizo tutauweka katika huduma za afya ya msingi, upatikanaji wa dawa kwenye zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kutoa huduma za kutekeleza afua mbalimbali za uchunguzi wa magonjwa ikiwemo huduma za maabara na huduma za radiolojia. Eneo ambalo tumefanya vizuri ni kwenye radiolojia na leo tunao Wajumbe wa

Chama cha Wataalamu wa Radiolojia ambao wamefika Bungeni kuonesha shukrani zao za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa huduma za radiolojia. Mfano sasa hivi *CT-Scan,* Wananchi wa Katavi, Songwe, Rukwa wanapata huduma hizi ndani ya mikoa yao badala ya kusafiri umbali mrefu. Takwimu zinaonesha kwa upande wa vipimo hivi vya *CT-scan* takribani wananchi 44,646 wamehudumiwa ndani ya mwaka huu lakini *MRI* pia tumezisogeza katika ngazi ya kanda, wananchi 18,056 wamehudumiwa.

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuhakikisha upatikanaji wa damu salama, katika hotuba yangu ukurasa wa 91 hadi 98.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za tiba tumeona ongezeko la vituo vya kutolea huduma za tiba ambapo pia maelezo yapo ukurasa wa 99 hadi 195 ya hotuba yangu. Pia tumeangalia mahudhurio ya wagonjwa, katika kipindi hiki mahudhurio ya wagonjwa yalikuwa milioni 37.5 kulinganisha na mahudhurio milioni 35.8 mwaka jana, lakini tukajiuliza Watanzania wanatibiwa wapi? Katika kipindi hiki 5.3% ya Watanzania wanatibiwa katika ngazi ya hospitali za Taifa maalum na kanda, 12.6% ngazi ya hospitali za mikoa, 15% hospitali za wilaya na 19.6% vituo vya afya, 38.7% ya Watanzania wanatibiwa katika zahanati. Takwimu hizi zinaonesha kwamba 82% ya Watanzania wanapata huduma katika ngazi ya afya msingi. Hii inamaanisha kwamba Serikali tutaendelea kuwekeza na kuongeza jitihada za kuboresha huduma za afya katika ngazi hii. Ukienda huko juu hakuna malalamiko, Muhimibili, *JKCI*, *MOI*. Kwa hiyo changamoto sasa imebaki huku chini tutashirikiana na wenzetu Ofisi ya Rais TAMISEMI katika kuboresha huduma.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambapo tunaona ongezeko la kasi ya wananchi wanaopata magonjwa yasiyo ya kuambukiza hususani kisukari na shinikizo la juu la damu. Kwa mfano tumeona mzigo au gharama kubwa za magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza. Kwa mfano, *NHIF* mwaka 2015/2016 ililipa shilingi bilioni 24.4 sawa na 12% ya fedha zake

zote kwa ajili ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Mwaka 2021/2022 ikapanda hadi shilingi bilioni 99.8; kutoka shilingi bilioni 24.4 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 99.8 sawa na 15% ya malipo yaliyolipwa. Mwaka wa Fedha 2022/2023 *NHIF* ililipa shilingi bilioni 137.8 sawa na 19% kwa ajili ya kugharamia magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, tumeona ipo haja ya kuangalia tena katika utekelezaji wa vipaumbele vyetu. Kubwa tumeangalia vyanzo vikuu vya magonjwa haya ni ulaji usiofaa wa vyakula, matumizi ya pombe kupita kiasi na kutoushughulisha mwili. Kipekee tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Majaliwa kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi ili kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, kipekee naomba pia nimshukuru Profesa Mohamed Janabi, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kuwahamasisha wananchi kuhusu ulaji wa vyakula unaofaa, ninawaomba sana Waheshimiwa Wabunge tusipuuze na kudharau maelekezo ya Profesa Mohamed Janabi na wataalam wengine wa afya. Wembamba siyo ugonjwa na unene siyo afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naulizwa hapa, umepungua unaumwa? Siumwi, nazingatia maelekezo ya Profesa Janabi, naangalia chakula ninachokula na ndiyo maana nimerudi katika usichana. Nitumie Bunge lako Tukufu kuwahimiza wananchi kuzingatia mfumo bora wa maisha ikiwemo chakula. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tumeona pia tukawekeze kwenye ngazi ya msingi, tumewezesha vituo vya afya 711 na kuvipatia vifaa, vikiwemo vifaatiba vya kupima shinikizo la juu la damu, mashine 700, kupima sukari mashine 700 pamoja na vitendanishi katika zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuimarisha huduma za afya ya kinywa na meno ambapo tumenunua viti vya huduma ya kinywa na meno 150 ambavyo tumevisambaza katika vituo mbalimbali, hospitali zinazotoa huduma ya kinywa na meno zimeongezeka kutoka 130 hadi 184. Tumenunua *x-ray* za meno 103 na kuzisambaza katika Halmashauri mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafurahi sasa huduma za kinywa na meno zinapatikana katika ngazi ya vituo vya afya na hospitali za Wilaya, zamani ilikuwa lazima watu waende kwenye hospitali za Rufaa za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito wa Watanzania kuwahi kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya kinywa na meno pindi wanapopata shida ya meno ili kuepuka kung'olewa meno kwa kuwa magonjwa ya meno yanatibika. Natumia Bunge lako Tukufu kusema dawa ya jino ni kulitibu siyo kuling'oa. Kwa hiyo, tunataka kupunguza idadi ya watanzania wanaoingia katika ubogoyo kukosa meno kwa dhana potofu kwamba dawa ya jino ni kuling'oa, Hapana! Sasa hivi uwekezaji ambao Mheshimiwa Rais Samia ameufanya, jino linatibika na unaweza ukarudi katika maisha yako ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya ya akili na huduma za utengemao wa tibashufaa. Tumeendelea kuchukua hatua ikiwemo kukamilisha andiko la hati idhini kwa ajili ya kuipandisha hadhi hospitali ya afya ya akili Mirembe, kuwa Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili. Tunaamini kabisa Mirembe ikiwa taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili itaimarisha utoaji wa huduma za afya ya akili ikiwemo kuimarisha huduma za kinga, tiba, miundombinu, kuimarisha mfumo wa kitaasisi na masuala mengine ya ubunifu na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha huduma za afya ya akili Wizara imekamilisha mtaala wa astashahada ya juu ya afya ya akili kwa Wauguzi *(Higher diploma ni mental health nursing)* ambapo tutaanza udahili mwaka huu wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi pia kulitaarifu Bunge lako Tukufu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili, kimeanzisha Shahada ya Sayansi ya Saikolojia Tiba *(Bachelor of Science in Clinical Psychology)* ambapo na wenyewe wataanza udahili mwezi Septemba mwaka huu. Lengo ni kupatikana wataalam wa afya ya akili katika ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za utengamao, tumehudumia wajongwa takribani 200,010, zikiwemo huduma za fiziotherapia, tibakazi, matamshi, lugha pamoja na vifaatiba saidizi na viungo tiba na viungo saidizi. Hospitali saba za Rufaa za Mikoa zimeweza kutoa seti tatu kati ya nne ya huduma za tiba za utengamao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakipongeza sana Chuo Kikuu cha *MUHAS*, tulipeleka maombi yetu kwamba, ipo haja ya kuanzisha *bachelor of science* kwenye masuala la *speech and language therapy*, mwaka huu wa fedha 2023/2024 zimeanza, kuna wataalam 15 wanasomea, pia wameanzisha *bachelor of science in occupational therapy,* ambapo ina wadahiliwa 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo hili ni muhimu sana kwa sababu nikiwa mama na mwanamke, tunaona watoto wenye ulemavu wakiendelea kuwa na ulemavu kutoishi maisha bora kwa sababu ya kukosa huduma za utengamao lakini mtoto mwenye ulemavu akipata huduma za tibakazi, anaweza akala chakula mwenyewe, akavaa nguo mwenyewe, akaenda kujisaidia mwenyewe na anaweza kuonyesha kwamba hapa panauma. Kwa hiyo, katika hili tutaonyesha nini tunafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Taasisi ya Lukiza *Autism Foundation*, wanafanya kazi nzuri katika kuhamasisha matibabu na huduma kwa watoto wenye usonji na watoto wengine wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea pia kuimarisha huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi. Kubwa ambalo tunataka kuliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, tumeendelea na ubunifu. Hospitali zetu zimeanzisha kada mpya au huduma

mpya za ubingwa na ubobezi 16. Kule kwetu Mbeya, Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda Mbeya imeanza pia upasuaji kwa njia ya matundu madogo lakini wameanzisha huduma za upasuaji kwenye masuala ya magonjwa ya moyo na magonjwa mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muhimbili wameweza kutenganisha mapacha walioungana kwa kutumia wataalam wa ndani. Haijawahi fanyika, ilifanyika miaka 30 iliyopita, walifanya hao, pia upasuaji wa kutoa kizazi na masuala ni mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwaunga mkono wataalam wa ndani kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi, Mheshimiwa Rais Samia ametoa bilioni tano na tumepeleka kwenye hospitali tatu. Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wagonjwa 91 wamenufaika na huduma za ubobezi, ikiwemo upandikizaji wa uloto na figo. Hospitali ya Jakaya Kikwete wameweza kuhudumia wagonjwa 100 ikiwemo huduma ya kuweka *valve* kwenye moyo (Upasuaji wa moyo kwa kuweka *valve (valve replacement surgery)* watu 50 pia waliweza kuwekewa vipandikizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Benjamini Mkapa imepata pia fedha hizi na wagonjwa 46 wamehudumiwa. Mwaka jana kwa Benjamini Mkapa, tulileta watoto ambao walifanyiwa upandikizaji wa uloto baada ya kuwa na changamoto ya *sickle cell. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kukupa taarifa na kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu, mwaka huu Benjamini Mkapa wameongeza watoto wanne na watoto hao wamepimwa kati ya wale nane jumla, watoto wanne wamepimwa hawana tena ugonjwa wa *sickle cell*, wamepona. Haya ni mapinduzi makubwa katika huduma zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zinatolewa katika hospitali zetu, tulipeleka Madaktari Bingwa katika ngazi za Mikoa na Madaktari Bingwa katika ngazi za Halmashauri. Madaktari Bingwa 217 wametoka katika ngazi za Mikoa na wengine wako hapa wamefanya kazi

nzuri sana za kutoa huduma za ubingwa kwa wananchi katika fani 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisikia kilio chenu cha Waheshimiwa Wabunge, tumepeleka Madaktari Bingwa wa fani tano katika hospitali zote za Halmashauri 184 na wamekaa pale kwa ajili ya kutoa huduma na kubadilishana uzoefu na wengine wako hapa, naamini tutawatambulisha baadae. Kwa hiyo, kwenye Madaktari Bingwa walioenda ngazi ya Halmashauri ni 920, wameenda kutoa huduma na tunaendelea na zoezi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wakuu wa Mikoa pamoja na Viongozi wengine wa Mikoa na Wilaya kwa kuwapa ushirikiano wataalam wetu. Pia, tunawashukuru wananchi, wamejitokeza wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hospitali zetu pia zimetoa huduma mkoba pamoja na kuhudumia wagonjwa kutoka nje ya nchi. Katika kipindi hiki wagonjwa 7,843 walihudumiwa kulinganisha na wagonjwa 7,509. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niseme, hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa - *MOI*, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani - *Ocean Road*, Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ambukizi – Kibong'oto, Hospitali ya Taifa afya ya akili – Mirembe, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini – Mtwara, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – *KCMC*, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya, Hospitali ya Kanda ya Ziwa – Bugando, Hospitali ya Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda – Chato, *CCBRT* na hospitali za Rufaa za Mikoa maelezo yao yako ukurasa wa 128 hadi 192 wa hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwa Jakaya Kikwete, kubwa walilolifanya ni kufanya upasuaji wa kubadilisha *valve* katika moyo kwa njia ya tundu dogo. Dkt. Kisenge amefanya kazi nzuri na timu yake jambo hili halijawahi kufanyika. Pia, Taasisi ya Mifupa – *MOI,* wamefanya upasuaji wa mgongo kwa njia ya tundu dogo. Profesa Makubi na timu yake wamefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Benjamin Mkapa, wamefanya upasuaji mkubwa wa moyo kwa watu wazima. Dodoma, hospitali ya Benjamin Mkapa walikuwa hawawezi ilikuwa lazima uende Dar es Salaam, sasa hivi Benjamin Mkapa wanaweza wakafanya upasuaji mkubwa wa moyo kwa watu wazima Dokta Shandika na timu yako hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kule kwetu Mbeya, Hospitali yetu ya Rufaa ya Kanda Mbeya hawawezi kufanya upasuaji mkubwa wa moyo kwa watu wazima, bajeti hii ya mwaka huu tunaomaliza tuliyoiwasilisha, Mbeya imeanza kufanya upasuaji mkubwa wa moyo kwa watu wazima. Daktari Bwanji na timu yako hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali yetu ya Taifa ya Muhimbili, Waheshimiwa Wabunge nyote ni mashahidi, mmeshuhudia mabadiliko makubwa ya miundombinu na huduma. Nampongeza Profesa Mohamed Janabi na timu yake, pia tunawapongeza Wakurugenzi wote ambao sijawataja, Waheshimiwa Wabunge, maelezo mahsusi yako katika hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea na jitihada za kudhibiti na kukabiliana na milipuko ya magonjwa, nimeonyesha katika ukurasa wa 265 hadi 275 ya hotuba yangu ikiwemo kugawa *ambulance* zaidi ya 600. Huduma za uuguzi na ukunga, nimeonyesha katika *paragraph* 274 hadi 278. Ubora wa huduma pia nimeeleza katika hotuba yangu *paragraph* 279 hadi 204. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu rasilimali watu katika sekta ya afya. Tumeendelea kuwekeza. Kwanza, kuzalisha, pili, kutoa motisha na tatu, kuajiri watumishi wa afya. Nimeonesha watumishi wa afya walioko katika sekta ya afya ni 126,929, ambapo watumishi wa afya 101,733 wako ngazi ya msingi, maana yake asilimia 30 ya watumishi wa afya wako katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za Wilaya na watumishi 25,192 sawa na asilimia 19.8 wako ngazi za Rufaa Mikoa, Kanda Maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeajiri watumishi wa afya 13,187 lakini pia kuna ajira za mikataba watumishi 4,838 waliajiriwa. Tumeweka mazingira mazuri ya kuvutia watumishi wa afya ikiwemo kutoa mikopo kwa watumishi wa afya pamoja na kufadhili masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Samia anaendelea kuandika historia nchini kwetu. Kupita Dkt. Samia Afya *Scholarship*, tumetoa ufadhili kwa Madaktari Bingwa, Madaktari Bingwa Bobezi na wataalam wengine wa afya 1,251 ambao wanasoma masuala ya ubingwa na ubingwa bobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kwa kukubali kutoa fedha hizi, bilioni tisa kwa ajili ya ufadhili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumshukuru MO Dewji *Foundation*, anatusomeshea madaktari bingwa wa upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu wawili *(Neuro Surgery)* katika Chuo Kikuu Nairobi - Kenya. Tunamshukuru sana na nitoe wito kwa sekta binafsi kuiunga mkono Serikali katika kuzalisha mabingwa na wabobezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ugharamiaji wa huduma za afya tumeonesha, fedha zilizotolewa na utekelezaji wa sera ya matibabu kwa makundi. Pia, tumezungumza kuhusu usambazaji wa dawa kwa watoto, wajawazito na tumezungumzia suala la bima ya afya kwa wote. Tunalishukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote, ambayo tayari imesainiwa na Mheshimiwa Rais. Kipekee tunaamini kabisa sheria hii inaweka msingi wa mfumo madhubuti na endelevu wa ugharamiaji wa huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu nimezungumza kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, pia nimezungumzia utekelezaji wa majukumu ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Naomba nizitaje tu ambazo ni Bohari ya Dawa, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Taasisi ya Taifa ya Udhibiti wa Magonjwa ya Binadamu ambapo tumeeleza katika hotuba yangu kwenye ukurasa wa 232 hadi 262. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla labda tu, kubwa ni lile la *NHIF* ambalo tumeweza kufanya maboresho katika kitita cha mafao cha *NHIF* cha mwaka 2023, ikiwemo kuongezeka kwa dawa mpya 254 zenye ufanisi ambazo awali wanachama walikuwa wanazilipia kwa fedha taslimu. Pia, tumeongeza dawa 178 ambazo hazikuwa kwenye orodha ya dawa muhimu ya taifa. Tumefanya *addendum* au nyongeza ya orodha ya dawa muhimu za taifa na hivyo sasa dawa hizi pia zimejumuishwa katika kitita cha *NHIF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa tumejitahidi pia kuweka usawa wa ada ya usajili na kumuona Daktari, wenye elimu na taaluma zinazofanana katika kuhudumia wanachama wa *NHIF*. Mathalani, Daktari Bingwa aliye katika ngazi ya rufaa ya Mkoa hivi sasa kupitia maboresho ya kitita kipya, atalipwa sawa na Daktari Bingwa aliyeko Muhimbili, *JKCI, MOI* na aliyepo Bugando. Tunaamini kabisa hatua hii itavutia Madaktari Bingwa kufanya kazi katika hospitali za Rufaa za Mikoa, hususani Mikoa ya pembezoni. Ndugu zangu wa Kigoma, Katavi, Rukwa, Simiyu na Shinyanga wanayo haki ya kuhudumiwa na Madaktari Bingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna baadhi ya huduma tumezifanyia maboresho. Katika hotuba yangu nimeeleza utekelezaji wa majukumu ya Mabaraza na Bodi za Kitaaluma katika ukurasa wa 262 hadi 286 ikiwemo Baraza la Madaktari, Baraza la Wauguzi na Ukunga, Baraza la Wafamasia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Baraza la Wataalam wa Macho na Mabaraza yote.

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi lakini naomba niseme, kwenye hotuba tumeonyesha yapi tumetekeleza, sasa vipaumbele vyetu ni vipi kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, tumekuja na vipaumbe 10 kutoka 13 vya mwaka jana. Vipaumbele vyetu 10 tutaongozwa na vipaumbele vikuu vitatu.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha kwanza ni kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa na hapa tutawekeza katika

masuala ya lishe, chanjo kwa watoto, huduma za usafi na afya ya mazingira na utekelezaji wa mpango jumuishi wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii, ambapo huduma za kinga, tumetenga kiasi cha bilioni 117.6.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha pili ni kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika vituo vya kutoa huduma za afya kuanzia ngazi zote za zahanati hadi Taifa.

Mheshimiwa Spika, kilio cha wananchi sasa hivi, tumewekeza sana kwenye majengo na vifaatiba lakini tunataka kuwekeza sasa kwenye ubora wa huduma. Kwenye hili, kubwa tutakalolifanya ni kuendelea kuimarisha upatikanaji wa dawa, damu salama, kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa, kuimarisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, tunaamini hatujayatumia vizuri maendeleo ya TEHAMA. Kwa hiyo, tukiwekeza kwenye TEHAMA, tutapata ufanisi, tutaimarisha udhibiti na kupunguza gharama katika utoaji wa huduma za afya. Pia, tutaimarisha ubora wa huduma za uuguzi na ukunga na tutaendelea kuimarisha masuala ya damu salama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kipaumbele cha tatu ni kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini.

Mheshimiwa Spika, ngoja nimalize kuvitaja vipaumbele kumi, hapafu nitoe ufafanuzi.

Nne, kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya watoto wachanga na wajawazito.

Tano, kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;

Sita, kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi;

Saba, kuendeleza na kusimamia afua za tiba asili na tiba mbadala;

Nane, kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko;

Tisa, kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu; na

Kumi, kusimamia tafiti na matokeo ya tafiti kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele hivi 10 tutavitekeleza kupitia afua 89 na Wizara imekadiria kutumia kiasi cha shilingi 1,311,837,466,000. Kama nilivyosema kwenye huduma za kinga tumetenga shilingi bilioni 117. 6, ubora wa huduma ni bilioni 219, suala la kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya ni bilioni sita.

Mheshimiwa Spika, hapa tutafanya mapitio ya mkakati wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya. Tutasimamia utekelezaji wa sheria ya bima ya afya kwa wote ikiwemo mfumo wa utambuzi wa wanufaika pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ni tunakwenda kuanza mchakato wa kuanzisha chombo cha Kitaifa cha udhibiti wa bei za huduma za afya katika ngazi zote. Kwa sababu sasa hivi kilio cha Watanzania kimekuwa, gharama ni kubwa. Ni kweli gharama ni kubwa kwa sababu tumewekeza sana na tumeboresha sana, lakini tunaamini tukiwa na chombo huru cha kusema upasuaji wa Mama mjamzito gharama zake ni hizi, tunaamini kabisa tutakuwa hatuna mvutano kati ya Serikali na watoa huduma za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini tukiwa na chombo huru cha kusema upasuaji wa mama mjamzito gharama zake ni hizi tunaamini kabisa tutakuwa hatuna mvutano kati ya Serikali na watoa huduma za afya. Pia, tutaendelea kuimarisha uhai na ustahimilivu wa *NHIF* na kuimarisha ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za afya ya uzazi (mama na mtoto) tumetenga shilingi bilioni 17.8 ambapo tutanunua na kusambaza dawa za uzazi salama *(Magnesium Sulphate, Oxytocin*, *Fefo* na *SP)* pamoja na dawa za uzazi wa mpango na dawa kinga za minyoo.

Mheshimiwa Spika, tutaimarisha upatikanaji wa dawa bila malipo kwa ajili ya watoto. Pia, tutajenga na kukarabati wodi maalumu za watoto wachanga 100 pamoja na watoto waliozaliwa na uzito pungufu. Katika eneo hili pia tutaimarisha wanawake wajawazito kuwahimiza kwenda kliniki pamoja na kuelimisha kuhusu huduma wanazopaswa kufanyiwa. UWT – Taifa wamesema ajenda hii pia wanaibeba kuwahamasisha wanawake kwamba ukienda kliniki unapaswa upimwe wingi wa damu, kundi la damu, uangalie maambukizi ya bakteria kwenye mkojo na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa wataalamu tumetenga shilingi bilioni 74 ikiwemo kuzalisha wataalamu pamoja na kusomesha madaktari na wataalamu wengine wa afya 1,300 ambapo 600 watakuwa wanaendelea na 700 ni wapya. Tumeonyesha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi. Tutaendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, tunakwenda kuanza hatua za awali za kuanzisha huduma za upasuaji ubongo na mishipa ya fahamu kwa kutumia *Artificial Intelligence Robot*. Nchi yetu inakwenda kuandika historia kwamba tutafanya upasuaji kwa kutumia *robot (robotic surgeries)* katika taasisi yetu ya mifupa ya *MOI*. Pia, Hospitali ya Kanda Bugando wanaenda kuanzisha huduma za upandikizaji wa figo, Hospitali ya Taifa Muhimbili wanaenda

kuanzisha huduma za upandikizaji wa ujauzito pamoja na Hospitali ya Benjamini Mkapa inaenda kuanzisha huduma ya upandikizaji wa ujauzito.

Mheshimiwa Spika, huduma hizi zipo lakini zinapatikana katika hospitali binafsi. Wanawake wengi wanatamani kupata mtoto lakini hawawezi kumudu gharama. Huduma hizi zikitolewa katika hospitali ya umma tunaamini wanawake ambao na wenyewe wengine labda wananyanyasika kwa sababu hawana watoto wataweza kupata huduma hii kwa gharama nafuu kwa sababu huduma hizi zitatolewa.

Mheshimiwa Spika, hatujakusahau kule Mbeya. Ulilipigania sana hili kwamba tunataka sasa Mbeya tutoe huduma ya kutibu moyo bila kufungua kifua. Tumewatengea Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya tutanunua mtambo wa *cath lab* ili kuwezesha upasuaji wa moyo bila kufungua kifua kwa sababu pia ni ombi ambalo Mheshimiwa Spika Mbunge wa Mbeya Mjini amekuwa akilisisitiza sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ndugu zangu wa Kanda ya Ziwa; Chato tunakwenda kufunga mtambo wa *cath lab* katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wetu. Tutaendeleza miundombinu katika hospitali zetu; *Ocean Road* anaenda kuanzisha Kituo cha Saratani Mbeya. Kwa Kanda ya Ziwa, Jakaya Kikwete anakwenda kuanzisha tawi la Jakaya Kikwete Chato kwa ajili ya watu wa Kanda ya Ziwa lakini pia tutaendeleza huduma nyingine muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeamua kuimarisha huduma za tiba asili na tiba mbadala. Kwa hiyo tunaanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa tiba asili na tiba mbadala na tunataka pia huduma hizi sasa ziendelee kutolewa au kujumuishwa katika hospitali zetu. Magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza tumetenga shilingi bilioni 84 ikiwemo kupambana na malaria, kifua kikuu na UKIMWI pamoja na kutoa elimu kuhusu vichocheo vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za afya ya akili. Huduma za utengamao tumetenga shilingi bilioni 9.3 ikiwemo kuanzisha huduma za afya ya akili kwa njia ya mtandao lakini pia tunaanzisha huduma tatu za utengamao katika hospitali za rufaa za mikoa. Tutaendelea pia kununua dawa na vifaa tiba pamoja na kuimarisha miundombinu kwa ajili ya huduma za afya ya akili na huduma za utengamao.

Mheshimiwa Spika, tutaratibu uanzishwaji wa klabu za afya za wazee katika ngazi za halmshauri. Tumeona wazee nao wanapaswa kuimarika katika masuala ya afya ya akili na huduma za *rehabilitation*. Kwa upande wa tafiti tumetenga shilingi bilioni 9.5.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao wameshirikiana nasi katika utekelezaji wa bajeti yetu. Kipekee napenda kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Ireland, Uswisi, Korea Kusini na mashirika ya maendeleo pamoja na Benki ya Dunia, *UNFPA* na *UNICEF* kwa kuchangia kupitia Mfuko wa Afya wa Pamoja *(Health Basket Fund)*. Naomba nizishukuru nchi za Marekani, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, China, Cuba, India, Italia, Japan, Misri, Sweden ma wote ambao wanatusaidia.

Mheshimiwa Spika, tunayashukuru mashirika yasiyo ya Kiserikali, vyama vya kitaaluma, vyama vya hiyari na wataalamu wa afya ambao nimewatambua kuanzia ukurasa wa 302 hadi 305 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Mbunge wa Siha kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika kunisaidia. Nina Naibu Waziri mzuri sana; msikivu, mwaminifu, *very loyal* na *humble* kwa Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana na ninaamini watu wa Siha watamrudisha Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe, Mganga Mkuu wa Serikali *Professor* Tumaini Nagu, Wakurugenzi na Wakuu wa

Vitengo, Wakurugenzi wa Taasisi na wote ambao nimewataja katika Hotuba yangu asubuhi uliweza kuwataja. Naomba pia kuwashukuru Wakurugenzi wa Taasisi zetu zote.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru wataalamu wote wa afya nchini. Niwaombe tuendelee kuwahudumia wananchi kwa kuzingatia weledi wa taaluma zetu, maadili pamoja na miiko. Kipekee niishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao, kuniombea na kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru wananchi wa Jimbo langu la Tanga Mjini kwa kuendelea kuniamini, kuniunga mkono na kushirikiana nami kikamilifu katika kujenga Tanga yetu. Leo watu wa Tanga Mjini wamewakilishwa na Kamati ya Siasa ya Wilaya lakini pia wamewakilishwa na Kamati ya Uendeshaji ya *Odo Ummy Cup* na Mbunge ambaye anafurahi kuwahudumia na kuwatumikia. Niwaambie tu tuendelee kushirikiana ili tujenge Tanga yetu. Odo Ummy bado yupo ngangari, Odo Ummy anaipenda Tanga Mjini na ataendelea kuwatumikia watu wa Tanga Mjini.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niombe fedha. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha shilingi 756,866,060,248. Kati ya fedha hizo, shilingi 70,828,500,189.69 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara. Shilingi 134,171,499,810 zinatarajiwa kukusanywa kutoka hospitali za rufaa za mikoa.

Mheshimiwa Spika, shilingi 551,860,060,248 zinatarajiwa kukusanywa kutoka taasisi na mashirika yaliyo chini ya Wizara. Jumla ya makusanyo yetu imeongezeka kwa kiwango cha 12% ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 676,621,168,390 kwa mwaka 2023/204.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani hapo mwanzo umesema bilioni 676 badala ya 677.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, samahani. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la 12% ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 677,621,168,390.95 mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya kawaida mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imepanga kutumia kiasi cha shilingi 632,267,220,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hii ni sawa na 48% ya bajeti iliyopangwa ambapo kiasi cha shilingi 484,935,496,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake na kiasi cha shilingi bilioni 147,331,724,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo. Wizara imepanga kutumia shilingi 679,570,246,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na 52% ya bajeti tengwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni shilingi 416,258,609,000 na fedha za nje ni shilingi 263,311,637,000. Jumla ya fedha zinazoombwa na Wizara ili kutekeleza vipaumbele 10 nilivyovibainisha katika mwaka wa fedha 2024/2025 ni shilingi 1,311,837,466,000.

Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. UMMY ALLY MWALIMU (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ambayo imepitia na kuchambua kwa kina bajeti ya Wizara ya Afya,

naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2023/24 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2024/25.

**2. Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Aidha, kipekee naomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini kusimamia Wizara ya Afya ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia Sekta ya Afya nchini. Sekta ambayo inagusa maisha ya kila siku ya kila mtu, mwanamke au mwanaume, kijana au mzee, tajiri au maskini kutokana na ukweli kuwa Mtu ni Afya na Afya ni Mtaji. Vilevile, nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuipa kipaumbele Sekta hii kwa kutoa miongozo, maelekezo mbalimbali na kufanya uwekezaji mkubwa wa rasilimali fedha ili kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi. Ningependa kutambua **mambo makubwa kumi (10)** yaliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake kama ifuatavyo:-

(a) Ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za Afya katika maeneo mbalimbali nchini ambao umewezesha **Vituo vya kutolea huduma za Afya kuongezeka** kutoka vituo 8,549 Mwaka 2021 hadi vituo 9,693 mwaka 2024 hii ni sawa na ongezeko la vituo 1,144;

(b) **Kuongezeka kwa Vifaa tiba vya kisasa vya uchunguzi na ugunduzi** wa magonjwa mbalimbali ikiwemo;- MRI kutoka 7 hadi 13, CTScan kutoka 12 hadi 45, Digital X-Ray kutoka 147 hadi 346, Ultrasound kutoka 476 hadi 668, Echocardiogram kutoka 95 hadi 102, Cathlab kutoka 1 hadi 4, Pet Scan 1 ambayo awali haikuwepo nchini;

(c) **Kuongezeka kwa idadi ya vitanda vya kulaza wagonjwa** katika vituo vya kutolea huduma za afya kutoka vitanda 86,131 mwaka 2021 hadi vitanda 145,374 Machi 2024;

(d) Kuongezeka kwa **idadi ya vitanda kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU)** katika vituo vya umma kutoka vitanda 258 vya mwaka 2021 hadi kufikia vitanda 1,362 Machi 2024;

(e) Kuimarika kwa **hali ya upatikanaji wa dawa na bidhaa za Afya** (aina 290) katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kutoka asilimia 58 kufikia asilimia 79 Machi 2024;

(f) Kuongezeka kwa idadi ya Hospitali zinazotoa **huduma ya magonjwa ya dharura (EMD)** kutoka saba (7) mwaka 2020 hadi kufikia 116 Machi 2024;

(g) Kupatikana kwa **huduma za ubingwa na ubingwa bobezi** kwa gharama nafuu nchini na pia kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi (Tiba Utalii) ambapo wagonjwa kutoka nje ya nchi wameongezeka kutoka 5,705 mwaka 2022 hadi 7,843 mwaka 2024;

(h) Kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya vyenye uwezo wa kutoa **huduma za dharura za uzazi** ikiwemo upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC) kutoka 388 mwaka 2021 hadi 523 mwaka 2024;

(i) **Kupungua kwa vifo vya wajawazito** kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi kufikia vifo 104 kwa kila vizazi hai 100,000 na **kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano** kutoka vifo 67 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi kufikia vifo 43 kwa kila vizazi hai 1,000; na

(j) **Kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI** kutoka vifo 29,000 mwaka 2022 hadi vifo 22,000 Machi 2024 na Kifua Kikuu kutoka vifo 25,800 mwaka 2022 hadi vifo 18,100 Machi 2024 .

**3. Mheshimiwa Spika,** Namba zinaongea, **Tumesikia, tumeona na kuthibitisha wenyewe** mambo makubwa ambayo yamefanyika ndani ya Sekta ya Afya chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha miaka mitatu tu. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ili maono yake ya kuboresha Sekta hii ya Afya na wananchi kuendelea kupata huduma bora za afya nchini yatimie. Kupitia mafanikio haya ni dhahiri kuwa Rais Samia ni kinara wa mageuzi chanya ndani ya Sekta ya Afya nchini na barani Afrika.

**4. Mheshimiwa Spika**, Nitumie fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawashukuru wataalam wote wa Afya ndani ya nchi walioshiriki katika jitihada za kumtibu kiongozi wetu. Hakika tutaendelea kumuenzi kiongozi huyu mahiri aliyeleta mageuzi makubwa ya mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza kwa kuyaishi kwa vitendo. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aipe roho ya Hayati pumziko la milele. Amina

**5. Mheshimiwa Spika,** Vilevile, nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na watanzania wote kwa kumpoteza mwanasiasa nguli na mahiri, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aipe roho ya Hayati pumziko la milele. Amina

**6. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa shukrani za dhati kwa **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele kuimarisha huduma za afya hususan usafi na afya

mazingira katika maeneo ya Mijini na Vijijini. Aidha, nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Afya nchini ikiwemo kuhamasisha wanaume kupima Virusi vya UKIMWI na mapambano dhidi ya Magonjwa Yasiyoambukiza. Vilevile, nampongeza kwa Hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 3 Aprili, 2024 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2024/25. Pia, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko,** kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini.

**7. Mheshimiwa Spika,** Napenda kukupongeza wewe binafsi **Mheshimiwa Spika** kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabaraza ya Kitaifa Duniani (IPU) na Baraza la uongozi la IPU ambacho ni chombo kikuu cha kufanya maamuzi kinachojumuisha wabunge kutoka Duniani kote. Aidha, nampongeza **Naibu Spika**, **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu**, kwa kuendelea kukusaidia vyema katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uadilifu mkubwa, lakini pia kwa kuzingatia na kusimamia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge lako tukufu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Tunapenda kukuhakikishia kuwa uongozi na watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutatekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma bora za afya kwa kuzingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zinazopitishwa na Bunge lako tukufu. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kusimamia vyema mijadala ndani ya Bunge.

**8. Mheshimiwa Spika,** Kipekee niwapongeze **Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi**, Mbunge wa Chamwino kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo**, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; na **Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba**, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ninaahidi kuwapa ushirikiano

viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya. Aidha, napenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao umeiwezesha Wizara kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za afya. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza Dira ya Afya ya kujenga Jamii yenye afya bora na ustawi itakayochangia kikamilifu maendeleo ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

**9. Mheshimiwa Spika,** Kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya afya na masuala ya UKIMWI, chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb)**, na Makamu wake, **Mheshimiwa Dkt. Faustine Englebert Ndugulile (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa katika kuboresha utendaji wa Wizara hususan katika kipindi cha maandalizi ya bajeti hii. Aidha, **nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote** kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za afya. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wenu katika utekelezaji wa majukumu yetu kwa wananchi. Vilevile, Wizara yangu itaendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu na kazi zetu za kuwatumikia Wananchi ndani na nje ya Bunge.

**10. Mheshimiwa Spika,** Napenda kutoa pongezi kwa **Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa **Jimbo la Mbarali**. Aidha, naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu, kwa Familia na Wananchi wa Jimbo la Mbarali kwa kifo cha **Mheshimiwa Francis Mtega** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali**, Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil** aliyekuwa Mbunge wa **Jimbo la Kwahani.** Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote, waliopoteza ndugu, Jamaa na marafiki zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga mbalimbali ikiwemo maporomoko ya ardhi na mafuriko yaliyotokea Wilayani Hanang Mkoani Manyara na Rufiji Mkoani Pwani. Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**11. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo ya awali, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya

Wizara kwa mwaka 2023/24, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na maombi ya fedha ya kutekeleza vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2024/25.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/24

**12. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/22 – 2025/26), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 20202025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya - HSSP V (2021/22 – 2025/26), Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na makubaliano ya Kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**13. Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti ya mwaka 2023/24, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala za Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha huduma za Kinga dhidi ya magonjwa;

(a) Kuimarisha upatikanaji, usambazaji, utunzaji na utoaji wa huduma za chanjo hususan chanjo za Watoto wenye umri chini ya miaka mitano;

(b) Kuimarisha huduma za Lishe nchini hususan kwa akinamama wajawazito, watoto wenye umri chini ya miaka mitano na vijana; na

(c) Kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya jamii.

ii. Kuimarisha ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma katika ngazi zote kwa;

Kuimarisha usimamizi wa huduma za afya katika Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya za Mikoa, Timu za Uendeshaji wa Huduma za Afya ngazi ya Halmashauri, Bodi za Usimamizi wa huduma za Afya ngazi ya Halmashauri na Kamati za Usimamizi wa huduma za Afya vituoni na uwajibikaji na ufanisi;

(a) Kufanya uhakiki wa mara kwa mara na wakushtukiza katika vituo vya kutolea huduma za afya vya Umma, Binafsi na Vya Mashirika ya Dini;

(b) Kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia weledi, maadili na miiko ya kitaaluma kupitia mabaraza na bodi za kitaaluma;

(c) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya zikiwemo Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum, Taifa na Vyuo vya Mafunzo ya Afya kwa;

- Kukamilisha ujenzi wa miundombinu inayoendelea.
- Kuanza Ujenzi mpya.
- Ukarabati wa Vituo vya kutolea huduma za afya.
- Kuweka miundombinu ya umeme na maji katika Vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya Msingi.
- Kuendeleza ujenzi wa nyumba za Watumishi. iii. Kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya.

(d) Kuimarisha huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa;

(e) Kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi;

(f) Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi; ikiwemo uimarishaji wa huduma za Mkoba na

(g) Tembezi katika ngazi ya msingi;

(h) Kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa ya kuambukiza;

(i) Kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwemo ajali;

(j) Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za ubingwa na bingwa bobezi;

(k) Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;

(l) Kuendeleza na kusimamia huduma za Tiba Asili na tiba mbadala nchini;

(m) Kusimamia tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za Afya; na

(n) Kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu.

## C. MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA

**14. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Fungu 52 hukusanya mapato kutokana na huduma za tiba zitolewazo katika Hospitali zilizo chini yake, tozo na uchangiaji wa huduma katika Taasisi mbalimbali, ada za Vyuo na uuzaji wa zabuni.

**15. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2023/24 Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 677,621,168,391** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 88,414,775,177** ni kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara ikiwemo Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma, **Shilingi 111,585,224,823** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi 477,621,168,391** ni kutoka

Hospitali za Kanda, Maalum, Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**16. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekusanya jumla ya kiasi cha **Shilingi 528,728,911,186.17** sawa na **asilimia 78** ya makadirio yote ya maduhuli ya Shilingi 677,621,168,391. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi 53,111,059,890.15 sawa na asilimia 60 ya makadirio kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha Shilingi 105,446,924,814.35 sawa na asilimia 94 kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha Shilingi 370,170,926,481.67 sawa na asilimia 78 kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara, kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 1 hadi Na. 3.**

**17. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu kutumia jumla ya kiasi cha **Shilingi 1,235,316,516,000** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 502,951,909,000** ni kwa ajili ya **Matumizi ya Kawaida** na **Shilingi 732,364,607,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa **Miradi ya Maendeleo**. Aidha, kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi cha Shilingi 148,609,423,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Shilingi 354,342,486,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara makao Makuu, Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Vilevile, kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, kiasi cha Shilingi 430,298,000,000 ni fedha za ndani na Shilingi 302,066,607,000 ni fedha za nje.

**18. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya kiasi cha **Shilingi 838,442,785,386.82** kimepokelewa sawa na asilimia 68 ya bajeti ya Shilingi 1,235,316,516,000 iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 404,859,107,830.80** sawa na asilimia 80 ya bajeti ya Shilingi 502,951,909,000 kimepokelewa kwa ajili ya **kugharamia matumizi ya kawaida** na kiasi cha **Shilingi 433,583,677,556.02** sawa na asilimia 59 ya bajeti ya Shilingi 732,364,607,000 kimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa **miradi ya Maendeleo**.

**19. Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kiasi cha **Shilingi 100,539,137,095.87** sawa na asilimia 68 ya bajeti ya Shilingi 148,609,423,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na kiasi Shilingi 304,319,970,734.93 sawa na asilimia 86 ya bajeti ya Shilingi 354,342,486,000 kimepokelewa kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Wizara Makao Makuu, Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa. Aidha, kati ya fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Shilingi 316,540,687,508.23 sawa na asilimia 74 ya bajeti ya Shilingi 430,298,000,000 ni kutoka vyanzo vya ndani na Shilingi 117,042,990,047.79 sawa na asilimia 39 ya bajeti ya Shilingi 302,066,607,000 ni fedha za nje kutoka kwa Washirika wa maendeleo.

**20. Mheshimiwa Spika,** Kati ya fedha zilizopokelewa kutoka vyanzo vya nje, kiasi cha **Shilingi 96,926,989,204.68** kilipokelewa kupitia mfumo wa D-Fund kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi Misonge ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Shilingi 73,735,718,410.08 ni kutoka Mfuko wa Dunia "Global Fund" kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, kiasi cha Shilingi 17,073,866,385.60 kutoka Benki ya Dunia na kiasi cha Shilingi 6,117,404,409 kutoka Susan Thompson Buffet Foundation Account kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Uwekezaji wa Afya ya Mama na Mtoto.

## D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA
## HUDUMA ZA KINGA

### Huduma za Chanjo

**21. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha huduma za kinga ikiwemo kuhakikisha huduma za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana kulingana na mahitaji ya Mikoa yote nchini. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, watoto chini ya miaka mitano, wajawazito na wasichana wenye umri wa miaka 9 hadi 14 ambao ni walengwa wa huduma za chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati.

**22. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha **chanjo za watoto wadogo** za kuwakinga na magonjwa 11 yanayozuilika kwa chanjo ambayo ni pamoja na Pepopunda, Kifaduro, Kupooza (Polio), Surua, Homa ya Uti wa Mgongo, Kifua Kikuu, Dondakoo, Nimonia, Homa ya Ini, Rubella na Kuharisha zinapatikana bure kulingana na mahitaji. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilinunua: dozi 1,200,000 za IPV (Inactivated Polio Vaccine) kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa Kupooza kwa watoto; Chanjo ya Pentavalent dozi 2,008,700 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya Kifaduro, Dondakoo, Kupooza, Homa ya Ini na Homa ya Uti wa Mgongo; Chanjo ya Pneumococal Conjugate Vaccine (PCV) dozi 5,320,000 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya Homa ya Mapafu (Nimonia) na Homa ya Uti wa Mgongo; Chanjo ya Bivalent Oral Polio Vaccine (BOPV) dozi 7,263,000 kwa ajili ya kuzuia virusi mbalimbali vinavyosababisha ugonjwa wa Kupooza kwa watoto; Chanjo ya Rotarix (Rota) dozi 6,716,750 kwa ajili ya kuwakinga watoto dhidi ya kuhara kukali; Chanjo ya Bacillus Calmette Geurin (BCG) dozi 2,000,000 kwa ajili ya kuwakinga watoto wachanga na ugonjwa wa Kifua Kikuu; Chanjo za kampeni ya Polio dozi 17,761,880. Chanjo ya HPV (dozi 400,240) kwa ajili ya kuwakinga mabinti dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi, Chanjo ya Surua na Rubella (MR) dozi 3,000,000 kwa ajili ya kukinga watoto na ugonjwa wa Surua na Rubella na Chanjo zingine za MR (dozi 10,409,000) zilinunuliwa kwa ajili ya kampeni ya kitaifa ya uchanjaji wa chanjo ya Surua Rubella kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya ugonjwa huo nchini.

**23. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara iliweka lengo la kuchanja jumla ya watoto 2,180,313. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, **jumla ya watoto 2,245,722 sawa na asilimia 103 walikuwa wamechanjwa chanjo ya Penta3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo** ikilinganishwa na uchanjaji wa watoto 1,596,951 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya utoaji wa chanjo nyingine uliendelea kuimarika ambapo chanjo ya Surua Rubella dozi ya kwanza (MR-1) ilifikia asilimia 101 na asilimia 98 kwa dozi ya pili (MR-2) ikilinganishwa na asimilia 97 na asilimia 95 kwa dozi ya pili kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Rota 2 asilimia 99 na PCV-3 asilimia 100, na Chanjo ya Polio dozi ya tatu (OPV 3) ilifikia asilimia

101. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha kuwa watoto wote wanaostahili kupata chanjo hizo wanapata kwa usahihi na wanakingwa dhidi ya magonjwa hayo yanayoweza kuzuilika kwa chanjo hapa nchini.

**24. Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hilo la viwango vya uchanjaji kwa watoto ni matokeo ya utekelezaji wa zoezi maalum la PIRI (Periodic Intensification of Routine Immunization) lililolenga kuwatafuta watoto ambao hawakuchanjwa au kutokamilisha ratiba za chanjo nchini pamoja na zoezi la REC (Reach Every Child) likiwa na lengo la kumfikia kila mtoto ili apate chanjo. Mafanikio haya ya utoaji wa huduma za chanjo nchini kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja yanakidhi vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) vya kuwafikia zaidi ya asilimia 90 ya walengwa wa Chanjo kitaifa. Kwa upande wa Tanzania, tulijiwekea lengo la kufikia kiwango cha uchanjaji cha asilimia 95 ambapo hadi kufikia Machi 2024 tayari lengo limefikiwa kwa asilimia 103.

**25. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imetekeleza awamu mbili za **kampeni ya chanjo ya Polio** ili kuzuia kuenea kwa ugonjwa wa Polio uliotokea Mkoa wa Rukwa na katika nchi jirani za Zambia, Congo na Burundi. Awamu ya kwanza Kampeni ilitekelezwa katika halmashauri 37 zilizopo katika Mikoa sita ya Rukwa, Kagera, Kigoma, Katavi, Mbeya na Songwe kuanzia tarehe 21 hadi 24 Septemba 2023 na kufanikiwa kuwachanja watoto 4,258,162 wenye umri chini ya miaka nane (8) kati ya watoto 3,250,598 waliolengwa ikiwa ni mafanikio ya asilimia 131. Aidha, awamu ya pili ya Kampeni ilifanyika katika mikoa sita iliyofanya awamu ya kwanza kuanzia tarehe 02 hadi 05 Novemba, 2023 kwa mafanikio makubwa ambapo watoto 4,634,921 wenye umri wa chini ya miaka nane (8) sawa na asilimia 108.8 kati ya walengwa 4,258,162 walipata Chanjo. Halmashauri zote 37 zillizoshiriki kwenye kampeni hii zilivuka malengo ya uchanjaji kwa zaidi ya asilimia 100. Kampeni hii ilifanyika kwa kujumuisha na utoaji wa chanjo ya surua kwa watoto ambao hawajawahi kupata au kukamilisha dozi za chanjo ya surua.

**26. Mheshimiwa Spika,** Ufuatiliaji wa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo ulibaini pia kuwepo kwa ugonjwa wa Surua nchini. Hatua za kudhibiti ugonjwa huu zilifanyika kwa kufanya **kampeni ya uchanjaji wa chanjo ya Surua Rubella** kwa mikoa yote nchini. Lengo la kampeni ilikuwa ni kufikia asilimia 95 ya uchanjaji. Wizara ya Afya mnamo tarehe 15 hadi 18 Februari 2024, kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo ilifanya Kampeni ya chanjo ya Surua Rubella kwa watoto wenye umri wa kuanzia miezi 9 hadi chini ya miaka mitano. Lengo la Kampeni hii lilikuwa ni kudhibiti milipuko ya magonjwa ya Surua na Rubella ili kupunguza vifo na madhara yatokanayo na magonjwa haya ambapo kampeni hii ililenga kuwapatia Chanjo watoto 8,908,810 kwa Tanzania bara ambapo jumla ya watoto 10,164,868 sawa na asilimia 114 ya walengwa walifikiwa.

**27. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka 14 dhidi ya **Saratani ya mlango wa kizazi** kwa kununua na kusambaza chanjo ya Human Papilloma Virusi (HPV) ambayo inatoa kinga dhidi ya saratani hiyo. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Juni 2024, Wizara iliweka lengo la kuchanja jumla ya wasichana 721,684 wenye umri wa miaka 14 kwa ajili ya chanjo ya HPV. Hadi kufikia Machi 2024 jumla wasichana 663,949 walikuwa wamepatiwa chanjo hii sawa na asilimia 92 ya walengwa ikilinganishwa na Wasichana 535,708 waliopata chanjo hiyo kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**28. Mheshimiwa Spika,** Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa kutokana na umuhimu wa chanjo ya kukinga ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi, Wizara imeendesha **Kampeni Maalum ya Chanjo ya HPV kwa Mabinti wenye umri wa miaka 9 hadi 14** kuanzia tarehe 22 hadi 28 Aprili 2024 iliyokuwa na kauli mbiu ya 'Binti makini timiza ndoto zako na chanjo ya HPV'. Kampeni hii imefanyika nchi nzima ambapo mabinti wameanza kupata chanjo ya HPV dozi moja tu. Uamuzi wa kutoka katika dozi mbili ya chanjo ya HPV na kuanza kutumia dozi moja, umetokana na matokeo ya kitafiti ambayo yameonesha kuwa, kupata dozi mbili au moja kote kuna matokeo sawa katika kumlinda mtoto wa kike dhidi ya ugonjwa wa saratani ya mlango wa kizazi.

**‘Mheshimiwa Spika, Nitumie Bunge lako tukufu kuwahakikishia Watanzania hususan wazazi na walezi kuwa chanjo hii ni salama na haina madhara, na ninatoa wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha mabinti wa umri wa miaka 9-14 wanapata chanjo hiyo ili kujikinga na saratani ya mlango wa kizazi’.**

**29. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za mnyororo baridi wa chanjo nchini, Wizara imeendelea kununua na kusambaza majokofu ya kuhifadhia chanjo hizo na kuyasambaza wilayani na katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Majokofu 1,601 yamenunuliwa kwa gharama ya Shilingi 21,023,327,723 ambapo majokofu 189 yanatumia nishati ya umeme na 1,412 yanatumia nishati ya jua. Majokofu hayo tayari yamesambazwa na kufungwa kwenye vituo vya kutolea huduma za chanjo nchini. Kuwepo kwa vifaa hivi vya mnyororo baridi katika ngazi zote kunatuhakikishia kuwa, utunzaji wa chanjo unafanyika katika viwango vinavyotakiwa kitaifa na kimataifa na hivyo, chanjo zinatolewa ni salama na bora kwa ajili ya kuchanja watoto na wahitaji wengine.

## HUDUMA ZA LISHE

**30. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa pili wa Kitaifa wa Lishe 2021/22 – 2025/26 ambapo kupitia Mpango huo Wizara imetekeleza afua za lishe zilizothibitishwa kuwa na matokeo makubwa ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo wa lishe duni (Malnutrition) na lishe ya kuzidi (Obesity). Baadhi ya afua hizo ni pamoja na; utoaji wa matone ya vitamin A, dawa za kutibu minyoo ya tumbo, matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoto, utoaji wa vidonge vya madini chuma na foliki asidi kwa wajawazito, uongezwaji wa virutubishi vya madini na vitamini kwenye vyakula vinavyoliwa kwa wingi na wananchi ikiwemo unga wa ngano, unga wa mahindi, chumvi, mafuta ya kula, utoaji wa elimu ya lishe na uhamasishaji wa masuala ya ulaji unaofaa kwa kutumia vyakula vinavyopatikana kwenye maeneo yetu pamoja na kufanya mazoezi.

**31. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha jamii inazingatia masuala ya **unyonyeshaji maziwa ya mama**, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa miongozo inayohimiza unyonyeshaji sahihi wa watoto ikiwemo **mtoto kuanza kunyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa** na unyonyeshaji wa watoto maziwa ya mama pekee kwa miezi sita (6) ya mwanzo. Elimu ya unyonyeshaji imeendelea kutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya, katika ngazi ya jamii na kupitia maadhimisho mbalimbali ikiwemo wiki ya unyonyeshaji. Kufuatia jitihada hizo, **unyonyeshaji wa maziwa ya mama kwa watoto ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa umeongezeka kutoka asilimia 59 kwa mwaka 2015 hadi asilimia 70 kwa mwaka 2022.** Hali kadhalika, hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita (6) imeimarika kutoka asilimia 58 ya mwaka 2015 hadi asilimia 64 mwaka 2022.

**32. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imeendelea kuimarisha afya na lishe ya watoto chini ya miaka 5 kwa kuendelea kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya **utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto walio chini ya miaka mitano.** Malengo ya kampeni yalikuwa ni kutoa matone ya Vitamin A kwa watoto 9,460,369 wenye umri wa kati ya miezi 6 mpaka miezi 59 nchi nzima. **Jumla ya watoto 9,456,436 walipatiwa matone ya vitamin A** ambayo ni sawa na asilimia 99 ya lengo. Kiwango cha utekelezaji kimeongezeka ikilinganishwa na watoto 9,052,340 waliofikiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma ya utoaji wa matone ya Vitamini A kwa watoto chini umri wa miaka 5 hufanyika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa utaratibu wa kawaida ambapo mtoto akitimiza umri wa miezi 6 hupewa matone ya vitamini A na huendelea kupatiwa matone hayo kila baada ya miezi 6 hadi atakapotimiza umri wa miaka 5.

**33. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea **kuhamasisha wasindikaji wa vyakula ili waongeze virutubishi kwenye vyakula vinavyoliwa kwa wingi nchini**, ambapo virutubishi vya madini na vitamini (Iron, Folate, Zinki, vitamin B12) huongezwa kwenye unga wa mahindi na ngano, Iodine kwenye chumvi na Vitamini A kwenye mafuta ya kula. Kwa sasa kuna jumla ya viwanda/wasindikaji wakubwa wa vyakula 31 ambapo wazalishaji

9 ni wasindikaji wa unga wa ngano, 13 wa mafuta ya kula na 9 ni wasindikaji wa chumvi. Viwanda hivi vyote vinaongeza virutubishi. Vilevile, kwa upande wa wasindikaji wa unga wa mahindi wadogo na wa kati hapa nchini, uhamasishaji wa kufunga mashine za kunyunyiza virutubishi (dosifiers) kwenye vyakula umefanyika ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya mashine 263 zimefungwa katika Mikoa 26 na hivyo kufikia jumla ya mashine 1,158 ikilinganishwa na mashine 895 zilizokuwepo kipindi kama hiki mwaka 2022/23. Kwa wastani, kila mashine inazalisha tani 30 za unga wa mahindi ulioongezwa virutubishi kwa mwezi hivyo inakadiriwa kiasi cha tani 34,740 zinazalishwa kwa mwezi. Mwelekeo wa Wizara ni kuimarisha ufuatiliaji wa wasindikaji wa vyakula wakubwa wa kati kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili kuhakikisha vyakula vinaongezwa virutubishi kwa viwango vinavyotakiwa.

**34. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Kampuni Binafsi ya SANKU inajenga **kiwanda cha kisasa cha kuzalisha virutubishi nchini** chenye uwezo wa kuzalisha tani 6 kwa siku na kinatumia teknolojia ya kisasa na inayokubalika kimataifa. Kwa sasa kiwanda cha aina hii kipo kimoja barani Afrika. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha aina hii hapa Tanzania kutasaidia upatikanaji wa virutubishi nchini, lakini pia kitazalisha ziada kwa ajili ya nchi za jirani na hivyo kuwa chanzo cha mapato ya fedha za kigeni kwa nchi yetu. Ujenzi wa kiwanda hiki unafanyika katika mkoa wa Dar es salaam na umefikia asilimia 95. Kiwanda hiki kinategemewa kuzinduliwa rasmi Juni 2024.

**35. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa mwezi Septemba 2022, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara imekamilisha mapitio ya Kanuni za kuongeza virutubishi kwenye vyakula za mwaka 2011 ili ziendane na hali halisi ya sasa, kwa sababu kanuni za awali ziliwahusu wasindikaji wakubwa pekee na kuwaacha wasindikaji wa kati na wadogo. katika kufanikisha suala la uongezaji wa virutubishi kwenye vyakula, Wizara itashirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuhakikisha kanuni hizi zinatekelezwa kwa kuimarisha ufuatiliaji wa wasindikaji wa vyakula

katika ngazi zote kupitia Maafisa Afya, uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa matumizi ya vyakula vilivyoongezwa virutubishi na kuwawezesha wasindikaji ikiwa ni pamoja kuwapatia mashine za kuongeza virutubishi kwenye vyakula.

**36. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea **kuhamasisha na kuelimisha makundi mbalimbali katika jamii juu ya masuala ya lishe na mtindo bora wa maisha** kupitia majukwaa mbalimbali. Mojawapo ya majukumu hayo ni maadhimisho **Siku ya Afya na Lishe ya Kijiji (SALiKi)** yanayofanyika mara nne kwa mwaka kwenye vijiji na mitaa. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya vijiji na mitaa 15,399 kati ya 16,581 sawa na asilimia 92.5 vilikuwa vimetekeleza zoezi hili. Mpango huu unaipa jamii fursa ya kufuatilia ukuaji na maendeleo ya mtoto, kupata elimu ya lishe kutoka sekta mbalimbali, kupata huduma za afya za mkoba pamoja na kujifunza namna ya kuandaa vyakula bora kwa kuzingatia vyakula vinavyopatikana kwenye jamii husika (mapishi darasa). Huduma zingine za afya na lishe zinazotolewa katika siku hiyo ni uhamasishaji kuhusu ulishaji sahihi wa watoto; uchangamshi wa watoto, usafi wa maji na mazingira na ulinzi wa watoto na utoaji wa chanjo, utoaji wa matone ya Vitamini A na dawa za kutibu minyoo ya tumbo kwa watoto. Huduma hizi za lishe pia hutolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya na kupitia watoa huduma ngazi ya jamii wanapotembelea kaya. **'Nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuhamasisha na kushiriki katika utekelezaji wa Siku ya Afya na Lishe ya kijiji/Mitaa ndani ya Majimbo yenu'.**

**37. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha masuala ya lishe yanatekelezwa na kusimamiwa vizuri katika ngazi za Mikoa, Halmashauri, Kata na vijiji. Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imeendelea kusimamia utekelezaji wa **Mkataba wa Lishe unaowapima viongozi wa Mikoa na Wilaya**.
Tathmini ya utekelezaji wa mikataba hiyo hufanyika kwenye ngazi ya Taifa mara moja kwa mwaka, ngazi ya Mikoa mara mbili kwa mwaka na ngazi ya Halmashauri kila robo mwaka. Kiashiria mojawapo kati ya viashiria 14 vinavyofuatiliwa katika mkataba huo ni matumizi ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya afua za Lishe. Tathmini ya utekelezaji ngazi ya Mkoa imefanyika Septemba 2023

ambapo matokeo yanaonesha kwamba, kiashiria cha matumizi ya fedha kimefanikiwa kwa **asilimia 77.18** ikilinganishwa na asilimia 63 ya tathmini iliyofanyika mwaka 2022. Viashiria vingine 13 vimefanikiwa kwa kati ya asilimia 93 - 100 ikilinganishwa na kati ya asilimia 85 - 100 ya kipindi kilichopita.

**38. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutumia majukwaa mbalimbali ikiwemo maadhimisho ya **Siku ya Lishe kitaifa** ili kuhakikisha kuwa jamii inakuwa na uelewa wa masuala ya Lishe. Kwa mwaka wa fedha 2023/24 maadhimisho hayo yaliyofanyika tarehe 29 hadi 30 Oktoba 2023 katika mikoa yote 26 ya Tanzania bara yakibeba kaulimbiu isemayo "**Lishe Bora kwa Vijana Balehe, Chachu ya Mafanikio Yao".** Wakati wa maadhimisho haya, jumla ya vipindi 361 vya lishe vilifanyika na kurushwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari (redio, runinga, magazeti, na mitandao ya kijamii) katika ngazi zote kote nchini ikilinganishwa na vipindi 93 pekee vilivyorushwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2022/23. Inakadiriwa wananchi 15,897,500 walifikiwa na ujumbe wa lishe kupitia vyombo vya Habari na majukwaa mbalimbali yaliyofanyika katika mikoa yote nchini. Halikadhalika, kupitia maadhimisho hayo, vijana balehe 235,913 kote nchini walipatiwa elimu ya lishe kwenye siku ya maadhimisho, ambapo 126,862 miongoni mwao walifanyiwa tathmini ya hali zao za lishe na 15,302 kati yao walipatiwa huduma ya unasihi wa lishe kulingana na hali zao za Lishe. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Chakula na Ulaji wa mwaka 2023 ambao ulizinduliwa Tarehe 16 Novemba, 2023. Mwongozo huo unalenga kuhamasisha matumizi sahihi ya chakula mchanganyiko kwa kuzingatia chakula kinachopatikana hapa nchini kwa ajili ya kuimarisha afya ya jamii. Mwongozo huo pia umelenga kuhamasisha kupunguza matumizi ya vyakula vyenye sukari, mafuta na chumvi kwa wingi ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza pamoja na kuhamasisha usafi wa mazingira yanayotumika kuandaa chakula katika jamii.

**Afya Mazingira na Usafi**

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua kuwa afya mazingira na usafi ni nguzo muhimu katika ustawi wa afya ya jamii. Katika

kutekeleza azma hiyo, Wizara kwa kushirikiana na Mikoa na Halmashauri inaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa afua za Afya Mazingira na Usafi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Afua hizo ni pamoja na kuwezesha ujenzi na matumizi ya vyoo bora, uwekaji wa vifaa vya kunawa mikono, udhibiti wa taka na usafishaji wa maeneo ya makazi, maeneo ya biashara na maeneo ya umma ili kuikinga jamii dhidi ya magonjwa ya kuambukiza kama vile Kipindupindu, Kuhara Damu, Dengue, Malaria na magonjwa mengine ya kuambukiza.

**40. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa eneo la **ujenzi na matumizi ya vyoo bora**, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **kaya zenye vyoo bora zimeongezeka** hadi kufikia kaya 7,775,181 sawa na **asilimia 77.5** ikilinganishwa na **kaya** 7,087,523 sawa na asilimia 73.2 zilizokuwa na vyoo bora katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hili ni sawa na ongezeko la kaya 687,658 sawa na asilimia 4.3 katika kipindi cha mwaka mmoja.
Lengo la Wizara ni kufikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, hivyo jitihada zinaendelea ili kuweza kufikia shabaha tuliyojiwekea. Kwa upande wa **usafi wa mikono**, kaya zenye vifaa vya kunawia mikono, kwa maji tiririka na sabuni zimeongezeka kutoka asilimia 42.7 mwaka 2022/23 hadi kufikia **asilimia 45** kwa mwaka 2023/24.

**41. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Wizara ya Maji imeendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa **Huduma Endelevu za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini** katika Sekta ya Afya (Sustainable Rural Water Supply and Sanitation - SRWSS) kwenye Halmashauri za Wilaya 137 zilizopo kwenye Mikoa 25 nchini. Katika mwaka wa fedha 2023/24, Wizara imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji safi, vyoo, mabafu, vifaa vya kunawia mikono, viteketezi taka (incinerators) na maboresho ya vyumba vya kujifungulia akina mama wajawazito kwenye Vituo 615. Ujenzi wa miundombinu hii unatarajiwa kukamilika mwezi Juni mwaka 2024 ambapo itafikisha jumla ya vituo 2,517 ambavyo vimenufaika kupitia mradi wa SRWSS. Hadi kufikia Machi 2024 utekelezaji wa miradi umefikia vituo

1902 sawa na asilimia 72.2 ya lengo la kufikia vituo 2,636 ifikapo Julai 2025. Aidha, Wizara imeratibu mashindano ya kitaifa ya Afya na Usafi wa Mazingira ambapo kwa mwaka 2023 washindi wa kwanza walikuwa kama ifuatavyo: Ngazi ya Shule za Msingi - Shule ya Msingi Endabash (Halmashauri ya Karatu); ngazi ya Shule za Sekondari za Bweni za Serikali na Binafsi – St. Francis Girls (Mbeya Jiji); ngazi ya Halmashauri ya vijiji – Kenikelele (Halmashauri ya Njombe); ngazi ya Halmashauri za Wilaya – Njombe DC; ngazi ya Halmashauri za Miji – Njombe TC; ngazi ya Manispaa – Shinyanga MC; ngazi ya Majiji – Tanga; ngazi ya Hospitali za Wilaya – Hospitali Teule ya Mugana (Misenyi DC); ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa – Arusha Lutheran Medical Centre; ngazi ya Mabenki – CRDB Makao Makuu Dar es Salaam; na ngazi ya Vyuo vya Elimu ya Juu – Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **Ninawapongeza washindi hawa na kusisitiza viongozi wa Serikali na Taasisi za ngazi zote kusimamia usafi na afya ya mazingira katika maeneo yao.**

**42. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kusimamia **afua za usafi wa mazingira na udhibiti wadudu waenezao magonjwa**. Lengo la utekelezaji wa afua hizi ni kuimarisha ushiriki wa wananchi katika udhibiti wa wadudu dhurifu, uimarishaji wa usafi wa mazingira. Miongoni mwa kazi zilizofanyika kwa mwaka 2023/24 ni udhibiti wa mazalia ya wadudu na usimamizi wa usafi katika ngazi za kaya, taasisi na maeneo ya biashara na umma. Katika kutekeleza afua hizi, kaguzi katika kaya 10,378,348, kaguzi 4,904 katika masoko, kaguzi 146,512 katika huduma za chakula, kaguzi 1,045 katika vituo vya mabasi, kaguzi 12,746 za ofisi za umma, kaguzi 9,492 katika Shule za Sekondari, kaguzi 23,233 katika Shule za Msingi na kaguzi 10,076 katika maeneo mengine zilifanyika. Katika kaguzi hizo, jumla ya ilani za marekebisho 82,738 zilitolewa kwa waliokiuka kanuni za Afya kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.

**43. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuratibu uimarishaji wa huduma za usafi na udhibiti wa taka ngumu kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Usafi wangu Mita Tano, Mita Tano Usafi Wangu. Mkakati huu

unalenga kuhakikisha maeneo ya makazi, taasisi, umma na biashara yanakuwa safi kuyazunguka kwa mita tano. Katika utekelezaji wa mkakati huu ambao umeambatana na utekelezaji wa siku ya usafi jumamosi ya mwisho wa mwezi, jumla ya kaya 10,378,348 na maeneo 2,416,838 ya biashara, umma na taasisi yalitembelewa. Aidha, jumla ya tani 1,375,088.65 za taka ngumu zilizozalishwa, tani 463,103.25 sawa na asilimia 25 zilikusanywa na kufikishwa maeneo maalum yaliyotengwa kutupia taka. Bado Halmashauri zinakabiliwa na changamoto ya udhibiti wa taka kwani taka zinazozalishwa hazipelekwi katika maeneo maalum ya kutupia taka, hali inayopelekea kuhatarisha afya ya jamii. **'Nachukua nafasi hii, kuielekeza Mikoa na Halmashauri, kusimamia kikamilifu afua ya udhibiti wa taka kwani ina mchango mkubwa katika udhibiti wa wadudu dhurifu ambao ni kichocheo cha maambukizi ya magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza'**.

**44. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa **huduma za Hedhi Salama** kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau kupitia jukwaa la hedhi salama (Menstrual Health and Hygiene Coalition) kwa kuelimisha jamii juu ya Umuhimu wa hedhi salama kwa Watoto wa kike waliopevuka kupitia ziara za mashuleni, utoaji wa elimu ya hedhi katika vituo vya kutolea huduma za afya na maadhimisho ya Siku ya Hedhi Salama yanayofanyika tarehe 28 Mei kila mwaka. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara imeanzisha kampeni ya **"Pedi Yangu Afya Yangu".** inayolenga kuhamasisha wadau wa ndani kuzalisha bidhaa za hedhi salama. Pia kampeni hii inalenga kuhamasisha wadau kuchangia paketi za pedi ambapo lengo ni kukusanya, kusambaza na kugawa paketi 5,000,000 kwa wanafunzi wa kike katika shule za msingi na sekondari nchini.

**45. Mheshimiwa Spika,** Wizara inakamilisha **Mwongozo wa Hedhi Salama** ambao licha ya kubainisha malighafi zinazokubalika kutumika wakati wa hedhi, utaelezea namna bora ya uhifadhi na utupaji wa pedi zilizotumika, usafi wakati wa hedhi na miundombinu muhimu ambayo inahitajika kuwepo ili kumwezesha msichana na mwanamke kujisitiri vyema wakati wa hedhi. Aidha,

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI, Shirika la Afya Duniani na Shirika la Kazi Duniani imeendelea kuimarisha **huduma za afya mahala pa kazi** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara imefanya mafunzo ya jinsi ya kujikinga na madhara ya kiafya kwa watumishi 1,038 wa Sekta ya Afya katika mikoa 10 na Halmashauri 73.

**46. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea **kudhibiti kuingia kwa magonjwa hatari yanayoambukiza** ikiwemo Ebola, Marburg, mafua ya Ndege (SARS), UVIKO-19, Homa ya manjano, pamoja na Homa ya Nyani (M-Pox) kuingia kupitia maeneo ya viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu kwa kufanya uchunguzi wa afya kwa wasafiri wanaotoka katika nchi mbalimbali kuangalia endapo wana magonjwa hatari ya kuambukiza. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wasafiri 8,375,047 walikaguliwa ambapo 1,733,502 sawa na asilimia 20.7 ni wasafiri wa nje (International Travelers) na wa ndani (domestic) ni 6,641,545 sawa na asilimia 79.3 ambapo hakuna msafiri aliyegundulika kuwa na magonjwa hatari ya kuambukiza. Aidha katika kudhibiti ugonjwa wa Homa ya Manjano, wasafiri 5,642,611 walikaguliwa kama wamepata chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya manjano ambapo wasafiri 11,747 walichanjwa chanjo ya ugonjwa huo, ikilinganishwa na wasafiri 4,889,591 waliokaguliwa na 10,583 waliochanjwa kipindi kama hiki mwaka 2022/23.

**47. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendeleza juhudi za kukabiliana na magonjwa hasa katika mipaka isiyo rasmi, Wizara imefanya zoezi la utambuzi wa mipaka hiyo isiyo rasmi na shughuli kuu za kijamii na kiuchumi zinazopelekea mikusanyiko mkubwa unaochochea kuenea kwa magonjwa. Kazi hii ilifanyika Mkoani Ruvuma na ilishirikisha Wilaya za
Songea na Nyasa ikiwa ni juhudi za kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu na Homa ya nyani inayoripotiwa katika nchi Jirani zinazopakana na Wilaya hizi. Aidha, tathmini hii ilienda sambamba na mafunzo kwa watumishi 25 wa afya wa Mikoa, Halmashauri na Mipaka ili kuwajengea uwezo wa kuchambua takwimu za wasafiri na kuwatambua wahisiwa wa magonjwa.

**48. Mheshimiwa Spika;** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za afya katika vituo vya Afya mipakani** ili viweze kutoa huduma madhubuti na kwa ufanisi kwa kusambaza magari 16 na pikipiki 20 katika vituo 36 vya afya mipakani. Aidha Wizara imefanikiwa kununua Vipima joto (Walkthrough Thermoscaners) 10 ambavyo vimesambazwa katika mipaka iliyopo mikoa ya Kagera, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Mara, Mbeya na Songwe kwa ajili ya kuendelea kuimarisha uchunguzi kwa wasafiri. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya kuambukiza katika maeneo ya mipakani ikiwa ni pamoja na ukarabati wa jengo moja (1) kwa ajili ya kuwatenga wasafiri washukiwa wa magonjwa ya kuambukiza (Isolation unit) katika mpaka wa Mutukula mkoani Kagera pamoja na ujenzi wa miundombinu ya kudumu ya kunawia mikono (Mass Hand Washing Facilities) inayojengwa katika mpaka wa Rusumo na bandari ya Kigoma ili kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza.

**49. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya mipakani kwa kushiriki katika **tathmini ya utekelezaji wa Kanuni za Afya za Kimataifa za Mwaka 2005.** Tathmini hiyo iliyofanyika mwezi Agosti 2023 ililenga kupima uwezo wa mipaka katika kutoa huduma wakati wote na wakati wa dharura. Matokeo ya tathmini hiyo yalionesha kuwa **uwezo wa huduma za afya mipakani umepanda kufikia wastani wa asilimia 73.3. Kiwango hicho ni cha juu kabisa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 40 tulizopata katika tathmini iliyopita iliyofanyika mwaka 2016.** Matokeo haya yameonesha kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kujengea uwezo wa mipaka katika utoaji wa huduma za afya katika mipaka kwa kuzingatia Kanuni za Afya za Kimataifa.

**Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko (Disease Surveillance)**

**50. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko** kwa kutumia mfumo wa kielektroniki wa

Integrated Disease Surveillance and Response (e-IDSR) ambapo vituo vyote vya kutolea huduma vimewezeshwa kutoa taarifa. Katika kipindi cha Julai 2022/23 hadi Machi 2023/24 jumla ya watumishi 2,300 ngazi ya vituo, Halmashauri na mikoa walipatiwa mafunzo. Pia maboresho yameendelea kufanyika kwa mfumo wa kielektroniki wa utoaji wa taarifa za tetesi zinazoweza kuwa na athari za kiafya kabla ya kuleta madhara kwenye jamii (Electronic Event Based Surveillance - eEBS). Uimarishaji huo umewezesha wanajamii kuweza kutoa taarifa za tetesi kwa kutuma ujumbe kwenda namba 199 bila malipo pamoja na kuchakata na kufanyia kazi taarifa toka vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

**51. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya tetesi 11,368 zimetolewa taarifa kupitia mfumo huu na kuchunguzwa ambapo kati ya hizo, magonjwa ya mlipuko kama vile **Kipindupindu, Kimeta na Surua** yaliweza kubainika. Kupitia mfumo huo, Wizara imeweza kuongeza utambuzi wa magonjwa ya milipuko mapema na kuweka mikakati ya haraka ya udhibiti. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuboresha dawati la kuchakata tetesi lenye lengo la kufuatilia tetesi zote zinazopokelewa na kuzitolea taarifa kwa ufuatiliaji. Aidha, hadi sasa, jumla ya watoa huduma wa afya ngazi ya jamii (CHWs) 1,434 wamejengewa uwezo na wanatoa taarifa za tetesi kwa kutumia mfumo huo.

**52. Mheshimiwa Spika,** Ugonjwa wa **Kipindupindu** ndio mlipuko uliojitokeza zaidi kuliko magonjwa mengine ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Mikoa 16 (Mara, Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Kagera, Singida, Simiyu, Shinyanga, Tabora, Ruvuma, Mwanza, Dodoma, Geita, Manyara, Morogoro na Katavi,) imetoa taarifa ya uwepo wa mlipuko wa ugonjwa huo ambapo jumla ya wagonjwa 1,853 waliripotiwa. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara mbalimbali katika kutumia dhana ya Afya moja katika kuendelea kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huu hapa nchini.

**Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs)**

**53. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kudhibiti na kutokomeza magonjwa matano yaliyokuwa hayapewi kipaumbele ambayo ni **Matende na Mabusha, Trakoma, Usubi, Kichocho na Minyoo ya Tumbo**. Shughuli za udhibiti wa magonjwa haya zimegawanyika katika maeneo makuu matatu ambayo ni shughuli za kinga kwa ugawaji wa kingatiba kwa magonjwa yote matano, shughuli za tiba kwa kufanya upasuaji wa mabusha na usawazishaji wa vikope na shughuli za utengamao kwa kutoa matunzo ya wagonjwa wa matende.

**54. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara iliendelea kufanya zoezi la **umezeshaji kingatiba** dhidi ya ugonjwa wa matende na mabusha, kichocho, minyoo ya tumbo na usubi Katika kipindi hiki Wizara iligawa kingatiba za Ivermectin na Albendazole katika Halmashauri saba (7) zenye maambukizi ya juu na kuhitaji kingatiba kati ya Halmashauri 119 zilizokutwa na kiwango cha juu cha maambukizi mwaka 2008 Halmashauri hizo ni Mafia, Pangani, Kilwa, Lindi MC, Lindi DC, Mtwara – Mikindani, na Kinondoni. (Halmashauri 112 tayari zimefanikiwa kutokomeza ugonjwa huo). Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya walengwa 909,569 walimezeshwa kingatiba, sawa na asilimia 76 ya lengo (1,203,359).

**55. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilifanya zoezi la tathmini ya kiwango cha maambukizi ya ugonjwa wa matende na mabusha kwa mkoa wa Dar es salaam. Matokeo ya Tathmini hiyo yalionesha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni na Manispaa ya Ubungo hazina maambukizi mapya ya Ugonjwa wa Matende na Mabusha kwa kipindi cha miaka 6 baada ya kusitisha umezeshaji wa Kingatiba katika Halmashauri hizo. Aidha, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam, Manispaa ya Temeke na Kata 10 za Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ambazo ni Bunju, Kawe, Kunduchi, Mabwepande, Makongo, Mbezi Juu, Msasani, Mbweni, Wazo na Mikocheni kwa sasa hazina maambukizi mapya ya ugonjwa wa Matende na Mabusha. Hivyo, Wizara imesitisha umezeshaji wa

Kingatiba dhidi ya Ugonjwa wa Matende na Mabusha katika maeneo hayo ambayo kwa sasa hakuna maambukizi mapya. Kupitia tathmini hizo ni faraja kwetu kuona kuwa, tumefanikiwa kuwanusuru wananchi zaidi ya milioni 3.7 katika kuwaepusha na hatari ya kupata maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa Matende na Mabusha.

**56. Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara iliweza kutoa kingatiba ya kudhibiti **ugonjwa wa Kichocho** (Praziquantel) katika Halmashauri 78 zilizotarajiwa kupata huduma hii katika kipindi hiki. Halmashauri hizo zinatoka katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Simiyu na Tanga, Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ambapo walengwa (Watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 - 14) walikuwa 5,503,212 na waliomezeshwa kingatiba ni watoto 4,127,409 sawa na asilimia 75 ya lengo.

**57. Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024**,** Wizara imeweza kutoa kingatiba ya kudhibiti **ugonjwa wa Minyoo ya tumbo** (Albendazole) katika Halmashauri 83 ilizotarajiwa kupata huduma hii katika kipindi hiki. Halmashauri zilizopata huduma hiyo ni kutoka katika Mikoa ya Arusha, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Simiyu, Tanga, Kagera, Kigoma, Mara, Mwanza na Shinyanga ambapo walengwa (Watoto wenye umri wa kwenda shule miaka 5 - 14) walikuwa 6,768,312 na waliomezeshwa dawa ni 5,076,234 sawa na asilimia 75 ya lengo.

**58. Mheshimiwa Spika;** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilifanya zoezi la umezeshaji wa dawa kinga ya Ivermectin ya kudhibiti **ugonjwa wa Usubi** katika Halmashauri 24 zilizokuwa zimelengwa katika kipindi hiki kati ya Halmashauri 30 zenye kiwango cha juu cha maambukizi ya vimelea vya ugonjwa wa usubi. Halmashauri hizo ni Mufindi DC, Njombe DC, Njombe TC, Gairo DC, Kilosa DC, Morogoro DC, Mvomero DC, Malinyi DC, Ifakara TC, Ulanga DC, Mlimba DC, Ludewa DC, Madaba DC, Mbinga DC, Mbinga TC, Namtumbo DC, Nyasa DC, Songea DC, Songea MC, Lushoto DC, Bumbuli DC, Korogwe DC, Muheza DC na Mkinga DC. Idadi ya walengwa katika Halmashauri hizo

walikuwa ni 5,380,328 na waliomezeshwa kingatiba walikuwa ni 5,246,328 ambao ni sawa na asilimia 97 ya lengo.

**59. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilifanikiwa kufanya zoezi la umezeshaji kingatiba kudhibiti **ugonjwa wa Trakoma** katika Halmashauri tisa 9 zenye maambukizi ya juu ya ugonjwa wa Trakoma nchini ambazo ni Longido, Monduli, Ngorongoro, Kiteto, Mpwapwa, Simanjiro, Chamwino, Kongwa na Kalambo. Lengo ilikuwa ni kuwafikia walengwa 1,926,935. Walengwa 1,400,691 sawa na asilimia 72.7 ya lengo walimezeshwa kingatiba

**60. Mheshimiwa Spika,** Katika Kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara iliendelea kutoa huduma za tiba kwa kufanya **upasuaji wa mabusha na usawazishaji wa vikope.** Huduma za upasuaji wa mabusha zilitolewa kwa njia ya kambi katika Hospitali za Rufaa ya Mkoa wa Lindi, Hospitali ya Wilaya ya Bagamoyo, Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga, Kituo cha Afya Kitangari Halmashauri ya Newala vijijini na Kituo cha Afya Kibiti; Halmashauri ya Kibiti ambapo jumla ya wagonjwa 409 walipata huduma hiyo ikilinganishwa na wagonjwa 212 waliopatiwa huduma hiyo kwa njia ya kambi mwaka jana, na jumla ya wagonjwa 302 walipata huduma katika vituo vingine vilivyojengewa uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa mabusha ikilinganishwa na wagonjwa 25 waliopata huduma hiyo mwaka jana. Aidha, Katika kusogeza huduma kwa **wagonjwa wa Matende na Mabusha**, Wizara imewajengea uwezo watumishi kutoka vituo vya afya 63 jinsi ya kutoa huduma na matibabu ya Matende na Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii 208 ili kuibua wagonjwa wa Matende na Mabusha katika Halmashauri za Newala vijijini, MtwaraMikindani na Mkuranga.

**61. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeratibu huduma za upasuaji mdogo wa **usawazishaji wa Vikope** kwa wagonjwa 1,789 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 katika Halmashauri za Wilaya 14 ikilinganishwa na wagonjwa 2,106 waliofanyiwa katika kipindi hiki mwaka uliopita. Lengo la upasuaji huo ni kuzuia wananchi walioathirika na ugonjwa wa vikope kupata upofu wa kudumu.

## ELIMU YA AFYA KWA UMMA NA HUDUMA ZA AFYA NGAZI YA JAMII

**62. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza **Kampeni Endelevu ya Elimu ya Afya Jumuishi** (Integrated Health Education and Social Behavioral Change Campaign) ili kuchochea mabadiliko chanya ya tabia na mitindo bora ya maisha kwa kuhamasisha jamii kuzingatia kanuni za afya kuhusu magonjwa mbalimbali ikiwemo Magonjwa Yanayoambukiza na Yasiyoambukiza, huduma za Lishe, Afya ya Vijana, Mama na Mtoto na Afya Mazingira. Aidha, Wizara iliandaa na kusambaza mabango (Posters) 455,000, vipeperushi (Brochures) 525,098. Jumla ya Matangazo ya Redio 14,400 yalirushwa. Matangazo hayo yalirushwa sambamba na ujumbe kupitia mitandao ya kijamii (Social Media Fliers, Jingles and Clips) ambapo jumbe 3,900 zilirushwa. Vilevile, vipindi vinavyohusisha ushiriki wa Wataalam katika vyombo vya habari vilifanyika mara 540 kwa Redio na mara 25 kwa vipindi vya Runinga. Utekelezaji wa zoezi hili ni endelevu na unafanyika kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kutekeleza **afua za elimu ya afya na ushirikishaji jamii kuhusu dharura mbalimbali za afya** (Risk Communication and Community Engagement, RCCE) na magonjwa ya mlipuko ikiwemo ugonjwa wa Polio, Surua, Kipindupindu, Homa ya Dengue, Red Eyes, UVIKO19 na magonjwa yanayotokana na Wanyama (Zoonotic Diseases) ikiwemo Kimeta. Vielelezo mbalimbali vya uelimishaji jamii viliandaliwa na kusambazwa ikiwemo mabango (Posters) 307,000 na vipeperushi (Brochures) 125,000. Usambazaji wa vielelezo hivi umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, Dar es Salaam, Katavi, Kigoma, Kagera, Mara, Arusha Kilimanjaro, Tanga, Singida, Dodoma, Simiyu, Mwanza, Shinyanga na Manyara.

**64. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko**, Wizara ilizishirikisha Kamati za Afya ya Msingi (Primary Health Committees - PHCs) ngazi za Mkoa na Wilaya, Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii, Wanahabari na Vyombo vya Habari

(Redio 5 za Kitaifa na Redio 41 za kijamii - Community Radios), pamoja na Viongozi wa Dini, wataalam wa afya, wawakilishi wa makundi mbalimbali ngazi ya jamii, walimu, vyombo vya habari, elimu ya nyumba kwa nyumba, kwenye nyumba za ibada, masoko, Hospitali na kutumia magari ya matangazo ambapo jumla ya magari 30 (PA system) yalitumika. Jumla ya wawakilishi 2,570,000 walijengewa uwezo na kushirikishwa katika kutoa elimu na hamasa kwa jamii dhidi ya magonjwa ya mlipuko.

**65. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya imeratibu uandaaji, uzinduzi na hatimaye kuanza utekelezaji wa **Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii** (Integrated and Coordinated Community Health Workers' Program). Chini ya Mpango huu, kila Kitongoji (kwa maeneo ya vijijini) na kila Mtaa (kwa maeneo ya Mjini) kutakuwa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHW) wawili (2) wanaoishi katika eneo husika. Mpango huu unatekelezwa kwa awamu katika Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara na ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania siku ya tarehe 31 Januari, 2024 katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC). **Jumla ya Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii wapatao 137,294 wanatarajiwa kunufaika kupitia Mpango huu kwa kipindi cha miaka mitano yaani 2023/24 hadi 2027/28** ambapo kwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji Wahudumu 28,000 watafikiwa. Aidha, katika kutekeleza Mpango huu, Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI imeanza zoezi la kuwachagua Wahudumu 8,900 ambao baada ya taratibu za kuwapata kukamilika, watanufaika kwa kupewa mafunzo maalum ya miezi sita (6) na kuwezeshwa kutekeleza majukumu yao katika Mikoa 10 ya Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mbeya, Njombe, Pwani, Songwe, Tabora na Tanga. Wahudumu wa Afya ngazi ya jamii watajikita katika kutekeleza afua za afya katika maeneo makuu sita (6) ambayo ni: Lishe; Afya ya Uzazi, Mtoto na Vijana; Afya na Usafi wa Mazingira; Magonjwa ya kuambukiza (Malaria, Kifua Kikuu na UKIMWI); Magonjwa Yasiyoambukiza; na

Magonjwa ya Mlipuko na Athari za Mabadiliko ya Tabia Nchi katika jamii.

‘**Afya ya Jamii Nyumba kwa Nyumba Hatuachi Mtu’.**

## HUDUMA ZA AFYA YA UZAZI, MAMA NA MTOTO

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 2030) ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia chini ya 70 kwa kila vizazi hai 100,000, vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano kufikia 25 kwa kila vizazi hai 1000 na vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa kila vizazi hai 1000 ifikapo mwaka 2030. Katika mwaka 2023/24 Sekta ya Afya imefanya uimarishaji wa huduma zifuatazo; huduma kabla ya ujauzito, huduma wakati wa uchungu na kujifungua, huduma baada ya kujifungua, huduma kwa watoto, afya ya uzazi kwa vijana wa rika balehe, na huduma za masuala ya kijinsia.

**67. Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji mkubwa ambao Serikali ya Awamu ya 6 imeufanya katika eneo hili ni pamoja na utekelezaji wa afua mbalimbali vimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza **vifo vitokanavyo na uzazi** kwa asilimia 80 kutoka 556 mwaka 2015/16 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000, kupunguza **vifo vya watoto walio chini ya miaka mitano** kutoka 67 mwaka 2015 hadi 43 kwa kila vizazi hai 1000, **kupunguza vifo vya watoto wachanga** kutoka 25 hadi 24 kwa kila vizazi hai 1000 kwa mujibu wa utafiti wa TDHS ya mwaka 2022. Mwenendo huo wa kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi na vile vya watoto chini ya miaka mitano inaonesha kuwa nchi yetu ipo kwenye mwelekeo mzuri katika kufikia malengo ya kidunia ifikapo 2030. Hali ya vifo vitokanavyo na uzazi kwa nchi za Afrika Mashariki na zile zinazotuzunguka ni kama ifuatavyo; Uganda 189 (UDHS 2022), Burundi 494 (UN 2023), Kenya 530 (WHO 2023), Malawi 381 (UN 2023), Msumbiji 127 (UN 2023), Somalia 621 (UN 2023), Sudan Kusini 1,223 (UN 2023), na Zambia 135 (UN 2023).

**68. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuwekeza kwenye **huduma za afya ya uzazi kabla ya ujauzito** ikiwemo kusimamia utoaji wa huduma za uzazi wa mpango ambapo Wizara ilinunua na kusambaza bidhaa za uzazi wa mpango kwenye vituo vya huduma kama ifuatavyo; Depo Provera dozi 3,874,810 sawa na asilimia 92 ya lengo, Vidonge vya uzazi wa mpango 3,610,038 sawa na asilimia 99 ya lengo, Vipandikizi aina ya Implanon NXT 297,721 sawa na asilimia 65 ya lengo, Vipandikizi aina ya Jadelle 277,942 sawa na asilimia 87 ya lengo, vitanzi aina ya Copper T 62,470 sawa na asilimia 82 ya lengo. Takwimu za Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji wa Huduma za Afya (MTUHA) zinaonesha kuwa njia za uzazi wa mpango za kisasa ambazo zilitumika katika kipindi cha Julai hadi Machi 2024 ni pamoja na vipandikizi (asilimia 38.3); Sindano (asilimia 23.1); vidonge (asilimia 11.3); kondomu (asilimia 10.4), vitanzi (asilimia 4.6); kufunga kizazi (asilimia 0.4), na asili ni asilimia 11.1.

**69. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, jumla ya watumiaji wa njia za kisasa za **uzazi wa mpango** walikuwa ni 6,702,212 sawa na **asilimia 58.75** ya wanawake wote walio katika umri wa kupata ujauzito, ikilinganishwa na wateja 5,785,731 sawa na asilimia 53.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati yao watumiaji wapya wa njia za uzazi wa mpango walikuwa 4,052,317. Aidha, mikoa iliyoongoza kwa kuwa na asilimia kubwa ya watumiaji wapya wa uzazi wa mpango kati ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 ni; Mara (asilimia 38.1), Kigoma (asilimia 37.0), Kilimanjaro (asilimia 34.3), Katavi (asilimia 32.5) na Geita (asilimia 32.4). Aidha, mikoa ambayo haifanyi vizuri ni Lindi (asilimia 22.3), Songwe (asilimia 23.6), Mtwara (asilimia 23.9), Kagera (asilimia 24.5), na Mbeya (asilimia 28.7). Tafiti zinaonesha kwamba uzazi wa Mpango unasaidia kuimarisha afya ya mama na mtoto kwa kuwa mama anayepata mapumziko ya kutosha kati ya uzazi na uzazi yupo kwenye nafasi nzuri zaidi ya kuwa na uzazi salama.
**'Naomba kuwahimiza akinamama walio katika umri wa kupata ujauzito kutumia huduma hizi kwa manufaa yao na watoto wao'.**

**70. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya wakati wa ujauzito** kwa kuhakikisha elimu inatolewa kuanzia ngazi ya jamii kuhusiana na

umuhimu wa wajawazito kuhudhuria kliniki kama inavyoainishwa katika Mwongozo wa Huduma za Kliniki kwa Wajawazito wa Mwaka 2018. **Wizara inaeendelea kusisitiza umuhimu wa wajawazito kuanza kuhudhuria kliniki mapema na haswa mimba ikiwa na umri chini ya wiki 12, lakini pia kuhakikisha mjamzito anahudhuria mahudhurio angalau manne mpaka anafikia kipindi cha kujifungua.** Wahudumu wa afya watatumia fursa hii kutambua na kutibu changamoto mbalimbali zinazohusiana na ujauzito na kujifungua. Changamoto hizo ni pamoja na; upungufu wa damu, maambukizi ya magonjwa ya ngono, Malaria, mimba kutunga nje ya kizazi; magonjwa ya moyo au changamoto zitokanazo na makundi madogo ya damu yasiyoendana baina ya wenza (Rh Incompatibility).

**71. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wajawazito waliohudhuria **mahudhurio manne** au zaidi walikuwa 2,208,391 sawa na asilimia 119.5 ya waliotarajiwa ikilinganishwa na idadi ya wajawazito 2,030,749 sawa na asilimia 112.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hata hivyo, pamoja na mafanikio ya mahudhurio ya wajawazito kliniki mara nne au zaidi kufikia asilimia 119.5, bado **mahudhurio ya kliniki ya wajawazito wenye umri wa mimba chini ya wiki 12** yameendelea kuwa katika kiwango cha chini kwa asilimia 44.4, sawa na wajawazito 822,194 ikilinganishwa na asilimia 40.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. **'Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama wajawazito pamoja na wenzi wao kuwahi kuanza kliniki mapema ili wataalam waweze kuwa na muda muafaka wa kutambua changamoto zinazohusiana na ujauzito na kujifungua na kuchukua hatua stahiki kwa wakati'.**

**72. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Afya kwa kuhakikisha vituo vinatoa huduma bora za kliniki **wakati wa ujauzito** ambazo ni pamoja na; kuwapatia elimu ya afya kuhusu vidokezo vya hatari na lishe, kuwafanyia vipimo vya msingi tisa (9) ambavyo ni uzito, shinikizo la damu (BP), kundi la damu, wingi wa damu, kuangalia protini kwenye mkojo, maambukizi ya Malaria, VVU, kaswende na homa ya ini. Aidha, wakati wa kliniki mjamzito anapewa kadi maalum ya

kliniki ya ujauzito, huduma za dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza wingi wa damu na dawa za kinga ya Malaria (SP).

**73. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wajawazito 1,752,843 sawa na asilimia 88.25 ya wajawazito wote walipatiwa dawa za kukinga na kuzuia Malaria (IPT2+) ikilinganishwa na wajawazito 1,663,808 sawa na asilimia 87.15 ya wajawazito katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Katika kipindi hiki, wajawazito waliopata dawa ya kuzuia upungufu wa damu (FEFO) walikuwa ni asilimia 96 ikilinganishwa na asilimia 92.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, wajawazito 1,721,734 sawa na asilimia 88 walipimwa wingi wa damu ikilinganisha na wajawazito 1,419,137 sawa na asilimia 74.95 waliopimwa wingi wa damu kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Asilimia 1.8 ya waliopimwa walikutwa na upungufu mkubwa wa damu na kupatiwa matibabu. Wajawazito 1,555,034 walipewa dawa za kutibu minyoo sawa na asilimia 78.95 ikilinganishwa na wajawazito 1,579,122 sawa na asilimia 82.85 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Vilevile katika kipindi hiki wajawazito 1,761,156 sawa na asilimia 88.6 walipima uwepo wa mambukizi ya kaswende ikilinganishwa na wajawazito 1,663,808 sawa na asilimia 98.8 waliopima maambukizi ya kaswende kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Katika kipindi hiki asilimia 0.65 ya wajawazito walikutwa na maambukizi ya kaswende na kupatiwa matibabu.

**74. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma wakati wa kujifungua** kwa kuendelea kutoa elimu kwa wajawazito kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupatiwa huduma na wahudumu wa afya wenye ujuzi. Takwimu za MTUHA zinaonyesha kuwa, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wajawazito 1,607,540 sawa na **asilimia 97.85 walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya** kati ya wajawazito wote 1,642,648 ambao walijifungua katika kipindi hiki, ikilinganishwa na wajawazito 1,504,384 sawa na asilimia 97.75 ya 1,538,710 waliojifungua katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, **wajawazito waliohudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi** walikuwa 1,543,856 sawa na **asilimia 93.7** ikilinganishwa na wajawazito 1,449,747 sawa na asilimia 94.3 ya wajawazito waliojifungua katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha

jumla ya wajawazito 188,885 sawa na **asilimia 11.65** ya wajawazito waliojifungulia katika vituo vya huduma **walijifungua kwa njia ya upasuaji**, Viwango vya upasuaji vinavyopendekezwa na shirika la afya duniani ni chini ya asilimia 15, kwahiyo Tanzania bado ipo katika viwango vinavyopendekezwa na shirika la afya duniani. Kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 Vituo vya afya vilivyotoa **huduma ya upasuaji kwa wajawazito (CEmONC centres) vilikuwa 475** ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **vilikuwa ni vituo 525**. Ongezeko hili linaendana na jitihada la Serikali kupeleka huduma hizi karibu na wananchi ili kuendelea kupunguza vifo vinavyotokana na uzazi.

**75. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa **huduma za afya baada ya kujifungua** (Postnatal Care Services) kwa akinamama na watoto. Katika kipindi cha mahudhurio haya mama pamoja na mtoto hupata huduma mbalimbali zikiwemo, kuangalia kama kuna changamoto zitokanazo na mabadiliko baada ya kujifungua kwa akina mama kama vile kupungukiwa damu, kupata uambukizi mkali, majipu ya matiti n.k; lakini pia watoto wachanga huchunguzwa ili kutambua wenye changamoto za kiafya, ulemavuwa viungo wa kuzaliwa na kuwapatia huduma stahiki na pia kutoa elimu ya unyonyeshwaji. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya akina mama 1,669,128 ambao ni sawa na **asilimia 91.7** ya akinamama wote waliojifungua walipata huduma baada ya kujifungua. Aidha, jumla ya watoto wachanga 1,666,772 sawa na asilimia 91.8 ya watoto waliozaliwa hai walipata huduma za Afya baada ya kuzaliwa. **'Nitumie fursa hii kuwahimiza akinamama waliojifungua pamoja na wenzi wao kuhudhuria na kuwapeleka watoto wachanga vituoni kupata huduma baada ya kujifungua (Postnatal Care Services) kwani kipindi hiki ni muhimu sana katika afya ya mama na mtoto mchanga'.**

**76. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuimarisha **matibabu ya fistula** zitokanazo na uzazi. Huduma za upasuaji wa fistula zimeendelea kutolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Kanda CCBRT, Mbeya, Bugando, Hospitali za Kivulini Maternity Africa (Arusha) na Nkinga (Tabora) ambapo wagonjwa 742 walipata huduma katika kipindi

cha Julai 2023 hadi Machi 2024 kulinganisha na wagonjwa 851 waliopata huduma hiyo kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023.**'Nawahimiza wajawazito kuwahi katika vituo vya kujifungulia wapate huduma bora na salama na jamii ishirikiane kuibuwa wagonjwa ambao wakati mwingine huwa wanajificha kwa kuona aibu kutokana na tatizo hili la fistula'.**

**77. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea kuboresha huduma za afya ya uzazi na mtoto, Wizara imetengeneza **Kitabu cha Afya ya Mama na kitabu cha Mtoto** cha kufuatilia makuzi ya mtoto vitakavyotumika kufuatilia afya ya mama mjamzito na mtoto ambapo sasa kuna kitabu cha mtoto wa kike na cha mtoto wa kiume kwa kuwa kiligundulika mtoto wa kike au wa kiume hukua kwa kasi tofauti hivyo ni lazima wafuatiliwe kwa kutumia chati tofauti za ukuaji. **Jumla ya vitabu 1,200,000** vya mtoto wa kike na wa kiume na vitabu vya wajawazito vimeanza kuchapishwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma na vitatolewa bure bila malipo. **Nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha za kutengeneza vitabu hivi. Nawataka Waganga wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha vitabu hivi vinatolewa bila Malipo kwa akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.**

**78. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma kwa Watoto wachanga** ambapo matokeo ya utafiti wa viashiria vya Afya na Malaria (TDHS 2022) yanaonesha uwepo wa kiwango kidogo cha kupungua kwa vifo vya watoto wachanga kutoka vifo 25 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16 hadi 24 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2022. Matokeo haya yanaonesha umuhimu wa Serikali kuongeza nguvu zaidi katika kupunguza
vifo vya watoto wachanga ili kufikia lengo la Kimataifa la kupunguza vifo vya watoto wachanga kufikia 12 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030.

**79. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na mikakati ya kupunguza vifo vya watoto wachanga ikiwemo kuziwezesha **Hospitali kuanzisha Wodi maalum za watoto wachanga (NCU).** Katika mwaka wa fedha wa 2023/24 jumla ya Hospitali 66

zimeanzisha NCU hivyo kuongeza upatikanaji wa NCU nchini kutoka Hospitali 175 Julai 2023 hadi kufikia **NCU 241** mwezi Machi 2024. Kati ya NCU hizo 156 ziko kwenye Hospitali zinazomilikiwa na Serikali na 85 zipo kwenye Hospitali za zinazomilikiwa na Mashirika ya dini na Binafsi. Aidha katika kipindi hiki Serikali imekarabati NCU kwenye Hospitali 31 (Hospitali za Rufaa za Mikoa 6 na Hospitali za Halmashauri 25) katika Mikoa 15 (Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara, Geita, Kagera, Mwanza, Manyara, Arusha, Tanga, Songwe, Mbeya, Mtwara, Dodoma na Morogoro). Kwa mujibu Shirika la Afya Duniani (WHO), Ili kupunguza vifo vya watoto wa changa kwa zaidi ya nusu ya viwango vilivyopo sasa ifikapo mwaka 2030, tunapaswa kuwa na angalau asilimia 80 ya Hospitali za Halmashauri ziwe na NCU ifikapo mwaka 2025. Tanzania tunakwenda vizuri na malengo ya kimataifa kwani hadi mwezi Machi 2024, asilimia 60 sawa na Hospitali 110 za halmashauri za Wilaya zilikuwa zimeanzisha NCU. Sambamba na uanzishwaji wa NCU kwenye Hospitali, Serikali imewezesha jumla ya Vituo vya Afya 92 vinavyotoa huduma za upasuaji wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC) kuanzisha huduma za NCU, hivyo kufanya idadi ya vituo vya CEmONC vyenye huduma ya NCU kuwa 174. **'Natoa wito kwa Mikoa, Halmashauri na Wadau kushirikiana na kuhakikisha Hospitali zote za Halmashauri zinakuwa na wodi za 'NCU' ifikapo mwaka 2025. Uanzishwaji wa wodi za NCU uende sambamba na ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba pamoja na kuwajengea uwezo watoa huduma katika wodi hizi'.**

**80. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imeongeza **ununuzi wa dawa za watoto** aina ya Amoxilin myeyuko kwa ajili ya kutibu homa ya mapafu (Nimonia) kutoka vidonge milioni 30.1 hadi vidonge milioni 38.95. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara imeongeza manunuzi ya dawa ya kutibu kuharisha pakiti za Zinc na ORS zilizofungashwa pamoja (ORS and Zinc Co-Pack) kutoka 94,300 hadi 1,348,001. Ununuzi wa dawa hizi uliwezesha kuimarika kwa upatikanaji wa dawa za watoto wenye umri chini ya miaka mitano katika vituo vya kutolea huduma nchini. **'Naomba kutumia fursa hii kusisitiza kwamba dawa za kidonge myeyuko cha Amoxicillin, Zinc na ORS kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, zinanunuliwa na**

**Serikali hivyo hazipaswi kuuzwa. Nawaelekeza Waganga wakuu wa Mikoa na Halmashauri wasimamie suala hili kwa ukamilifu**'.

**81. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kuboresha **huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana wenye umri kati ya 10 hadi 24** kwa kutoa elimu ya afya uzazi kwa vijana kuhusu namna ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya VVU, mimba za utotoni, ukatili wa kijinsia, ukatili dhidi ya watoto, Afya ya akili na lishe. Katika kipindi hiki, Wizara iliongeza vituo vya huduma rafiki ya Afya ya uzazi kwa vijana 210 na kufikia **vituo 1,111** mwezi Machi 2024 ikilinganishwa na vituo 901 mwaka 2022/23. Aidha katika kipindi hiki, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendesha mafunzo ya huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana kwa watoa huduma za Afya 750 katika Mikoa (9) ya Mara, Shinyanga, Dar es Salaam, Katavi, Arusha, Manyara, Geita, Tabora na Dodoma.

**82. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma kwa manusura wa matukio ya **ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (GBV & VAC).** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imeongeza vituo vitatu vinavyotoa huduma jumuishi kwa manusura wa ukatili wa Kijinsia na watoto; katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Singida, Manyara na Kituo cha Afya Makole ambapo vituo vimeongezeka kutoka 26 Mwaka 2023 hadi 29 Machi 2024. Aidha ukarabati wa vituo nane (8) unaendelea kwenye Hospitali za rufaa za Mikoa; Ligula, Bombo, Mawenzi, Sokoine, Kitete, Bukoba, Mbeya na Temeke. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya visa 149,081 (watoto wa jinsia ya kike 9,133 na wa kiume 6,312) vimeripotiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na visa 194,368 mwaka 2022/23. Waathirika wa GBV & VAC waliotokea katika Mikoa 10 iliyoongoza ni; Dar es salaam (13,719), Shinyanga (12,300), Mara (9,823), Mwanza (9,242), Geita (7,697), Kigoma (7,544), Kagera (7,496), Tabora (7,471), Ruvuma (7,425) na Tanga (6,827). **'Natoa wito kwa jamii kuachana na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto, lakini pale inapotokea matukio hayo yatolewe taarifa mapema, manusura wafikishwe kwenye vituo vya kutolea huduma mapema kwa uchunguzi na matibabu stahiki'.**

**83. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha ubora wa utoaji huduma za afya ya uzazi mama na mtoto, stadi na ujuzi wa watoa huduma ni kigezo muhimu cha kupata matokeo chanya. Tumetekeleza program mbalimbali zinazolenga kutoa mafunzo kazini ikiwemo Mafunzo kwa wakufunzi ngazi ya vituo katika Mkoa wa Kigoma, Tanga, Dar Es Salaam, Mara na Kagera, kuendesha mafunzo elekezi kazini kwa huduma za Mama na Mtoto kupitia programu ijulikanayo kama **"Mama Samia mentorship program"** ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, zaidi ya watoa huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto 6,000 wamefikiwa kutoka Mikoa yote 26 ya Tanzania
Bara.

**84. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 wanawake wapatao **278,406** walifanyiwa **uchunguzi wa Saratani ya mlango wa kizazi** na kati yao wanawake 7,767 sawa na asilimia 2.8 waligundulika kuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na kupatiwa matibabu, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2022/23. Katika kipindi hiki Serikali imefanikiwa kuanzisha **vituo vipya 311 vya kutolea huduma za uchunguzi wa saratani ya Mlango wa Kizazi** na matiti hapa nchini na hivyo kufikia jumla ya **vituo 1,308** ikilinganishwa na vituo 997 mwaka 2022/23. Aidha, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Juni 2023 wanawake 2,827,088 walifanyiwa **uchunguzi wa saratani ya matiti** ambapo 11,418 walionekana kuwa na viashiria vya saratani na kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 kati ya wanawake 2,459,498 waliofanyiwa uchunguzi 7,723 waligundulika kuwa na viashiria vya saratani. **'Naomba kuwasisitiza wanawake kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa saratani za mlango wa kizazi na matiti kwani zinatibika zikigundulika mapema'**.

**85. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki Serikali kwa kushirikiana na Wadau imenunua **mashine tiba joto** (Thermocoagulators) 140 zinazotibu mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na kusambazwa katika **vituo 140** vya kutolea huduma za afya hapa nchini katika halmashauri 140 za mikoa yote 26. Aidha, watoa huduma 100 wamejengewa uwezo namna ya kuzitumia mashine hizo.

**MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI, HOMA YA INI NA MAGONJWA YA NGONO**

**86. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Mpango Jumuishi wa kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini** (National AIDS, STI's and Hepatitis Control Program - NASHCoP), imeendelea kusimamia utekelezaji wa afua mbalimbali zenye lengo la kuzuia maambukizi mapya na kutoa huduma za tiba kwa magonjwa ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono. Afua hizo ni pamoja na: kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU/UKIMWI; kutoa huduma za ushauri nasaha; upimaji; matunzo na huduma za dawa kwa wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI; huduma ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto; kuhamasisha wananchi kwenda kwenye vituo vya afya kupima na kupata chanjo ya kujikinga na maambukizi ya Homa ya Ini; na kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na kuhamasisha wananchi hususan wajawazito kupima maambukizi ya magonjwa ya ngono na kupata matibabu sahihi.

**87. Mheshimiwa Spika,** Nia ya Serikali ni kuhakikisha magonjwa hayo matatu yanatokomezwa ifikapo mwaka 2030. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali kupitia Wizara inajipima kupitia **Malengo ya Maendeleo Endelevu ambayo yanayojulikana kama 95-95-95**. Malengo hayo yanaelekeza kwamba; asilimia 95 ya watu wanaokadiriwa kuwa na VVU/UKIMWI wawe wamepima na wanatambua hali zao, asilimia 95 ya waliopima wawe wameanza dawa na asilimia 95 ya waliopo katika dawa wawe wamefubaza makali ya VVU. Malengo mengine ni pamoja na kupunguza maambukizi ya kaswende kwa asilimia 90; kupunguza maambukizi ya Kisonono kwa asilimia 90; kupunguza maambukizi ya kaswende ya kuzaliwa kwa watoto wachanga kufikia visa 50 au chini kwa kila watoto 100,000 waliozaliwa hai**.**

**88. Mheshimiwa Spika,** Kulingana na takwimu za utafiti wa viashiria vya UKIMWI (Tanzania HIV Impact Survey - THIS) ya mwaka 2022/23, inaonesha kuwa kiwango cha ushamiri wa **VVU kimepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/2017 hadi kufikia asilimia 4.4** mwaka 2022/2023 kwa watu wenye umri kuanzia miaka 15. Haya ni mafanikio makubwa sana katika mapambano

dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI nchini. Aidha, katika utafiti uliofanyika wa mwaka 2017 (THIS 2017) ulionyesha maambukizi ya Homa ya Ini aina ya B yapo kwa asilimia 4.1, aina ya C asilimia 1 ambapo kiwango kikubwa kimeonekana kwa wajidunga dawa za kulevya (6.3%).

**89. Mheshimiwa Spika,** Takwimu zilizokusanywa kutoka katika vituo vya afya vinavyotoa huduma za matunzo na matibabu kwa Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) zinaonesha kuwa, hadi kufikia Machi 2024, kulikuwa na watu 1,700,246 wanaokadiriwa kuishi na maambukizi ya VVU. Watu 1,643,840 kati ya 1,700,246 ya wanaokadiriwa kuishi na maambukizi ya VVU walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ikiwa ni sawa na **asilimia 96.7** ya watu wanaokadiriwa kuishi na Virusi vya UKIMWI nchini **(95 ya kwanza).** Aidha, watu 1,577,901 kati ya waliopima na kutambua hali zao za maambukizi walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, hii ikiwa ni sawa na **asimilia 96 (95 ya pili).** Katika kipindi hiki, jumla ya vipimo 389,095 vya kujua wingi wa Virusi vya UKIMWI kwa wagonjwa walioanza kutumia dawa vilifanyika ambapo kati ya vipimo hivyo, vipimo vya wagonjwa 369,807 sawa na **asilimia 95** walikuwa wamefubaza Virusi vya UKIMWI chini ya nakala 1,000 **(95 ya tatu).**
**Jedwali Na. 1** hapo chini linaonesha ufafanuzi huo.

**Jedwali Na. 1:** Mafanikio kuelekea kufikisha malengo ya 95-95-95

| Na. | Kiashiria | Machi 2023 | Machi 2024 | Hali ya 95-95-95 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi (PLHIV) | 1,729,408 | 1,700,246 | **95 ya kwanza** |
| | Wanaotambua hali zao za Maambukizi | 1,631,968 | 1,643,840 | |
| | Asilimia ya wanaotambua hali zao (on care) | **94.4** | **96.7** | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | Wenye maambukizi na wameanza dawa | 1,612,143 | 1,577,901 | **95 ya pili** |
| | Asilimia ya walioanza dawa (on ART) | **98.8** | **96** | |
| 3 | Idadi ya waliopimwa makali ya VVU (VL test) | 309,263 | 389,095 | **95 ya tatu** |
| | Idadi ya makali yaliyofubazwa | 298,657 | 369,807 | |
| | Asilimia ya waliofubazwa makali (VL<1000) | **96.6** | **95** | |

**90. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa **huduma kwa WAVIU zinasogezwa karibu zaidi na jamii,** Wizara kwa kushirikiana na Wadau wa maendeleo, imekuwa ikifanya jitihada za makusudi za kuhakikisha kila kituo cha afya nchini kinakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, idadi ya vituo vinavyotoa **huduma ya Tiba na Matunzo (CTC)** imefikia **vituo 7,396** kutoka vituo 7,072 mwaka 2022/23, hii ni sawa na asilimia 76.3 ya vituo vyote 9,693 vinavyotoa huduma za afya nchini. Lengo ni kufikia asilimia 95 ya vituo vyote vya afya viwe vinatoa huduma ya tiba na matunzo kwa WAVIU ifikapo mwaka 2025.

**91. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea **kupanua huduma za kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto** kwa kujumuisha huduma za kuzuia maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini aina 'B' katika afua hizo. Lengo la kujumuisha huduma hizo pamoja ni kutumia rasilimali za kuzuia maambukizi ya VVU kutokomeza maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini aina 'B' kwa watoto. Takwimu zinaonesha kwamba, jumla ya vituo 7,830 sawa na asilimia 96 ya vituo 8,164 vinavyotoa huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto viliweza kutoa huduma za kuzuia Maambukizi ya VVU na Kaswende kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, jumla ya **wajawazito 1,453,235 sawa na asilimia 97.4 ya wajawazito**

1,492,931 waliohudhuria kliniki walipimwa VVU katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ikilinganishwa na Wajawazito 1,627,685 sawa na asilimia 98.9 ya wajawazito 1,645,417 waliopimwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wajawazito 43,323 sawa na asilimia 2.98 ya wajawazito wote walibainika kuwa na maambukizi ya VVU kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ikilinganishwa na wajawazito 47,475 sawa na asilimia 2.85 waliobainika kuwa na maambukizi ya VVU kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**92. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wajawazito 38,951 sawa na asilimia 90 ya wajawazito waliobainika kuishi na maambukizi ya VVU waliunganishwa na huduma za matibabu ya dawa za kufubaza VVU (ARVs) ikilinganishwa na wajawazito 43,208 sawa na asilimia 91 ya wajawazito 47,475 waliobainika waliunganishwa na huduma za matibabu ya VVU kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**93. Mheshimiwa Spika,** Utoaji wa huduma kwa wajawazito unaenda sambamba na utoaji wa **huduma kwa watoto ili kumkinga na maambukizi ya VVU kutoka kwa mama**.
Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya watoto 27,808 sawa na asilimia 80 ya watoto 34,998 waliozaliwa na akina mama wanaoishi na maambukizi ya VVU walipimwa vinasaba vya VVU katika umri wa miezi miwili ikilinganishwa na watoto 31,021 sawa na asilimia 79 ya watoto 42,788 waliopimwa vinasaba vya VVU ndani ya umri wa miezi miwili katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Katika upimaji huo, watoto 307 sawa na asilimia 1.09 ya watoto 27,808 waliopimwa walibainika kuwa na maambukizi ya VVU na kuunganishwa na huduma za matibabu ya kufubaza VVU ikilinganishwa na watoto 334 sawa na asilimia 1.07 ya watoto 31,021 waliobainika kuwa na VVU katika umri wa miezi miwili kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23.

**94. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha **upatikanaji wa dawa kwa WAVIU** wote na vipimo vya maabara kwa WAVIU vinapatikana muda wote katika vituo vyote vya afya vinavyotoa huduma hiyo hapa nchini. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, WAVIU wote wameweza kupata dawa kwa asilimia 100. Pia WAVIU wameendelea kupata vipimo vya

maabara ili kuangalia mwenendo wa afya zao. Aidha, Wizara imeongeza idadi ya mashine za kupima wingi wa Virusi vya UKIMWI na maambukizi ya Virusi kwa watoto kutoka mashine 169 Juni 2023 hadi kufikia mashine 173 mwezi Machi 2024. Kati ya hizo, mashine 43 zipo kwenye vituo vya ngazi za Hospitali za Rufaa za Mikoa, Maabara ya Taifa na maabara maalum na 130 zipo katika Hospitali za wilaya na baadhi ya vituo vya Afya. Upimaji wa wingi wa VVU umeongezeka kutoka asilimia 90 kipindi kama hicho mwaka 2022/23 hadi kufikia asilimia 96 Machi 2024. Pia upimaji wa VVU kwa watoto (HEID) umeongezeka kutoka asilimia 79 kwa mwaka 2023 hadi asilimia 80 mwezi Machi mwaka 2024. Mafanikio haya yametokana na kuimarika kwa upatikanaji wa vitendanishi nchini, uwepo wa mashine zinazofanya kazi vituoni pamoja na maboresho yaliyofanyika kwenye usafirishaji wa sampuli.

**95. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha **ubora wa huduma** na takwimu kwa wapokea huduma katika vituo vya kutolea huduma za tiba na matunzo hapa nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau imechukua hatua madhubuti ya kuanzisha mfumo wa kuchukua alama za vidole kwa WAVIU (Biometric Registration) kwa ajili ya ufuatiliaji wa upokeaji huduma kwa kila MVIU ili kuhakikisha ufuasi wa dawa za kufubaza VVU na kuwezesha kuainisha mahitaji halisi ya watu walioko kwenye huduma. Hadi kufikia mwezi Machi 2024, vituo 2,447 kati ya vituo 7,396 sawa na asilimia 33 vinatumia mfumo huo. Aidha, wapokea huduma wapatao 881,297 kati ya 1,643,840 ambayo ni sawa na asilimia 56 wamesajiliwa.

**96. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kutoa elimu ya kujikinga dhidi ya maambukizi ya Homa ya Ini hapa nchini. Katika utafiti wa Tanzania "HIV Indicator Survey" wa mwaka 2022/23 umeonesha maambukizi ya Homa ya Ini aina ya B ni asilimia 3.5 na C ni asilimia 0.2. kulingana na hali hiyo Wizara imehuisha huduma ya Homa ya Ini kwenye Mpango wa Taifa wa kudhibiti UKIMWI ambapo Mpango huu umekuja na Mikakati ya kutokomeza ugonjwa wa wa Homa ya Ini ifikapo mwaka 2030. Mpango mkakati huo unalenga kuwafikia asilimia 60 ya wagonjwa wenye Homa ya Ini aina B au C ifikapo mwaka 2026 kwa kuwapatia huduma za kinga na tiba. Vile vile huduma za

upimaji wa Virusi vya Homa ya Ini zinaendelea kutolewa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali zote za kanda, Rufaa na za Wilaya. Sambamba na hilo Wizara imeshaandaa miongozo mbalimbali itakayosimamia huduma hizi za Homa ya Ini ili watumishi wa afya waweze kutoa huduma bora kwa watakaobainika kuwa wana Virusi vya Homa ya Ini kulingana na viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO). **'Nitoe rai kwa wananchi kujitokeza kupima hali ya maambukizi ya Homa ya Ini katika vituo vya kutolea huduma za afya ili wale ambao watakuwa hawajaambukizwa waweze kupatiwa chanjo ya Homa ya Ini'.**

**Mapambano Dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma**

**97. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa **huduma za Kifua Kikuu na Ukoma** sanjari na Mpango Mkakati wa Sita (2020/21-2025/26) wa mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma. Malengo makuu ya mpango huu ni: kupunguza maambukizi mapya ya Kifua Kikuu kwa asilimia 50; kupunguza vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu kwa asilimia 75 na kutokomeza Ukoma katika Halmashauri zenye wagonjwa wa Ukoma ifikapo mwaka 2025.

**98. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Machi 2024, Tanzania ilikuwa imepunguza **maambukizi mapya ya Kifua Kikuu** kwa **asilimia 36** kutoka wagonjwa 306 kwa kila watu 100,000 mwaka 2015 hadi kufikia wagonjwa 195 kwa kila watu 100,000 kwa mwaka 2023. Aidha, takwimu zinaonyesha **vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu vimepungua kwa asilimia 67 kutoka vifo 56,000 mwaka 2015 hadi vifo 18,000 mwaka 2023** na hivyo kuwa kwenye njia sahihi ya kufikia lengo la kupunguza maambukizi kwa asilimia 50 na vifo kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2025.

**99. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara ilipanga **kuibua wagonjwa wapya wa Kifua Kikuu 58,052** ambapo wagonjwa 56,023 waliibuliwa ikiwa ni sawa na asilimia 96 ya lengo. Kwa kipindi cha 2022/23, jumla ya wagonjwa 74,418 sawa na asilimia 100.1 waliibuliwa ikilinganishwa na lengo la kipindi hiki la kuibua wagonjwa 74,513. Mafanikio haya

yametokana na kuwashirikisha watoa huduma ngazi ya jamii hasa wale waliougua kifua kikuu na kupona, waganga wa Tiba Asili na sekta binafsi. Aidha, asilimia 95 ya wagonjwa wa Kifua Kikuu walioanzishiwa matibabu kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 walitibiwa na kupona ikilinganishwa na asilimia 92 kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Aidha, Wizara inaendelea na ufuatiliaji wa kimkakati wa karibu kwa wagonjwa vituoni na ushirikishwaji wa watoa huduma katika ngazi ya jamii kusimamia umezaji dawa na kufikia lengo la Shirika la Afya Duniani (WHO) la kuponyesha zaidi ya asilimia 90 ya wagonjwa wanaoanza matibabu. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wagonjwa 194 wa Kifua Kikuu Sugu waligundulika na kuanzishiwa matibabu ambao ni sawa na asilimia 43 ya lengo la kugundua wagonjwa 453 ikilinganishwa na wagonjwa 266 waliogundulika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 sawa na asilimia 40 ya lengo la kuibua wagonjwa 664 wa Kifua Kikuu Sugu.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha **huduma za upimaji wa Kifua Kikuu**, Serikali kupitia Wizara ya Afya imenunua mashine za upimaji za **GeneXpert 75** na **Truenat 110** ambazo zitasimikwa kwenye vituo **110** vya kutolea huduma za afya vya ngazi ya msingi na Hospitali mpya za Halmashauri **70** ambazo zitafanya jumla ya **GeneXpert na Truenat** kufikia **411 na 152** mtawalia. Wizara imeendelea kutoa **huduma mkoba** za kliniki tembezi zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya Kifua Kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla wateja 11,605 walichunguzwa na kupimwa kifua kikuu ambapo wateja 3,172 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu ikilinganishwa na kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, ambapo jumla ya watu 8,298 walichunguzwa na kupimwa Kifua Kikuu, kati yao wagonjwa 2,368 sawa na asilimia 29 waligundulika kuwa na ugonjwa wa Kifua Kikuu na kuanzishiwa matibabu. Vilevile, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za utoaji wa elimu juu ya ugonjwa wa Kifua Kikuu kwa jamii kupitia mifumo mbalimbali ya utoaji elimu hasa redio za jamii, mitandao ya kijamii pamoja na runinga.

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanzisha huduma ya utoaji wa dawa kinga ya Kifua Kikuu kwa kutumia Dawa Mseto za muda mfupi  za Rifapentine na Isonizid (3HP) ambazo mnufaika atapewa na kuz itumia kwa muda wa miezi mitatu mara moja kwa wiki na Rifampicin na Isoniazid (3HR) kwa watoto chini ya umri wa miaka 15 kwa miezi mitatu badala ya dawa tiba kinga zilizokuwa zikitumika za aina ya Isoniazid kwa kila siku kwa kipindi cha miezi sita. Afua hii itapunguza sana wanufaika walio katika makundi hatarishi ya kuugua ugonjwa wa Kifua Kikuu hasa watu wanaoishi na maambukizi wa virusi vya Ukimwi, watoto wadogo, watu wanaoishi na mgonjwa wa Kifua Kikuu, wajidunga na wachimbaji wa madini wenye magonjwa ya mapafu ili wasipate ugonjwa wa Kifua Kikuu.

**102. Mheshimiwa Spika**, Katika jitihada **za kutokomeza Ukoma nchini**, Wizara imeendelea kusimamia huduma za uchunguzi na kutoa tiba kwa wale wanaogunduliwa kuwa na Ugonjwa wa Ukoma. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wagonjwa 761 waligundulika na ugonjwa wa Ukoma ikilinganishwa na wagonjwa 1,227 waliogundulika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Sambamba na uibuaji huu, wana Kaya 847 walifanyiwa uchunguzi ambapo jumla ya wagonjwa 28 waliibuliwa na kuanzishiwa matibabu. Aidha, Wizara imeendelea kutoa vifaa tiba saidizi kwa kugawa jozi za viatu maalum 240 ili kupunguza athari za ulemavu kwa waathirika wa Ukoma.

**Mapambano Dhidi ya Malaria**

**103. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitano wa kipindi cha 20212025 wenye lengo la kupunguza maambukizi ya Malaria kutoka asilimia 7.5 kwa mwaka 2017 hadi chini ya asilimia 3.5 mwaka 2025. Pamoja na hilo, Serikali imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ikiwepo ugawaji wa vyandarua kwa makundi maalum (kina mama wajawazito, Watoto na watu wenye ulemavu), upuliziaji wa viuatilifu ukoko na kuhakikisha dawa za kutibu Malaria zinapatikana kwa kipindi chote bila malipo katika vituo vya kutolea huduma ili kuwakinga wajawazito, watoto chini ya miaka mitano na jamii kwa ujumla dhidi ya ugonjwa wa Malaria.

**104. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, **vipimo vya haraka vya Malaria** (mRDT) 24,171,900 na vichupa 1,755,363 vya dawa ya sindano ya kutibu Malaria kali vilinunuliwa na kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na vipimo vya mRDT 22,578,350 na vichupa 2,890,242 vya dawa ya sindano ya kutibu Malaria kali kwa mwaka 2022/23. Pia, Dawa na vitendanishi vimeendelea kusambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kupitia Bohari ya Dawa (MSD) kulingana na mahitaji ya vituo. Kwa kipindi hiki, utoshelevu wa dawa za Malaria ni asilimia 98 ambayo ni sawa na upatikanaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23.

**105. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha 2023/24 jumla ya **vyandarua vyenye dawa 14,269,970** vimenunuliwa, ikilinganishwa na vyandarua 6,119,732 vilivyonunuliwa katika kipindi hiki mwaka 2022/23. Vyandarua hivyo vimesambazwa kupitia wanafunzi wa shule za msingi katika mikoa 13 ambayo ni; Rukwa, Njombe, Songwe, Mbeya, Dar es Salaam, Singida, Kigoma, Katavi, Geita, Mara, Mwanza, Lindi na Mtwara. Aidha, vyandarua hivyo vimesambazwa pia kupitia kliniki za wajawazito na watoto chini ya mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma za afya nchi nzima na kwa njia ya kampeni kwenye kaya zote katika Halmashauri 19 za mikoa ya Tabora, Kagera na Simiyu.

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza **mradi wa kuelekea utokomezaji wa Malaria** (Towards Elimination of Malaria in Tanzania-TEMT) unaotekelezwa katika Halmashauri tatu za Mkoa wa Tanga ambazo ni Handeni Lushoto na Tanga Jiji. Katika kipindi cha 2023/24, jumla ya lita 19,880 za viuadudu vya kibaiolojia zilinunuliwa kutoka kiwanda cha Kibaha cha Tanzania Biotech Product Limited (TBPL) na kusambazwa kwa Halmashauri hizo tatu. Jumla ya mazalia 9,850 yenye eneo linalokadiriwa kuwa mita za mraba 352,438 yamenyunyiziwa viuadudu ili kuua viluilui vya mbu.

**107. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa **Afua ya kutokomeza Malaria** katika maeneo yenye kiwango cha chini cha maambukizi, ambapo Ufuatiliaji wa Ugonjwa wa Malaria hufanyika hadi katika Ngazi ya Kaya

(Malaria Case Based Surveillance - MCBS) na kufanya tathmini katika Halmashauri 29 za mikoa ya Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Njombe na Iringa. Katika utekelezaji wa Afua hii, wagonjwa wanaogundulika kuwa na maambukizi ya Malaria katika vituo vya kutolea huduma za Afya hufuatiliwa mpaka katika kaya zao ambapo wanakaya hupimwa na kutibiwa pale wanapobainika kuwa na maambukizi ya Malaria. Idadi ya wagonjwa wanaofuatiliwa na wanakaya wanaopimwa Malaria imeongezeka ambapo kwa kipindi cha mwaka 2023/24, jumla ya wagonjwa 2,501 na wanakaya 7,431 walipimwa Malaria. Watu 152, sawa na asilimia 2, walikutwa na maambukizi ya Malaria na kupewa matibabu, ikilinganishwa na wagonjwa 1,401 waliofuatiliwa na wanakaya 1,518 waliopimwa Malaria, ambapo watu 54, sawa na asilimia 3.6, walibainika kuwa na maambukizi ya Malaria na kupewa matibabu katika kipindi cha 2022/23.

**108. Mheshimiwa Spika,** Wizara imewajengea uwezo **Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii (CHWs) 300,** juu ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kudhibiti Malaria katika Halmashauri zote za mikoa tisa (9) ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Geita, Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa na Kagera. Aidha, matangazo 1,817 ya Redio kuhusu elimu na ujumbe wa kinga, matibabu sahihi ya dawa za Malaria yamerushwa katika vituo vitatu vya Kitaifa na radio za kijamii katika Mikoa saba (7) yenye kiwango cha juu na cha kati cha mambukizi ya Malaria ambayo ni: Lindi, Tabora, Kagera, Katavi, Mara, Tanga na Geita. Matangazo 390 ya picha mnato yamerushwa katika vituo vitatu vya runinga na uelimishaji kupitia ujumbe wa mitandao ya kijamii umefanyika. Aidha, ili kuendelea kufikisha zaidi elimu na ujumbe wa Malaria katika ngazi za chini zaidi, uhamasishaji kupitia njia za kijamii ukihusisha matangazo ya magari, elimu - burudani na Ushirikishwaji wa Asasi za Kijamii katika kutoa elimu umefanyika katika mikoa 15 ya Tabora, Mtwara, Lindi, Mara, Geita, Shinyanga, Simiyu, Kagera, Kigoma, Katavi, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Tanga na Pwani; na michoro ya kudumu yenye ujumbe wa "Ziro Malaria inaanza na mimi" imewekwa katika Halmashauri tatu kwa kila mkoa katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.


## HUDUMA ZA DAWA, VIFAA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

**109. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika **upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara** kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) hununua, hutunza na husambaza aina mbalimbali za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya maabara. Kati ya hizo, aina 290 zimeainishwa kuwa ni bidhaa za afya muhimu na za kipaumbele hivyo Wizara ina lengo la kuhakikisha kuwa bidhaa hizi zinapatikana wakati wote katika Bohari ya Dawa (MSD). Aidha, Serikali imepeleka MSD kiasi cha **Shilingi 103,333,333,343.67** sawa na asilimia 50.3 ya bajeti ya Shilingi 205,000,000,000 iliyoidhinishwa kwa ajili ya ugharamiaji wa mnyororo mzima wa upatikanaji wa bidhaa za afya. Aidha, vituo vya kutolea huduma za afya kupitia **fedha za uchangiaji vimepeleka MSD kiasi cha Shilingi 57,528,128,119.49** na kufanya jumla ya fedha zilizopelekwa MSD kwa ajili ya ugharamiaji wa bidhaa za afya kufikia Shilingi 160,861,461,463.16. Pia katika kuijengea uwezo MSD kuwa na dawa na bidhaa za afya, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi 100,000,000,000** ikiwa ni sehemu ya **mtaji wa MSD** kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa dawa nchini.

**110. Mheshimiwa Spika**, Kupatikana kwa fedha hizo kumewezesha **upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele aina 290** kuongezeka kutoka wastani wa asilimia 73 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2023 hadi kufikia wastani wa **asilimia 79** katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya kufikia Machi 2024. Hali ya upatikanaji wa dawa kwenye Zahanati ni asilimia 71, Vituo vya Afya ni asilimia 57, Hospitali za Wilaya ni asilimia 73, Hospitali za Rufaa za Mikoa ni asilimia 94 na Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa ni asilimia 90.
Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2022/23, Wizara ilifanya mapitio ya bidhaa muhimu za kipaumbele 290 kwa lengo la kuendelea kuboresha upimaji wa bidhaa hizo vituoni. Kufuatia mapitio hayo, kwa sasa Zahanati zinapimwa kwa aina 100 ya bidhaa za afya; Vituo vya Afya aina 178, Hospitali za Halmashauri aina 203; Hospitali za Rufaa za Mikoa aina 245 na Hospitali za

Kanda na Taifa ni aina 290. Upimaji huo pia umezingatia mahitaji ya Hospitali Maalum kama JKCI, ORCI, Mirembe na Kibong`oto.

**Kielelezo Na. 1.** Hali ya Upatikanaji wa Bidhaa za Afya katika Vituo vya kutolea Huduma nchini.




**111. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha **upatikanaji wa dawa za hydroxyurea na Anti D injection bila malipo** kwa makundi maalum, Wizara imesambaza dawa ya hydroxyurea kiasi cha dozi 49,720 zenye thamani ya Shilingi 100,000,000 kwa watoto wenye ugonjwa wa Seli mundu (Sickle Cell) pamoja na dawa aina ya Anti D injection kiasi cha dozi 2,889 zenye thamani ya kiasi cha Shilingi 200,000,000 kwa ajili ya akina mama wajawazito wenye kundi la damu la Rhesus negative wanaokadiriwa kufikia asilimia moja ya wajawazito wote kila mwaka ambapo sindano hii inatolewa bila malipo.

**112. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia watumishi wake waliopo katika kanda za Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kufanya ufuatiliaji wa bidhaa za afya zilizopo katika hatari ya kuchotora (Expire) hasa za miradi misonge na kutekeleza afua za kuzinusuru dawa hizo kwa kuhakikisha ulinganifu wa upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini na kushauri Bohari ya Dawa kufanya "inter-zonal transfers". Aidha, Wizara ilifanya tathmini ya uanzishwaji na uendeshaji wa maduka ya dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Tathmini ilionyesha kuwa Hospitali za Rufaa za Mikoa 12 tayari

zimeshaanzisha maduka hayo na yanafanya kazi, Hospitali tatu (3) za Rufaa za Mikoa zipo katika hatua za mwisho za uanzishaji na Hospitali 14 bado hazijaanzisha maduka hayo. Nia ya Wizara ni kuhakikisha Hospitali zote za Rufaa za Mikoa zinakuwa na maduka haya ya dawa, hii ikiwa ni mojawapo ya mkakati wa wizara wa kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana wakati wote katika Hospitali hizo za rufaa.

**113. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza makubaliano ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika kutoa kipaumbele kwenye **mapambano ya Usugu wa Vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa**. Katika kutekeleza makubaliano hayo Wizara inafanya usimamizi na uratibu wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa(culture and susceptibility test for AntiMicrobial Resistance and Survaillance-AMR). Wizara imesimamia uanzishwaji wa timu za usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya dawa za antibiotiki kwa Hospitali 20 nchini, hilo limeenda sambamba na kuimarisha ufuatiliaji wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa kwa kuanzisha utaratibu wa kukusanya taarifa kwa Hospitali 9 ili kusaidia katika maandalizi ya National antibiograms kwa ajili ya kutoa mwongozo wa matibabu ya vimelea nchini.

**114. Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanya ufuatiliaji wa matumizi ya **dawa za antibiotiki katika ngazi ya Hospitali** kwa kutumia WHO Point prevalence survey ambapo matokeo yameonyesha matumizi ya antibiotiki kwa wagonjwa waliolazwa ni wastani wa asilimia 62.7 hadi asilimia 87 ikilinganishwa na kiwango cha Shirika la Afya Dunia (WHO) inayosema isizidi asilimia 30 ya matumizi ya antibiotiki kwa wagonjwa wanaoenda kutibiwa. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine kwenye suala la usugu wa dawa imeweza kufanya utafiti kwa baadhi ya dawa za antibiotiki ili kuona kama zinaweza kutibu vimelea (Antibiotic Susceptibility Testing). Tathmini kupitia mfumo huo imeonesha kuna matumizi makubwa ya dawa za antibiotiki nchini na baadhi zimefikia usugu wa asilimia 56.1 hivyo juhudi za pamoja kukabiliana na janga hili zinahitajika. Aidha, Wizara imejipanga kupambana na usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya matumizi holela ya dawa kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kuja na kampeni itakayozinduliwa

tarehe 25 Mei, 2024 yenye kauli mbiu ya **"HOLELA HOLELA ITAKUKOSTI".**

**115. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza sera ya viwanda, Serikali ya awamu ya sita (6) imeendelea kutengeneza **mazingira bora na rafiki ya uwekezaji** katika eneo la **uanzishaji wa viwanda vya bidhaa za afya** kwa wawekezaji wa ndani na wa nje, ili kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za afya nchini na kupunguza utegemezi na uchelewaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2024, kulikuwa na jumla ya viwanda 13 vya kutengeneza dawa za binadamu, ikiwa ni ongezeko la viwanda viwili ambavyo ni Cure Afya na Katwaza Pharmaceutical Industry. Aidha, viwanda vya kuzalisha vifaa tiba vidogo kwa vikubwa vimefikia 54 na pia viwanda viwili (2) kwa ajili ya kuzalisha vitendanishi vimeanzishwa kikiwepo kiwanda pekee Afrika Mashariki na Kati cha kuzalisha vitendanishi vya hematolojia (Diluent, Lyse na Distilled water). Katika kuviwezesha viwanda vya dawa nchini, Serikali kupitia MSD imeendelea kununua bidhaa zinazozalishwa nchini, kati ya Julai 2023 hadi Machi 2024 bidhaa zenye thamani ya Shilingi 16,920,000,000 zimeweza kununuliwa kutoka katika viwanda.

## HUDUMA ZA UCHUNGUZI WA MAGONJWA

**116. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua umuhimu wa huduma za uchunguzi wa Magonjwa kama nguzo muhimu katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya. Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa Magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwekeza kwenye maeneo makuu matatu ambayo ni huduma za maabara, Radiolojia na matengenezo ya vifaa tiba.

**117. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa **huduma za maabara**, hadi kufikia Machi 2024 jumla ya maabara zote nchini ni 10,782. Kati ya hizo, maabara 6,827 ni za Serikali na 3,955 ni za binafsi. Katika kipindi hiki, maabara zilizopata ithibati ya kimataifa kwa Hospitali ngazi ya Taifa ni (2), Maalum (4), Kanda (4), Mkoa (26),

Halmashauri na binafsi (39) ambapo vipimo vinavyofanyika katika maabara hizo vinaaminika na kukubalika duniani kote. Wizara inaendelea kuzijengea uwezo maabara zilizobaki za binafsi na za umma kufikia viwango vya Kimatafa.

**118. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeandaa miongozo sita (6) inayoelekeza namna ya kupima, kutafsiri matokeo ya vipimo na kuripoti majibu ya mgonjwa kwa usahihi ili kuongeza kasi ya ubora wa huduma za Maabara katika ngazi zote. Miongozo hiyo imesaidia kuhakikisha kuwa majibu ya vipimo yanatolewa kwa usahihi ikilinganishwa na hapo awali ambapo majibu ya Maambukizi kwa njia ya mkojo (UTI), Homa ya tumbo (Typhod) na Malaria yalikuwa na changamoto. Pia, Serikali imesimika jumla ya mashine za maabara zilizosanifishwa 2,405 ambapo mashine za Hematolojia 891, Kemia 746 na Mkojo 768 katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**119. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za Radiolojia** nchini kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imenunua na kusimika vifaa vya Radiolojia katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini ambapo **mashine za Digital X-Ray** zenye thamani ya Shilingi 875,750,006 zimenunuliwa na kufanya kuwa na jumla ya Digital X-Ray 349. Mashine hizo zinatarajiwa kusimikwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma-Maweni, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora-Kitete na Hospitali ya Mission ya Mbozi – Moravian.

**120. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha ununuzi wa **Ultrasound 125** zenye gharama ya Shilingi 4,695,000,000 ambapo zimesimikwa na kuanza kutoa huduma katika vituo vya kutolea huduma za Afya na Vyuo vya mafunzo ya wataalaam wa mionzi na picha na hivyo kuwa na jumla ya Ultrasound 677. Aidha, hadi kufikia Machi 2024 usimikaji wa jumla ya **mashine za CT scan 27** ulikuwa umekamilika na huduma kuanza kutolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo jumla ya vipimo 44,646 vilikuwa vimefanyika. Vilevile, kwa upande wa MRI usimikaji ulikamilika na kuwezesha jumla ya **vipimo 18,056** kufanyika katika ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum. Pia, Wizara imezindua kituo cha kitaifa cha

mafunzo kazini ya matengenezo ya vifaa na vifaa tiba kilichopo mkoani Dodoma. Vilevile, Wizara imejenga karakana tatu (3) zilizopo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Iringa, Arusha - Mt. Meru na Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga.

**Huduma za Damu Salama**

**121. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu ya kuhakikisha **damu salama** inapatikana kwa wakati na ya kutosha ili kuokoa maisha ya wagonjwa wenye uhitaji mkubwa wa damu wakiwemo akinamama wajawazito haswa wakati wa kujifungua, watoto walio chini ya miaka mitano, wagonjwa wa upasuaji pamoja na wagonjwa wa dharura wanaopata ajali na kuhitaji damu. Wizara inahakikisha upatikanaji wa damu salama unakuwa wa kuridhisha kwa kukusanya damu kutoka kwa wachangiaji damu wa hiari wenye afya njema na wasio kwenye makundi hatarishi. Aidha, Wizara hupima sampuli za damu zilizokusanywa kwa kutumia vipimo vya maabara vyenye viwango vya kimataifa vyenye uwezo wa kugundua maambukizi kwa muda mfupi tangu mtu ameambukizwa magonjwa kama Homa ya Ini, Kaswende na VVU pamoja na kupima makundi ya damu.

**122. Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2024, Wizara imefanikiwa **kukusanya chupa za damu 352,821** sawa na asilimia 89.7 ya lengo la kukusanya chupa 590,000. Idadi hii ni sawa na ongezeko la chupa 48,718 ikilinganishwa na chupa za damu zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, Serikali imeongeza vituo 3 vya kutengeneza **Mazao ya Damu** kama vile majimaji ya damu (Fresh Frozen Plasma-FFP), chembe sahani za damu (Platelets), na kufanya kuwa na jumla ya vituo 18 kutoka vituo 15 vilivyokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama, imeweza kutengeneza chupa 20,800 ikilinganishwa na chupa 25,658 za mazao ya damu aina ya Plasma (FFP) zilizotengenezwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23 ambazo zilitumika kusaidia akinamama wanaopata matatizo ya kutokwa na damu nyingi wakati wakijifungua, na chupa 6,197 za chembe sahani (Platelets) zilizotumika kutibu wagonjwa wa saratani, sikoseli (Seli Mundu) pamoja na wagonjwa waliokuwa na matatizo mengine

ikilinganishwa na chupa 6,625 za chembe sahani zilizotengenezwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii**

**123. Mheshimiwa Spika,** Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ni ngazi ya juu ya rufaa kwa sampuli za magonjwa ya mlipuko na yanayojirudia. Majukumu ya msingi ya Maabara hii ni pamoja na; Kutoa mafunzo kwa wataalam wa maabara zinazokusanya sampuli za magonjwa ya mlipuko; Kuratibu zoezi la ugatuzi wa upimaji wa magonjwa ya milipuko (Decentralization) na kuanzisha kituo cha uchambuzi wa anuai za magonjwa ya mlipuko (Gene sequencing); Kuwa kituo kikuu cha upimaji wa UVIKO-19 na utoaji wa vyeti kwa wasafiri nje ya nchi; Kuanzisha kituo cha "National Calibration Centre"; Kutoa huduma za rufaa za uchunguzi wa VVU na magonjwa mengine; Kutoa mafunzo kazini kwa Wataalam wa maabara; Kuandaa na kutoa sampuli za kupimia ubora; Kufanya tathmini ya teknolojia mpya za upimaji; na Kufanya ufuatiliaji wa magonjwa mapya na ya milipuko. Aidha, kwa kuwa maabara hii inahusisha upimaji wa sampuli za magonjwa ya hatari kama Ebola, Maburg, UVIKO – 19 maabara hii ilijengwa kwa kujumuisha viwango vya kiusalama daraja la tatu (Biosafety Level 3) kulingana na vigezo vya kimataifa ili kuweza kuchakata sampuli hizo.

**124. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 mpaka Machi 2024, Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii imefanikiwa kupima jumla ya **sampuli 14,636** za magonjwa mbalimbali ya milipuko ambapo kati ya sampuli hizo, sampuli 2,051 zilikutwa na maambukizi na sampuli 12,585 zilikuwa hazina maambukizi. Baadhi ya sampuli hizo ni pamoja na sampuli 226 za ugonjwa wa **Kipindupindu** ambapo zenye maambukizi zilikuwa ni 147 na zisizo na maambukizi zilikuwa sampuli 79, Sampuli za ugonjwa wa **Surua** 2,041, zenye maambukizi 548 zisizo za maambukizi 1,493, **Rubella** sampuli 1,903 zenye maambukizi 137 zisizo na maambukizi ni 1,766, **Rotavirus** sampuli 489 zenye maambukizi 87 na zisizo na maambukizi ni 402, **Mafua makali** sampuli 9,167 ambapo sampuli 692 zilikutwa na influenza na sampuli 430 zilikutwa na **UVIKO-19**, Vilevile sampuli 14 za **Marburg** zilichunguzwa ambapo sampuli 10

zilikuwa na maambukizi na sampuli nne (4) hazikuwa na maambukizi. Pamoja na upokeaji wa sampuli kutoka kwenye kanda na mikoa mbalimbali, Maabara ya Taifa pia imeendelea kuandaa na kutuma sampuli za ubora kwa vituo 150 nchi nzima kwa ajili ya kuhakiki ubora wa huduma zinazotolewa na Maabara nchini ikiwemo kuendelea kupata na kudumisha ithibati za ubora wa huduma za maabara.

**125. Mheshimiwa spika,** Wizara imefanikiwa kusimika mashine kwa ajili ya upimaji wa ugonjwa wa Kansa ya Shingo ya kizazi "Alinity-M" yenye thamani ya kiasi cha dolla za kimarekani 165,000. Hatua za uthibitishaji wa mashine hii zinaendelea na pindi utakapokamilika itaanza rasmi uchunguzi wa ugonjwa huo. Aidha, katika kipindi hiki Maabara imeweza kuchaguliwa na African CDC kuwa kituo cha umahiri cha ulinzi na usalama wa vimelea kwa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati ambapo kituo kimefanikiwa kutoa mafunzo ya ulinzi na usalama wa vimelea kwa wataalam kutoka nchi 14 za Afrika ambazo ni Zambia, Malawi, Kenya, Uganda, Somalia, Zimbabwe, Rwanda, Comoro, Ushelisheli, Afrika ya Kusini, Madagascar, Djibouti, Sudani ya Kusini, Ethiopia na Mali. Vilevile, Maabara ya Taifa imeweza kufanyiwa tathmini na Shirika la Afya Duniani ili kuwa na uwezekano wa kupima ugonjwa wa Polio nchini ambao umekuwa ukipimwa nchini Uganda.


## UTOAJI WA HUDUMA ZA TIBA

**126. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma bora za afya zinazotolewa na watoa huduma wenye weledi na ujuzi, pamoja na uboreshaji wa miundombinu ya vituo vilivyopo lakini pia imeendelea kujenga vituo vipya ili kuleta huduma karibu kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 **vituo vya kutolea huduma vimeongezeka kufikia 12,266** kutoka vituo 11,040 vilivyokuwepo mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la vituo 1,226 ambayo ni asilimia 10.1.

**127. Mheshimiwa Spika,** Ongezeko hilo la vituo limewezesha kupunguza umbali ambao wananchi hutembea kufuata huduma za afya ambapo kwa sasa asilimia 80 ya wananchi wanapata

huduma za afya ndani ya wastani wa kilometa 5. Kati ya vituo hivyo 12,266, Vituo vya umma vilikuwa 7,375 sawa na asilimia 60.1 na binafsi ni 4,891 sawa na asilimia 39.9 ya vituo vyote nchini. Kwa ujumla Hospitali ni 444 sawa na asilimia 4.6, Vituo vya Afya ni 1,187 sawa na asilimia 12.2, Zahanati ni 8,062 sawa na asilimia 83.2 na kufanya jumla ya Hospitali, Vituo vya afya na Zahanati kufikia 9,693. Aidha, vituo vingine ni kliniki 970, Maabara Binafsi 1,499 na vituo vinginevyo 104. Hii ni kulingana na takwimu zinazopatikana katika mfumo wa kusajili Vituo vya kutolea huduma za Afya (Health Facility Registry - HFR). Vilevile, zaidi ya vituo 1,324 vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi na vitakapokamilika vitasaidia kupunguza umbali ambao wananchi wamekuwa wakitembea kufuata huduma za afya hapa nchini.

**Kielelezo Na. 2.** Idadi na Mgawanyo wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya nchini.




**128. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa wananchi na imeendelea kuhakikisha inaongeza upatikanaji wa huduma ambapo kufikia mwezi Machi 2024 kulikuwa na jumla ya **vitanda 145,374** sawa na ongezeko la asilimia 15.3 ikilinganishwa na **vitanda 126,036**

vilivyokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, kati ya vitanda 145,374 vitanda 47,177 vipo katika ngazi ya Hospitali, vitanda 34,328 vipo katika Vituo vya Afya, vitanda 42,390 vipo katika Zahanati na vitanda 21,539 vinapatikana katika kliniki na vituo vinginevyo kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 2:** Mchanganuo wa idadi ya vitanda katika vituo vya kutolea huduma za Afya hadi kufikia Machi 2024.

| Ngazi ya kituo | Vinavyohitajika | Vilivyopo Wodini | Vitanda vya Kujifungulia | Vitanda vya uchunguzi | Jumla ya Vitanda |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 58,185 | 32,272 | | 3,674 | 47,117 |
| Vituo vya | 38,498 | 17,118 | 11,171<br>13 ,124 | 4,086 | 34,328 |
| Zahanati | 42,969 | 9,756 | 20,971 | 11,663 | 42,390 |
| Kliniki | 18,013 | 16,762 | 2,552 | 2,225 | 21,539 |
| **Jumla** | **157,665** | **75,908** | **47,818** | **21,648** | **145,37** |

**4**

**129. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi ambapo, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya mahudhurio **38,031,200** ya wateja walipata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya hapa nchini ikilinganishwa na wateja 35,873,466 waliopata huduma katika vituo hivyo kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati yao, asilimia 6.46 walipata huduma katika ngazi ya Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda, asilimia 12.42 ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, asilimia 14.80 Hospitali za Wilaya, na asilimia 19.35 vituo vya afya na asilimia 38.26 katika zahanati **(Jedwali Na. 3)**. Takwimu za utoaji wa huduma za afya zinaonesha takriban asilimia 82.1 ya wananchi wanapata huduma katika ngazi ya afya ya msingi.

**Jedwali Na. 3: Idadi ya wagonjwa katika vituo vya huduma za afya Julai 2023 hadi Machi 2024.**

| **Aina ya kituo** | **Wagonjwa wa nje** | **Wagonjwa waliolazwa** | **Jumla kuu** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Taifa, Maalum na Kanda | 2,225,089 | 231,857 | 2,456,946 | 6.46 |
| Ngazi ya Mkoa | 4,326,914 | 398,035 | 4,724,949 | 12.42 |
| Ngazi ya wilaya | 5,139,509 | 490,595 | 5,630,104 | 14.80 |
| Vituo vya afya | 6,926,608 | 434,125 | 7,360,733 | 19.35 |
| Zahanati | 14,541,888 | 8,553 | 14,550,441 | 38.26 |
| Kliniki | 2,209,503 | 178 | 2,209,681 | 5.81 |
| Nyinginezo | 998,470 | 99,876 | 1,098,346 | 2.89 |
| **Jumla** | **36,367,981** | **1,663,219** | **38,031,200** | **100** |

**130. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) wenye umri chini ya miaka mitano** yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (asilimia 37.97), kuharisha pasipo kupungukiwa maji mwilini (asilimia 9.45) na Malaria (asilimia 9.44). Kwa **umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa yaliyoongoza** yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa (asilimia 17.97), Maambukizi katika njia ya mkojo (asilimia 15.9) na Shinikizo la juu la damu (asilimia 5.96). **Idadi ya wagonjwa wenye magonjwa yasiyoambukiza imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka** kwa mfano, mwaka 2022/23 shinikizo la juu la damu ilishika nafasi ya nne (4) na Kisukari nafasi ya nane (8) kati ya magonjwa kumi yaliyoongoza kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**. Kwa mwaka 2023/24 magonjwa hayo yamepanda hadi kushika nafasi ya tatu (3) na saba (7) mtawalia.

**Jedwali Na. 4:** Mchanganuo wa idadi ya Mahudhurio ya nje (OPD) kwa magonjwa yote katika ngazi za zote huduma za afya

| **Wagonjwa wa nje wenye umri zaidi ya miaka mitano** | | | **Wagonjwa wa nje wenye umri chini ya miaka mitano** | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** | **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** |
| Maambukizi katika Mfumo wa | 2,224,817 | 17.97 | Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 2,460,844 | 37.97 |
| Maambukizi katika Njia ya | 1,968,564 | 15.9 | Kuharisha pasipo kupungukiwa maji | 612,335 | 9.45 |
| Shinikizo la juu la Damu | 737,730 | 5.96 | Malaria | 611,587 | 9.44 |
| Malaria | 725,031 | 5.86 | Maambukizi katika | 488,614 | 7.54 |
| Vidonda vya tumbo | 482,086 | 3.89 | Kichomi kikali | 448,804 | 6.92 |
| Other Non-Infectious GIT | 404,404 | 3.27 | Other Non-Infectious GIT | 270,207 | 4.17 |
| Kisukari | 333,567 | 2.69 | Magonjwa ya | 245,525 | 3.79 |
| Kichomi kikali | 324,616 | 2.62 | Minyoo ya tumbo | 193,722 | 2.99 |
| Minyoo ya tumbo | 285,791 | 2.31 | Kuhara na upotevu wa maji | 166,595 | 2.57 |
| Rheumatoid and Joint Diseases | 281,238 | 2.27 | Magonjwa ya ngozi | 153,548 | 2.37 |

**131. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki **magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa waliolazwa (IPD)** wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni Kichomi kikali asilimia 23.87, Malaria asilimia 18.9 na Kuhara kulikopelekea kuishiwa maji mwilini asilimia 17.83. Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wenye umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni Malaria asilimia 13.74, Magonjwa ya mfumo wa mkojo asilimia 9.31 na Shinikizo la juu la damu asilimia 8.81 **(Jedwali Na. 5).** Kama ilivyokuwa kwa wagonjwa wa nje, magonjwa yasiyoyakuambukiza yamekuwa yakiongezeka hata kwa wagonjwa waliolazwa ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la wagonjwa wa ajali na mivunjiko.

**Jedwali Na. 5:** Magonjwa yalioongoza kwa wagonjwa wa kulazwa chini ya umri wa miaka mitano na umri zaidi ya miaka mitano.

| | **Wagonjwa wa kulazwa wenye umri zaidi ya Miaka Mitano** | | | **Wagonjwa ya kulazwa wenye umri chini ya Miaka Mitano** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na.** | **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** | **Aina ya ugonjwa** | **Idadi** | **Asilimia** |
| 1 | Malaria | 47,118 | 13.74 | Kichomi kikali | 43,518 | 23.87 |
| 2 | Magonjwa ya mfumo wa mkojo | 31,928 | 9.31 | Malaria | 34,445 | 18.9 |
| 3 | Shinikizo la juu la damu | 30,211 | 8.81 | Kuhara sana (chini ya siku 14) | 32,503 | 17.83 |
| 4 | Upungufu w damu | 29,913 | 8.72 | Upungufu wa damu | 15,195 | 8.34 |
| 5 | Kichomi kikali | 24,847 | 7.25 | Magonjwa ya mfumo wa hewa | 10,361 | 5.68 |
| 6 | Vidonda vya tumbo | 21,637 | 6.31 | Changamoto za watoto wanaozaliwa | 10,156 | 5.57 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Magonjwa y akina Mama | 18,760 | 5.47 | Magonjwa ya mfumo wa mkojo | 6,206 | 3.4 |
| 8 | Kisukari | 16,065 | 4.69 | Kushindwa kupumua baada ya kuzaliwa | 6,178 | 3.39 |
| 9 | Kuvunjika | 14,028 | 4.09 | Kuungua | 2,556 | 1.4 |
| 10 | Magonjwa y mfumo wa hewa | 12,703 | 3.7 | Seli mundu | 2,420 | 1.33 |

**Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza**

**132. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na ongezeka la kasi yamagonjwa yasiyoambukiza (Non-Communicable Diseases – NCDs) nchini na duniani kote, Serikali imekuwa na mzigo mkubwa wa gharama katika kutibu magonjwa haya ikiwemo Afya ya Akili na Ajali. Mathalan **tumeona ongezeko kubwa la fedha inayolipwa na NHIF kugharamia magonjwa yasiyoambukiza ambapo mwaka 2015/16 Shilingi Bilioni 24.4 sawa na asilimia 12 ya fedha zote zilizolipwa; mwaka 2021/22 Shilingi Bilioni 99.8 (15%); mwaka 2022/23 Shilingi Bilioni 137.8 (19%) kwenye Vituo vya kutolea huduma za afya**. Katika kukabiliana na hali hiyo Serikali kupitia Wizara ya Afya, inaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Tatu wa kuzuia na kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, Afya ya Akili na Ajali wa 2021 - 2026 kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kuimarisha uratibu jumuishi kuanzia ngazi ya kijiji/mtaa mpaka taifa, kuongeza kasi ya elimu na uhamasishaji wa jamii katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza, Afya ya Akili na Ajali, kujengea uwezo mifumo ya utoaji wa huduma za Afya katika kufanya uchunguzi na matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza, Afya ya Akili na ajali na kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa afua hizo. Miongoni mwa **vyanzo vikuu** vinavyohusishwa na magonjwa hayo ni pamoja na ulaji usiofaa ikiwemo matumizi ya chumvi na sukari kupita kiasi, tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya pombe

kupita kiasi na kutoshughulisha mwili. **Kipekee nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuwa mstari wa mbele kuhamasisha wananchi kufanya mazoezi ili kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza.**

**133. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, idadi ya wagonjwa waliohudhuria katika vituo vya kutolea huduma kutokana na Magonjwa Yasiyoambukiza walikuwa wagonjwa 4,656,579 ambao ni sawa na asilimia 13 ya wagonjwa wote wa nje (OPD). Idadi hii ni ongezeko la wagonjwa 4,263,597 sawa na asilimia 12.8 waliohudhuria katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa waliolazwa walikuwa ni 271,068 sawa na asilimia 20.1 ikilinganishwa na wagonjwa 242,596 sawa na asilimia 19.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. **Kipindi cha mwaka 2023/24 Shinikizo la Juu la Damu liliongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa nje kwa magonjwa yasiyoambukiza** wakichangia asilimia 26.1 sawa wagonjwa 1,214,911 ikifuatiwa na **Ugonjwa wa Kisukari**, asilimia 12.0 sawa na wagonjwa 559,597 **(Jedwali Na. 6).**

**134. Mheshimiwa Spika,** Magonjwa mengine yasiyoambukiza yaliyoongoza kwa OPD ni Magonjwa ya Ngozi (asilimia 8.3), Ugonjwa wa Pumu (asilimia 6.3) na magonjwa ya macho (asilimia 5.4). Magonjwa Yasiyoambukiza yaliyoongoza kwa upande wa IPD ni Shinikizo la juu la Damu (asilimia 18.6), Upungufu wa Damu (asilimia 17.3), Ugonjwa wa Kisukari (asilimia 10.1), kuvunjika mifupa (asilimia 9.3) na Ajali za Barabarani (asilimia 8.1). Hali hiyo inaonesha kuwa Magonjwa Yasiyoambukiza yasipodhibitiwa yanaweza kusababisha ongezeko la vifo pamoja na gharama za matibabu nchini.

**Jedwali Na. 6:** Magonjwa 10 Yasiyoambukiza yaliyoongoza kwa wagonjwa wa OPD na IPD

| Na. | Wagonjwa wa Nje - OPD | Julai 23 - Machi 24 | % | Wagonjwa wa Kulazwa - IPD | Julai 23 - Machi 24 | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Shinikizo la Damu | 1,214,911 | 26.09 | Shinikizo la Damu | 50,303 | 18.56 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Kisukari | 559,597 | 12.02 | Severe Anaemia | 46,758 | 17.25 |
| 3 | Magonjwa ya Upasuaji | 530,820 | 11.40 | Kisukari | 27,286 | 10.07 |
| 4 | Magonjwa ya ngozi yasiyoambukiza | 384,898 | 8.27 | Kuvunjika | 24,960 | 9.21 |
| 5 | Pumu | 291,683 | 6.26 | Ajali za Barabarani | 21,927 | 8.09 |
| 6 | Magonjwa ya macho yasiyoambukiza | 251,525 | 5.40 | Pumu | 14,814 | 5.47 |
| 7 | Magonjwa ya masikio | 241,821 | 5.19 | Selimundu | 11,937 | 4.40 |
| 8 | Magonjwa mengine ya moyo | 191,119 | 4.10 | Magonjwa ya akili (Psychoses) | 10,653 | 3.93 |
| 9 | Kuvunjika | 185,123 | 3.98 | Magonjwa mengine ya moyo | 9,959 | 3.67 |
| 10 | Magonjwa ya akili | 140,505 | 3.02 | Moyo Kusimama | 9,603 | 3.54 |
| | (Epilepsy) | | | (Cardiac Failure) | | |

**135. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za Magonjwa yasiyoambukiza katika ngazi ya Msingi. Wizara imewezesha vituo vya afya 711 kwa **kuvipatia vifaa** vikiwemo, vifaa vya kupima shinikizo la juu la damu mashine 700, kupima sukari mashine 700, vitendanishi 300 kwa kila kituo na vifaa vya kupima saratani ya mlango wa kizazi 700**.** Aidha, jumla ya **watumishi 2,890** kutoka **Halmashauri 184 walipatiwa mafunzo** kuhusu kugundua na kutibu magonjwa haya. Kutokana na mafunzo hayo kumekuwa na ongezeko la kugundua magonjwa yasiyoambukiza ambapo wagonjwa **4,097,319** waligunduliwa ikilinganishwa na wagonjwa **3,742,141**

waliogunduliwa mwaka 2022/23 na wote walipata ushauri na matibabu.

**136. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha **upatikanaji wa takwimu, ufuatiliaji wa utoaji na upatikanaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukiza kwenye ngazi zote na jamii,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeunganisha vituo 350 katika mfumo wa GoTHOMIS na kujengea uwezo wataalam katika vituo hivyo ambapo rejista maalum ya kukusanya taarifa za magonjwa ya saratani, Selimundu, Kisukari, Kiharusi na Shinikizo la juu la damu.
Aidha, Wizara ipo katika hatua za mwisho za kuunganisha mfumo huu na mfumo wa DHIS2 ili kuruhusu matumizi ya takwimu kwenye ngazi zote za usimamizi wa huduma za afya. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya binadamu (NIMR), Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa Tanzania (NBS) na Zanzibar (OCGS), Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na wadau wengine ilifanya ufuatiliaji wa viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza (STEPS Survey) ili kuweza kutambua mwenendo wa magonjwa hayo katika jamii. Matokeo ya awali yameshapatikana na Wizara ya Afya ipo katika hatua za mwisho za kufanya usambazaji wa taarifa hizo kwa watanzania.

**137. Mheshimiwa Spika,** Kwa kutambua hali ya **ugonjwa na vifo vitokanavyo na Sikoseli** nchini, Wizara imeamua kutoa kipaumbele katika kuvunja mduara wa ugonjwa na kuimarisha utambuzi wa mapema kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja (1) kwa **kusambaza na kusimika mashine za kupima Sikoseli katika mikoa 12** yenye wagonjwa wengi ambayo ni Tabora, Kigoma, Mwanza, Mara, Kagera, Shinyanga, Geita, Simiyu, Morogoro, Pwani, Tanga na Dar es Salaam. Wizara imepanga kufikia **watoto 1,200,000** katika mikoa hiyo pamoja na kuongeza huduma za unasihi wa vinasaba kwa wazazi, kuelimisha na kupima vinasaba (**Genetic Counselling**) kwa vijana rika - balehe kabla ya kufanya maamuzi ya kupanga na kuanzisha familia.

**138. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuelimisha jamii kupitia njia mbalimbali kuhusu ulaji unaofaa, kushughulisha mwili,

kuacha matumizi ya tumbaku na madhara ya unywaji wa pombe kupita kiasi ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza. Kupitia jitihada hizo jumla ya watu zaidi ya **milioni 11** wamefikiwa na elimu ya kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na wadau wengine iliandaa Kampeni ya uhamasishaji, uelimishaji na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza mahala pa kazi, na kuwezesha kuwafikia **watumishi 1,107** wa Wizara 17 ambazo ni Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Wizara ya Fedha; Wizara ya Ardhi; Wizara ya Habari; Wizara ya Viwanda; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Madini; Wizara ya Uchukuzi; Wizara ya Elimu; Wizara ya Utalii na Maliasili; Wizara ya Maji; Wizara ya Fedha; Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Halmashauri moja (1) ya Bahi. Aidha, katika upimaji wa uelewa uliofanyika kwa watumishi kupitia dodoso, limeonesha kuwa zaidi ya nusu ya watumishi (64%) hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na hatua za kuchukua. '**Nitumie fursa hii kuwapongeza wataalam wote kwa kutoa elimu dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, kipekee nampongeza Prof. Mohamed Janabi kwa jitihada anazozifanya katika kuelimisha jamii kuhusu magonjwa hayo'. Tusidharau mafundisho ya Prof Janabi na wataalam wengine wa afya. 'Mtu ni Afya' na 'Kinga ni bora kuliko Tiba'.**

**139. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **wagonjwa 341,677 wa macho** walihudhuria katika vituo vya kutolea huduma ambayo ni pungufu ya wagonjwa 383,560 waliohudhuria katika kipindi cha mwaka 2022/23. Aidha, wagonjwa wa macho yasiyoambukiza waliohudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya walikuwa 251,525 sawa na asilimia 5.4 ikilinganishwa na wagonjwa 232,656 kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Idadi ya wagonjwa wenye kuumia macho ilikuwa 40,640 ikilinganishwa na 37,349 katika kipindi cha mwaka 2022/23. Hadi kufikia Machi 2024, Wizara imetoa mafunzo kwa waalimu 178 wa shule za msingi kutambua watoto wenye

matatizo ya macho shuleni. Watoa huduma wa Afya 188 wamepatiwa mafunzo ya Afya ya Msingi ya Macho (PEC) kuwawezesha kutoa huduma ya kwanza kwa wagonjwa wa macho.

**140. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha uratibu wa magonjwa yasiyoambukiza Wizara ya Afya na Ofisi ya Waziri Mkuu ilifanya kikao cha Makatibu Wakuu kutoka Sekta 15 nchini kwa lengo la kuandaa mikakati jumuishi itakayowezesha watalaam kupitia na kufanya tathmini ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo kwa lengo la kupata suluhisho pale sera au miongozo inapopishana katika kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza. Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo wa Elimu kwa Jamii kuhusu Mtindo wa Maisha na Magonjwa Yasiyoambukiza.

**Afya ya Kinywa na Meno**

**141. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za **Afya ya Kinywa na Meno** hapa nchini, kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara imenunua na kusimika **viti vya kutolea huduma za kinywa na meno 150** vilivyosambazwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa minne (4) na vituo vya halmashauri 142. Hatua hii imewezesha Hospitali za Halmashauri zenye viti hivyo kuongezeka kutoka 130 hadi 184. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza **X-Ray za meno 103 kwenye halmashauri 87 nchini**. Serikali pia ilinunua na kusimika mashine kubwa tatu (3) za kisasa zenye teknolojia ya hali ya juu ya kutambua magonjwa ya kinywa na meno kwa mfumo wa kiRadiolojia aina ya 3D - Dental Cone Beam Computerized Tomography (CBCT) zilizofungwa kwenye Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Rufaa Kanda Mbeya na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mount Meru. **Tanzania ni nchi pekee katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati** kununua vifaa hivyo katika Hospitali za umma.

**142. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki, jumla ya Wagonjwa **592,732** wa kinywa na meno walihudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma. Magonjwa ya kinywa na meno yaliyoongoza ni kuoza meno, wagonjwa **395,685** asilimia **66.8;** magonjwa ya fizi wagonjwa 57,091, asilimia 9.6; Jipu la jino

wagonjwa 15,633, asilimia 2.6; na mpangilio mbaya wa meno 13,734 asilimia 2.3. Wagonjwa **144,607** asilimia 36.5 waliooza meno walipata matibabu ya kuziba meno, wagonjwa **251,078** asilimia 63.5 waling'olewa meno. **'Naomba kutoa wito kwa watanzania wote kuwahi kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya meno mapema pindi wanapopata shida ya meno ili kuepuka kung'olewa meno kwa kuwa magonjwa ya meno yanatibika, ''dawa ya jino siyo kung'oa".**

**Huduma za Afya ya Akili na Dawa za Kulevya**

**143. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha **huduma za afya ya akili** kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo na inakamilisha mkakati wa utoaji wa huduma za Afya ya Akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii. Magonjwa ya Akili yanajumuisha magonjwa yanayotokana na Matumizi ya Dawa za kulevya, Psychoses, kifafa na Neuroses. Aidha, Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 waliohudhuria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa shida ya magonjwa ya afya ya Akili walikuwa 293,952 sawa na asilimia 6.3 ya wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza ikilinganishwa na 246,544 sawa na asilimia 6 kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Kwa wagonjwa waliolazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya wenye magonjwa ya afya ya Akili walikuwa 19,506 sawa na asilimia 7 ya wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza ikilinganishwa na wagonjwa 13,262 sawa na asilimia 5 katika kipindi cha mwaka 2022/23. Ongezeko hili la wagonjwa wa afya ya akili limetokana na kuongezeka kwa uelewa wa jamii kuhusu magonjwa haya na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma.**'Natoa wito kwa wananchi kuacha kuwanyanyapaa wagonjwa wa akili na kuwahi kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya uchunguzi na matibabu ya mapema'**.

**144. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekamilisha andiko la mapendekezo ya Hati Idhini (Instrument) kwa ajili ya kuipandisha hadhi Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe kuwa **Taasisi ya Taifa ya Afya ya Akili**. Upandishwaji hadhi wa Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe kuwa Taasisi unatarajiwa kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya akili nchini kwa kuimarisha huduma za kinga,

tiba, miundombinu, kuimarisha mfumo wa kitaasisi, kuongeza ubunifu na ufanisi, kukuza taaluma na tafiti zinazohusiana na huduma za afya ya akili, huduma za ubingwa na ubingwa bobezi na kuimarisha Tiba Utalii katika eneo la huduma za afya ya akili.

**145. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa Kushirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imewafikia **Waraibu wa dawa za kulevya aina ya heroin takriban 16,500** na kuongeza vituo vya matibabu kufikia 15 katika mikoa 13 nchini ambayo imeathirika zaidi na matumizi ya dawa hizo. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 Wizara imetoa **huduma za utengamao (Mental Health Rehabilitation) na ujasiriamali** kwenye kituo cha Itega, Dodoma, Hospitali ya Rufaa ya Mt. Meru Arusha na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Bombo Tanga ambapo mashine za kufyatua matofali zenye uwezo wa kuzalisha matofali 1,000 kwa siku zilikabidhiwa, mashine za kushona na kudarizi 10 kwa kila kituo pamoja na mashine za kutengeneza samani za aluminium pamoja na vifaa vya kuoshea magari na saluni vilitolewa kwa waraibu kwa lengo la mafunzo ya stadi za kazi na huduma za utengamao kama njia rasmi ya kuwajengea uwezo ili kuwarejesha rasmi katika jamii pamoja na kuwasaidia kwenye shughuli za uzalishaji na kusaidia uchumi wa mtu mmoja mmoja na familia kwa ujumla.

**146. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau walitoa **huduma endelevu za msaada wa kisaikolojia** kwa **watu 8,370** wa Wilaya ya Hanang' katika Mkoa wa Manyara waliokumbwa na maafa ya mafuriko. Waathirika hao walipatiwa fursa ya huduma za matibabu zilizojumuisha msaada wa kisaikolojia pamoja na dawa kwa baadhi yao. Serikali kwa kushirikiana na wadau ilianzisha kampeni maalum shuleni kwa ajili ya kuimarisha afya ya akili kwa wanafunzi hususan katika shule zilizoathirika zaidi.

**Huduma za Utengamao, Wazee na Tiba Shufaa**

**147. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu utoaji wa huduma za utengamao hususan kwa watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum ikiwemo watoto na wazee. Kwa kipindi

cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **wagonjwa 210,382** walipatiwa huduma. Aidha, katika kipindi hiki huduma zifuatazo zilitolewa; Fiziotherapia wateja 177,417, tiba kazi (Occupational Therapy) wateja 25,245, Matamshi na Lugha (Speech and Language Therapy) wateja 1,674, Vifaa Tiba Saidizi (Assistive Devices) wateja 4,234. Viungo tiba na viungo tiba saidizi (Prosthesis and Orthosis) vilitengenezwa na kugawiwa kwa wateja 1,812. Katika kuimarisha Huduma za Utengamao **Hospitali saba (7) zimeweza kutoa seti tatu (3) kati ya nne (4)** ya huduma za utengamao ambazo ni Fiziotherapia, Occupational Therapy na Prosthesis and Orthosis. Aidha, Wizara inaendelea kujenga uwezo kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa zilizobaki. Ili kuhakikisha upatikanaji wa wataalam wa huduma za utengamao, **kozi mpya mbili (2)** katika ngazi ya Shahada zimeanzishwa Chuo Kikuu cha Muhimbili (MUHAS) ambazo ni Speech and language therapy yenye wadahiliwa 15 na occupational therapy yenye wadahiliwa 30 na kufanya jumla ya **wadahiliwa 45** wanaoendelea na mafunzo hayo.

**148. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuimarisha **huduma za afya zinazowalenga wazee na watu wenye ulemavu** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ilisambaza na kugawa vifaa saidizi (Assistive products & Technology) kwa **wazee na watu wenye ulemavu 22,927**. Vifaa vilivyosambazwa ni pamoja na Mikongojo (White Cane), Magongo, Fremu za kutembelea, Vitimwendo na Fremu za kusimamia. Kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara itaanzisha klabu za afya za wazee (Healthy Ageing Club) kwenye ngazi za Kata ikiwa na lengo la kuhamasisha wazee kufanya mazoezi ya pamoja, kujifurahisha na kupinga tabia bwete ili kujilinda na magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya uzeeni.

**149. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Wizara ilitoa **mafunzo ya lugha ya alama** kwa jumla ya **watoa huduma 87** kutoka Hospitali zote za Rufaa za Mikoa na Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe. Katika kipindi hiki, Hospitali tatu (3) ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando na Hospitali ya AgaKhan zilianza kutoa huduma

kwa kutumia mashine yenye uwezo wa kubaini tatizo la ulemavu wa kusikia kwa watoto wachanga. Aidha, jumla ya watoto wachanga 2,507 walipimwa usikivu mara baada ya kuzaliwa na watoto 400 kati yao walihitaji uchunguzi zaidi.

**150. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kutoa **elimu kuhusu ulemavu wa kusikia** ambapo jumla ya wanafunzi wa shule za msingi **3,352** katika maeneo mbalimbali walifikiwa na kuelimishwa. Aidha, wanafunzi **1,957** walipimwa afya ya masikio na usikivu ambapo kati yao **488** sawa na **asilimia 25** waligundulika kuwa na matatizo ya masikio na kupewa rufaa kwa ajili ya matibabu.

**Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala**

**151. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Tiba Asili nchini ambapo **huduma jumuishi za Tiba Asili** zimeanzishwa rasmi na kuanza kutolewa katika **Hospitali saba (7) za Rufaa za Mikoa ya Mwanza, Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Mbeya na Dodoma**. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wagonjwa 223 walipata matibabu katika Hospitali hizo baada ya kufanyiwa vipimo vya uchunguzi wa kisasa. Katika kipindi hiki, **jumla ya dozi 4,748 za dawa za Tiba Asili** zenye thamani ya Shilingi 138,000,000 zilisambazwa katika Hospitali hizo za Mikoa. Magonjwa yaliyotibiwa zaidi kupitia huduma jumuishi za Tiba Asili ni **vidonda vya tumbo, pumu, homa ya matumbo na mvurugiko wa homoni kwa wanawake**. Uanzishwaji wa huduma hizo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa umerahisisha upatikanaji wa huduma za Tiba Asili ukienda sambamba na utoaji wa tiba za kisasa.

**152. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma za Tiba Asili na tiba mbadala, Wizara ya Afya imeanzisha mfumo wa kidigitali wa kuwasajili waganga wa Tiba Asili na kufanya jumla ya waganga waliosajiliwa nchini kuwa **51,593 ikilinganishwa na mwaka 2022/23 ambapo walikuwa 43,854**. Aidha, jumla ya vituo **225** vya Tiba Asili na tiba mbadala vimesajiliwa kuanzia kipindi cha Julai 2023 hadi sasa na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa kufikia **1,600.** Hii imeenda sambamba na usajili wa dawa 19 na kufanya jumla ya

dawa za Tiba Asili zilizosajiliwa kufikia **112**. **Kiambatisho Na. 4** Kinaonesha dawa asili zilizosajiliwa.

**153. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha upatikanaji wa dawa za Tiba Asili salama na zenye ubora, Wizara imeendelea kuboresha kiwanda cha kimkakati chenye maabara ya utafiti kilichopo **NIMR-Mabibo**, Dar es Salaam kwa kununua vifaa vya maabara na **mashine 39** zenye thamani ya **Shilingi 2,200,000,000**. Mashine hizo zina uwezo wa kuchakata kiasi cha **nusu tani na kujaza lita mia sita** kwa saa hivyo kutengeneza dawa za Tiba Asili zilizo na ubora na salama. Kiwanda hiki kimeanza kufanya kazi ambapo kwa sasa jumla ya **dozi 40,000** za aina tano (**5**) za dawa zinazalishwa kwa mwaka kwa ajili ya matibabu **ya uvimbe wa saratani, tezi dume, mfumo wa upumuaji, upungufu wa damu na magonjwa nyemelezi.** Uzalishaji huu ni **mara tatu zaidi** ya uzalishaji wa dawa za Tiba Asili ikilinganishwa na mwaka 2022/23 ambapo mashine hizo zilikuwa hazijasimikwa. Aidha, uzalishaji wa dawa asili unaenda sambamba na uhamasishaji wa upandaji wa miti dawa. Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa kitabu chenye orodha ya miti dawa 100 yenye kipaumbele. **'Napenda kuchukua fursa hii kuiomba na kuihamasisha jamii kupanda na kutunza miti dawa asili ili tusipoteze dawa zetu za asili.'**

**Uimarishaji wa Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi**

**154. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ngazi ya Taifa, Kanda, Maalum na Hospitali za Rufaa za Mikoa. **Jumla ya wagonjwa 4,766,910** walihudumiwa katika Hospitali hizo ambapo kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 4,277,363 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 489,547 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7:** Idadi ya wagonjwa waliohudumiwa katika Katika Hospitali ya Taifa, Kanda na Maalum katika Julai 2023 hadi Machi 2024.

| Hospitali | Idadi ya wagonjwa waliohudumiwa OPD | Idadi ya wagonjwa waliohudumiwa IPD | Jumla |
|---|---|---|---|
| Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga | 320,899 | 34,027 | 354,926 |
| Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila | 136,669 | 10,402 | 147,071 |
| Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete | 230,080 | 7,052 | 237,132 |
| Taasisi ya Mifupa Muhimbili | 172,838 | 7,242 | 180,080 |
| Taasisi ya Saratani | 45,204 | 2,759 | 47,963 |
| Hospitali ya Benjamin Mkapa | 183,864 | 7,664 | 191,528 |
| Hospitali ya Taifa afya ya akili – Mirembe | 86,688 | 77,954 | 164,642 |
| Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ambukizi – Kibong'oto | 15,681 | 493 | 16,174 |
| Hospitali ya Rufaa ya Kanda – Mbeya | 227,167 | 35,844 | 263,011 |
| Hospitali ya Kanda ya Ziwa – Bugando | 338,145 | 27,116 | 365,261 |
| Hospitali ya Rufaa ya Kanda – KCMC | 326,445 | 14,010 | 340,455 |
| Hospitali ya Rufaa ya Kanda – Chato | 38,136 | 2,234 | 40,370 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini – Mtwara | 21,121 | 1,001 | 22,122 |
| Hospitali ya CCBRT | 82,152 | 4,059 | 86,211 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 | 2,052,274 | 257,690 | 2,309,964 |
| | **4,277,363** | **489,547** | **4,766,910** |

**155. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uwekezaji wa kimkakati uliofanywa na Serikali wa kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, **huduma mpya 16** za ubingwa bobezi zilianzishwa nchini. Huduma hizo zinajumuisha; Kutenganisha mapacha walioungana kwa kutumia watalam wa ndani; Tiba hewa Mgandamizo (Hyperbaric Chamber Oxygen Therapy); Upasuaji kwa njia ya matundu madogo; Kutoa Kizazi (Laparascopic Hysterectomy), Upasuaji kwa watu wenye shida ya kumeza chakula (Laparascopic Cardiomyotomy); Upasuaji rekebishi wa vipara (tissue expander); huduma ya upasuaji wa kupunguza mfuko wa chakula (Laparascopic Sleeve Gastrectomy) kwa wagonjwa wenye uzito uliopitiliza; Transcatheter Aortic Valve Implantation (TAVI); kufungua mishipa ya miguuni iliyoziba (Endovascular Procedure – kuweka stent kwenye mishipa mikubwa ya damu iliyopasuka); Endoscopic Minimal Invasive Spine Surgery; Microscopic Minimal Invasive Spine Surgery; Spine Facet Injections for chronic Pain; Aneurysm Clipping; Intensity Modulated Radiotherapy – IMRT; 3D brachytherapy na immunotherapy. Vilevile, Wizara imewezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa nane (8) kutoa huduma za kibingwa katika fani nane (8) ikilinganishwa na Hospitali za Rufaa za Mikoa mitano (5) kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**156. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini kwa kutumia wataalam wa ndani, kiasi cha **Shilingi 5,000,000,000** kimetolewa kwa ajili ya kugharamia matibabu kwa **wagonjwa 237** wasio na uwezo wa matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi. Huduma hizo zimetolewa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ambapo jumla ya **wagonjwa 91** walipatiwa huduma zifuatazo; **watoto 16**

wamenufaika kwa kuwekewa **vifaa vya kusikia** (Cochlear implants); **upandikizaji wa uloto** (Bone marrow transplant) **wagonjwa 9; upandikizaji wa figo** (Kidney transplant) **wagonjwa 29** na **vipandikizi vya Moyo wagonjwa 37** ambapo huduma hizo zimegharimu kiasi cha Shilingi 2,600,000,000. Kwa upande wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kiasi cha **Shilingi 900,000,000** kimetumika kwa ajili ya kugharamia **wagonjwa 100,** kati yao **wagonjwa 50** walipatiwa huduma za **Valvular Replacement Surgery** na **wagonjwa 50** walipatiwa huduma za **Implantable Cardiac Devices.** Aidha, Hospitali ya Benjamin Mkapa imetumia kiasi cha **Shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya kugharamia **wagonjwa 46** waliopatiwa huduma za **Upandikizaji wa Uloto** (Bone Marrow Transplant) **wagonjwa 10**, **Upandikizaji wa Figo** (kidney transplant) **wagonjwa wanne (4)**, **kuweka valve kwenye moyo mgonjwa mmoja (1)** na kufanya **Valvular Replacement mgonjwa mmoja (1)**. Pia, maandalizi yanaendelea kwa ajili ya kupandikiza wagonjwa wengine wa uloto wagonjwa 10, kupandikiza figo wagonjwa 10 na Valvular Replacement Surgery wagonjwa 10.

**157. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha na kuhakikisha wananchi wengi wanafikiwa na huduma za ubingwa na ubingwa bobezi, Wizara inaendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa kusogeza Huduma za Kibingwa kupitia huduma za Mkoba (Dkt. Samia Specialized Outreach Program) katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri. Lengo kuu la Mpango huu ni kusogeza huduma karibu na wananchi, kupunguza gharama za upatikanaji wa huduma za kibingwa na kujenga uwezo wa wataalam katika kuendelea kutoa huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi. **Kwa upande wa huduma za Mkoba za Kibingwa ngazi ya Mikoa**, Wizara imehitimisha kambi sita (6) za Kibingwa na Ubingwa Bobezi zilizoendeshwa katika Mikoa ya Ruvuma, Geita, Tanga, Kigoma, Lindi na Morogoro kuanzia tarehe 29 Aprili hadi tarehe 11 Mei, 2024. Katika kambi hizo jumla ya **Madaktari Bingwa 217** kutoka katika Hospitali zote za Mikoa, Kanda na Taifa wameshiriki kutoa huduma ambapo **wagonjwa 13,802** wameonwa na **wagonjwa 417** wamefanyiwa huduma za **upasuaji mkubwa. Huduma za kibingwa 12** zilizotolewa kwa kutumia madaktari bingwa kutoka katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa ni pamoja na: Ubingwa wa Akinamama na Uzazi (Obstetrics and

Gynaecology); Ubingwa wa Watoto (Paediatrics); Upasuaji (General Surgery); Magonjwa ya Ndani (Internal medicine); Upasuaji Mifupa (Orthopaedic and Trauma); Dharura na Ajali (Emergency); Radiolojia (Radiology); Utoaji wa Dawa za Ganzi na Usingizi (Anaesthesia); Huduma za Macho (Opthalmology); Huduma za Afya ya Akili (Psychiatry); Huduma za Kinywa na Meno (Dental) na Huduma za Utengemao (Rehabilitation).

**158. Mheshimiwa Spika,** Aidha, Wizara inaeendelea kutekeleza **Mpango wa Huduma za Mkoba za Kibingwa katika ngazi ya Halmashauri** zote 184 na vituo vya afya 72 ambapo seti ya **Madaktari Bingwa wa fani tano (5)** wanashiriki katika kila Hospitali ya Halmashauri kutoa huduma za kibingwa na kujenga uwezo wa wataalam katika ngazi ya Halmashauri. Fani hizi ni Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Uzazi na Wanawake (Obstetrician/Gynoecologist); Daktari Bingwa wa Watoto na Watoto Wachanga (Paediatrician/Neotologist); Daktari bingwa wa Upasuaji (General Surgeon); Daktari bingwa wa Magonjwa ya Ndani (Physician) na Daktari bingwa wa ganzi na huduma za dawa za usingizi (Anesthesiologist). Kupitia Mpango huu, Jumla ya Madaktari Bingwa 920 wanashiriki ambapo hadi kufikia tarehe 10 Mei 2024 Hospitali 38 za Halmashauri zimefikiwa na wagonjwa 7,025 wameonwa. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa 971 wamefanyiwa upasuaji. Mpango huu utaendelea hadi kukamilisha Halmashauri zote ifikapo tarehe 28 Juni 2024 chini ya Kaulimbiu **'Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia Tumekufikia, Karibu Tukuhudumie'**. Naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha za kuendesha zoezi hili. Aidha, nawashukuru wataalamu wetu kwa utayari wao wa kwenda kutoa huduma hizo. **'Niwashukuru pia viongozi wote katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kwa kuwapokea na kuwawekea wataalamu wetu mazingira mazuri ya kufanya kazi. Nitoe rai kwa wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi pindi huduma hizi zinaposogezwa karibu na maeneo yao. Ninawaahidi kuwa Mpango huu utaendelea mpaka tutakapokamilisha Mikoa yote na Halmashauri zote.**

**159. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma za kibingwa na kibingwa bobezi zinasogezwa karibu na wananchi, Hospitali

ngazi ya Taifa, Maalum na Kanda zimeendelea na utoaji wa huduma hizo kwa njia ya **Mkoba** (Outreach Services). Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **wagonjwa 85,036** walifikiwa na huduma mbalimbali ikiwemo upasuaji, upasuaji wa mifupa na mishipa ya fahamu, huduma za Akinamama na Uzazi; huduma za Watoto (Paediatrics); Magonjwa ya Ndani; Dharura na Ajali (Emergency); Radiolojia (Radiology); vipimo ya ECHO na ECG; Huduma za Macho (Opthalmology); Huduma za Afya ya Akili (Psychiatry); Huduma za Kinywa na Meno (Dental) na Huduma za Utengamao
(Rehabilitation).

**160. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya Tiba Utalii, Wizara imeendelea kuzijengea uwezo Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda ili ziweze kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi kwa wananchi na raia wa kigeni. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya **raia wa kigeni 7,843** Kutoka nchi mbalimbali walipata huduma hizo kupitia wataalam wa ndani ikilinganishwa na **raia wa kigeni 5,705** mwaka 2022/23.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) – Upanga**

**161. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imetoa huduma kwa **wagonjwa 354,926** ikilinganishwa na wagonjwa 375,057 waliohudumiwa katika kipindi cha mwaka 2022/23 sawa na pungufu ya asilimia 5. Kati yao wagonjwa wakulazwa ni 34,027 na wagonjwa wa nje ni 320,899. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu, Hospitali ilianzisha **huduma mpya tano (5)** za ubingwa bobezi ambazo ni:- Kutenganisha mapacha walioungana kwa kutumia watalam wa ndani. Huduma hii imefanyika kwa mara nyingine baada ya miaka 30 toka huduma hii kufanyika hapa nchini mwaka 1994; Tiba hewa Mgandamizo (Hyperbaric Chamber Oxygen Therapy) kwa wagonjwa wenye vidonda sugu wa Kisukari na waliopata ajali - (Wagonjwa 141); Upasuaji kwa njia ya matundu madogo mfano oparesheni za kifua (Unipolar Video Assisted Thoracoscopic Surgery – VATS); kutoa kizazi (Laparascopic Hysterectomy); Upasuaji kwa watu wenye shida ya kumeza chakula (Laparascopic Cardiomyotomy) wagonjwa 237;

na Upasuaji rekebishi wa vipara (Tissue Expander) wagonjwa wawili (2).

**162. Mheshimiwa Spika,** Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi zimeendelea kutolewa na Hospitali ambapo Upandikizaji wa figo (Wagonjwa 9) hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 81 tangu huduma ilipoanzishwa mwaka 2017; Upandikizaji uloto (wagonjwa 11) tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2021; Upandikizaji wa vifaa vya usikivu (Cochlear Implant) Wagonjwa 15, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 70 tangu huduma hiyo ilipoanzishwa mwaka 2017 na Tiba Radiolojia (Intervention Radiology) wagonjwa 726.

**163. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** kwa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo **58,102** vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa **4,349,** CT - Scan **9,201,** Mammography **84**, X-Ray **15,874** na Ultrasound **25,340**. Pia, Hospitali imefanya huduma za tiba Radiolojia ambapo wagonjwa **3,254** walihudumiwa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **vipimo vya maabara 785,370** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 761,754 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hali ya upatikanaji wa dawa ni asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 90 kipindi kama hiki mwaka 2022/23.

**164. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea **kuboresha miundombinu** ya kutolea huduma za afya kwa kujenga na kununua majokofu 99 ya kuhifadhia maiti yenye gharama ya **Shilingi 1,972,000,000**. Aidha, Serikali imeanza **utekelezaji wa mpango wa maboresho ya Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH Redevelopment Project)** kwa kushirikiana na Serikali ya Korea kupitia Benki ya Exim ambapo upembuzi yakinifu wa kufanya maboresho ya miundombinu ya Hospitali hiyo unaendelea. Mradi huu unatarajia kugharimu Dola za Kimarekani 237,060,000 sawa na **Shilingi 605,688,300,000.**

**165. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalam 40 walienda masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa 28 na

ubingwa bobezi 12 ndani na nje ya nchi. Katika kuboresha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, wataalam 18 wa ubingwa na ubingwa bobezi katika fani mbalimbali waliongezeka ambapo wataalam hawa walirejea kazini baada ya kukamilisha masomo yao na hivyo kufanya jumla ya wataalam bingwa kufikia 306.

**166. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Sera ya kutoa **msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, Hospitali ya Taifa Muhimbili imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 10,507,770,196** kwa wagonjwa 32,615 ikilinganishwa na gharama ya **Shilingi 12,800,000,000** kwa wagonjwa 47,390 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na usafishaji wa damu (Dialysis), huduma za ICU, huduma za vipimo vya CT scan na MRI pamoja na huduma za dawa.

**167. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Taasisi ya Afya (IHI), National Institutes of Health (NIH, Marekani), Bill and Melinda Gates foundation (Marekani) katika **tafiti mbalimbali za kimatibabu**. Moja ya tafiti zinazoendelea ni majaribio ya dawa kwa ajili ya wanawake wanaovuja damu wakati wa kujifungua (Post partum bleeding Haemorrage). Tafiti hii itasaidia katika juhudi za kuzuia upotevu wa damu wakati wa kujifungua kwa wanawake nchini na duniani kwa ujumla. Hospitali pia imeweza kutoa machapisho ya kitabibu 148 katika majarida mbalimbali katika kipindi hiki. Katika kipindi hiki **Tiba Utalii** iliendelea kushika kasi ambapo wagonjwa 567 toka nchi mbalimbali (Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mauritius na Zambia) walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 333 katika kipindi cha mwaka 2022/23.

**Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mloganzila**

**168. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imetoa huduma kwa **wagonjwa 147,071** ikilinganishwa na **123,981** wa mwaka 2022/23 sawa na ongezeko

la asilimia 18.6. Kati ya wagonjwa hao, waliolazwa walikuwa **10,402** na wagonjwa wa nje ni **136,669.** Ongezeko la wagonjwa ni kutokana na uboreshwaji wa huduma pamoja na uanzishwaji wa huduma mpya.

**169. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imeanzisha **huduma mpya nne (4)** za kibingwa na ubingwa bobezi za upandikizaji wa nyonga na magoti (Hip and Knee Transplant), wagonjwa 140 walipatiwa huduma hizi, Upandikizaji wa nyonga (Total Hip Replacement) wagonjwa **40,** na Upandikizaji wa magoti (Total Knee Replacement), wagonjwa **100**, huduma ya upasuaji wa kupunguza mfuko wa chakula (Laparascopic Sleeve Gastrectomy) kwa wagonjwa wenye uzito uliopitiliza ambapo jumla ya wagonjwa saba **(7)** walipata huduma hii na huduma ya kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kupitia matundu ya puani (Endoscopic Transnasal Transphinoidal Pituitary Surgery) ambapo jumla ya wagonjwa watano **(5)** walifanyiwa huduma hiyo.

**170. Mheshimiwa Spika,** huduma **za ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa** na Hospitali ni pamoja na **Upandikizaji wa Figo** ulifanyika kwa wagonjwa 3 na kufanya jumla ya wagonjwa kuwa 8 tangu huduma hii ilipoanza mwaka 2023. Gharama ya upandikizaji wa figo kwa mgonjwa ni Shilingi 37,400,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 120,000,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Aidha, Hospitali imeendelea kutoa huduma ya kuweka **Puto Tumboni** kwa wagonjwa 79 kwa ajili ya kupunguza uzito wa mwili hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliohudumiwa tangu huduma hiyo kuanza mwaka 2022 kufikia 166. Gharama ya huduma hii ni Shilingi 4,200,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 26,565,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Vilevile, Hospitali imeendelea kutoa huduma ya **matibabu ya kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo** kwa kutumia mawimbi mshtuko (Extracorporeal Shock Wave Lithotripsy) ambapo hadi Machi 2024 jumla ya wagonjwa 403 walipatiwa matibabu hayo kwa gharama ya Shilingi 850,000 kwa mgonjwa, ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 3,000,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Uwepo wa huduma hizi

ndani ya nchi umesaidia wananchi kuokoa gharama ambazo wangetumia kufuata huduma nje ya nchi.

**171. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali ambapo vipimo 35,075 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo, MRI vipimo 5,247, CT Scan vipimo 2,850, X-Ray vipimo 15,196, na Ultrasound vipimo 11,782. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **vipimo vya maabara** 267,675 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 265,514 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 89 ikilinganishwa na asilimia 85 kipindi kama hiki mwaka 2022/23.

**172. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea **kuratibu mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalam 37 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kwa ufadhili wa Serikali.
Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba** (Outreach Services), ambapo jumla ya wagonjwa 800 walipatiwa huduma na kati yao wagonjwa 720 walipatiwa huduma za uchunguzi wa usikivu. Aidha, katika kutekeleza Sera ya kutoa **msamaha kwa wagonjwa** wasio na uwezo wa kumudu gharama, Hospitali ilitoa misamaha ya huduma yenye thamani ya Shilingi 2,562,703,988 kwa wagonjwa 12,417 ikilinganishwa Shilingi 2,424,239,320 iliyotolewa kwa wagonjwa 16,887 katika kipindi cha mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na usafishaji wa damu, ICU, vipimo vya CT Scan, MRI na huduma za kulazwa.

**173. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa **Tiba Utalii**, hadi kufikia Machi 2024 wagonjwa 114 kutoka nchi za Comoro,Uganda,
Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Kenya walipatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Huduma walizopatiwa ni pamoja na upandikizaji wa nyonga na magoti bandia, huduma za kupunguza uzito kwa kuwekewa puto pamoja na huduma za uchunguzi kwa vipimo vya maabara na Radiolojia.

**Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)**

**174. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imetoa huduma kwa **wagonjwa 237,132** ikilinganishwa na **wagonjwa 93,017** waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 7,052 na wagonjwa wa nje ni 230,080. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu, Hospitali ilianzisha **huduma mpya** mbili (2), ya kwanza ni ya ubingwa bobezi ambayo ni kubadilisha valvu ya moyo bila kupasua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implamentation (TAVI)) ambapo matibabu haya hufanyika nchi chache Afrika na hata Hospitali chache katika nchi zilizoendelea. Gharama ya mgonjwa mmoja kutibiwa nchini ni Shilingi 80,400,000 na kutibiwa nje Shilingi 220,000,000 na huduma ya kufungua mishipa ya miguuni iliyoziba (Endovascular Procedure – kuweka stent kwenye mishipa mikubwa ya damu iliyopasuka) ambapo gharama ya mgonjwa mmoja kutibiwa nchini ni Shilingi 6,000,000 na kutibiwa nje ni Shilingi 13,000,000. Huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 120, kufunga vifaa visaidizi vya moyo kwa wagonjwa 93, kuzibua mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 105 na kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo kwa wagonjwa 87.

**175. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Taasisi **imeendelea kutoa huduma bobezi** za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu kwa wagonjwa 457 ikilinganishwa na wagonjwa 409 waliofanyiwa huduma kama hii mwaka 2022/23 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia 7,794 toka kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2015. Gharama ya kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu ni wastani wa Shilingi 15,450,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 50,800,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Vilevile, Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 1,920 ikilinganishwa na wagonjwa 1,790 waliofanyiwa huduma kama hii mwaka 2022/23 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia 33,390 tangu huduma hizi zianze. Gharama ya kufanya upasuaji

huo katika Taasisi ni wastani wa Shilingi 6,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 20,000,000 kwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Aidha, Taasisi imeboresha huduma za kliniki ya watu mashuhuri (VIP Clinic) ambapo jumla ya wagonjwa 2,970 walipata huduma hiyo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024.

**176. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa ya moyo ambapo vipimo vya ECHO, X-Ray, Ultra Sound, ECG, Lung Functional Test, ABP, Holter, Stress ECG, Dobutamine, Stress ECHO na Sparkle Traching Echo vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya ECHO vilikuwa 20,247, Holter vilikuwa 1,941, Stress ECG vilikuwa 2,388, Dobutamine vilikuwa 210, Stress ECHO vilikuwa 18, na Sparkle Traching ECHO vilikuwa 846, X-Ray vilikuwa 10,845, Ultra Sound vilikuwa 5,223, ECG vilikuwa 17,085, Ultra Functional Test vilikuwa 120 na ABP vilikuwa 1,893. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya vipimo vya **maabara** 248,409 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 215,142 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 90 kipindi kama hiko mwaka 2022/23.

**177. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalam 100 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi katika masuala ya moyo ndani na nje ya nchi. Taasisi imetumia jumla ya kiasi cha Shilingi 301,500,000 kutoka katika mapato yake ya ndani kuwalipia watumishi hao. Katika kutekeleza **Dkt. Samia Cardiac Outreach Program**, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 7,422 walifikiwa, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma tangu taasisi imeanza kutoa huduma za mkoba mwaka 2015 kufikia 35,813. Jumla ya wagonjwa 5,230 waliopatiwa vipimo ya ECHO na ECG kupitia huduma hizo za mkoba na wagonjwa wapya 2,192 waligundulika kuwa na magonjwa ya moyo.

**178. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Sera ya kutoa **msamaha kwa wagonjwa** wasio na uwezo wa kumudu gharama, Taasisi imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 1,146,206,145** kwa wagonjwa 1,167 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 521,962,007 kwa wagonjwa 747 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo, ada ya kumwona daktari na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi. Vilevile, msamaha huu ulijumisha wagonjwa waliopata huduma bobezi kama vile Transcatheter Aortic Valve Implamentation (TAVI).

**179. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya **wagonjwa 744** ikilinganishwa na wagonjwa 650 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa waliohudumiwa ni kutoka nchi za Msumbiji, Comoro na Malawi. Vilevile, Taasisi imehudumia raia wa kigeni walioko nchini kutoka nchi za India, Poland na Marekani. Aidha, kutokana na kuimarika kwa huduma za ubingwa za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua, Taasisi imezijengea uwezo nchi za Malawi, Rwanda na Zambia kutoa matibabu hayo.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

**180. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Taasisi ya Mifupa (MOI) imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 180,080** ikilinganishwa na wagonjwa 170,071 waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati yao wagonjwa wa kulazwa ni 7,242 na wagonjwa wa nje ni 172,838. **Kipekee nichukue fursa hii kuishukuru Taasisi ya MO Foundation kwa kugharamia matibabu ya Watoto hamsini (50) wenye changamoto ya Vichwa Vikubwa na Mgongo Wazi. Nitoe wito kwa wanananchi kuendelea kutowaficha watoto wenye changamoto hizo.**

**181. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya ubunifu na upanuzi wa huduma, Taasisi ilianzisha **huduma mpya** (4) za ubingwa bobezi ambazo ni Upasuaji wa mgongo kwa njia ya tundu kwa msaada wa video (Endoscopic Minimal Invasive Spine Surgery) wagonjwa (2), Upasuaji wa mgongo kwa kupitia tundu

dogo (Microscopic Minimal Invasive Spine Surgery), wagonjwa (7), Matibabu ya maumivu makali ya muda mrefu ya mgongo kwa njia ya sindano za mgongoni (Spine Facet Injections for chronic Pain), wagonjwa (392) na Matibabu ya mishipa iliyotanuka kwenye ubongo (Aneurysm Clipping) wagonjwa (10). Huduma hizo zimegharimu kiasi cha Shilingi 2,109,398,200. Aidha, endapo huduma hizi zingefanyika nje ya nchi zingeigharimu Serikali jumla ya kiasi cha Shilingi 2,674,596,400. Huduma za **ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa na Hospitali ni pamoja na upasuaji wa Nyonga (Total Hip Replacement), Upandikizaji wa goti bandia (Total Knee Replacement), upasuaji wa uti wa mgongo (Spine Surgeries), upasuaji wa ubongo (Brain Surgery), upasuaji wa ubongo kwa matundu kupitia puani (Transsphenoidal Surgery), Upasuaji wa Magoti kwa Matundu (Arthroscopic Surgery), Upasuaji wa vichwa vikubwa (Hydrocephalus Surgery) na upasuaji wa Kibyongo (Scoliosis Surgery) ambapo jumla ya wagonjwa 6,134 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 5,477 waliopatiwa huduma kwa kipindi kama hicho 2022/23.

**182. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali ambapo vipimo 139,081 **vya Radiolojia** vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa 5,379, CT Scan vipimo 3,807, X-Ray vipimo 33,111 na Ultrasound vipimo 1,318 pamoja na vipimo vingine 95,466 vya Radiolojia. Aidha, kwa kipindi tajwa, jumla ya **vipimo vya maabara** 101,036 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 72,343 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 96 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**183. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalam 16 wapo masomoni katika fani za kibingwa na ubingwa bobezi za upasuaji wa mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu ndani na nje ya nchi. Aidha, Taasisi imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 6,026 walipatiwa huduma na kati yao wagonjwa 4,578 walipatiwa huduma za Kliniki na wagonjwa 1,448 walifanyiwa upasuaji wa mifupa mbalimbali.

**184. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza Sera ya kutoa **msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, Taasisi imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 2,702,038,334** kwa wagonjwa 4,318 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 1,244,248,518 kwa wagonjwa 2,869 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na Upasuaji, Mionzi (Radiology), Kulazwa (Admission), Vipimo vya Maabara pamoja na Dawa.

**185. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 121 kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na 119 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa waliohudumiwa ni kutoka nchi za, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Comoro, Botswana, Zimbabwe, Uganda, Burundi, Malawi, Msumbiji na Rwanda. Aidha, Hospitali imehudumia raia 10 wa kigeni waliopo nchini, raia wa Canada, India, Urusi, Marekani na Uingereza; hii inatokana na kuimarika na kuaminika kwa huduma za ubingwa bobezi hapa nchini kwani siku za nyuma raia wa kigeni walikuwa wanasafirishwa kwenda kutibiwa katika nchi zao au Nairobi na Afrika ya Kusini.

**186. Mheshimiwa Spika,** Kwenye eneo la **miundombinu** na vifaa, Taasisi imekamilisha ujenzi wa kliniki ya Wagonjwa Mashuhuri na wa kigeni (Premier and International patients' Clinic), vyumba vya mashine za Radiolojia, eneo la kisasa la kupumzika wagonjwa wa kawaida (Clients' Lounge) na kusimika Mitambo mipya ya CT na MRI, vyote vikiwa na thamani ya Shilingi 5,500,000,000. Hivyo, usimikaji wa vifaa hivyo umewezesha Hospitali kuwa na CT mbili na MRI mbili (2) ambazo zinapunguza muda wa wagonjwa kusubiria vipimo kutoka siku tatu (3) hadi siku moja na kuongeza ufanisi katika ugunduzi na upasuaji wa magonjwa ya Mifupa na Ubongo.

**Taasisi ya Saratani Ocean Road**

**187. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Taasisi ilihudumia **jumla ya wagonjwa 47,963** ikilinganishwa na wagonjwa 43,922 waliohudumiwa kipindi cha mwaka 2022/23. Kati ya hao, wagonjwa wa nje (OPD) ni 45,204 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 2,759. Huduma za kibingwa na ubingwa bobezi

ambazo zimetolewa katika kipindi hiki ni pamoja na uchunguzi wa maabara, uchunguzi wa Radiolojia, tiba mionzi nje, tiba kemia, tiba mionzi ndani na tiba nyuklia. Aidha, Taasisi imeanzisha **huduma mpya tatu (3)**.
Huduma hizo ni; tiba mionzi bobezi (Intensity Modulated Radiotherapy –IMRT) ambayo ina usahihi zaidi katika kutibu uvimbe wa saratani; Tiba ya mionzi ya ndani (3D brachytherapy) ambayo inatumia teknolojia ya 3D kutibu saratani ya mlango wa kizazi kwa ufanishi zaidi kuliko ile ya awali ya 2D na tiba bobezi dawa za immuno (Immunotherapy) ambayo ni teknolojia inayohakikisha mwili unaimarisha seli maalum za kupambana na saratani. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wagonjwa 508 walitibiwa kwa tiba mionzi ya IMRT, wagonjwa 2,674 walitibiwa kwa tiba mionzi ya 3D brachytherapy, na wagonjwa 102 walitibiwa kwa tiba ya immunotherapy.

**188. Mheshimiwa Spika,** Taasisi **imeendelea kutoa huduma** za tiba mionzi (3D-CRT) ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, tiba mionzi 163,166 zimetolewa ikilinganishwa na tiba mionzi 159,763 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa 2022/23. Tiba mionzi ya 3D-CRT ilianza mwaka 2019 ambapo hadi sasa jumla ya tiba mionzi 933,120 zimetolewa. Gharama ya tiba mionzi hapa nchini ni Shilingi 5,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na Shilingi 12,000,000 kama mgonjwa akitibiwa nje ya nchi. Vile vile, Taasisi imetoa Tiba kemia 46,873 kwa kutumia mashine za infusion pumps ikilinganishwa na Tiba kemia 44,321 katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022/23. Hadi sasa jumla ya tiba kemia 343,021 zimetolewa tangu kuanzishwa kwa huduma hii mwaka 2017. Gharama ya tiba kemia kwa mgonjwa mmoja ni wastani wa Shilingi 4,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 10,000,000 akitibiwa nje ya nchi. Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba shufaa ikiwemo dawa ya oral morphine kwa ajili ya kupunguza maumivu kwa wagonjwa 37,228 ikilinganishwa na wagonjwa 34,543 kwa mwaka 2022/23. Aidha, Taasisi imeendelea kushikilia ithibati ya kimataifa ya maabara kutoka Chombo cha Ithibati cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADCAS) iliyopatiwa toka mwaka 2021.

**189. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya **vipimo vya maabara 158,607** vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 151,321 katika kipindi cha mwaka 2022/23. Kwa upande wa **Radiolojia**, vipimo 19,090 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 14,520 vilivyofanyika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 7,599 ni vya X-Ray, 7,664 vya Ultrasound, 2,113 vya CT Scan, 1,290 vya MRI na 424 vya mammograph. Hali ya **upatikanaji wa dawa** za saratani ni wastani wa asilimia 100 ikilinganishwa na asilimia 98 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**190. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa **mradi wa PET/CT Scan** ambao ulihusisha ujenzi wa Bunkers na ununuzi na usimikaji wa mashine za PET/CT Scan na Cyclotron kwa jumla ya Shilingi 18,200,000,000 umekamilika. Ukaguzi wa jengo na mashine zilizosimikwa umefanywa na Tume ya Nguvu ya Atomiki Tanzania (TAEC) na hatua inayofanyika sasa ni kukamilisha majaribio ya mashine ya Cyclotron ya kuzalisha mionzi dawa na **huduma zitaanza kutolewa Juni 2024**. Aidha, mradi wa ujenzi wa Kituo cha Saratani Mbeya (ORCI Mbeya Cancer Centre) unaendelea ambapo mkandarasi mshauri alipatikana na kwa sasa zabuni ya kumpata mkandarasi wa ujenzi imetangazwa na itakamilika Juni 2024. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha kuhudumia wagonjwa kutoka mikoa 11 na nchi jirani zipatazo sita (6). Vile vile, utekelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Jengo la Multi-purpose Oncology kwa kutumia mapato ya ndani unaohusisha jengo litakalokuwa na huduma za wodi binafsi, famasi, maabara na kliniki binafsi unaendelea. Aidha, ununuzi na usimikaji wa mashine ya CT Scan kwa gharama ya Shilingi 2,300,000,000 umekamilika. Pia, Taasisi imenunua na kusimika mashine mpya ya mionzi ya ndani (3D brachytherapy) kwa gharama ya Shilingi 450,000,000 ambapo sasa inatoa huduma za tiba kwa wagonjwa.

**191. Mheshimiwa Spika,** Taasisi inaendelea kuendeleza **rasilimali watu** ikiwemo kusomesha wataalam wa kozi za kibingwa na ubingwa bobezi za muda mfupi kwa wataalam 17 na za muda mrefu wataalam 32. Kozi hizi ni pamoja na Radiotherapy Scientist, Famasia na Medical Physicist. Taasisi ina watumishi wa mikataba

madaktari tisa (9), wauguzi 17 na wafamasia 18 na wanagharamiwa kwa mapato ya ndani.

**192. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Taasisi imetoa **huduma za mkoba** katika mikoa sita (6) ya Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Kagera, Morogoro, na Tanga ambapo wateja 14,985 walihudumiwa ikilinganishwa na wateja 12,732 waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2022/23. Huduma hizi zilijumuisha:- uchunguzi wa saratani ya matiti, saratani ya mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana na tezi dume; utoaji wa elimu; utoaji wa chanjo; na matibabu yalitolewa kwa waliogundulika na matatizo. Aidha, katika kutekeleza sera ya kutoa **misamaha** kwa wagonjwa, Taasisi ilitoa misamaha ya **Shilingi 28,254,601,599.99** kwa wagonjwa 15,475 ikilinganishwa na misamaha ya Shilingi 37,293,822,470 kwa wagonjwa 13,740 iliyotolewa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma za misamaha zimepungua kutokana na wagonjwa wengi kutumia kadi za bima ya afya na pia kuweka utaratibu madhubuti kupitia Ofisi ya Ustawi wa Jamii. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni tiba mionzi, dawa za tiba kemia, uchunguzi wa maabara, Radiolojia na huduma za kulazwa.

**193. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii,** Taasisi imeendelea kuimarisha huduma ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 wagonjwa 526 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikilinganishwa na wagonjwa 152 waliopata huduma hiyo kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Malawi, Kenya, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Msumbiji, Sudani ya Kusini, Zambia, Burundi na Uganda.

**194. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha huduma kwa wagonjwa, **tafiti** mbalimbali za kimatibabu zimeendelea kufanyika, ambapo kwa sasa Taasisi inafanya tafiti 19 kwa kushirikiana na Taasisi zingine ndani na nje ya nchi ikiwemo MUHAS, NIMR, University of Zambia, University of California San Francisco (UCSF) na Lousiana State University (LSU). Faida ya tafiti hizi ni kuongeza uelewa kuhusu vyanzo vya magonjwa ya saratani, vihatarishi, na pia kuelewa matokeo ya matibabu ya

saratani. Matokeo ya tafiti hizi yatakuwa na manufaa katika tiba ya saratani nchini. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya machapisho ya kitafiti 38 yalifanyika katika majarida ya kimataifa ikilinganishwa na machapisho 26 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23

**195. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili iliendelea kutoa **mafunzo** kwa wanafunzi 135 katika fani za uchunguzi na Tiba ya Radiografia, Onkolojia na Uuguzi katika Onkolojia. Mafunzo hayo yameongeza uwepo wa wataalam wa huduma za saratani nchini.

**Hospitali ya Benjamin Mkapa**

**196. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 191,528** ikilinganishwa na wagonjwa 178,299 waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 7,664 na wagonjwa wa nje ni 183,864. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu, Hospitali ilianzisha **huduma mpya** mbili za ubingwa bobezi ambazo ni upasuaji wa Moyo kwa watu wazima ambapo wagonjwa saba (7) wamenufaika na kuweka vipandikizi kwenye uume (Penile Inplants) kwa wagonjwa wawili (2). Aidha, gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja wa upasuaji wa moyo ni wastani wa Shilingi 70,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 210,000,000 iwapo matibabu hayo yangefanyika nje ya nchi. Vile vile gharama ya kuweka vipandikizi kwenye uume kwa mgonjwa mmoja ni wastani wa Shilingi 10,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 30,000,000 nje ya nchi.

**197. Mheshimiwa Spika,** Huduma za **ubingwa bobezi zilizoendelea** kutolewa na Hospitali ni pamoja na upandikizaji wa uloto kwa ajili ya matibabu ya ugonjwa wa selimundu (Sikoseli), upandikizaji wa figo, uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia miale (Ureteroscopy plus Laser Lithotripsy - URS), upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa wanne (4) ikiwa ni idadi sawa na wagonjwa waliofanyiwa huduma hiyo kipindi kama hicho mwaka 2022/23, na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa

waliofanyiwa huduma hii kufikia nane (8) toka huduma imeanzishwa mwaka 2023. Pia, Hospitali imefanikiwa kupandikiza figo wagonjwa wanne (4) ikilinganishwa na wagonjwa sita (6) kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 na kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia wagonjwa 39 tangu kuanzishwa 2018. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali ilifanikiwa kufanya huduma ya uvunjaji wa mawe (ureteroscopy plus laser lithotripsy - URS) kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 307 ikilinganishwa na wagonjwa 266 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Huduma zingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upasuaji wa nyonga na magoti ambapo jumla ya wagonjwa 49 wamewekewa vipandikizi kwenye nyonga (Total Hip replacement) na vipandikizi kwenye magoti (Total Knee Replacement) ambapo katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23 waliwekewa wagonjwa 30.

**198. Mheshimiwa Spika,** Huduma nyingine za **ubingwa bobezi zilizotolewa** ni Upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu (Neuro endovascular surgery) ambapo jumla ya wagonjwa 310 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 379 waliofanyiwa huduma hii kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma nyingine ni upasuaji wa moyo na huduma zitolewazo kwa kutumia mtambo maalum wa cathlab ambapo wagonjwa 194 wamepatiwa huduma katika maabara hiyo ikilinganishwa na wagonjwa 174 waliopatiwa huduma hii katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hospitali imegharamia kiasi cha Shilingi 800,500,000 kuwezesha huduma hizo ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 5,505,000,000 kama wagonjwa wangetibiwa nje ya nchi.

**199. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo **vipimo 51,624 vya Radiolojia** vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo MRI vilikuwa 3,325, CT Scan vipimo 2,770, X-Ray vipimo 18,389 na Ultrasound vipimo 25,972. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **vipimo vya maabara 186,002** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 141,957 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Hali ya upatikanaji wa dawa

ni asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 97 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**200. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** kwa wataalam ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalam 50 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, watumishi 31 wanagharamiwa na Wizara, 17 wanagharamiwa na mapato ya ndani ya Hospitali ambapo jumla ya Shilingi 260,000,000 zimetumika, na wawili wanagharamiwa na mashirika ya nje ya nchi. Hospitali pia imegharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 48 ambapo kiasi cha Shilingi 130,000,000 kimetumika. Vilevile Hospitali imeandaa mtaala wa diploma ya Radiolojia ambao umetolewa na kuanza kutumika katika vyuo vinne kwa lengo la kuzalisha wataalamu kwa wingi kulingana na mahitaji ya sasa. Vyuo hivyo ni; Noble college, Kolandoto, Ruaha University, na Sengerema Training Institute.

**201. Mheshimiwa Spika,** Hospitali kupitia mapato yake ya ndani imewekeza jumla ya Shilingi 4,539,443,249.49 kwa ajili ya; ukarabati wa vyumba vitatu vya upasuaji pamoja na ununuzi wa vifaa tiba, ukarabati wa maabara maalum ya kujifunzia, ukarabati wa kituo cha matibabu ya figo pamoja na ununuzi wa vifaa tiba, ukarabati wa kituo cha upandikizaji mimba pamoja na ununuzi wa vifaa tiba. Hospitali imeendelea kutoa **huduma mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 4,094 walipatiwa huduma na kati yao wagonjwa 2,139 walipatiwa huduma za Macho, Wagonjwa 253 walipatiwa huduma za Mifupa na ajali, wagonjwa 456 walipatiwa huduma za magonjwa ya kinamama na uzazi, wagonjwa 225 walipatiwa huduma ya koo, masikio na pua, wagonjwa 38 walipatiwa huduma ya upasuaji wa mishipa ya fahamu na ubongo, wagonjwa 300 walipatiwa huduma za upasuaji, wagonjwa 120 walipatiwa huduma za mfumo wa mkojo na uzazi kwa wanaume, wagonjwa 179 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya watoto, wagonjwa 176 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya ndani na wagonjwa 58 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya moyo.

**202. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Sera ya kutoa **msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama,

Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 279,943,046** kwa wagonjwa 1,463 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 244,555,860 kwa wagonjwa 2,200 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na uchujaji damu, vipimo vya maabara, kitengo cha wagonjwa mahututi (ICU), huduma za upasuaji, kumuona daktari na dawa.

**203. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imefanya **tafiti** tano (5) ikiwa ni pamoja na Clinical Presentation and Treatment Outcomes of Pregnancy Related Acute Kidney Injury among Pregnant Women Admitted at the Benjamin Mkapa Hospital in Tanzania ambapo, matokeo ya tafiti hizo yatawezesha kuboresha utoaji wa huduma za afya katika Hospitali, mathalani utafiti kuhusu. Pregnancy Related Acute Kidney Injury among Pregnant Women umesaidia kuweka mikakati ya kupunguza vifo vya akinamama wajawazito.

**Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

**204. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imeendelea kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili kwa raia na wahalifu waliothibitishwa na vyombo vya kisheria kama vile Mahakama, Polisi na Magereza. Vilevile Hospitali inatoa huduma za matibabu kwa waraibu wa aina mbalimbali ikiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilihudumia **jumla ya wagonjwa 164,640** kati yao wagonjwa 86,688 walikuwa wagonjwa wa nje (OPD) na wagonjwa 77,952 walikuwa ni wagonjwa wa kulaza (IPD). Aidha, wagonjwa 97,664 sawa na asilimia 59 ni wagonjwa wa Akili na wagonjwa 66,976 sawa na asilimia 41 ni wagonjwa wa kawaida, ikilinganishwa na wagonjwa waliotibiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 ambapo jumla ya wagonjwa 125,223 kati yao wagonjwa 82,763 sawa na asilimia 66 walikuwa wagonjwa wa Akili na wagonjwa 42,460 sawa na asilimia 34 walikuwa ni wagonjwa wa kawaida. Hata hivyo, kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa akili wahalifu waliothibitishwa na vyombo vya kisheria wanaotibiwa sehemu ya Isanga, kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya wagonjwa 456 walithibitishwa na wanaendelea na

matibabu ikilinganishwa na wagonjwa 383 waliopata matibabu kipindi kama hicho 2022/2023.

**205. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeanzisha **huduma mpya** za ubingwa bobezi ya kurejesha kumbukumbu na Afya ya Akili kwa Wazee (Memory and Psychogeriatric services) ambapo wagonjwa 121 wamepatiwa huduma hizo. Aidha Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ambazo ni pamoja na matibabu ya Afya ya akili kwa watoto na vijana (Child and Adolescence Mental Health Clinic) wagonjwa 136, kliniki ya Afya ya Akili kwa akina mama (Maternal Mental Health Clinic) wagonjwa 126, kliniki ya matibabu ya mfumo wa fahamu (Neurology Clinic) wagonjwa 248 na kliniki ya matibabu ya saikolojia na utengamao (Psychology Clinic) wagonjwa 326 walihudumiwa.

**206. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ikiwemo uchunguzi wa magonjwa ya akili ambapo vipimo 5,360 vilifanyika. Kati ya hivyo, kipimo cha umeme wa Ubongo EEG kilifanyika kwa wagonjwa 386, vipimo vya X-Ray 3,814, na vipimo vya Ultrasound 1,160. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 36,321 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 27,421 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 98 ikilinganishwa na asilimia 93 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**207. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **jumla ya wataalam 13** wamefanikiwa kupata nafasi ya kujiendeleza kuwa mabingwa na mabingwa bobezi katika fani mbalimbali za afya ya akili ikilinganishwa na wataalam watatu (3) waliopata mafunzo katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Vilevile, kupitia fedha za mapato ya Hospitali watumishi 6 wamefadhiliwa kujiunga na masomo katika kada mbalimbali za muda mfupi na muda mrefu. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 59** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza uhaba wa watumishi ambapo kati yao watumishi saba (7) ni Madaktari, Watumishi 27 ni Wauguzi na watumishi 23 wa kada nyingine. Vilevile, katika kipindi cha Julai

2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilifanya **huduma za Mkoba** ikiwemo kutoa elimu zilizolenga huduma za afya ya Akili na msaada wa kisaikolojia kwa wananchi takriban 32,581 za aina tatu (3) shule za msingi na sekondari Jijini Dodoma, Iringa RRH na kwenye maafa yaliyotokea Mkoani Manyara wilaya ya Hanang mwezi Desemba 2023 ikilinganishwa na huduma mkoba ya aina moja iliyofanyika kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**208. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza **sera ya msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama hizo, Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 626,921,346 kwa wagonjwa 964. Huduma zilizotolewa misamaha ni pamoja na matibabu, chakula, mavazi na malazi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali kwa kushirikiana na Hospitali nyingine na chuo Kikuu cha Dodoma imefanya **tafiti** kubwa mbili (2) ikiwemo tafiti ya matumizi ya akili bandia. Tafiti hizi zitaboresha huduma za afya ya akili nchini.

**Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto**

**209. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto imeendelea kutoa huduma za tiba, kinga na tafiti. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilihudumia **jumla ya wagonjwa 16,174** ikilinganishwa na wagonjwa 20,749 waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2022/23. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa, wagonjwa wa nje (OPD) ni 15,681 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 493. Aidha, kati ya wagonjwa 16,174 waliohudumiwa wagonjwa wa **Kifua kikuu (TB)** walikuwa **1,285** (TB kawaida 1,204 na TB sugu 81). Wagonjwa 81 wa Kifua kikuu sugu ni rufaa kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao hulazwa kwa muda wa wastani wa miezi 6 na kuendelea wakipatiwa matibabu, chakula, chakula dawa kwa wenye utapiamlo mkali na mahitaji mengine muhimu ya kijamii. Pia, Hospitali inatoa utaalamu wa kimatibabu kwenye mikoa na halimashauri kwa njia ya teknolojia ya masafa (MDRTB -ECHO) kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu ambapo wagonjwa 87 wamehudumiwa katika kipindi hiki.

**210. Mheshimiwa spika,** Hospitali hii imeendelea kuhudumia wagonjwa wa **Silicosis, walioathirika mapafu kutokana na vumbi la ulanga (silica dust)** katika shughuli za uchimbaji madini, ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi machi 2024 Jumla ya wagonjwa 67 walilazwa. Wagonjwa hawa hukaa Hospitali wakipatiwa matibabu na **hutumia hewa tiba ya oksijeni** kwa muda wote, ambapo wamekuwa wakitumia wastani wa mitungi ya oksijeni 25 hadi 30 kwa siku na hukaa Hospitali kwa wastani wa muda wa mwaka mmoja na zaidi. Aidha hospital imeendelea kuimarisha huduma za kinga dhidi ya athari za vumbi hili kwenye migodi hasa mgodi wa Mererani kwa kufanya uchunguzi, utoaji elimu na ushirikishaji jamii ili kutambua na kuchukua hatua stahiki ikiwemo kushirikisha mamlaka zingine kama OSHA.

**211. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilianzisha **huduma mpya** ya matibabu ya mapafu kwa waliougua kifua kikuu na kupona na kupata athari za mapafu (Post TB lung Diseases), huduma hii alianza kama utafiti kwa watu 554 na baadaye kuonesha matokeo chanya na hatimaye kutambulika kimataifa, na hivi sasa Hospitali imepewa jukumu na Mfuko wa Dunia wa Kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria (Global fund) ya kuongoza utoaji wa huduma hii barani Afrika ambapo imeanza na nchi tatu za Kenya, Malawi na Uganda.

**212. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi wa magonjwa** mbalimbali ambapo vipimo **5,509** vya **Radiolojia** vilifanyika.
Kati ya hivyo vipimo vya X-Ray ni 4,736 na Ultrasound vipimo 773, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **vipimo vya maabara 33,085** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 37,986 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, hali ya upatikanaji wa dawa za Kifua Kikuu na kufubaza virusi vya UKIMWI ni asilimia 100 kwa dawa za mstari wa kwanza na wa pili. Dawa nyingine muhimu (essential medicine) upatikanaji wake ni asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 82 kwa mwaka 2022/23.

**213. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imetoa **huduma za mkoba** kwa wateja 2,268 ambapo kati yao, wateja 204 waligundulika kuwa na Kifua Kikuu, wagonjwa watatu (3) waligundulika kuwa na VVU na wateja wawili (2) waligundulika kuwa na Kifua Kikuu pamoja na VVU. Maeneo yaliyohudumiwa ni pamoja na jamii za wachimbaji wa madini katika Mkoa wa Manyara (Mererani na Simanjiro), Tanga, Dar es Salaam na Morogoro.

**214. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ilihudumia wagonjwa 3,712 kwa **misamaha** kwa gharama ya Shilingi **58,382,803** ikilinganishwa na jumla ya wagonjwa 3,484 waliotibiwa kwa misamaha wa gharama ya Shilingi **38,096,276** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni dawa, kumuona daktari, huduma za maabara pamoja na huduma za uchunguzi kwa kutumia mionzi.

**215. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imeendelea na **ujenzi wa jengo la sakafu tatu (3) la Radiolojia** ambao ulianza kwa kutumia mapato yake ya ndani. Aidha imefanya ukarabati wa njia za kupita wagonjwa zenye urefu wa mita 152 pamoja na uzio wa Hospitali wenye mita 1,288 ambapo Hospitali imetumia mapato yake ya ndani kiasi cha Shilingi 197,300,000. Vilevile, Hospitali inasomesha **watumishi 12** kwenye fani mbalimbali zikiwemo za ubingwa na ubingwa bobezi kati yao watumishi 7 wanasomeshwa kwa kutumia mapato ya ndani ambapo watumishi wanne (4) ngazi ya uzamivu (PhD), watumishi 3 ngazi ya Diploma katika fani nyinginezo za uwezeshaji katika uendeshaji wa Hospitali. Aidha, Hospitali imeweza kuajiri **watumishi wa kujitolea na mkataba** wapatao 17 ambapo watumishi 12 wanalipwa toka mapato ya ndani ya Hospitali

**216. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kufanya **tafiti** mbalimbali za kuboresha tiba na ugunduzi, Jumla ya tafiti 9 zinaendelea kufanyika ambapo matokeo ya tafiti hizo yanategemewa kutoa mchango katika kuboresha tiba. Aidha baadhi ya tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa kupunguza muda wa matibabu ya kifua kikuu cha kawaida kutoka miezi 6 hadi 4 ambapo Hospitali inaongoza katika nchi 4 za afrika kwenye utafiti huo (Gabon, Malawi, Msumbiji na Tanzania) ikishirikiana na nchi

nyingine za ulaya, pia Hospitali inafanya utafiti wa kuboresha matibabu ya uambukizo katika damu wa vimelea vya Kifua Kikuu na UKIMWI (TB sepsis) kwa wagonjwa ili kuona uwezekano wa kupunguza vifo katika kundi hili ikishirikiana na chuo kikuu cha mbarara na Virginia nchini Marekani.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

**217. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa kwa wananchi wa mikoa saba (7) ambayo ni Mbeya, Iringa, Ruvuma, Njombe, Songwe, Rukwa na Katavi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 263,011** ikilinganishwa na wagonjwa 259,505 waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 35,844 na wagonjwa wa nje (OPD) ni 227,167**.** Aidha, katika kutekeleza dhana ya ubunifu, Hospitali ilianzisha **huduma mpya** tano (5) za Ubingwa bobezi ambazo ni Upasuaji wa moyo (wagonjwa 173), ubongo na mishipa ya fahamu (wagonjwa 1,028) na matibabu ya mfumo wa chakula na ini (Gastroentorology) wagonjwa 5,928, huduma ya mfumo wa upumuaji (Pulmunology) wagonjwa 6,128 pamoja na huduma ya upasuaji wa watoto wachanga ulifanyika kwa wagonjwa 396. Kabla ya huduma hizo kuanzishwa wagonjwa walikuwa wanapewa rufaa na kusafiri hadi Jijini Dar es Salaam.

**218. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi 2024, Hospitali **imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi** za Pua, Koo na Masikio, Saratani, Upasuaji na upasuaji wa mifupa, Huduma za magonjwa ya wanawake na uzazi na watoto, Ajali na Dharura (EMD), pamoja na magonjwa ya ndani na ngozi. Aidha, kwa upande wa huduma za watoto Hospitali imeendelea kutoa huduma za watoto wachanga (Neonatology) ambapo jumla ya wagonjwa 1,872 walipatiwa huduma ikilinganishwa na wagonjwa 1,473 waliopatiwa huduma kipindi cha mwaka 2022/23 na kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma hiyo kufikia 3,345. Huduma kwa wagonjwa mahututi (Critical Care) ilitolewa kwa wagonjwa 904 ikilinganishwa na wagonjwa 866 katika kipindi cha mwaka 2022/23 na kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma hiyo kufikia 1,770.

**219. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo jumla ya vipimo 34,090 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa 415, CT Scan vipimo 2,050, X-Ray vipimo 10,480, Fluoroscopy vipimo 1,042 na Ultrasound vipimo 20,103. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya vipimo vya **maabara** 155,660 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 130,167 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 92 ikilinganishwa na asilimia 90 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**220. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imeendelea na **uboreshaji wa miundombinu** ya kutolea huduma. Katika kipindi hiki Hospitali imeanza ujenzi wa jengo maalum la upasuaji wa moyo, mishipa ya fahamu na ubongo kwa fedha za ndani na michango ya wadau. Jengo hili likikamilika litakuwa na vyumba vitatu (3) vya upasuaji na wodi maalum ya wagonjwa mahututi (ICU) yenye uwezo wa vitanda sita (6). Jengo hili limekadiriwa kutumia kiasi cha Shilingi 700,000,000. Vilevile katika mwaka wa fedha 2023/24 Hospitali imeweza kupata mashine ya MRI kutoka katika mradi wa ORIO, mashine hii imesimikwa na kuanza kutoa huduma, ambapo jumla ya vipimo 415 vimefanyika.

**221. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha ubora wa huduma na kuimarisha huduma kwa mteja, Hospitali kwa kutumia wataalam wa ndani imeweza **kutengeneza gari dogo maalum la kubebea wagonjwa ndani ya Hospitali**. Gari hili linatumia umeme na ni mbadala wa 'Wheel chairs and Stratchers'. Aidha, kwa kutumia wataalam wa ndani, Hospitali imebuni mfumo wa 'automatic temperature control' katika chumba cha watoto wachanga na watoto njiti. Pia, mfumo wa e-Medical unaotumika katika shughuli mbalimbali za Hospitali ikiwemo kuona wagonjwa umebuniwa na wataalam wetu na umefungwa katika baadhi ya Hospitali za kanda, Taifa na Hospitali binafsi. Wabunifu hawa wametambuliwa na kupewa hati za ufanyakazi hodari na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya Mei Mosi.

**222. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea **kuratibu mafunzo** kwa wataalam, ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla wataalam 42 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kati ya hao wataalam 19 wanasomeshwa kupitia mapato ya Hospitali na wataalam 23 Wanagharamiwa na Wizara. Aidha, jumla ya **ajira za mkataba 606** zilitolewa na Hospitali ili kupunguza upungufu wa watumishi. Kati yao 72 ni Madaktari 286 ni Wauguzi na 248 wa kada nyingine.

**223. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha huduma za Kibingwa na kibingwa bobezi zinawafikia wananchi waliombali na vituo vya kutolea huduma, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 7,143 walipatiwa huduma katika mikoa ya Songwe, Iringa, Rukwa pamoja na Halmashauri mbili (2) za mkoa wa Mbeya ambazo ni Mbarali na Busokelo. Kati yao wagonjwa 6,788 walipatiwa huduma za Macho, 241 huduma za upasuaji wa mifupa na 114 huduma za moyo na magonjwa ya ndani ikilinganishwa na wagonjwa 4,028 waliopatiwa huduma za mkoba kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**224. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza **Sera ya kutoa msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo, Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 603,730,000 kwa wagonjwa 17,700 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 526,675,000 kwa wagonjwa 16,490 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na kumuona daktari, kulazwa pamoja na upasuaji kwa akinamama wajawazito (Caesarian Section).

**225. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 97 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ikilinganishwa na wagonjwa 86 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa waliohudumiwa ni kutoka nchi za Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Aidha, Hospitali imehudumia raia wa kigeni kutoka nchi za China, Zambia na Msumbiji. Vilevile, kutokana na kuimarika kwa huduma za ubingwa wa Moyo, Mapafu na Radiolojia Hospitali imeendelea

kuzijengea uwezo nchi za Malawi na Zambia katika kutoa matibabu hayo.

**226. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhana ya kufanya **tafiti** za ndani ili kuboresha matibabu kwa wananchi, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilifanya tafiti juu ya ugonjwa wa Sikoseli kwa kutumia taarifa za watoto 264 waliolazwa. Lengo la utafiti huu ni kutathmini mwenendo wa matibabu na athari zitokanazo na ugonjwa wa Seli Mundu (Sikoseli) kwa watoto. Matokeo ya utafiti huo yalibaini miongoni mwa sababu zinazoongoza kwa watoto wenye ugonjwa wa Sikoseli kulazwa Hospitali ni maumivu makali ya mwili asilimia 68 maambukizi ya vijidudu vya magonjwa asilimia 44 na upungufu mkubwa wa damu asilimia 28. Sambamba na matokeo haya, utafiti ulibaini matumizi hafifu ya dawa ya hydroxyurea kwa asilimia 11.4 kutokana na kuchelewa kuanzishiwa matibabu katika vituo vya chini pamoja na Pen V asilimia 26. Dawa hizi husaidia kupunguza makali ya ugonjwa wa Sikoseli na maambukizi ya bakteria. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha umuhimu wa kuwa na mikakati ya kuongeza matumizi ya dawa tajwa ili kupunguza madhara na gharama zitokanazo na ugonjwa wa Sikoseli.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando**

**227. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya Rufaa Kanda Bugando hutoa huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi katika Mikoa nane (8) ambayo ni Mwanza, Geita, Simuyu, Mara, Shinyanga, Tabora, Kagera na Kigoma yenye jumla ya wakazi wapatao milioni 22**.** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 365,261** ikilinganishwa na wagonjwa 336,340 waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 27,116 na wagonjwa wa nje ni 338,145.

**228. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za kibingwa na ubingwa bobezi** katika eneo la tiba kama ifuatavyo: Matibabu ya figo, Matibabu ya Kisukari, Matibabu ya magonjwa ya damu, Matibabu ya magonjwa ya kuambukiza, Matibabu ya njia ya chakula,

Matibabu ya Ngozi, Matibabu ya magonjwa ya watoto, Matibabu ya saratani, Matibabu ya mfumo wa upumuaji, Huduma za dharura na ajali, Matibabu ya magonjwa ya afya ya akili, huduma ya tiba viungo na utengemano. Pia, Hospitali imeendelea kutoa huduma za Upasuaji wa ubingwa bobezi kwenye maeneo ya Kubadilisha nyonga na magoti, Upasuaji wa kinywa na Meno, Upasuaji wa Watoto wenye mdomo sungura (cleft tip/palate), Upasuaji wa macho, Upasuaji wa Koo, pua na masikio, Upasuaji wa Kifua na moyo, Upasuaji wa Ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo, Upasuaji wa Mfumo wa mkojo, Upasuaji sanifu, Upasuaji maalumu wa Watoto, Upasuaji wa matundu madogo na Huduma ya Viungo Tiba (Saidizi) na Vifaa Tiba Saidizi (Orthopedic – Prosthetics and Orthotics Unit). Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 zaidi ya wagonjwa 12,836 walifanyiwa upasuaji kati yao 12,600 walifanyiwa upasuaji mkubwa na 236 upasuaji mdogo.

**229. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wagonjwa 15,379 wamepatiwa huduma ya matibabu ya Saratani kati ya hao, wagonjwa 10,386 ni wagonjwa wa nje 1,155 ni wagonjwa wa kulazwa, wagonjwa 2,802 walipatiwa tiba ya saratani kwa kutumia dawa (Chemotherapy) na wagonjwa 1,036 walipatiwa tiba kwa kutumia mionzi (Radiotherapy). Aidha, utoaji wa huduma hizo umepunguza adha ya wagonjwa kufuata huduma hizo mbali kwa kupewa rufaa kwenda Taasisi ya Saratani Ocean Road Dar es Salaam.

**230. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 vipimo 58,959 vya radiología vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa 2,572 CT-Scan vipimo 7,718 X-Ray vipimo 22,530, Ultrasound vipimo 25,588, Mammography vipimo 223 na Fluoroscopy vipimo 328. Katika kipindi hiki, jumla ya **vipimo vya maabara** 853,116 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 768,011 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Aidha, **hali ya upatikanaji wa dawa** ni asilimia 97 ikilinganishwa na asilimia 95 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**231. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea **kuratibu mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wataalamu 52 wamepelekwa masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi, kati ya hao jumla ya watumishi 16 wamepata ufadhili wa **"Dkt. Samia Afya Scholarship"** na watumishi 36 wamepata ufadhili wa Hospitali kupitia fedha za mapato ya ndani. Pia, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imeajiri jumla ya watumishi 810 kwa njia ya mikataba na wakujitolea. Aidha, Hospitali imeingia mkataba ya ununuzi wa Mashine Tiba ya Mionzi kwa ajili ya matibabu ya Saratani yenye thamani ya Shilingi 1,540,639,241 kwa ufadhili wa Serikali. Ununuzi wa mashine hii utasaidia kuongeza idadi ya wagonjwa watakao hudumiwa toka wagonjwa 80 hadi 160 kwa siku. Pia, kupitia mapato ya ndani Hospitali imefanya ununuzi wa C-Arm machine kwa ajili ya Internvation Radilogy yenye thamani ya Shilingi 407,000,000 patients monitors Shilingi 455,400,000, Pentax Gastroscope EG 2990K Shilingi 32,338,726 na Complete Dental Chair Shilingi 15,590,700. Hospitali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la gorofa kwa wagonjwa wa nje (OPD Complex) hatua ilipofikia kwa sasa ni usanifu wa jengo na michoro jumla ya Shilingi 80,000,000 ameshalipwa Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi hiyo. Vile vile, Shilingi 100,000,000 kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa vyumba 12 kwa ajili ya kuongeza vyumba vya kutolea huduma kwa wagonjwa wa nje. **232. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba** kwa vituo 27 ambavyo ni,
Hospitali ya rufaa ya mkoa Mara, Hospitali ya rufaa ya mkoa Maweni, Hospitali ya rufaa ya mkoa Kagera, Hospitali ya rufaa ya mkoa Katavi, Hospitali ya rufaa ya mkoa Shinyanga, Hospitali ya rufaa ya mkoa Simiyu, Hospitali ya wilaya Ruangwa, Hospitali ya wilaya Magu, Hospitali ya wilaya Nyamagana, Hospitali ya wilaya Igunga, Hospitali ya Kabanga, Hospitali ya Tarime, Hospitali ya Kagondo, Hospitali ya Bwisya, kituo cha afya Nyarugusu, kituo cha afya Karume, Hospitali ya Sumve, Hospitali ya Inyonga, Hospitali ya Biharamulo na Hospitali teule ya Songambele ambapo jumla ya wagonjwa 6,095 walipatiwa huduma kati yao wagomjwa 558 walifanyiwa Upasuaji.

**233. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza **Sera ya kutoa msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama,

Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 3,619,939,055 kwa wagonjwa 22,277 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 3,195,853,658 kwa wagonjwa 9,596 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na, mionzi tiba, utoaji wa dawa za mionzi, magonjwa ya akili, huduma za matibabu ya watoto wachanga, mama wajawazito, huduma ya usafishaji wa damu na figo na huduma kwa wazee wasiojiweza.

**234. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 194 ikilinganishwa na wagonjwa 139 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hospital imehudumia raia wa kigeni kutoka nchi za China, Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia. Pia, Hospitali imefanya **tafiti** 125 katika maeneo mbalimbali ya afya. Tafiti hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika kutengeneza miongozo mbalimbali ya matibabu hapa nchini, kati ya miongozo ni ya usugu wa dawa za Antibayotiki, ambapo Hospitali ilipata cheti cha kufanikiwa kuwa na tafiti moja kati ya hamsini bora nchini Tanzania iliyohusu matumizi ya dawa ya ‘’Hydroxyurea” kwa wagonjwa wenye selimundu kupuguza uwezekano wa kupata kiharusi. Vilevile Hospitali inaendelea na utafiti wa jani la mgomba katika kuwezesha matibabu ya vidonda vya kuungua na moto.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC**

**235. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali ilihudumia **jumla ya wagonjwa 340,455** ikilinganishwa na Wagonjwa 339,945 waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya hao wagonjwa wa nje (OPD) ni 326,445 na wagonjwa wa ndani (IPD) ni 14,010. Hospitali imeendelea kutoa **huduma za kibingwa na ubingwa bobezi** ambapo ubadilishaji wa nyonga wagonjwa 96 walipatiwa huduma hiyo ikilinganishwa na wagonjwa 83 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23; Upasuaji wa laparoskopiki hususan operesheni za kolorektali kwa wagonjwa watano (5) ikilinganishwa na wagonjwa watatu (3) kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, Hospitali imeendesha Kliniki ya utasa na endokrinolojia wagonjwa 809; upandikizaji wa kornea wagonjwa 66, Upasuaji wa

Saratani wagonjwa 6,910, matibabu ya Saratani wagonjwa 5,902, upasuaji wa njia ya mkojo wagonjwa 1,780, matibabu ya ngozi wagonjwa 8,644, na matibabu ya macho wagonjwa 15,756. Teknolojia hizo za kisasa hutoa nafuu ya haraka ya baada ya operesheni na kupunguza gharama kwa wagonjwa. Kwa kutoa huduma hizo ndani ya nchi kumegharimu kiasi cha Shilingi 760,000,000 Aidha, endapo huduma hizi zingefanyika nje ya nchi zingeigharimu Serikali jumla ya kiasi cha Shilingi 2,280,000,000.

**236. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za bingwa bobezi** za kimatibabu, ambapo wagonjwa wa njia ya mkojo na kibofu 1,302 walipatiwa huduma hiyo, wagonjwa 167 walipatiwa huduma ya upasuaji wa Kinywa na Uso (Oral Maxillofacial), wagonjwa 19 walipatiwa huduma ya upandikizaji wa Taya, wagonjwa 17,397 walipatiwa huduma ya ngozi, wagonjwa 334 walipatiwa huduma za Viungo Bandia (Prostheses), Vifaa 998 vya Msaada wa Viungo (Orthoses) vilitengenezwa na wagonjwa 576 walipatiwa huduma ya upasuaji wa Retina ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2022/23 ambapo wagonjwa wa njia ya mkojo na kibofu walikuwa 1,345, Huduma ya Upasuaji wa Kinywa na Uso (Oral Maxillofacial) wagonjwa walikuwa 154, Upandikizaji wa Taya walikuwa wagonjwa 18, wagonjwa wa ngozi walikuwa 17,380, Viungo bandia (Prostheses) 328 vilitengenezwa kwa ajili ya wagonjwa, na vifaa vya msaada wa viungo (Orthoses) 987 vilitengenezwa na wagonjwa 594 walipatiwa huduma ya Upasuaji wa Retina.

**237. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** ambapo wagonjwa 1,089 walifanyiwa kipimo cha MRI, vipimo vya CT Scan wagonjwa 3,627, vipimo vya Ultrasound wagonjwa 10,315, vipimo vya X-Ray wagonjwa 15,775, ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23 ambapo Hospitali ilitoa huduma za uchunguzi ambapo wagonjwa 1,182 walifanyiwa kipimo cha MRI, vipimo vya CT Scan wagonjwa 3,642, vipimo vya Ultrasound wagonjwa 11,532 na vipimo vya X-Ray wagonjwa 17,709. Kwa upande wa **vipimo vya maabara**, Taasisi ilifanya jumla ya vipimo 372,879 ikilinganishwa na vipimo 1,557,517 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, hali

ya **upatikanaji wa dawa** katika Hospitali ni asilimia 98.5 ikilinganishwa na asilimia 98 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**238. Mheshimiwa Spika,** Hospitali inaendelea kuendeleza rasilimali watu ikiwemo **kusomesha wataalam** wa kozi za kibingwa na ubingwa bobezi za muda mfupi na mrefu. Katika kipindi hiki, jumla ya Wataalam 154 wapo masomoni katika fani mbalimbali za Kibingwa ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kukabiliana na upungufu wa Watumishi, Hospitali imeajiri jumla ya watumishi 44 wa mikataba ikiwemo madaktari tisa (9), wauguzi 17 na wafamasia 18 ambao wanagharamiwa kwa mapato ya ndani ya Hospitali.

**239. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea na **uimarishaji wa miundombinu**, ambapo ujenzi wa vyumba 11 vya upasuaji umefikia wastani wa asilimia 60 hadi 75. Vyumba hivyo vitasaidia kupunguza msongamano wa wahitaji wa huduma za upasuaji uliopo kwa sasa. Aidha, Hospitali inaendelea na ujenzi wa jengo la mionzi (bunker) ambapo kwa sasa ujenzi umefikia asilimia 79 ya utekelezaji na umegharimu kiasi cha Shilingi 3,000,000,000. Hospitali kwa kushirikiana na Omah Foundation imeendelea na ujenzi wa mabweni (hostel) za wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani, ambapo ujenzi huu umefikia asilimia 72. Pia Hospitali kwa kushirikiana na kampuni ya Roche imeendelea na ujenzi wa maabara Jumuishi (KCMC Centre of Excellence Laboratory) ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 59. Vilevile Hosiptali imendelea kuboresha huduma za mama na mtoto kwa kukarabati na kuboresha miundombinu ya wodi ya wazazi ambapo ukarabati huu umekamilika kwa asilimia 98.

**240. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 3,574 walipatiwa huduma. Kati yao wagonjwa 1,422 walipatiwa huduma za saratani, macho na VVU/UKIMWI katika maeneo ya Rombo, Moshi DC, Marangu na Same ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2022/23, ambapo wagonjwa 2,520 walihudumiwa kupitia huduma za Mkoba. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imetoa huduma kwa wagonjwa wa msamaha 4943 ambapo jumla ya Shilingi 16,221,789,512 zimetumika ikilinganishwa

na kipindi kama hiki 2022/23 ambapo Hospitali ilitoa **misamaha** kwa wagonjwa 6,084 kwa gharama ya **Shilingi 19,189,800,400.** Huduma zilizoongoza kutolewa kwa njia ya msamaha zilikuwa ni matibabu ya Saratani, Dawa, Vipimo na Kulazwa.

**241. Mheshimiwa Spika**, Katika dhana ya kuendeleza **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilipokea jumla ya wagonjwa 384 waliotoka katika nchi za Kenya, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na hii ni kutokana na uboreshaji wa huduma za Kibingwa na bobezi zinazofanyika. Aidha, katika kipindi Julai 2023 hadi Machi 2024, Hospitali iliwapatia huduma za matibabu jumla ya raia wa kigeni 333 kutoka nchi mbalimbali waliofika nchini kwa shughuli mbalimbali, wakiwemo 291 kutoka Afrika Mashariki na wengine kutoka Marekani, Uingereza na Canada.

**242. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa **tafiti,** jumla ya tafiti 49 zimefanyika na tafiti hizo zimejikita katika maeneo ya magonjwa ya kuambukiza, usimamizi wa matibabu ya dharura, uchunguzi wa vinasaba vya magonjwa kama VVU na uchunguzi wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama Kisukari na shinikizo la damu. Tafiti hizo hufanyika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Duke University, mashirika ya utafiti kama Tropical Diseases Research Centre. Ushirikiano huu umesaidia kuleta utaalamu na rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kufanya tafiti zenye tija zaidi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato**

**243. Mheshimiwa Spika,** Hospitali ya rufaa ya kanda chato imeendelea kuhudumia mikoa mbalimbali ya kanda ya ziwa na nchi za jirani kama ifuatvyo , Kagera Kigoma, Geita, baadhi ya wilaya za mkoa wa Shinyanga na nchi za jirani mfano Burundi, aidha katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imetoa huduma kwa **jumla ya wagonjwa 40,370** ikilinganishwa na wagonjwa 15,681 waliohudumiwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 2,234 na wagonjwa wa nje ni 38,136. Katika kutekeleza dhana ya ubunifu, Hospitali ilianzisha **huduma mpya** sita (6) za ubingwa bobezi ambazo ni huduma ya kuchuja damu (Dialysis)(481), huduma ya kliniki ya moyo wagonjwa (12,320), kliniki ya kibingwa ya mfumo wa

chakula (Endoscopy) (125), huduma za uchunguzi wa mfumo wa hewa (bronchoscopy 26), uchunguzi wa kutambua wingi wa VVU (HVL) na huduma ya kibingwa ya pua na koo (ENT) (79).

**244. Mheshimiwa Spika,** Huduma za ubingwa bobezi **zilizoendelea kutolewa** ni pamoja na huduma za afya ya kina mama wajawazito na uzazi, huduma za Watoto, huduma za magonjwa ya ndani, huduma za upasuaji na huduma za mfumo wa mkojo. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wagonjwa 9,000 walipewa huduma ya afya ya uzazi ikilinagishwa na wagonjwa 7,000 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23, jumla ya wagonjwa 6,053 walipatiwa huduma za Watoto ikilinganishwa na wagonjwa 5,090 kwa mwaka 2022/23, jumla ya wagonjwa 4,443 walipatiwa huduma ya upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 2,252 kwa mwaka 2022/23, jumla ya wagonjwa 6,372 walipatiwa huduma ya magonjwa ya ndani ikilinganishwa na wagonjwa 5,126 mwaka 2022/23. Pia, Hospitali imeanzisha kliniki maalum ya magonjwa ya moyo kwa kushirikiana karibu na Taasisi ya moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) ambapo hadi sasa wagonjwa 12,320 wamefaidika na huduma hiyo ambayo ni endelevu kwa kila wiki moja ndani ya kila mwezi.

**245. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 26,006 vya radiolojía vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI vilikuwa 118, CT Scan vipimo 482, X-Ray vipimo 12,690 na Ultrasound vipimo 12,207 na ECHO 509. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **vipimo vya maabara 34,414** vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 9,700 vilivyofanyika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Vilevile hali ya **upatikanaji wa dawa** ni asilimia 97 ikilinganishwa na asilimia 96 kipindi kama hiki mwaka 2022/23.

**246. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kuratibu **mafunzo** ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wataalamu 17 wapo masomoni katika fani mbalimbali za kibingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kati ya wataalmu hawa 17, watumishi wanne (4) wanasomeshwa kupitia mapato ya ndani, sambamba na hili Hospitali kupitia

mapato ya ndani imeweza kuajiri kupitia mikataba ya muda taribani watumishi 30 wa kada mbalimbali.Pia, Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba**, ambapo jumla ya wagonjwa 1,150 walipatiwa huduma na kati yao wagonjwa 350 walipatiwa huduma za afya ya uzazi, 452 huduma za watoto, 112 huduma za upasuaji na 236 huduma za magonjwa ya ndani. Katika kutekeleza **Sera ya msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 94,679,090** kwa wagonjwa 314 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 16,700,670 kwa wagonjwa 79 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na huduma ya Dawa, huduma za maabara na Upasuaji.

**247. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii**, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 12 kutoka nchi za Rwanda na Burundi. Aidha, katika jitihada za kuboresha huduma Hospitali kupitia tafiti, Hospitali imefanya tafiti nne (4) zinazo husu uboreshaji huduma matibabu mbalimbali. Tafiti hizo zipo katika hatua mbalimbali ambapo zimelenga kutambua vimelea vya wadudu wanao sababisha madonda ya tumbo na magonjwa ya kuhara kwa watoto tafiti hizi mbili (2) tayari zipo katika hatua za kuchapisha.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara**

**248. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kuwekeza katika Hospitali hii ili kuiwezesha kuwa na uwezo wa kutoa huduma nyingi za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali imehudumia **jumla ya wagonjwa 22,122** ikilinganishwa na wagonjwa 7,918 waliohudumiwa kipindi kama hiki mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) ni 21,121 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) ni 1,001.

**249. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali **imeendelea kutoa huduma za kibingwa bobezi** ambapo jumla ya wagonjwa sita (6) walifanyiwa upasuaji wa fuvu la kichwa kuondoa damu iliyovilia, pia wagonjwa 134 walifanyiwa

upasuaji wa kibingwa, wagonjwa 794 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya moyo ya kibingwa, wagonjwa 1,327 walipatiwa matibabu ya kibingwa ya magonjwa ya mifupa, wagonjwa 977 walipatiwa huduma za dharura na wagonjwa 473 walipatiwa matibabu ya magonjwa ya akina mama na uzazi.

**250. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za uchunguzi** wa kibingwa ambapo katika kipindi cha Julai 2023 mpaka machi 2024, wagonjwa 172 walifanyiwa kipimo cha MRI, wagonjwa 388 walifanyiwa kipimo cha CT- Scan, wagonjwa 2,607 walifanyiwa kipimo cha ultra-sound na wagonjwa 3,080 walifanyiwa kipimo cha X-Ray. Kwa **upande wa maabara** jumla ya vipimo 40,331 vilifanyika ikilinganishwa na vipimo 12,498 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Pia Hospitali imenunua na kusimika mashine kubwa mpya tano na kuifanya maabara kuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia wagonjwa kwa muda mfupi. Mashine hizo ni Erba XL 640 Chemistry analyser, MindRay CL I 900 Hormone analyser, Dynamind DH 76 Haematology analyser, Coagulation analyser ECL 105 na Q line allergic scanner. Mafunzo kwa wataalam juu ya matumizi
yake yamefanyika.

**251. Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza wigo wa huduma za kibingwa, Hospitali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya imefanikiwa **kuwaendeleza wataalam** wake katika huduma za kibingwa ambapo jumla ya madaktari 13 wamepelekwa kujiendeleza katika fani za ubingwa wa mifupa, watoto, macho, upasuaji, magonjwa ya ndani magonjwa ya kina mama, uzazi na ngozi. Aidha, Hospitali imeajiri **watumishi wa mkataba** 49 ambapo kati ya hao madaktari ni watano (5) na wauguzi nane (8) ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi.

**252. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za kibingwa za Mkoba** kwa ajili ya matibabu ya mifupa na meno ambapo jumla ya wagonjwa 175 walipatiwa matibabu ya meno na wagonjwa 416 walipatiwa huduma ya matibabu ya mifupa. Katika kutekeleza Sera ya kutoa huduma ya **msamaha** kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu, Hospitali imetoa msamaha wenye gharama ya Shilingi 14,091,153

kwa wagonjwa 241 ikilinganishwa na Shilingi 1,689,500 kwa wagonjwa 24 mwaka 2022/23. Huduma zilizoongoza kwa kutolewa msamaha ni huduma za dawa, vipimo, upasuaji na huduma za kumuona daktari.

**253. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii** nchini, Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 76 kutoka nchi ya Msumbiji pamoja na kuhudumia raia wa kigeni waliopo nchini kutoka India, China, Nigeria, Denmark, Pakistan na Uingereza. Mafanikio haya yametokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika Hospitali hii na Mkoa wa Mtwara kupakana na nchi za Msumbiji na Comoro. Katika eneo la **utafiti,** Hospitali inafanya utafiti wa kimatibabu wenye lengo la kuelewa sababu zinazohusiana na mifupa iliyovunjika kwenye mfupa wa paja kwa watu wanaoathiriwa na ajali za barabarani kusini mwa Tanzania. Utafiti huu utasaidia kutoa takwimu sahihi kuhusu kiwango cha mifupa ya paja iliyovunjika kwa watu walioathirika na ajali za barabarani na kusaidia kuboresha mikakati ya matibabu na kuzuia ajali za barabarani zinazosababisha mifupa kuvunjika.

**Hospitali ya CCBRT**

**254. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa huduma mbalimbali za kibingwa na bobezi, ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **wagonjwa 86,211** walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 90,577 waliohudumiwa katika mwaka 2022/23. Kati yao wagonjwa wa nje (OPD) ni 82,152 na wagonjwa wa ndani (IPD) ni 4,059. Aidha, **wagonjwa wenye ulemavu** waliohudumiwa walikuwa 5,614 ikilinganishwa na wagonjwa 5,661 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya wagonjwa hao waliohudumiwa wengi wao walikuwa na ulemavu wa macho, mdomo sungura, miguu kifundo, mtindio wa ubongo, ulemavu mwingine wa viungo na fistula kwa wanawake. Katika kipindi hiki, jumla ya wanawake wajawazito waliojifungua ni 737, kati yao wanawake 8 sawa na asilimia 1.1 walikuwa wana ulemavu; mabinti wenye mimba za utotoni 88 sawa na asilimia 11.9.

**255. Mheshimiwa Spika**, Hospitali imetoa **Huduma mpya** tatu (3) ambazo ni upasuaji kwa njia ya matundu madogo (Laparascopic surgery) ikiwemo kutoa Kizazi (Total Laparoscopic Hysterectomy) wagonjwa wawili (2); kutoa uvimbe kwenye mayai ya uzazi (Laparoscopic Ovarian Cystectomy) wagonjwa nane (8), kufunga mirija ya uzazi kama njia ya uzazi wa mpango (Laparoscopic Tube Ligation) wagonjwa watatu (3), upasuaji wa ndani ya kizazi kwa njia ya kamera (Histerescopy and Resectoscopy) wagonjwa tisa (9) na huduma ya uchunguzi kwa njia ya matundu madogo (Diagnostic Laparascopy) wagonjwa 22. Huduma mpya nyingine ni Iris claw Lenses ambapo wagonjwa 85 ambao endapo jicho haliwezi kuwekewa kioo (artificial lens) cha bandia cha kawaida baada ya upasuaji wa mtoto wa jicho hufanyiwa upasuaji maalum wa kibobezi na kuwekewa kioo spesheli kinacho shikamanishwa na mboni. Upasuaji huu unaepusha ulemavu wa kutokuona na umechukua nafasi ya ule wa awali (AC IOL) ambao baadaye mgonjwa alikuwa anapata madhara na wengine kupoteza uoni kabisa. Hospitali pia imeongeza huduma ya ziada ya Upasuaji wa makengeza kwa watoto wasiopungua 19. Hii ni ziada ya ule upasuaji uliozoeleka wa resess-resect ambapo misuli ya oblique ya macho hubanwa kitaalam ili kurekebisha kengeza la juu au chini. Upasuaji huu humwezesha mtoto kuboresha uoni wake na mwonekano wake. Bila upasuaji huu watoto hao huishia kuwa na uoni hafifu au kupoteza kabisa uwezo wa kuona achilia mbali unyanyapaa wanaoupata kwa kuwa na mwonekano wa kengeza.

**256. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa **huduma za upasuaji zilizoendelea**, jumla ya wagonjwa 5,008 walifanyiwa upasuaji. Kati yao, wagonjwa 3,558 walikuwa na matatizo ya Macho, wagonjwa 288 Fistula itokanayo na Uzazi; wagonjwa 959 upasuaji wa Mifupa; wagonjwa 72 upasuaji wa Mdomo Wazi (Cleft lip/palate), watoto 56 wenye Miguu Kifundo (Clubfoot) walitibiwa kwa njia ya upasuaji na watoto 295 wenye miguu kifundo walitibiwa kwa njia ya Ponseti, wagonjwa 127 wenye matatizo ya figo walipata huduma ya kusafisha damu na wagonjwa 606 walipata viungo saidizi. Aidha, Hospitali kupitia kitengo chake cha huduma za utengemao kilichopo Moshi ilitoa huduma ya

utengemao kwa jumla ya wagonjwa 1,882. Hospitali iliendelea kutoa huduma za kibobezi za upasuaji wa macho kwa wagonjwa 743 ikilinganishwa na wagonjwa 1,147 kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Wagonjwa hao walipatiwa huduma za upasuaji wa mtoto wa jicho kwa njia ya vitundu vidogo (Phacoemulsification), Upasuaji wa Pazia la jicho, Makengeza, na Upasuaji wa nyonga na goti bandia. Huduma hizo zimeboresha maisha ya watu ambao wangepaswa kuwa walemavu wa macho au viungo vingine.

**257. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024, Hospitali imeimarisha **huduma za uchunguzi** za Maabara zinazoendana na huduma za kibingwa na bingwa bobezi kwa kudumisha utendaji wa vifaa vya maabara ambapo jumla ya vipimo 120 vilitolewa. Katika kipindi hiki, wagonjwa 277 walifanyiwa kipimo cha CT - Scan, wagonjwa 6,037 walifanyiwa kipimo cha ultra-sound na wagonjwa 6,209 walifanyiwa kipimo cha X-Ray. Sambamba na hilo, Hospitali imefanya ununuzi wa mashine ya kisasa ya utrasound ya macho, (B-Scan ultrasonograph) kwa ajili ya upimaji wa kibobezi wa pazia la nyuma ya jicho. Hospitali pia imeweza kupeleka wataalam wake katika kozi mbalimbali nje na ndani ya nchi kwa ufadhili wa Hospitali ambapo jumla ya wataalam tisa (9) wapo masomoni kwa kozi za kibingwa na ubingwa bobezi wa masuala ya macho na utengamao.

**258. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza sera ya kutoa **huduma kwa msamaha** kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama, Hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya **Shilingi 6,695,986,236** kwa wagonjwa 4,552 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 9,984,349,215 kwa wagonjwa 9,711 kwa kipindi cha mwaka 2022/23. Upatikanaji wa dawa ulikuwa kati ya asilimia 90 mpaka asilimia 95.

**259. Mheshimiwa Spika,** Hospitali imeendelea kutoa **huduma za mkoba** kwa wagonjwa 678 katika kipindi cha 2023/24. Aidha, kupitia kitengo cha huduma za utengemao kilichopo Moshi, huduma za mkoba zilitolewa kupitia vituo vya utengemao vilivyoko kwenye jamii (Community Support Units) kwa kuhudumia

wateja 583 na watu 664 walihudumiwa kupitia huduma za nyumbani katika Mkoa wa Kilimanjaro. Katika kutekeleza dhana ya **Tiba Utalii**, Hospitali imekuwa ikitoa huduma za matibabu ya afya ya macho, vifaa saidizi vya macho, mifupa na Fistula ya uzazi kwa wageni kutoka Comoro, Kenya, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Msumbiji na wageni wanaoishi nchini kama raia wa Ubelgiji, Ireland ya Kaskazini, India na Nigeria. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 135 ikilinganishwa na wagonjwa 119 kipindi kama hicho mwaka 2022/23.

**Hospitali za Rufaa za Mikoa**

**260. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **wagonjwa 2,309,964** walihudumiwa katika Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa ikilinganishwa na wagonjwa 2,529,971 waliohudumiwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati yao, wagonjwa wa nje (OPD) walikuwa 2,052,274 na wagonjwa wa kulazwa (IPD) walikuwa 257,690. Aidha, katika kutekeleza Sera ya Afya ya kuhakikisha haki ya kila mtanzania anapata huduma bila kuangalia uwezo wa kulipia, Hospitali zilitoa msamaha kwa **wagonjwa 302,999** sawa na asilimia 13.1 ya wagonjwa wote waliohudumiwa katika ngazi hiyo kwa gharama ya **Shilingi 2,920,786,230**. **Kiambatisho Na. 5.**

**261. Mheshimiwa Spika**, Serikali ina nia ya kuhakikisha kuwa Hospitali zote za Rufaa za Mikoa zinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za fani za kibingwa 14 ambazo ni magonjwa ya akinamama, afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, Afya ya watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, afya ya macho, magonjwa ya Ngozi, huduma za dharura, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi na Radiolojia. **Kiambatisho Na. 6** kinaonesha hali ya utoaji huduma muhimu 14 za kibingwa katika Hospitali za rufaa za mikoa.

**262. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeweza kuongeza idadi ya **Madaktari bingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa** kutoka 316 Machi 2023 hadi kufikia Madaktari bingwa 328 Machi 2024. Aidha,

hadi kufikia Machi 2024, Hospitali 8 sawa na 29% zimeweza kufikisha lengo la kutoa huduma za fani nane (8) za Kibingwa ikilinganishwa na Hospitali 5 mwaka 2022/23**. Kiambatisho Na. 7** kinaonesha hali ya madaktari bingwa katika Hospitali za rufaa za mikoa.

**263. Mheshimiwa Spika,** Hospitali za Rufaa za Mikoa **zimeendelea kutoa huduma za kibingwa** za Afya ya uzazi, mama na mtoto kwa akinamama wanaohudhuria katika Hospitali hizi pamoja na wale wanaopewa rufaa kutoka katika vituo vya Afya ya Msingi kwa kuhitaji kupatiwa huduma za kibingwa. Katika kipindi hiki, jumla ya akinamama 46,604 walijifungua katika Hospitali hizi ikilinganishwa na akinamama 66,577 waliojifungua katika mwaka 2022/23.

**264. Mheshimiwa Spika,** Hospitali za Rufaa za Mikoa zimetoa **huduma za Mkoba** wa kibingwa kwa kushirikiana na watumishi wa vituo vilivyopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya wagonjwa 35,281 walihudumiwa na kati yao 2,356 walifanyiwa upasuaji.

**UTAYARI, UDHIBITI NA KUKABILIANA NA MAGONJWA YA MILIPUKO NA MAJANGA**

**265. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kusimamia, kuratibu na kutekeleza afua za kujiandaa na kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza, milipuko na matukio mengine ya dharura za afya, ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 **dharura kubwa zilizojitokeza ni Maporomoko yaliyotokea Hanang, Mlipuko wa Kipindupindu** na **Mafuriko** yaliyosababisha athari nyingi ikiwemo za kiafya.

**266. Mheshimiwa Spika,** Katika janga la maporomoko lililotokea Hanang mkoani Manyara Mwezi Desemba 2023, Wizara iliratibu **utoaji wa huduma za afya na udhibiti wa athari za kiafya** kwa kupeleka jumla ya wataalam 266 wenye taaluma mbalimbali (Madaktari, Wauguzi, Wafamasia, Wataalam wa afya ya akili, Maafisa Ustawi wa Jamii, wataalam wa Saikolojia, washauri nasaha na wataalam wa afya mazingira) kutoka mikoa

mbalimbali nchini ili kutoa huduma za afya kwa waathirika na kutekeleza afua za kuzuia na kudhibiti magonjwa ya mlipuko yasitokee. Vilevile, jumla ya majeruhi 139 walipatiwa matibabu katika vituo vya kutolea huduma na kupeleka bidhaa za afya zenye thamani ya **Shilingi 652,902,003.06**. Aidha, Wizara ilitoa elimu ya afya kwa jamii, kutibu maji katika ngazi ya kaya, kufanya ukaguzi na kuweka miundombinu ya vyoo vya muda pamoja na ugawaji wa vyandarua 250,000 katika makambi ya waathirika na kaya zilizoathirika.

**267. Mheshimiwa Spika,** Kufuatia mvua juu ya wastani zinazoendelea kunyesha nchini, baadhi ya maeneo yalikumbwa na mafuriko yaliyosababisha athari nyingi ikiwemo athari za kiafya. Wizara kwa kushirikiana na timu za wataalam wa Mikoa ya Lindi, Pwani na Morogoro imeendelea kutekeleza afua za kinga na tiba za athari za kiafya zilizojitokeza ikiwemo kuhakikisha urejeshwaji na uendelevu wa huduma za afya katika vituo vilivyoathirika. Jumla ya **vidonge 900,000** vya kutibu maji (aquatabs) katika ngazi ya kaya vilipelekwa Mkoani Lindi, Pwani na Morogoro.

**268. Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuendelea na utekelezaji wa **afua za utayari wa kukabiliana na dharura** mbalimbali nchini, kati ya mwezi Desemba 2023 hadi Machi 2024 jumla ya mikoa 19 iliathirika na mlipuko wa kipindupindu kwa nyakati tofauti. Mikoa iliyoathirika ni Arusha, Manyara, Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Ruvuma, Kilimanjaro, Katavi, Kagera, Geita, Tabora, Mara, Dar es salaam, Kigoma, Pwani, Rukwa na Morogoro. Katika kudhibiti mlipuko huo Wizara imetekeleza afua mbalimbali na kufanikiwa kudhibiti mlipuko wa ugonjwa huo katika mikoa 11. Aidha, udhibiti umeendelea katika mikoa nane (8) ya Morogoro, Simiyu, Dar es salaam, Mwanza, Dodoma, Mara, Geita na Pwani. Jumla ya Shilingi 385,683,905 zimetumika kwa ajili ya kugharamia vifaa tiba, dawa za kutibu maji, usafi wa mazingira na wataalam wa kukabiliana na mlipuko huo.

**269. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha uratibu wa kukabiliana na milipuko na majanga, Wizara imeanzisha **vituo vipya vya Operesheni ya Matukio ya Dharura ya Afya ya Jamii (PHEOCs)**

katika Mikoa mitano (5) ya Mara, Tanga, Ruvuma, Rukwa na Mbeya. Vituo hivyo vimewekewa samani na ufungaji wa vifaa vya TEHAMA vyenye thamani ya Shilingi 849,575,000 unaendelea. Idadi hii itawezesha kuwa na jumla ya vituo 16 kutoka 11 vilivyokuwepo kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Vituo vinaratibu afua za kujiandaa na kukabiliana na matukio ya dharura ya afya katika mikoa husika kwa kufanya tathmini ya kubaini matukio ya dharura ya kipaumbele yenye madhara makubwa na uwezekano mkubwa wa kutokea, kuandaa mipango ya kujiandaa kukabiliana na matukio haya, kufanya mazoezi ya utayari dhidi ya matukio haya, kufanya ufuatiliaji wa kila siku wa taarifa za matukio ya dharura yanayoathiri afya ya jamii ndani ya mikoa na matishio kutoka nje ya nchi. Aidha, vituo hivyo pia vinaratibu upelekaji na utendaji wa wataalam wa kudhibiti matukio hayo yanapotokea.

**270. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha huduma za matibabu dhidi ya magonjwa hatari ya kuambukiza na magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuimarisha **upatikanaji wa hewa tiba ya**

**Oksijeni** kwa kununua mitambo 66 ya uzalishaji wa hewa tiba. Kati ya mitambo hiyo, **mitambo 40** imesimikwa katika vituo mbalimbali nchini ambapo mitambo saba (7) imesimikwa katika ngazi ya Taifa, Kanda na Maalum, 19 katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na mitambo 14 imesimikwa katika Hospitali za Wilaya nchini. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za usambazaji na usimikaji wa Mitambo mingine 26. Upatikanaji wa mitambo hii utasaidia kuboresha huduma kwa wagonjwa mahututi ili kunusuru maisha na kuleta unafuu wa gharama kwa wananchi.

**271. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha na kusimamia huduma za **dharura na ajali,** Wizara imekamilisha usimikaji wa vifaa vya EMD katika Hospitali tano (5) ambazo zilikuwa bado hazijapata vifaa vyote kupitia MSD, ikiwemo Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Kigoma, Lindi, Kagera, Katavi na Hospitali ya Lugalo. Aidha, Wizara imeendelea na usambazaji wa magari ya kubebea wagonjwa **603** yaliyonunuliwa na Serikali kwa ajili ya Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Kanda, Maalum na Taifa,

lengo likiwa ni kuimarisha huduma za dharura, ajali na rufaa nchini. Vilevile, Wizara inakamilisha mfumo wa uendeshaji, ufuatiliaji na uratibu wa magari yote ya wagonjwa (ambulance tracking devices) ili kuboresha huduma hizi na kuepusha vifo vinavyozuilika. Mfumo huu utakapokamilika utawezesha wananchi kuita msaada wa magari ya kubebea wagonjwa kupitia namba ya dharura 115 kote nchini ziweze kuwafikia eneo la ajali au alipo mgonjwa wa dharura. Pia, mfumo wa kielektroniki wa takwimu za ajali (Trauma registry) unaendelea kufungwa kwenye idara zote za dharura nchini ili kuratibu taarifa za kiafya za wahanga wa ajali na kuwezesha mikakati ya kuzuia na kupunguza madhara yanayotokana na ajali.

**272. Mheshimiwa Spika**, Ili kuhakikisha idara za dharura zilizojengwa katika Hospitali za ngazi zote zinaendeshwa na watoa huduma wenye ujuzi na weledi, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa mafunzo kwa wataalam wa idara za dharura na ICU. Kwa mwaka 2023/24, Wizara imetoa mafunzo kwa jumla ya **watoa huduma 1,230** hivyo kufikisha jumla ya **watoa huduma 5,385** waliopata mafunzo katika ngazi za halmashauri, mikoa, kanda na Taifa.

**273. Mheshimiwa Spika**, Wizara ilipanga kujenga vituo maalum vya mafunzo ya huduma za dharura kwa vitendo kwa kila kanda. Vituo hivyo vitatumika kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watoa huduma waliopo katika Hospitali zinazozunguka mikoa husika, lengo likiwa ni kuboresha huduma za EMD, ICU na ambulance. Hadi kufikia Machi 2024, Serikali imekamilisha ukarabati wa kituo cha mafunzo katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa. Vituo vingine vitajengwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya kanda KCMC, Hospitali ya kanda Bugando na Hospitali ya rufaa ya kanda Mbeya.

## HUDUMA ZA UUGUZI NA UKUNGA

**274. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua kuwa huduma za Uuguzi na Ukunga ni mhimili muhimu katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini ambapo asilimia 80 ya huduma za afya zinatolewa na wauguzi na wakunga. Hivyo basi, Wizara

imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa kujengea uwezo watoa huduma ili kuweza kutoa huduma kwa kuzingatia **utu, staha na mawasiliano madhubuti**. Mpaka sasa jumla ya watoa huduma 6,544 katika halmashauri 184 kutoka mikoa yote 26 wamejengewa uwezo kuhusu utoaji wa huduma zenye staha na kuimarisha huduma kwa mteja (customer care).

**275. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanza kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuweza kutoa **huduma za mama mwambata** (birth companionship) kwa kuboresha miundombinu ya vyumba vya kujifungulia ambapo mama anaruhusiwa kukaa na msindikizaji aliyemchagua wakati wa kujifungua. Jumla ya vituo vya kutolea huduma 42 katika mikoa ya Katavi, Pwani, Kigoma, Dar es salaam na Morogoro vimeanza kutekeleza afua hii. Sambamba na hilo, Wizara imejengea uwezo watoa huduma 1,285 katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Katavi, Geita na Dar es Salaam kuhusu matumizi sahihi ya chati uchungu ili kuendana na mapendekezo ya Shirika la Afya Duniani ya kuimarisha ubora wa huduma wakati wa kujifungua.

**276. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha ubora wa utoaji huduma, Wizara imeendelea kufanya **ukaguzi wa kimatibabu** katika vituo vya kutolea huduma. Kwa kipindi hiki, Wizara imefanya ukaguzi wa kimatibabu kwa huduma za Uuguzi na Ukunga katika Hospitali 72 za Halmashauri katika Mikoa kumi na nne (14). Matokeo ya ukaguzi huo yanaonesha kiwango cha ubora wa huduma za Uuguzi kimeongezeka kutoka asilimia 29 mwaka 2022/23 hadi asilimia 66 mwaka 2023/24 na huduma za Ukunga kutoka asilimia 53 mwaka 2022/23 kufikia asilimia 75 mwaka 2023/24. Ongezeko hilo limechangiwa na kujengea uwezo wauguzi 7,829 katika kutekeleza mipango kazi ya kushughulikia mapungufu yanayobainika pamoja na kuimarisha usimamizi wa ndani kwenye ngazi ya vituo. Pamoja na uwepo wa hali ya kuimarika kwa ubora wa huduma, Wizara inaendeleza juhudi ili kufikia lengo ambalo ni asilimia 90. Hivyo, Wizara itaendelea kuimarisha ukaguzi wa kimatibabu hasa kwa ngazi ya msingi kwani ndiko wananchi wengi wanapata huduma na wanastahili huduma bora.

**277. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza program ya kuboresha upatikanaji wa huduma za ushauri nasaha, upimaji wa VVU, kuanzisha dawa za kufubaza makali ya VVU kwa wakati (kwa saa 24 siku zote za wiki) katika ngazi zote za kutolea huduma na kutoa rufaa kwa wakati kwa kuwatumia wauguzi na wakunga (Nurse Initiated Management of AntiRetroviral). Jumla ya wauguzi na wakunga 3,769 wamepatiwa mafunzo ili kuendelea kusogeza huduma hizi kwa wagonjwa waliopo pembezoni ambapo kuna upungufu wa madaktari.

**278. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga kwa **kutambua mafunzo ya Stashahada na Shahada ya Ukunga** ambayo awali yalikuwa hayatambuliki katika muundo wa Maendeleo ya Watumishi (Scheme of Service). Serikali inakamilisha taratibu za kuandaa muundo rafiki kwa Wakunga wa ngazi za Stashahada ya juu ya Ukunga, Shahada na Shahada ya umahiri ili kuitambua taaluma ya ukunga. Kufuatia mabadiliko haya, Wakunga wenye Stashahada na Shahada wataajiriwa kama Maafisa Wakunga na siyo Maafisa Wauguzi. Aidha, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa Wakunga wanatoa huduma katika mazingira stahiki na yenye rasilimali zinazohitajika kutekeleza majukumu yao kwa tija na ufanisi.

**KUIMARISHA UBORA WA HUDUMA ZA AFYA**

**279. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu kubwa la kuhimiza na kufuatilia ubora wa huduma mbalimbali za afya zinazotolewa katika ngazi zote nchini. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliendelea kutekeleza afua mbalimbali za uboreshaji wa huduma za Afya ikiwemo kuandaa na kusimamia utekelezaji wa miongozo, viwango na taratibu za kiutendaji zinazokubalika katika Kukinga na Kudhibiti Maambukizi, uimarishaji wa Ubora wa huduma na kuratibu Usimamizi Shirikishi. Aidha, Wizara imeendelea kusisitiza vituo vya kutolea huduma katika ngazi zote kuweka mazingira rafiki ya huduma kwa mteja (customer care) ambayo ni pamoja na kuweka vibanda au madawati mahsusi ya maulizo, kupanga waongozaji maalum (Niulize Mimi), kuweka vibao/ishara zinazoelekeza maeneo zinapopatikana huduma ndani ya vituo. Hii ni katika kuhakikisha mwananchi anapata huduma bora

anazostahili kuzipata awapo katika maeneo kutolea huduma za afya.

**280. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha mteja awapo katika maeneo ya vituo vya huduma anapata **huduma bora na bila usumbufu wowote**, Wizara imeelekeza na imeendelea kusimamia kuhakikisha vituo vimeweka **mabango** yanayoainisha haki na wajibu wa mteja, gharama za huduma, mazingira wezeshi ya upatikanaji huduma mahsusi kwa wenye mahitaji maalum, namba za simu za viongozi wa vituo ambazo mteja ana uhuru wa kupiga endapo anahitaji msaada. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha uwepo wa madawati maalum ya huduma

kwa mteja (customer care desk) na visanduku vya kutolea maoni ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma rafiki na kwa wakati. Kwa sasa, Hospitali zote kuanzia ngazi ya rufaa ya mkoa hadi Taifa na baadhi ya Hospitali za Halmashauri zina madawati ya huduma kwa mteja. Pamoja na jitihada zilizofanyika za kuboresha huduma za afya kwa wateja, Wizara inatambua kuwa ubora wa huduma ni suala endelevu na linahitaji miongozo, ushirikiano kutoka kwa wateja na watoa huduma na tathmini za mara kwa mara. Hivyo, Wizara itaendelea kuelimisha wananchi kuhusu kuwajibika kwao katika kuhakikisha wanapatiwa huduma zilizo bora.

**281. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisha usimamizi shirikishi, Wizara imeendelea kutoa msisitizo wa kuimarisha utekelezaji wa usimamizi shirikishi ngazi ya mkoa na Halmashauri ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinazingatia miongozo. Vilevile, Wizara imedhamiria kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za afya na tayari imekamilisha andiko kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) pamoja na Shirika la Afya Duniani ili kufanya marekebisho makubwa ya muundo, sifa na ujuzi wa viongozi katika ngazi zote ikiwemo Mikoa, Halmashauri na Vituo (RHMT, CHMT na HMT).

**282. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha maeneo ya kutolea huduma pamoja na wahudumu wanatoa huduma kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo, Wizara imeendelea kufanya usimamizi shirikishi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini,

ambapo ubora wa huduma zinazotolewa hukaguliwa, lakini pia watoa huduma hufanyiwa mafunzo maalum (Mentorship) na kuelekezwa namna bora zaidi ya utoaji huduma ili waweze kurekebisha mapungufu ambayo yameonekana wakati wa zoezi hilo la usimamizi shirikishi. Aidha, Wizara imeendesha mafunzo ya utekelezaji wa Mwongozo wa Uboreshaji wa Utoaji wa Huduma za Lishe kwa mikoa ya Songwe na Njombe ambapo mafunzo haya yamehusisha jumla ya Watumishi 104 kutoka Timu za Uendeshaji Huduma za Afya Mkoa na Halmashauri ikijumuisha RHMT mbili (2) na CHMT 11 (Njombe sita na Songwe tano).

**283. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha usimamizi shirikishi kwenye vituo vya afya nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilianzisha mfumo wa kielektroniki unaoitwa Afya Supportive Supervision (AFYASS) ambao unatumika na wataalam wa Sekta ya Afya wanapokuwa katika zoezi la usimamizi shirikishi. Katika kuwezesha matumizi ya mfumo huu wa kidijitali, Wizara imekuwa ikifanya mafunzo kwa njia ya nadharia na vitendo kuhusu matumizi yake kwa watumishi, ambapo katika kipindi hiki, imefanya mafunzo katika mikoa 11 ya Mwanza, Geita, Mara, Shinyanga, Simiyu, Dodoma, Manyara, Katavi, Dar es Salaam, Tanga na Tabora. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo huu wa kielektroniki ili kuwajengea uwezo wataalam mbalimbali wa Sekta ya Afya ili waweze kuwa na uelewa mpana wa matumizi ya mfumo kwa ajili ya kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za usimamizi shirikishi katika ngazi zote.

**284. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miongozo na viwango vya kukinga na kudhibiti maambukizi na usalama wa huduma kwa mteja. Katika kutekeleza hilo, Wizara ilijikita katika afua kuu tatu (3) ambazo ni tathmini ya uwezo wa vituo vya afya katika kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza, kufundisha watumishi wa afya jinsi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa afua za kukinga na kudhibiti maambukizi na kuendelea kupambana na usugu wa vimelea dhidi ya dawa. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Wizara imefanya mafunzo ya namna ya kufanya ufuatiliaji na tathmini ya afua za kukinga na kudhibiti maambukizi yanayotokana na huduma za

afya (health care associated infections) katika mikoa mbalimbali nchini.

**285. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha utekelezaji wa afua za **kukinga na kudhibiti maambukizi** katika Hospitali za rufaa ambapo imefanya tathmini na mafunzo kwa vitendo kwa Watoa Huduma za Afya katika Hospitali 8 za Rufaa ambazo ni Hospitali za Rufaa za Kanda (Mbeya, Benjamin Mkapa na Bugando), na Hospitali za Rufaa za Mikoa (Morogoro, Amana, Temeke, Sekou Toure na Mbeya). Katika tathmini hii, wastani wa utekelezaji wa Viwango vya ubora katika Kukinga na Kudhibiti Maambukizi (infection prevention and control – IPC) umeongezeka kutoka asilimia 63 mwaka wa fedha 2022/23 hadi asilimia 74 mwaka 2023/24. Jumla ya Watoa Huduma 1,050 kutoka katika Hospitali hizo wamefanyiwa mafunzo kwa vitendo kwa kuzingatia viwango vya ubora katika Kukinga na Kudhibiti Maambukizi.

## RASILIMALI WATU KATIKA SEKTA YA AFYA

**286. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na uboreshaji mkubwa uliofanyika katika eneo la miundombinu ya kutolea huduma za afya kuanzia katika majengo, upatikanaji wa dawa na vifaa vya uchunguzi, Wizara inatambua kuwa uwepo wa watoa huduma za afya wenye ujuzi na weledi wa kazi ni moja ya nguzo muhimu inayohitajika kwa ajili ya kuwa na mfumo imara na wenye ufanisi kwa ajili ya utoaji wa huduma bora za afya kwa wananchi. Lengo hilo litawezekana iwapo vyuo vya afya vitaendelea kuzalisha wataalam wenye ujuzi na weledi pamoja na kuajiri watumishi wa kutosha katika vituo vya kutolea huduma za afya.

### Ajira katika Sekta ya Afya

**287. Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi 2024, Sekta ya Afya ilikuwa na jumla ya **watumishi wa afya 126,925** ambao ni sawa na asilimia **57.9** ya watumishi wote 219,061 wanaohitajika katika Sekta ya Afya kulingana na IKAMA. Kati ya watumishi waliopo, watumishi 101,733 sawa na asilimia 80.2 wapo katika ngazi ya afya ya msingi na watumishi 25,192 sawa na asilimia 19.8

wanafanya kazi katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa. Hata hivyo kutokana na kuongezeka kwa vituo vya utoaji huduma za afya, kuongezeka kwa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi, upanuzi wa huduma za afya katika ngazi za vituo vya afya kwa kuweka huduma za dharura za upasuaji kwa akina mama wajawazito wanaojifungua (CEmONC) pamoja na huduma za Idara za Dharura (EMD) na wagonjwa mahututi (ICU), mahitaji halisi ya watumishi wa afya kwa sasa ni watumishi 348,923 na kufanya upungufu kufikia asilimia 64.

**288. Mheshimiwa Spika,** Katika kukabiliana na changamoto ya sasa ya uhaba wa watumishi, Wizara imewasiliana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kupata vibali vya ajira vya watumishi. Katika mwaka wa fedha 2023/24, **Serikali imetoa kibali cha kuajiri jumla ya watumishi 13,187** katika Sekta ya Afya. Hatua nyingine ni pamoja na kutekeleza Mwongozo wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani, kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika Sekta ya Afya kwa kuwashawishi kutumia sehemu ya rasilimali fedha zinazotumika katika kutekeleza programu hizo kugharamia ajira za muda mfupi kwa wataalam wa afya na kuendelea kufanya uchambuzi wa uzito wa majukumu dhidi ya idadi ya watumishi kwa kila kituo na hatimaye kuwa na uwiano sahihi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya wataalam 4,838 waliajiriwa kwa utaratibu wa **ajira za mikataba** ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani. Kati yao, watumishi 4,183 wameajiriwa kwenye Hospitali za Rufaa za Mikoa, kanda, maalum na Hospitali ya Taifa Muhimbili na watumishi 655 wameajiriwa ngazi ya afya ya msingi.

**289. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea **kuweka mazingira mazuri na yenye kuvutia kwa watumishi wa Sekta ya Afya** ili kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya katika maeneo yao ya kazi. Katika mwaka wa fedha 2023/24, Serikali ilinunua jumla ya magari 873 kwa ajili ya kuwahudumia watumishi ili kuwarahisishia usafiri wanapokwenda kutekeleza majukumu yao ya kikazi. Aidha, Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi 3,650,000,000 kama mikopo yenye riba nafuu** kwa watumishi wa afya ili waweze kumudu gharama za

maisha. Wizara inawaelekeza waajiri mbalimbali kuweka mazingira mazuri yatakayo wavutia na kuwabakiza watumishi wa Sekta ya Afya kama vile kujenga nyumba za makazi karibu na maeneo ya kutolea huduma, kununua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuwahudumia watumishi, kuendelea kutoa posho ya masaa ya ziada na kuboresha posho za kuitwa kazini (Oncall Allowance), kutoa mikopo kwa watumishi wa afya na kuwaendeleza watumishi hao ili wabaki katika maeneo yao kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi.

**Uzalishaji wa Wataalam wa Afya – Kada za kati**

**290. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la kuhakikisha uwepo wa wataalam wa kutosha, kwa uwiano sahihi na wanaotoa huduma zilizo bora za afya kwa wananchi. Katika kuhakikisha hilo, Wizara imeendelea **kusimamia vyuo** vilivyopo chini ya Wizara, Vyuo Binafsi na Taasisi za Dini ili kuhakikisha vinazalisha wataalam wenye ujuzi na weledi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) ilifanya uchaguzi wa wanafunzi 26,820 sawa na asilimia 27 ya waombaji 100,934 waliotuma maombi ya kujiunga na vyuo vya afya ngazi ya kati katika kipindi cha Juni hadi Oktoba, 2023. Kati yao wanafunzi 3,440 sawa na asilimia 13 walichaguliwa kujiunga na vyuo vya Serikali na wanafunzi 23,380 sawa na asilimia 87 walichaguliwa kujiunga na vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za dini katika program za Uuguzi na Ukunga na Sayansi Shirikishi za Afya. Vilevile, katika kuhakikisha kuwa mitaala inayotumika kufundishia katika vyuo inakidhi mahitaji ya kipindi husika, Wizara imekuwa ikipitia mitaala hiyo mara kwa mara na kuifanyia marejeo.

**291. Mheshimiwa Spika,** Ili kukidhi mahitaji ya utoaji wa huduma za afya kuanzia ngazi ya Msingi hadi Taifa, Wizara imeandaa mitaala mipya ya fani za Stashahada ya Tiba Lishe (Clinical Nutrition) na Stashahada ya Juu ya Afya ya Akili kwa Wauguzi (Higher Diploma in Mental Health Nursing) ambapo inatarajiwa kutumika kudahili wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2024/2025. Mtaala wa Tiba Lishe unatarajiwa kuzalisha wataalam ambao watakwenda kutoa huduma katika ngazi ya Afya ya Msingi ambako ndiko kwenye mahitaji makubwa ya huduma hizo. Kwa

sasa asilimia 30 ya watoto wana udumavu, asilimia 12 wana uzito pungufu, asilimia 03 wana ukondefu, asilimia 04 wana uzito uliozidi na kiribatumbo na asilimia 59 wana upungufu wa damu. Aidha, kwa upande wa wanawake walio katika umri wa kuzaa asilimia 42 wana upungufu wa damu, asilimia 36 wana uzito uliozidi na kiribatumbo hali inayochangia ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza kama vile Kisukari, shinikizo la damu, kansa na magonjwa ya moyo. Uwepo wa wataalam hawa katika jamii utasaidia utekelezaji wa afua za kinga katika masuala ya lishe kwenye jamii. Aidha, Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Afya ya Akili kwa Wauguzi (Mental Health Nursing) utasaidia kuongeza idadi ya wataalam wa fani ya afya ya akili na kusaidia kukabiliana na ongezeko la wagonjwa wenye changamoto ya afya ya akili ambao wanaendelea kuongezeka kwa kasi huku uzalishaji wa wataalam hao ukiwa mdogo.

**292. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2024/2025 Wizara itaweka msisitizo kwenye uzalishaji wa wataalam wa kada za kati za afya zenye upungufu mkubwa. Kada hizo ni pamoja na wataalam wa huduma za utengamao (Rehabilitation), dawa za usingizi na ganzi (Anaesthesia), Uchunguzi kwa njia ya mionzi (Diagnostic Radiography), wataalam wa tiba ya macho (Clinical Opthalmology), Tiba kazi (Occupational Therapy), Tiba kwa njia ya mazoezi (Physiotherapy), Utengenezaji wa Viungo Bandia/Saidizi (Orthopedic Technology), Tiba kwa njia ya saikolojia (Clinical Psychology) na kusaidia kuona kwa kutumia miwani (Optometry). '**Nitoe wito kwa vyuo vya binafsi na taasisi za dini kuunga mkono Serikali kwa kuanzisha mafunzo ya kada zenye uhitaji mkubwa ili kuimarisha huduma za afya hasa katika ngazi ya msingi'.**

**293. Mheshimiwa Spika,** Katika kuimarisisha huduma za ukunga nchini, Wizara inaandaa mitaala mahsusi ya **Stashahada ya juu ya Ukunga, Shahada na Shahada ya umahiri** ya Ukunga**.** Mitaala hiyo itatoa fursa kwa wauguzi na wakunga wenye sifa kujiendeleza katika fani ya Ukunga. Hii itaongeza umahiri na weledi kwa wakunga na kusaidia nchi kufikia malengo endelevu ya Millenia namba tatu (3) ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia vifo 70 kati ya vizazi hai 100,000, vifo vya watoto

wachanga kufikia vifo 12 kati ya vizazi hai 1,000 na vifo vya watoto chini ya miaka mitano kufikia vifo 25 kati ya vizazi hai 1000 ifikapo mwaka 2030.

**Ufadhili wa Masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi**

**294. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufadhili wanafunzi na wataalam wa afya katika kada mbalimbali za kitabibu ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya na zinazotolewa na watoa huduma wenye ujuzi wa kutosha. Katika kuimarisha na kuzisogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu zaidi na wananchi, Wizara imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa ngazi hizo kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaojulikana kama **Dkt. Samia Afya Scholarship** wa kutoa ufadhili kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa utaratibu wa SETI. Mpango huu ni mahsusi kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye vituo na Hospitali za Serikali ikiwemo madaktari na wataalam wengine wa afya wanaojiendeleza katika ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi kwenye maeneo ya kimkakati na yenye uhitaji mkubwa.

**295. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Serikali imetoa **ufadhili wa masomo** kwa fani mbalimbali na ngazi tofauti kutegemeana na mahitaji na uwezo wa kifedha. Jumla ya **wataalam 1,251** wanaosomea ubingwa na ubingwa bobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi walipata ufadhili wa masomo. Kati ya watumishi hao, 934 wanasoma vyuo vya ndani na 317 wanasoma vyuo vya nje ya nchi ambapo wataalam 601 ni wapya na 650 ni wale wanaoendelea na masomo. Aidha, wataalam 83 wanasoma kwa mfumo wa seti ili kukamilisha huduma za kibobezi kwenye Hospitali za kanda, maalum na Taifa. **Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kutoa fedha kiasi cha Shilingi Bilioni 9 kwa ajili ya mafunzo ya wataalam bingwa na bingwa bobezi nchini.**

**296. Mheshimiwa Spika**, Naomba pia nichukue fursa hii kutambua **mchango wa wadau** mbalimbali ambao

wameonyesha nia ya dhati kuunga mkono Serikali kupitia Wizara ya Afya katika jitihada za kuhakikisha upatikanaji wa wataalam bingwa nchini. Natambua mchango wa **Taasisi ya Mo Dewji Foundation** ambao wamejitolea kufadhili wataalam bingwa wawili (2) kwa miaka yote mitatu (3) ya mafunzo katika fani ya Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu (Neurosurgery) katika Chuo Kikuu cha Nairobi nchini Kenya. Pia, natambua **mchango wa Benki ya NMB** katika kuchangia gharama za mafunzo kwa kutenga jumla ya Shilingi 34,762,500 kwa ajili ya kuchangia gharama kwa wanafunzi wanaosoma taaluma ya utengemao na tiba shufaa. **'Niendelee kutoa wito kwa mashirika, taasisi na wadau wengine kushirikiana na Wizara katika kufanikisha jitihada za Serikali za kuhakikisha tunaboresha huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ili kusogeza huduma karibu na wananchi'.**

**297. Mheshimiwa Spika**, Wizara kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 imeanza utaratibu wa kutoa **mikopo kwa wanafunzi wa afya ngazi za kati** katika fani zenye upungufu mkubwa wataalam hao. Jumla ya kozi 11 ziliainishwa katika fani za Tiba Kazi, Tiba Mazoezi, Viungo Saidizi, Teknolojia ya Vifaa Tiba, Tiba Miwani, Teknolojia ya Mionzi, Teknolojia ya Maabara ya Meno, Tiba ya Kinywa na Meno, Sayansi za Afya ya Mazingira, Sayansi za Maabara ya Tiba, Teknolojia ya Utunzaji wa Kumbukumbu za Afya ambapo hadi sasa wanafunzi walionufaika na mikopo hiyo ni 773 kati yao wasichana ni 355 sawa na asilimia 46 na wavulana ni 418 sawa na asilimia 54. Ufadhili wa Serikali kwa wanafunzi wanaosoma kozi hizo utahamasisha na kuongeza idadi ya wanafunzi watakaoomba kujiunga na mafunzo, kuongezeka kwa wahitimu wa kada hizo na hatimaye kuongezeka kwa wataalam wa kada husika nchini. Juhudi nyingine zilizofanywa na Wizara kwa kushirikiana na shirika liitwalo **Campaign for Female Education (CAMFED)** ni kuendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa kike 287 wa fani ya Uuguzi na Ukunga katika ngazi ya Stashahada wanaotoka kwenye familia masikini.

**Usimamizi wa mafunzo endelevu (CPD)**

**298. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha watumishi wa afya wanakuwa na ujuzi unaoendana na mahitaji ya wakati kwa lengo la kuboresha huduma, Wizara kupitia mabaraza ya kitaaluma imeendelea kuhakikisha **mafunzo endelevu** (Continuous Professional Development-CPD) kwa watumishi wa Sekta ya Afya yameendelea kutolewa kwa wataalam wanaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Jukumu hilo limefanywa kwa kushirikiana na Mabaraza ya Kitaaluma yanayosimamia mafunzo husika kwa mujibu wa Sheria na Miongozo ya Mabaraza hayo. Aidha, Wizara inatambua changamoto ya uhaba wa watumishi, hivyo ili kupunguza au kuepuka watumishi kuondoka kwenye vituo vyao vya kazi kwa ajili ya kwenda katika mafunzo endelevu (CPD), Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya mfumo maalum wa mafunzo kwa njia ya kielektroniki yaani **National e-learning Platform for Health**. Mfumo huu unatumiwa na watumishi walioko kazini wanaotaka kujiendeleza kupitia moduli za mafunzo zilizopo kwenye mfumo huo. Katika kipindi cha mwezi Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya moduli 65 zimeandaliwa na kufanya jumla ya moduli zilizopo katika mfumo huo hadi sasa kufikia 256. Watumishi waliotumia mfumo huo kujiendeleza ni 116,152 ambapo watumiaji wapya kuanzia mwezi Julai, 2023 hadi Machi 2024 walikuwa ni 16,200. **'Naomba nitoe wito kwa watumishi wote wa Sekta ya Afya nchini kuweka utaratibu wa kujiendeleza kitaaluma ili waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani ili waweze kutoa huduma bora za afya kwa wananchi zinazoendana na wakati'**.

**TEHAMA**

**299. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha na kuongeza **matumizi ya TEHAMA** katika kuboresha utoaji huduma za afya, ikiwa ni pamoja na kupunguza mifumo na kuwa na mifumo michache inayosomana, Wizara inaendelea na usimikaji wa mfumo mmoja ambao utatumika katika Hospitali zote za Rufaa za Mikoa. Hadi kufikia mwezi Oktoba 2024, Hospitali zote za Rufaa za Mikoa zitakua zimesimikwa mfumo huo. Aidha, mfumo huu utaunganishwa katika kanzi data (database) ya wizara (DHIS)

ili kuwezesha taarifa hizi kupatikana kwa urahisi katika ngazi zote za maamuzi na ngazi za utoaji huduma nchini. Vilevile mashine za vipimo vya maabara, Radiolojia na zitaunganishwa na mfumo huu ili kuwezesha kupata taarifa za mteja kutoka kituo kimoja hadi kingine, vilevile mfumo huu utawezeshwa kusomana na mifumo ya Wizara ya Fedha, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Bohari ya Dawa kwa ajili ya kupata taarifa sahihi za wateja na madai. Ni matarajio yetu kuwa mfumo huu utasaidia kuboresha ufanisi, kuimarisha udhibiti wa mapato ya Hospitali na kupunguza gharama katika utoaji wa huduma za afya. Mfumo pia umezingatia eneo la ubora wa huduma kwa kuhakikisha mteja anatumia muda mfupi kupata huduma kwa kusimika **Mfumo wa kuratibu miadi ya wateja** (Online Appointment System) ambapo mteja ataweza kuweka miadi na mtoa huduma bila kufika kituoni.

**300. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha huduma kibingwa na bigwa bobezi zinafika katika Hospitali ambazo hazina huduma hizo, Wizara imepeleka huduma za **Tiba Mtandao** (Telemedicine) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 17 ambazo ni Mount Meru, Manyara, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mwl. Nyerere Memorial, Sekotoure, Geita, Bombo, Bukoba, Mawenzi, Kitete, Sumbawanga, Songwe, Njombe, Iringa ikilinganishwa na Mikoa minne (4) iliyokuwepo mwaka 2022/23. Hospitali hizi 17 zimeunganishwa na Hospitali 4 za kibingwa (Bugando, Benjamin Mkapa, Mbeya Zonal na ORCI) ambazo ni "Zonal Hub" na "Super Hub". Hadi sasa huduma hii imewanufaisha zaidi ya wateja 7,055 ambapo imewaondolea gharama na kadhia ya kusafiri kufuata huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

**301. Mheshimiwa Spika,** Katika kuendelea kukabiliana na magonjwa ya mlipuko Wizara imeanzisha **mfumo wa kuratibu tetesi za magonjwa** (electronic Event Based Surveillance - eEBS) ambapo kupitia kikao maalum kilichoitishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na kushirikisha Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais Utumishi na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Mfumo wa eEBS ulipitishwa kuwa mfumo utakaotumika na Wizara zote zinazohusika na matukio ya dharura na utekelezaji ya sera ya Afya Moja. Vile vile mfumo eEBS umetangazwa kuwania tuzo za kidunia katika Mkutano wa Kidunia wa Mifumo **(World Summit on the Information**

**Society - WSIS)** wa mwaka 2024 ikiwa ni kati ya miradi ya TEHAMA 360 inayowania Tuzo hiyo baada ya kuchaguliwa kutoka miradi 1,049 ya TEHAMA iliyoshindanishwa.

**UGHARAMIAJI WA HUDUMA ZA AFYA**

**302. Mheshimiwa Spika,** Serikali imeendelea kutenga fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia huduma za afya kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka 2023/24 kiasi cha Shilingi trilioni 2.5 kilitengwa ukilinganisha na kiasi cha Shilingi trilioni 2.1 kilichotengwa mwaka 2022/23. Fedha hizi zimetumika kugharamia vipaumbele mbalimbali katika Sekta ya Afya ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, rasilimali watu.

**303. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kutoa fedha za ugharamiaji wa huduma za afya, Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inaelekeza **Wananchi kuchangia** huduma za afya. Hivyo, Wizara imeendelea kutekeleza Mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi kupata huduma za afya bila ya kikwazo cha fedha. Moja ya Mikakati hiyo, ni pamoja na kuhamasisha na kuhimiza wananchi kujiunga na mifuko mbalimbali ya **Bima ya Afya** ya Umma na Binafsi ambapo hadi sasa ni asilimia 15 ya watanzania wamejiunga na Mifumo ya Bima za Afya. Kati ya hao wanufaika wa NHIF asilimia 8, CHF na Bima Binafsi asilimia 7. Hata hivyo mwitikio umekuwa mdogo na wananchi wengi hujiunga na Mifuko za Bima ya Afya pale ambapo tayari wakiwa na matatizo ya kiafya. **Nitoe rai kwa wananchi kujiunga na Bima za afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua.**

**304. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza maelekezo ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 kuhusu utoaji huduma za **matibabu bila malipo kwa makundi maalum** (Wajawazito, Watoto chini ya miaka mitano, wazee wa zaidi ya miaka 60 wasio na uwezo), Serikali imeendelea kutekeleza Sera hiyo hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha. Hadi kufikia Machi 2024, kiasi cha **Shilingi 126,746,199,080** kimetumika kwa ajili ya

ununuzi, usambazaji na utoaji wa **chanjo kwa watoto** ili kuwakinga na magonjwa kama vile pepopunda, kupooza, nimonia, surua na kuharisha na kiasi cha **Shilingi 788,736,000** kimetumika kwa ajili ya ugharamiaji wa **chanjo kwa wajawazito**. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Jumla ya fedha zilizotumika kugharamia huduma za chanjo kwa akinamama wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano (5) ni **Shilingi 127,534,935,080** ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 118,787,795,750 kilichotumika katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

**305. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa dawa, kiasi cha **Shilingi 3,431,724,619** kimetumika kugharamia **ununuzi na usambazaji wa dawa za watoto** wenye umri chini ya miaka mitano ambazo ni dawa ya kutibu kuharisha (ORS na ZINC), dawa ya kutibu Nimonia (vidonge vya Amoxylin na sindano), dawa za kutibu Malaria (dawa mseto na sindano). Vilevile, kiasi cha **Shilingi 10,700,124,245** kimetumika **kugharamia dawa za wajawazito** ikiwemo dawa za kuongeza damu (Fefol) dawa za kuzuia kutoka damu nyingi baada ya kujifungua (Oxytocin), dawa ya kukinga na kutibu kifafa cha mimba (Magnesium Sulfate), dawa kinga ya Malaria (SP), chanjo ya Tetenasi (TT) na dawa ya Misoprostol. Hivyo, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya fedha zilizotumika kugharamia huduma za dawa kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ni **Shilingi 14,131,848,864.00** ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 5,650,818,292.00 kilichotumika katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Vilevile, Serikali imeendelea kuhakikisha Wananchi wanapata huduma za matibabu bila malipo kwa magonjwa ya UKIMWI, Kifua Kikuu (TB) na Malaria ambapo katika kipindi hiki kiasi cha **Shilingi 469,020,000,000** zimetumika.

**306. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuhakikisha **wananchi wasio na uwezo wanapata huduma za afya** kwa kupitia utaratibu wa **misamaha mbalimbali inayotolewa na Hospitali**. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Hospitali za kitaifa, Hospitali maalum, Hospitali za rufaa za kanda na mikoa zimeweza kutoa huduma za afya kwa njia ya msamaha zenye thamani ya **Shilingi 79,277,579,622** kwa wagonjwa **425,157** waliopatiwa huduma hizo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Kanda, Maalum na Taifa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.**

**8**. Huduma zilizoongoza kutolewa misamaha ni huduma za uchujaji damu (Dialysis), huduma za mionzi kwa wagonjwa wa saratani, vipimo vya maabara, huduma za radioiojia, huduma za upasuaji, gharama za kumuona daktari, dawa na huduma za wagonjwa mahututi (ICU). **'Nitumie fursa hii kuwakumbusha watoa huduma za afya kuzingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayotambua uwepo wa makundi maalum na wasio na uwezo. Aidha, nitoe rai kwa wananchi kufuata utaratibu uliowekwa na Serikali katika kupata misamaha ya matibabu kwa mujibu wa Sera'.**

**Jedwali Na. 8:** Idadi ya wagonjwa waliopata misamaha na gharama za msamaha katika hospital za Kanda, Maalum na Taifa.

| Na. | Hospitali | Idadi ya Wagonjwa | Gharama ya Msamha |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 32,615 | 10,507,770,196 |
| 2 | Hospitali ya Mloganzila | 12,417 | 2,562,703,988 |
| 3 | Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) | 1,167 | 1,146,206,145 |
| 4 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) | 4,318 | 2,702,038,334 |
| 5 | Taasisi ya Sratani Ocean Road (ORCI) | 15,475 | 28,254,601,600 |
| 6 | Hospitali ya Kanda ya Benjamin Mkapa | 1,463 | 279,943,046 |
| 7 | Hospitali ya Afya ya akili Mirembe | 964 | 626,921,346 |
| 8 | Hospitali ya Kibong'oto | 3,712 | 58,382,803 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya | 17,700 | 603,730,000 |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando | 22,277 | 3,619,939,055 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda-KCMC | 4,943 | 19,189,800,400 |
| 12 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Chato | 314 | 94,679,090 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mtwara | 241 | 14,091,153 |
| 14 | CCBRT | 4,552 | 6,695,986,236 |
| 15 | Hospitali 28 za Rufaa za Mikoa | 302,999 | 2,920,786,230 |
| | **Jumla** | **425,157** | **79,277,579,622** |

**307. Mheshimiwa Spika;** Katika kutatua changamoto zilizopo katika ugharamiaji wa huduma za afya nchini sambamba na kuhakikisha Watanzania wote wanakuwa na uhakika wa kupata huduma za Afya bila ya kikwazo cha fedha, tarehe 1 Novemba, 2023 Bunge lako tukufu lilipitisha muswada wa **Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote** ambao ulisainiwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 19 Novemba, 2023 kuwa Sheria namba 13 ya mwaka 2023. Lengo la kutungwa kwa Sheria hiyo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watanzania wote bila kikwazo cha kifedha pindi wanapohitaji huduma za afya. **'Kipekee nipende kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge pamoja na Bunge lako tukufu kwa kupitisha muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote Na. 13 ya mwaka 2023. Kupitishwa kwa Sheria hii kunaweka msingi wa mfumo madhubuti na endelevu wa ugharamiaji huduma za afya nchini'.**

**308. Mheshimiwa Spika,** Hatua inayoendelea sasa ni kuanza maandalizi ya utekelezaji wa baadhi ya vifungu vinavyolenga kuimarisha uwezo wa Taasisi zinazotegemewa katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Taasisi hizo ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) yenye jukumu la kuweka mfumo imara wa usimamizi na udhibiti wa bima za afya nchini. Kuanza kutekelezwa kwa jukumu hilo kutaondoa ombwe la usimamizi lililopo sasa hususan kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) hali inayosababisha kuwepo kwa malalamiko kutoka kwa wadau wakiwemo watoa huduma za afya binafsi pamoja na wanufaika wa bima za afya.

## MIRADI YA MAENDELEO

**309. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi 77 yenye

thamani ya **Shilingi 335,347,823,653.86** iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Fedha hizo zinajumuisha fedha za mapato ya ndani na fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 jumla ya fedha kiasi cha **Shilingi 193,915,266,271.66** sawa na asilimia 58 kimetolewa kwenye miradi kwa ajili ya utekelezaji.

**310. Mheshimiwa Spika,** Kati ya miradi hiyo inayotekelezwa na Wizara, miradi minne (4) **imekamilika** kwa asilimia 100 ya utekelezaji na imeanza kutoa huduma. Miradi hii ni pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya unaohusisha ujenzi wa jengo kwa ajili ya huduma za uzazi, ujenzi wa jengo la maabara ya kisasa – BSL3 katika Hospitali maalum ya magonjwa ambukizi Kibong'oto, ujenzi wa jengo lenye huduma za upasuaji, wodi ya wagonjwa mahututi na utakasaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya na ujenzi wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe inayohusisha ujenzi wa jengo la nje, afya ya mama na mtoto, upasuaji na mifupa, ufuaji, uchomaji taka na ujenzi wa nyumba tano (5) za watumishi.

**311. Mheshimiwa Spika,** Miradi 11 imefikia **zaidi ya asilimia 80** ya utekelezaji. Miradi hiyo ni pamoja na: ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la wodi za wagonjwa, kazi za nje na jengo la huduma za Radiolojia katika Hospitali ya Kanda-Chato; ujenzi wa jengo la wodi maalum awamu ya pili katika Hospitali ya Taifa Muhimbili; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje kwa awamu ya kwanza na ujenzi wa jengo la Damu Salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma
- Maweni. Miradi mingine iliyofikia hatua hiyo ni; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje kwa awamu ya kwanza katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara; ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara awamu ya Nne; ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi; ujenzi wa jengo la Huduma za Afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa

Mwanza- Sekou Toure na ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara katika eneo la Mtumba.

**312. Mheshimiwa Spika,** Miradi sita (6) inayoendelea na utekelezaji umefikia **wastani wa asilimia 60** ambayo ni:- ujenzi wa jengo la huduma za tiba mionzi kwa matibabu ya magonjwa ya saratani katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC; ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje, EMD, ICU na jengo la damu salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora Kitete; ujenzi wa jengo la huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe; na ujenzi wa jengo la damu salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa.

**313. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza miradi mitatu (3) ambayo utekelezaji wake umefikia **wastani wa asilimia 40**. Miradi hiyo ni: ujenzi wa jengo la afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita; ujenzi wa kituo cha umahiri kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na milipuko Kisopwa na ujenzi wa jengo la Radiolojia katika Hospitali maalum ya magonjwa ambukizi - Kibong'oto.

**314. Mheshimiwa Spika,** Aidha, miradi mitano (5) utekelezaji wake umefikia **wastani wa asilimia 20**. Miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la tiba mionzi katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Benjamin Mkapa; ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Kanda Chato unaojumuisha jengo la utakasaji, chumba cha maiti na jengo la kufulia; ujenzi wa jengo la "Covid-19 Containment Centre" katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida unaojumuisha wodi, vyumba vya upasuaji, famasi, maabara na jengo la wagonjwa mahututi; ujenzi wa jengo la madarasa na maabara katika Chuo cha Uuguzi na Ukunga Nachingwea na ujenzi wa jengo lenye huduma za damu salama na utengenezaji wa maji tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga Bombo.

**315. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatarajia kuendelea na utekelezaji wa miradi 48 ambayo ipo katika **hatua za awali**

inayohusisha; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili, ujenzi wa kituo cha mionzi kwa ajili ya matibabu ya saratani - Mbeya, ujenzi wa jengo la huduma ya afya ya mama na mtoto katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Shinyanga, Tanga, Kagera, Morogoro na Hospitali maalum ya afya ya mama na mtoto Dodoma; ujenzi na ukarabati wa wodi ya watoto wachanga katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Iringa, Kigoma, Mbeya, Mtwara, Rukwa,Mara, Geita, Simiyu, Tabora, Dodoma, Singida, Manyara, Songwe, Pwani na Ruvuma. Miradi mingine ni ujenzi wa miundombinu ya huduma za damu salama katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Shinyanga, Singida, Songwe, Katavi, Mara na Ruvuma; ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya afya vya Mpwapwa, Mbulu, Kahama, Maswa, Geita, Mbozi, Sumbawanga, Same, Rombo, Kibondo, CEDHA, Tukuyu, Muheza; ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa hatarishi na mlipuko Kagera; ujenzi wa jengo la wodi na jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro Mawenzi; ujenzi wa jengo la huduma jumuishi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure; ujenzi wa miundombinu awamu ya pili katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara inayohusisha jengo la mama na mtoto, jengo la kufulia, kichomea taka na nyumba tano (5) za watumishi; ujenzi wa Hospitali mpya ya Kanda ya Magharibi Kigoma; ujenzi wa jengo la kutoa huduma za kibingwa katika Hospitali Teule ya Rufaa yenye hadhi ya Mkoa Ukerewe; na ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya. **Kiambatisho Na. 8.** Kinaonesha hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

### Bohari ya Dawa (MSD)

**316. Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa imeendelea kutekeleza majukumu yake makuu manne (4); **uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji** wa bidhaa za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara. Katika kutekeleza majukumu hayo, Bohari imefanya ununuzi, utunzaji na usambazaji wa zaidi ya aina 2,926 ya dawa, vifaa, vifaa tiba na

vitendanishi, ambapo kati ya hizo, aina 126 ni bidhaa za afya zilizo katika utaratibu wa Miradi Msonge - (Vertical Program) ambazo zinahusu magonjwa ya Ukimwi, Kifua Kikuu, Malaria, Ukoma na bidhaa za Mama na Mtoto. Aidha, bidhaa aina 382 zimeainishwa na Wizara kuwa ni bidhaa za afya muhimu na za kipaumbele kwa nchi. Lengo la kuwa na bidhaa za afya muhimu na za kipaumbele ni kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinapatikana nyakati zote na kuweza kuhudumia vituo vya kutoa huduma za afya nchini.

**317. Mheshimiwa Spika,** Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya kwenye maghala ya Bohari ya Dawa imeendelea kuimarika ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2023/24 upimaji wa hali ya **upatikanaji wa bidhaa za afya ashiria** umeongezeka kutoka bidhaa za afya 290 hadi 382. Lengo likiwa ni kupanua wigo wa upatikanaji wa bidhaa nyingine zinazohitajika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Ongezeko hili ambalo lilianza mwezi Julai 2023, lilihitaji Bohari ya Dawa kujipanga na kuanzisha taratibu za manunuzi kwa bidhaa hizi. Hadi kufikia Machi 2024, **upatikanaji wa dawa** ulikuwa ni asilimia 61 ikilinganishwa na asilimia 52 iliyoripotiwa mwezi Julai 2023. Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Miradi Msonge – "Vertical Programs'' umeendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2024, upatikanaji wa bidhaa hizi ni asilimia 82. Kwa ujumla hali ya utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za Afya nchini kwa mwezi Machi 2024 umefikia asilimia 80 ikilinganishwa na asilimia 49 iliyoripotiwa mwezi Machi 2023. Sambamba na hilo, Bohari ya Dawa imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kusafisha damu, MRI, CT- Scan, Ultrasound na Digital X-Ray. Uwepo wa mitambo hiyo umeimarisha utambuzi wa magonjwa kwa usahihi na kutolewa kwa tiba sahihi.

**318. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na maboresho yanayoendelea kufanywa na Serikali, **mapato ya Bohari ya Dawa** yameendelea kuongezeka. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Bohari ya Dawa imekusanya mapato yatokanayo na majukumu yake ya msingi kiasi cha Shilingi 347,460,000,000 sawa

na asilimia 124.5 ya lengo la Shilingi 279,070,000,000 ikilinganishwa na makusanyo ya Shilingi 240,660,000,000 Mwaka 2022/23.

**319. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Bohari ya Dawa imenunua na kusambaza bidhaa za Afya, kwa ajili ya kuboresha vituo vya afya na kuhakikisha vinatoa **huduma ya dharura ya uzazi na mtoto** - Comprehensive Emergency Obstetric and New-born Care - CEmONC. Hadi kufikia Machi 2024, bidhaa za afya 354 kati ya bidhaa 398, sawa na asilimia 89 ya bidhaa zote zilikuwa zimekwisha sambazwa na kusimikwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 300. Aidha, kiasi cha Shilingi 84,210,000,000 sawa na asilimia 81.4 ya Shilingi 103,450,000,000 zilizopokelewa zimetumika kufanya ununuzi huo. Kati ya bidhaa za afya zilizonunuliwa kwa kupitia fedha hizo ni pamoja na mashine za uchunguzi zenye lengo la kutoa matibabu sahihi kwa wagonjwa. Uwepo wa mashine hizo katika ngazi za vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi (PHC), utasaidia kusogeza huduma za vipimo na uchunguzi karibu na wananchi ambapo huduma za uchunguzi wa damu (haematolojia na kemia ya mwili) na uchunguzi wa mkojo zitatolewa katika vituo hivyo.

**320. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza **sera ya viwanda** na kuongeza ufanisi wa usimamizi wa shughuli za uzalishaji na kuhakikisha utekelezaji wa miradi kwa wakati, Bohari ya Dawa imeanzisha Kampuni Tanzu inayoitwa "MSD Medipharm Manufacturing Company Limited" ambayo itakuwa na jukumu la usimamizi wa shughuli za uzalishaji wa bidhaa za afya na itakuwa na uwezo wa kuingia ubia na wawekezaji wengine. Kwa sasa kampuni hiyo itasimamia Kiwanda cha Mipira ya Mikono Idofi - Njombe, eneo la viwanda la Zegereni - Pwani, Kiwanda cha Barakoa - Dar es Salaam pamoja na eneo la viwanda Ng'hami Simiyu linalotarajiwa kuzalisha bidhaa za afya zitokanazo na malighafi ya pamba na hivyo kuipunguzia Serikali mzigo wa kuagiza bidhaa za afya nje ya nchi ambapo kwa sasa asilimia 80 za bidhaa zote za afya huagizwa nje ya nchi.

**321. Mheshimiwa Spika,** Katika kufanikisha azma ya Serikali ya **kushirikisha sekta binafsi,** Bohari ya Dawa imefanya utambuzi wa maeneo yanayohitaji ushirikiano na sekta binafsi, imeyetangaza

kwa wawekezaji wenye nia na sasa inafanya uchambuzi ili wawekezaji wenye sifa waweze kushiriki kwenye uanzishaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya. Aidha, Bohari ya Dawa imekuwa ikifanya mawasiliano na balozi zetu zikiwemo Balozi za China, Korea Kusini, Urusi, Algeria na maeneo mengine duniani ili kuweza kufanya utambuzi wa wazalishaji, wawekezaji na kuwezesha ununuzi wa bidhaa za afya kwa uhakika, ubora na gharama nafuu. Aidha, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuvijengea uwezo viwanda vya ndani ambapo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi 16,930,000,000 zimenunuliwa kutoka kwa wazalishaji wa ndani. Dhamira hii itasaidia kuongeza uzalishaji na kuvutia wawekezaji ambapo matumizi ya fedha za kigeni yatapungua na wananchi wengi zaidi wataweza kupata ajira.

**322. Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa kupitia **kiwanda cha barakoa** kilichopo eneo la Keko, Dar es Salaam kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, kimezalisha jumla ya barakoa 732,800 (Surgical mask) sawa na asilimia 92 ya lengo la kuzalisha barakoa 800,000 na kuwezesha upatikanaji wa Shilingi 366,400,000. Vilevile, kiwanda cha kutengeneza mipira ya mikono (Gloves) kilichopo Idofi- mkoani Njombe kimezalisha mipira ya mkono 68,961.

**323. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali kwenye ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya na ongezeko la fedha za kununua bidhaa za afya, uhitaji wa miundombinu ya kuhifadhia bidhaa za afya umeongezeka. Kwa kutambua ongezeko hilo, mnamo mwezi Agosti 2023, Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeanza **ujenzi wa maghala** katika Kanda ya Mtwara na Dodoma ili kukidhi upungufu uliojitokeza na kuwezesha kuwa na maghala yanayokidhi viwango vinavyostahili. Mradi wa ghala la Dodoma umefikia asilimia 31 na ghala ya Mtwara asilimia 30 ya utekelelezaji. Mradi huu wa ujenzi unatarajiwa kukamilika mwishoni wa mwezi Julai 2024 na utagharimu kiasi cha Shilingi 40,000,000,000. Aidha, Bohari ya Dawa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa maghala mengine katika Kanda zake zingine. **Kukamilika kwa ujenzi wa maghala kutasaidia kusogeza huduma karibu na vituo vya kutolea huduma za afya,**

**kupunguza gharama za uhifadhi na kuimarisha utunzaji wa bidhaa za afya.**

**324. Mheshimiwa Spika,** Bohari ya Dawa inatumia mifumo ya TEHAMA katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yake kuanzia kupokea takwimu za maoteo ya vituo vya kutolea huduma za afya na kwenye manunuzi, utunzaji wa bidhaa za afya katika maghala na usambazaji wa bidhaa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Hadi kufikia Machi 2024 miongoni mwa mifumo iliyotengenezwa ili kuimarisha utendaji ni mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa magari (Fleet Management System), mifumo ya usimamizi na utoaji taarifa kwa lengo la kutoa maamuzi kwa viongozi (Executive decisions' dashboards) na mfumo wa ununuzi wa bidhaa za afya kwa nchi za SADC kwa njia ya kielektroniki (Electronic SADC Pool Procurement - eSPPS).

**Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

**325. Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni Taasisi ya Umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Sura 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa Umma na wategemezi wao kupitia bima ya afya.
Sheria ya Mfuko imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali ili kuwezesha kupanua wigo wa walengwa kwa kuingiza makundi mbalimbali. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya, Mfuko unajumuisha watumishi katika Sekta ya Umma, wafanyakazi kutoka katika Sekta Binafsi na makundi mbalimbali katika Sekta zisizo rasmi.

**326. Mheshimiwa Spika,** Majukumu ya Kisheria ya Mfuko ni pamoja na Kuandikisha wanachama, Kukusanya michango na kuitunza, Kusajili watoa huduma na Kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni Kuwekeza fedha za ziada katika vitega uchumi mbalimbali, kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma, Kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa Umma.

**327. Mheshimiwa Spika,** Mfuko umesajili **wanachama wapya 506,751** sawa na asilimia 85.8 ya lengo la kusajili wanachama

wapya 590,917. Kulinganisha na wanachama 576,509 waliosajiliwa kipindi kama hicho 2022/23. Idadi ya wanachama waliosajiliwa imewezesha Mfuko kuwa na **wanachama wachangiaji 1,298,195** wenye jumla ya **wanufaika 4,891,679** sawa na asilimia 8% ya Watanzania wote. Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

**328. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi husika, Mfuko **umekusanya** mapato jumla ya **Shilingi 481,167,800,157.33** ambapo kati ya hizo, kiasi cha Shilingi 450,584,425,658.13 ni kutoka katika michango ya wanachama, Kiasi cha Shilingi 27,355,799,109.14 ni mapato yatokanayo na uwekezaji na kiasi cha Shilingi 3,227,575,390.06 ni kutoka katika vyanzo vingine vya mapato. Mapato yaliyokusanywa ni ongezeko la asilimia 15 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 417,401,987,980.76 kipindi kama hicho mwaka 2022/23 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 9**.

**Jedwali Na. 9:** Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mfuko kati ya mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24.

| **Chanzo cha Mapato** | **Makusanyo Julai hadi Machi 2022/23** | | **Makusanyo Julai hadi Machi 2023/24** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kiasi Kilichokusanywa** | **Asilimia** | **Kiasi Kilichokusanywa** | **Asilimia** |
| Michango ya wanachama | 378,048,985,083.63 | 90.57 | 450,584,425,658.13 | 93.64 |
| Mapato yatokanayo na uwekezaji | 37,642,568,475.41 | 9.02 | 27,355,799,109.14 | 5.69 |
| Mapato yatokanayo na vyanzo | 1,710,434,421.72 | 0.41 | 3,227,575,390.06 | 0.67 |
| vingine | | | | |
| **Jumla** | **417,401,987,980.76** | **100** | **481,167,800,157.33** | **100** |

**329. Mheshimiwa Spika,** Michango kutoka kwa wanachama imeendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 ilikuwa ni asilimia 93.64 ya mapato yote yaliyokusanywa na ni asilimia 95.8% ya lengo la kukusanya kiasi cha Shilingi 470,298,018,297.95. Kiasi hicho ni ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 378,048,985,083.63 kilichokusanywa kwa kipindi kama hiki kwa mwaka uliopita. Aidha, Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 **Mfuko umetumia jumla ya Shilingi 493,893,051,320.52** ambapo kiasi cha Shilingi 445,784,821,361.92 ni kwa ajili ya ulipaji wa madai kwa watoa huduma, kiasi cha Shilingi 40,643,930,444.17 matumizi ya kiutawala ikijumuisha malipo ya mishahara na kiasi cha Shilingi 7,464,299,514.43 ni matumizi mengineyo ikijumuisha miradi ya maendeleo. Matumizi ya malipo ya madai kwa watoa huduma yameongezeka kutoka asilimia 88.7 ya matumizi yote mwaka 2022/2023 na kufikia asilimia 90.3 ya matumizi yote mwaka 2023/24. Aidha, **matumizi ya uendeshaji wa Mfuko yamepungua kutoka asilimia 9.8 ya matumizi mwaka 2022/23 hadi kufikia asilimia 8.2 ya matumizi mwaka 2023/24** kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 10.**

**Jedwali Na. 10:** Mwenendo wa Matumizi ya Fedha ya Mfuko kwa kipindi cha mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24

| **Aina ya Matumizi** | **Matumizi Julai 2022 hadi Machi 2023** | | **Matumizi Julai 2023 hadi Machi 2024** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Kiasi Kilichotumika** | **Asilimia** | **Kiasi Kilichotumika** | **Asilimia** |
| Malipo kwa watoa huduma(Benefit payment | 434,387,420,142.26 | 88.7 | 445,784,821,361.92 | 90.3 |
| Matumizi ya kiutawala (Administrative expences) | 47,903,216,010.60 | 9.8 | 40,643,930,444.17 | 8.2 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi mengineyo (other charges) | 7,409,207,390.85 | 1.5 | 7,464,299,514.43 | 1.5 |
| **Jumla** | **489,699,843,543.71** | 100 | **493,893,051,320.52** | **100** |

**330. Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa huduma za afya hauwezi kuelezewa pasipo kutambua mchango na jitihada zinazotekelezwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).** Mathalani, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 jumla ya Shilingi 445,780,000,000 zimelipwa kwa vituo vya kutolea huduma za afya ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.6 ikilinganishwa na Shilingi 434,390,000,000 zilizolipwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. **Takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.** Aidha, katika kipindi husika, Mfuko **umelipa madai** kwa wastani wa siku 49 ambazo ni ndani ya matakwa ya Sheria, lengo la Mfuko ni kufikia wastani wa siku 45.

**331. Mheshimiwa Spika,** Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa **usajili wa vituo** vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024 Mfuko umesajili jumla ya vituo 2,668 ikiwa ni ongezeko la asilimia 40.2 ikilinganishwa na vituo 1,903 vilivyosajiliwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2022/23. Kati ya vituo vilivyosajiliwa, vituo vya Serikali ni 2,360 sawa na asilimia 88.5, vituo vya Mashirika ya Dini ni 88 sawa na asilimia 3.3 na vituo vya watu binafsi ni 220 sawa na asilimia 8.2. Aidha, usajili huu umefanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa na Mfuko kufikia 9,620.

**332. Mheshimiwa Spika,** Katika kuboresha huduma za matibabu nchini, Mfuko unatoa **mikopo nafuu** ya vifaa tiba, dawa na ukarabati wa vituo. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo, jumla ya vituo 402 vilivyokidhi vigezo vimenufaika na mikopo yenye thamani ya Shilingi 41,560,000,000. Kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi 2024 vituo 12 vimepatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi 2,570,000,000 ikiwa ni pungufu ya asilimia 70 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 8,550,000,000 kilichotolewa mwaka 2022/23 kipindi kama hicho.

Aidha, kati ya mikopo iliyotolewa kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Machi 2024, Shilingi 1,710,000,000 sawa na asilimia 67 zilitolewa kwa vituo vinavyomilikiwa na Serikali, kiasi cha Shilingi 750,000,000 sawa na asilimia 29 ni vituo vya Madhehebu ya Dini na kiasi cha Shilingi 110,000,000 sawa na asilimia 4 ni vituo vinavyomilikiwa na watu binafsi. Utaratibu huo umesaidia kujenga uwezo wa vituo katika kutoa huduma za afya kwa wanachama na wananchi kwa ujumla kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 11.**

**Jedwali Na. 11:** Mchanganuo wa Mikopo iliyotolewa hadi kufikia Machi 2024

| **Umiliki wa Vituo** | **Mikopo iliyotolewa Julai 2022 hadi Machi 2023** | | | **Mikopo iliyotolewa Julai 2023 hadi Machi 2024** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Idadi Ya Vituo** | **Kiasi Kilichotolewa (Bilioni)** | **Asilimia** | **Idadi Ya Vituo** | **Kiasi Kilichotolewa (Bilioni)** | **Asilimia** |
| Vituo vya Serikali | 6 | 1.61 | 19 | 6 | 1.71 | 67 |
| Vvituo vya madhehebu ya Dini | 7 | 5.27 | 62 | 4 | 0.75 | 29 |
| Vituo vya Binafsi | 15 | 1.67 | 19 | 2 | 0.11 | 4 |
| **Jumla** | **28** | **8.55** | **100** | **12** | **2.57** | **100** |

**333. Mheshimiwa Spika,** Mfuko unaendelea na **mapambano dhidi ya vitendo vya udanganyifu** wa huduma zitolewazo na Mfuko ambapo katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/24 Mfuko ulifanya chunguzi 34 za matukio ya viashiria vya vitendo vya udanganyifu ikiwa ni pungufu ya asilimia 8 ikilinganishwa na chunguzi 37 zilizofanyika mwaka uliopita kipindi kama hicho. Kutokana na chunguzi hizo Mfuko ulibaini madai yasiyo halali ya Shilingi 4,790,000,000 kutoka kwa watoa huduma mbalimbali. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 25.7 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 3,810,000,000 kilicho bainiwa kipindi kama hicho

mwaka 2022/23. Mfuko umeendelea kuchukua hatua stahiki kwa wote waliobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu dhidi yake.

**334. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi hadi Machi 2023/24 Mfuko **umesitisha mikataba** na vituo 13 vilivyojihusisha na vitendo vya udanganyifu ikiwa ni ongezeko la asilimia 44 ikilinganishwa na vituo 9 vilivyositishiwa mkataba kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Mfuko umeanzisha zoezi la uhakiki wa wanachama katika vituo vya kutolea huduma pamoja na kuimarisha utambuzi wa wanufaika katika vituo vya kutolea huduma kwa kutumia alama za vidole na sura
(Biometric identifation).

**335. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza takwa la kisheria la kufanya **tathmini ya uhai na uendelevu wa Mfuko**, NHIF ilitekeleza takwa hilo kwa kufanya tathmini ya uhai na uendelevu wake (actuarial valuation) kwa kipindi cha kuishia tarehe 30 Juni 2021. Matokeo na mapendekezo ya taarifa ya tathmini hiyo yametumika katika kufanya mapitio ya Kitita cha Mafao cha NHIF cha mwaka 2016 na kupitishwa kwa kitita kipya cha mafao cha NHIF cha mwaka 2023. Maboresho ya Kitita hicho yanalenga kuongeza huduma ambazo hazikuwepo katika Kitita cha awali; kufanya maboresho ya huduma na gharama zake kwa kuzingatia maendeleo ya teknolojia katika tiba na hali halisi ya bei katika soko. Kadhalika, kuwianisha kitita cha Mafao na miongozo ya tiba iliyoboreshwa. Maeneo yaliyofanyiwa mapitio na maboresho katika Kitita kipya cha Mafao ni pamoja na; Huduma za Usajili na Kupata Ushauri wa Daktari, Huduma za Dawa na Huduma za Upasuaji na Vipimo.

**336. Mheshimiwa Spika,** Tarehe 01 Machi 2024 Mfuko ulianza utekelezaji wa Kitita cha Mafao cha mwaka 2023 cha NHIF kilichoboreshwa. Hata hivyo, utekelezaji wa Kitita hicho ulisababisha uwepo wa malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau hususan Sekta binafsi kutoridhika na bei zilizopangwa katika huduma za dawa, upasuaji na vipimo. Wizara imechukua hatua ya kupata ufumbuzi wa malalamiko ya wadau kwa kuunda Kamati ya Wataalam kutoka Serikalini na Sekta Binafsi

iliyoongozwa na **Dkt. Baghayo Saqware, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)**.

**337. Mheshimiwa Spika,** Kamati pamoja na masuala mengine ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ya Serikali ya utoaji wa huduma za afya inayosimamiwa na Wizara ya Afya ikiwemo Mwongozo wa Huduma za Matibabu (Standard Treatment Guideline - STG 2021) na Orodha ya Taifa ya Dawa Muhimu – (National Essential Medicine List for Tanzania Mainland - NEMLIT 2021). Aidha, Kamati ilifanya vikao vya majadiliano baina yake na Wadau na **kuweka msingi wa vigezo mahsusi vya ukokotoaji wa bei za huduma za afya**. Vigezo hivyo vilipitiwa, kujadiliwa na kukubaliwa kwa pande zote na hivyo kuzingatiwa katika kuboresha bei za huduma za Kitita cha NHIF cha mwaka 2023.

**338. Mheshimiwa Spika,** Katika **kukokotoa gharama za dawa** vigezo vilivyotumika ni pamoja na kutumia bei za jumla katika soko kwa huduma za dawa kutoka katika maduka ya dawa yasiyopungua 10 pamoja na Bohari Kuu ya Dawa (MSD); Kuweka asilimia 20 hadi 30 kwa gharama za uendeshaji katika kukokotoa mapendekezo ya bei ikiwemo gharama za usafiri, utunzaji, umeme, n.k; Kuweka asilimia 10 hadi 20 kama kiwango cha faida katika kukokotoa mapendekezo ya bei; na Kugawanya asilimia ya gharama za uendeshaji na faida kwa kuzingatia mzunguko wa matumizi ya dawa katika kituo (fast, moderate and slow moving).

**339. Mheshimiwa Spika,** Katika **kukokotoa gharama za huduma za upasuaji na vipimo**, vigezo vilivyotumika ni pamoja na Rasilimali watu, Uchakavu wa Vifaa, Dawa, Vitendanishi na Vifaa Tiba, gharama za uendeshaji kwa kiwango cha asilimia 20 hadi 30 na Faida (Markup) kwa kiwango cha asilimia 10 hadi 30. **Kipekee ninaishukuru Kamati ya Wataalam kwa kubainisha vigezo mahsusi vya kutumia katika kukokotoa gharama za huduma za afya na hivyo kuweka msingi kwa Wizara kufanya maboresho zaidi ya gharama za huduma za afya**.

**340. Mheshimiwa Spika,** Mambo makubwa yaliyofanyiwa maboresho katika Kitita cha Mafao cha NHIF cha mwaka 2023 ni pamoja na;

a. Kuongezeka kwa dawa mpya 254 zenye ufanisi ambazo awali wanachama walilazimika kutoa fedha taslimu kwakuwa hazikuwa sehemu ya Kitita cha mwaka 2016;

b. Dawa 178 ambazo hazikuwa kwenye Orodha ya Dawa Muhimu ya Taifa (NEMLIT) zimeongezwa baada ya Wizara kufanya mapitio ya NEMLIT na kutoa nyongeza (addendum) na hivyo kujumuishwa katika kitita cha NHIF cha mwaka 2023;

c. Kuwaepusha wanachama kuendelea kutumia dawa zisizo na matokeo chanya hivyo kuwaepusha na magonjwa yasiyoambukizwa kutokana na usugu wa dawa husika;

d. Kusogeza huduma za kibingwa na ubingwa bobezi karibu na wananchi kuanzia Hospitali za ngazi mkoa na Kanda, kuondoa usumbufu wa kukosa baadhi ya dawa na huduma nyingine. Huduma hizo ni pamoja na matibabu ya saratani, upasuaji wa mifupa, upasuaji wa moyo ambazo awali zilikuwa zinatolewa katika Hospitali za ngazi ya Taifa tu;

e. Kuweka usawa wa ada ya usajili na kumuona madaktari wenye elimu na taaluma zinazofanana kwa wanufaika wa NHIF. Mathalani, kwa kitita kipya Daktari Bingwa katika ngazi ya Rufaa Mkoa ada imeongezeka kutoka Shilingi 15,000 hadi Shilingi 25,000 ambapo ni sawa na ada ya kumuona Daktari aliyeko ngazi ya Kanda na Taifa. Hatua hii itavutia madaktari bingwa kufanya kazi katika Hospitali za Rufaa za Mikoa hususan ya pembezoni;

f. Ada ya usajili na kumuona daktari kwa wanufaika wa NHIF kwa ngazi ya Wilaya imeongezeka kutoka Shilingi 5,000 hadi Shilingi 7,000; kwa ngazi ya Kituo cha Afya ada imeongezeka kutoka Shilingi 2,000 hadi Shilingi 7,000 na kwa ngazi ya Zahanati ada imeongezeka

kutoka Shilingi 1,000 hadi Shilingi 3,000. Hatua hiyo itaongeza mapato katika vituo na motisha kwa watumishi wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya na hivyo kuvutia Madaktari kufanya kazi katika vituo hivi.

**341. Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua kuwa huduma za afya zinabadilika mara kwa mara kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia na hali halisi ya soko, ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza na kukua kwa Sekta ya Afya ya umma na binafsi, NHIF itafanya mapitio ya kitita cha mafao yake kila baada ya miaka miwili (2). Aidha, Serikali inakusudia kuanzisha **Chombo cha Kitaifa cha Udhibiti wa Bei za Huduma za Afya** katika ngazi zote nchini kama inavyofanyika kwenye udhibiti wa gharama za maji, umeme na mafuta. Lengo ni kudhibiti ukuaji holela wa gharama za afya kwa wananchi hususan wasio na bima ya afya.

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**342. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya, imeanzishwa chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219 yenye jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakiki ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa zitokanazo na tumbaku. TMDA ilianzishwa ikiwa na lengo la kuongeza tija na ufanisi katika udhibiti wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi ili kulinda afya ya jamii. Katika kipindi cha 2023/24 Maabara ya Uchunguzi wa Vifaa Tiba ya TMDA iliyoko jijini Dar es Salaam imepata ithibati (accreditation) baada ya kufanyiwa ukaguzi na Shirika la Uthibitishaji la Jumuiya ya Kikanda ya nchi za SADC (SADCAS Accreditation Body). Hii maana yake Maabara hii sasa imetambuliwa kuwa na ubobezi na umahiri kwenye uchunguzi wa vifaa tiba na hivyo vipimo vyake vitatambulika kimataifa

**343. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha **usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi** na hatimaye kulinda afya ya jamii, kati ya maombi 1,615 ya dawa za binadamu yaliyokuwepo katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024. Mamlaka ilitathmini maombi 1,175 ikiwa ni ongezeko la

maombi 315 sawa na asilimia 36.6 ikilinganishwa na maombi 860 yaliyofanyiwa tathmini katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya maombi yaliyofanyiwa tathmini, maombi 660 yaliidhinishwa na kusajiliwa. Vilevile, jumla ya maombi 199 ya usajili wa dawa za mifugo yalipokelewa ambapo maombi 129 yalifanyiwa tathmini na maombi 95 yaliidhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Aidha, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi, kati ya maombi 221 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi maombi 201 yalifanyiwa tathmini na jumla ya maombi 145 yaliidhinishwa. Kuongezeka kwa idadi ya bidhaa zinazokidhi viwango na kusajiliwa ni kiashiria kuwa wafanyabiashara wameendelea kuzingatia matakwa ya kisheria.

**344. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki kulikuwa na maombi 379 ya **usajili wa maeneo ya biashara** zinazohusiana na dawa ambapo maombi 369 sawa na asilimia 99 yalifanyiwa tathmini ambapo 347 sawa na asilimia 94 yalikidhi vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara. Vilevile, maombi 457 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa ambapo 450 yalitathminiwa na maeneo 448 sawa na asilimia 99 yalikidhi vigezo na hivyo kusajiliwa. Aidha, TMDA ilifanya ukaguzi wa maeneo 7,693 ya biashara ya bidhaa zinazohusiana na dawa nchini ambapo maeneo 6,727 sawa na asilimia 87 yalikidhi vigezo. Ukaguzi wa viwanda 139 ndani na nje ya nchi ulifanyika katika kipindi hiki ili kuhakikisha kuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinatengenezwa kwa kufuata taratibu za utengenezaji bora (GMP) na hivyo kuwalinda watumiaji.

**345. Mheshimiwa Spika**, Kwa kutambua madhara yanayoweza kusababishwa na matumizi ya bidhaa za tumbaku, TMDA imepewa jukumu la kudhibiti uzalishaji, usambazaji, matangazo na mauzo ya bidhaa za tumbaku. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 ukaguzi wa maeneo 117 yanayojihusisha na uendeshaji wa biashara ya bidhaa za tumbaku ulifanyika ambapo yote yalikidhi vigezo. Vilevile, TMDA ilifanya ukaguzi wa shehena tatu (3) za vifungashio vya bidhaa za tumbaku zenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 2.2 katika vituo vya forodha. Aidha, bidhaa za tumbaku zenye uzito wa tani 0.11 na thamani

ya takriban Shilingi 157,358,940.22 ziliteketezwa baada ya kubainika kuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu.

**346. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha **Serikali inamlinda mwananchi dhidi ya matumizi ya bidhaa** za afya ambazo hazikidhi viwango vya ubora, usalama na ufanisi na hivyo kutokuwa salama kwa matumizi ya binadamu, TMDA hufanya kaguzi za bidhaa mbalimbali za afya, na pale inapobainika bidhaa hizo hazijakidhi vigezo huteketezwa ili kuepusha **bidhaa duni, bandia na hafifu** zisitumiwe na wananchi. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 TMDA iliteketeza jumla ya tani 1,846.3 za bidhaa mbalimbali zenye thamani ya takriban Shilingi bilioni 10.5 na hivyo kuzuia bidhaa zenye madhara kuweza kumfikia mwananchi. Aidha, TMDA imeendelea kulinda mipaka ya nchi kwa kuzuia uingizwaji wa bidhaa duni, bandia na ambazo hazijasajiliwa kwa kufanya doria na ukaguzi kwa kushirikiana na vyombo vya dola.

**347. Mheshimiwa Spika**, Katika kuimarisha **utoaji wa elimu kwa umma**, TMDA ilitoa elimu kwa umma kupitia njia tofauti ikiwa ni pamoja na; kufanya mihadhara, vipindi na matangazo mafupi ya redio na runinga. Pia, elimu juu ya matumizi sahihi ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na tumbaku ilitolewa. Jumla ya mihadhara 190 ilifanyika katika Mikoa ya Songwe, Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Lindi, Tanga, Mtwara, Pwani, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro na Arusha ambapo washiriki 61,474 walifikiwa.

**348. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki, Bunge liliridhia Mkataba wa Kuanzisha Taasisi ya Udhibiti wa Dawa Barani Afrika (The Treaty for Establishment of African Medicines Agency - AMA). Mkataba husika umewasilishwa (deposited) kwenye Ofisi za AU zilizoko jijini Addis Ababa - Ethiopia na hivyo kuifanya Tanzania kuwa mwanachama rasmi sasa. Kupitia Mkataba huu Tanzania itanufaika kwa kuwezesha viwanda vyetu vya ndani kupata soko barani Afrika ikiwa ni pamoja na kufaidika na ununuzi wa pamoja kupitia MSD (pooled procurement) na hivyo kusaidia katika upatikanaji wa dawa kwenye nchi yetu.

**Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)**

**349. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya, iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura 177 yenye majukumu makuu ya kufanya uchunguzi wa Kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo, utoaji ushahidi wa kitaalam mahakamani na usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani nchini.

**350. Mheshimiwa Spika**, Katika kutekeleza jukumu la kufanya **uchunguzi wa Kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo nchini**, Mamlaka katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 iliendelea kutoa huduma ya **uchunguzi wa Kimaabara** wa sampuli mbalimbali na vielelezo ambapo jumla ya sampuli 145,273 zilipokelewa. Kati ya sampuli hizo, sampuli 141,683 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 97.6 ya sampuli zilizopokelewa. Aidha, sampuli zilizofanyiwa uchunguzi ni sawa na ongezeko la asilimia 43 ikilinganishwa na sampuli 99,159 zilizochunguzwa kwa kipindi kama hicho cha Mwaka wa Fedha 2022/23. Matokeo ya uchunguzi huo yalisaidia Serikali na Mamlaka nyingine za usimamizi na udhibiti kufanya maamuzi stahiki katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi. Vile vile, katika kuhakikisha ubora wa matokeo ya uchunguzi yanayokubalika kitaifa na kimataifa, Mamlaka imepata Ithibati ya Mifumo ya Ubora ya Maabara (ISO 17025:2017) katika Maabara ya Sayansi Jinai Toksikolojia.

**351. Mheshimiwa Spika**, Katika kuchangia utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Mamlaka ilitoa ushahidi wa kitaalam mahakamani kwa mashauri 882 sawa na asilimia 71.4 ya lengo la kutoa ushahidi wa mashauri 1,236. Aidha, kulikuwa na ongezeko la asilimia 117 ikilinganishwa na mashauri 407 yaliyotolewa ushahidi mahakamani kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2022/23. Mafanikio haya yamechangiwa na Mfumo wa Kielekitroniki wa Kuratibu Taarifa za Wataalam Watoa ushahidi Mahakamani - Expert Witness Management Information System.

**352. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ilisajili wadau 974 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 82.8 ya lengo la kusajili wadau 1176. Wadau waliosajiliwa waliongezeka kwa asilimia 33.2 ikilinganishwa na Wadau 731 waliosajiliwa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2022/23. Lengo la kusajili wadau hawa ni kuendelea na juhudii za kulinda afya, mazingira na usalama wa nchi dhidi ya kemikali hatarishi na bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya au silaha za kemikali. Mamlaka pia ilitoa mafunzo kwa jumla ya madereva 2,961 juu ya usafirishaji salama wa Kemikali nchini. Mafunzo hayo yamesaidia kuwapa uelewa wa namna bora ya kujilinda, kulinda watu wengine pamoja na kulinda mazingira wakati wa usafirishaji wa kemikali hizo.

**353. Mheshimiwa Spika,** Katika kuhakikisha kuwa Mamlaka inakuwa na Vifaa vya kutosha kulingana na mahitaji na vyenye teknolojia ya kisasa, Serikali imeiwezesha Mamlaka kununua mitambo mikubwa mitatu (3) aina ya Gas Chromatography Mass Spectrometer (GC-MS/MS), MinLab 153 (OSA4) na Gas Chromatography (GC) pamoja na vifaa vingine vya maabara vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.57. Uwekezaji huu umeiwezesha Mamlaka kuwa na ufanisi na kuendelea kusogeza huduma karibu zaidi kwa wananchi.

**Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)**

**354. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ina majukumu ya kuratibu, kukuza na kuendeleza utafiti wa afya nchini, kufanya utafiti wa afya ili kupunguza magonjwa yanayosumbua jamii kwa kufanya utafiti wa Tiba Asili na tiba mbadala, kusajili tafiti za afya zinazofanywa nchini, kuwajengea uwezo watafiti wa kitanzania katika kufanya utafiti wa afya na kukuza matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

**355. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali kutoka katika Taasisi za tafiti ndani na nje ya

nchi. Taasisi kupitia Kamati ya Kuratibu Tafiti za Afya (Medical Research Coordination Committee) imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yale yanayokidhi vigezo hupatiwa kibali (ethical clearance) kwa ajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Taasisi ilipokea na kutoa jumla ya maombi **511** ya watafiti ambapo ni sawa na asilimia **85** ya vibali 600 vilivyotegemewa kutolewa kwa ajili ya kuanza tafiti.

**356. Mheshimiwa Spika,** Katika eneo la Utafiti, Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazolenga magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya na pia kuelewa viashiria vya kijamii na mazingira vya afya pamoja na tiba asili. Katika kipindi hiki, Taasisi imetekeleza miradi 127 ambayo ni ongezeko la asilimia 9.6 ya miradi 113 iliyotekelezwa katika kipindi kama hiki kwa mwaka 2022/23. Maeneo yalifanyiwa utafiti ni pamoja na eneo la VVU/UKIMWI (Miradi 11), Malaria (Miradi 17), Kifua kikuu (Miradi 23), Magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Miradi 14), Magonjwa yasiyoambukiza (Miradi 10), Usugu wa dawa (Miradi 4), Afya ya mama na mtoto (Miradi 14), Uimarishaji wa mifumo ya afya (Miradi 2), VVU na magonjwa yasioambukizwa (Miradi 5), VVU na magonjwa yasiyopewa kipaumbele (Mradi 1), Kifua kikuu na Kisukari (Mradi 1), Mahusiano ya hali ya jamii na afya (Miradi 3), Tiba Asili (Mradi 1), Afya Digitali (Miradi 2) na miradi mingineyo 7.

**357. Mheshimiwa Spika**, Taasisi imeendelea na utafiti wa kuboresha tiba ya Malaria kutumia dawa tatu (Triple artemisnin-based combination therapy). Ili kuendelea kuboresha tiba ya Malaria, tokea mwaka 2022, Taasisi imekuwa inafanya utafiti wa kuangalia iwapo tiba ya Malaria yenye dawa tatu (triple artemisinin-based combination therapy) inaweza kuwa bora ikilinganishwa na dawa inayotumika katika hatua ya kwanza kwa sasa ambayo ina dawa mbili. Hivyo, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, washiriki 340 kati ya 432 wanaohitajika wamesajiliwa na tayari **298** kati yao walimaliza kipindi cha ufuatiliaji cha siku **63**.

**358. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kufanya majaribio ya dawa mpya zitakazofupisha urefu wa matibabu ya kifua kikuu kutoka miezi sita (6) hadi minne (4). Matokeo ya awali ya tafiti hizo yameonesha kuwa dawa mpya zina uwezo wa kufupisha urefu wa matibabu toka miezi sita (6) hadi miezi minne (4) kwa wagonjwa wasio na kifua kikuu sugu. Hata hivyo tafiti zaidi zinaendelea ili kupata mchanganyiko wa dawa ambao una maudhi kidogo kwa wagonjwa. Pia Taasisi imetekeleza utafiti wa kuangalia hali ya afya baada ya matibabu ya kifua kikuu (TB sequel study). Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa hali ya afya ya mapafu sio nzuri kwa asilimia 70 ya wagonjwa wanaomaliza dawa za kifua kikuu. Utafiti zaidi unaendelea kuangalia mbinu za kuboresha afya ya mapafu baada ya kumaliza dawa za kifua kikuu. Aidha, Taasisi inaendelea na tafiti za chanjo ya kifua kikuu ambazo zinalenga kupunguza uwezo wa kurudia kupata ugonjwa wa kifua kikuu kwa wagonjwa ambao hawajaathirika na VVU/UKIMWI na pia kuzuia kupata kifua kikuu kwa watoto wachanga.

**359. Mheshimiwa Spika,** Tangu mwaka 2017, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu kwa kushirikiana na washirika wa kiutafiti imekuwa ikifanya utafiti kuangalia ikiwa dozi moja ya chanjo ya Human Papilloma Virus (HPV) ina ufanisi sawa na dozi mbili au tatu katika kutengeneza kinga dhidi ya virusi vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana takribani 1,000 wa miaka kati ya 9 hadi 14. **Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa dozi moja ya chanjo dhidi ya HPV ina ufanisi kama dozi mbili au tatu kwa kipindi cha muda wa miaka miwili**. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, wasichana hawa wamefuatiliwa ili kujua ikiwa ufanisi wa chanjo hii utadumu kwa miaka 6 baada ya kupokea chanjo. Matokeo yatakapokamilika yatasaidia kujua ikiwa dozi hii ya HPV inayotolewa kwa mara moja itatoa kinga kwa muda mrefu baada ya miaka 2 ya kwanza.

**360. Mheshimiwa Spika,** Taasisi inaendelea na mradi wa utafiti wa majaribio ya kutoa huduma za kibingwa kwa baadhi ya magonjwa yasiyoambukiza kama vile ugonjwa wa moyo, shinikizo la juu la damu, Kisukari na seli mundu kwenye Hospitali za wilaya. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya za Kondoa na Karatu na ni

mategemeo yetu kuwa **matokeo ya utafiti huu yatafanya nchi yetu iwe na miongozo madhubiti ya kuhudumia magonjwa haya makubwa yasiyoambukiza katika ngazi za wilaya**. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Taasisi imemaliza utafiti wa awali wa kubaini uelewa wa wananchi na watoa huduma za afya katika kuhudumia magonjwa haya. Matokeo yanaonyesha kuwa uelewa wa jamii kuhusu magonjwa haya yasiyoambukiza bado upo chini ambapo zaidi ya asilimia 80 ya wananchi waliohojiwa hawakuwa na uelewa wa kutosha. Hali kadhalika kwa upande wa maboresho ya huduma matokeo ya utafiti yameonyesha kuwa watoa huduma waliowezeshwa kwenye ngazi ya wilaya wameonyesha uwezo mkubwa wa kutoa huduma hizi kwenye ngazi hiyo. Mpaka mwisho wa mwezi Machi 2024 zaidi ya wagonjwa 150 ambao wangehitaji huduma kwenye Hospitali za rufaa wanahudumiwa katika Hospitali za ngazi ya wilaya za mradi na kati ya hawa wagonjwa 4 ndio waliopatiwa rufaa. **Matokeo zaidi ya utafiti huu yatasaidia kujua namna bora ya kufikisha huduma karibu na wananchi na kupunguza gharama za huduma za afya** na kuongeza ubora wa maisha kwa wagonjwa wenye magonjwa hayo.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MABARAZA NA BODI ZA KITAALUMA.

### Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)

**361. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni mamlaka ya Kisheria, yenye jukumu la kusimamia taaluma na wanataaluma wa Uuguzi na Ukunga Tanzania. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga "The Nursing and Midwifery Act 2010". Aidha, majukumu mengine ya Baraza ni kulinda; kuimarisha na kuhifadhi afya ya jamii; usalama na ustawi kupitia usimamizi na udhibiti wa shughuli za mafunzo ya uuguzi na ukunga na utoaji wa huduma; na kuhakikisha jamii inapata huduma bora zenye kiwango na salama.

**362. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **wauguzi na wakunga 2,179 wamesajiliwa** sawa na asilimia 54.4 ya lengo la kusajili wataalam 4,000 ikilinganishwa na

wataalam 2,455 waliosajiliwa katika kipindi kama hichi mwaka 2022/23. Idadi hiyo inafanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi Machi 2024 kufikia 52,118. Aidha, wauguzi na wakunga 576 wamepewa usajili wa awali (Provisional registration) na wanaendelea na mafunzo ya utarajali katika vituo 31 zikiwemo Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda nne (4) na Hospitali za Rufaa za Mikoa 27.

**363. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya **wauguzi na wakunga 4,246** waliomba na kukidhi sifa za kufanya **mtihani kwa ajili ya usajili** ikilinganishwa na **4,865** mwaka 2022/23. Idadi hiyo ilijumuisha watahiniwa 542 sawa naasilimia 13 wa ngazi ya shahada, watahiniwa 3,608 sawa na asilimia 85 wa ngazi ya stashahada na watahiniwa 96 sawa na asilimia mbili (2) wa ngazi ya astashahada. Watahiniwa waliofaulu walikuwa 2,179 sawa na asilimia 51.3 ambapo watahimiwa 395 sawa na asilimia 73 wa ngazi ya shahada walifaulu, watahiniwa 1,737 wa ngazi ya stashahada sawa na asilimia 48 walifaulu na watahiniwa 169 wa ngazi ya astashahada sawa na asilimia 2 pia walifaulu. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya maombi 10 ya kuanzisha mafunzo ya uuguzi na ukunga yalipokelewa. Kati ya maombi hayo vyuo saba (7) vilivyoomba vilikuwa na sifa na kupata kibali cha kuanzisha mafunzo. Aidha, katika kipindi hiki Baraza la Uuguzi na Ukunga lilipokea maombi manne (4) ya kuanzisha huduma binafsi za Uuguzi na Ukunga ambapo vituo vyote vilikaguliwa na kukidhi vigezo na kufanya vituo vyote vilivyosajiliwa na Baraza kufikia 94.

**364. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki, wauguzi na wakunga 32,643 wamefanya **mafunzo ya kujiendeleza (CPD)** kwa njia ya mtandao, kuhudhuria semina na kufanya tafiti ili kukidhi takwa la kisheria la kuhuisha leseni za kutoa huduma. Aidha, jumla ya moduli 38 za mafunzo ya kujiendeleza zenye maudhui mbalimbali zilipokelewa na kuhakikiwa ambapo moduli zote zilikidhi sifa na kupata ithibati.

**365. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **mashauri 11 ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa**. Mashauri manane (8) yalifuatiliwa na kutolewa

maamuzi kama ifuatavyo: wauguzi watatu (3) walisimamishwa kutoa huduma za uuguzi na ukunga kwa vipindi vya miezi sita (6) na miaka miwili (2), muuguzi mmoja (1) alipata karipio kali, wauguzi watatu (3) walipewa onyo na muuguzi mmoja hakupatikana na makosa na mashauri mawili (2) yanaendelea kufuatiliwa.

**Baraza la Madaktari Tanganyika**

**366. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia usajili, utendaji na maadili ya wataalam pamoja na taaluma ya udaktari kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **wataalam 6,578 wamesajaliwa na Baraza** ikilinganishwa na wataalam 5,106 waliosajiliwa katika kipindi cha Julai 2022/23 sawa na ongezeko la asilimia 29 na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa mpaka Machi 2024 kufikia 39,133.

**367. Mheshimiwa Spika,** Baraza katika kutekeleza jukumu lake la usimamizi wa **mitihani ya watarajali** huaandaa mitihani kabla watarajali hawajaanza mafunzo na baada ya kumaliza mafunzo. Jumla ya maombi yaliyopokelewa ya mtihani wa kabla ya utarajali uliofanyika Oktoba 2023 yalikuwa **1,026** ambapo watahiniwa wa Udaktari walikuwa 957, udaktari wa meno walikuwa 64, fiziotherapia walikuwa wanne (4) na wataalam wa tiba kazi mmoja (1). Baada ya mtihani waliruhusiwa kuendelea na mafunzo ya utarajali. Aidha, jumla ya watarajali 1,493 walifanya mtihani wa baada ya mafunzo mwezi Desemba 2023; kati yao watarajali wa udaktari ni 1,451, udaktari wa meno 41 na mmoja (1) mtarajali wa fiziotherapia. Jumla ya wanataaluma 1,195 sawa na asilimia 80 walifaulu na wanataaluma 298 wote wakiwa wa taaluma ya udaktari hawakufikia ufaulu unaohitajika.

**368. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza kupitia Kamati ya Mafunzo endelevu ya kitaaluma imefanya uhamasishaji wa **Mafunzo endelevu kwa Wanataaluma (CPD)** kwenye mikutano mitano (5) ya vyama vya kitaaluma ambayo ni mkutano wa chama cha Wanafiziotherapia Tanzania (APTA), mkutano wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT),

Mkutano wa Chama cha Madaktari wa Meno Tanzania (TDA) na Chama cha Wataalam wa Viungo saidizi (APOT). Pia kamati imefanya uhamasishaji wa mafunzo endelevu kwa wanataaluma kwenye makongamano manne (4) ya Afya ambayo ni Rehabilitation Summit, Tanzania Health Summit, Netcare Foundation na Neonatal Conference. Katika kipindi hiki, Baraza limetoa ithibati kwa watoa mafunzo endelevu 18 na kufanya kuwa na jumla ya watoa mafunzo endelevu waliosajiliwa 152. Aidha, kozi za mafunzo endelevu 143 zilipewa ithibati na kufanya kuwa na jumla ya kozi za mafunzo endelevu kufikia 973.

**369. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Baraza lilifuatilia **ukiukwaji wa maadili** ambapo jumla ya **malalamiko 26** yalipokelewa. Malalamiko 21 yalichunguzwa na Kamati ya Uchunguzi wa Mashauri ya Kitaaluma na mashauri 19 yalisikilizwa na Baraza dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya taaluma zao. Baada ya mashauri kusikilizwa na Baraza, wanataaluma watano (5) walipewa onyo, wawili (2) karipio kali, saba (7) walifungiwa leseni kwa miezi sita (6) pamoja na kutakiwa kuhudhuria mafunzo ya maadili kwa miezi sita (6), watatu (3) walisitishiwa leseni kwa miaka miwili (2) na kutakiwa kuhudhuria mafunzo ya maadili kwa miezi sita (6), wanne (4) walifutiwa leseni na mmoja alihisiwa kuwa na ugonjwa wa akili nakupelekea kuendelea kuchunguzwa hali yake ya kiafya.

**Baraza la Famasi**

**370. Mheshimiwa Spika**, Baraza la Famasi ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya, iliyoanzishwa kupitia Kifungu Na. 3 cha Sheria ya Famasi, Sura 311 kwa lengo la kusimamia taaluma ya wanataaluma wa dawa, utendaji wake ikiwa ni pamoja na usajili na kutoa vibali katika maeneo yanayotoa huduma za dawa na kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa. Baraza la Famasi limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika.

**371. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 wafamasia **164 wamesajiliwa**, **fundi dawa sanifu 1,438 wameandikishwa na fundi dawa wasaidizi 105 wameorodheshwa** katika kipindi hiki na kufikisha **jumla ya wanataaluma 12,975** ambapo kati ya hao, wafamasia ni 3,673; fundi dawa sanifu ni 8,292; fundi dawa wasaidizi ni 1,010. Idadi hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15 ya wanataaluma wote ikilinganishwa na idadi ilivyokuwa hadi kufikia Julai 2023 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 12**. Aidha, hadi kufikia Machi 2024 wanataaluma 9097 sawa na asilimia 70.1 wamehuisha leseni zao ikilinganishwa na 6,900 sawa na asilimia 65.4 katika mwaka 2022/23.

**Jedwali Na. 12:** Mchanganuo wa idadi ya Wanataaluma wa dawa kwa kuzingatia kada

| **Aina ya Wanataaluma** | **Julai 2022 – Machi 2023** | | **Julai 2023 – Machi 2024** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| Wafamasia | 331 | 17 | 164 | 9.6 |
| Fundi dawa sanifu | 1,564 | 79 | 1,438 | 84.2 |
| Fundi dawa wasaidizi | 89 | 4 | 105 | 6.2 |
| **Jumla** | **1,984** | **100** | **1,707** | **100** |

**372. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya vyuo 25 viliwasilisha **maombi ya kuanzisha kozi ya famasi ngazi ya stashahada (NTA Level 04 - 06)** ambapo kati ya hivyo, vyuo 12 vilikidhi vigezo na kuidhinishwa kuanzisha mafunzo ya famasi na hivyo kufanya vyuo vilivyoidhinishwa kutoa mafunzo ya famasi ngazi ya stashahada na shahada, kufikia 99 hadi sasa. Aidha, kati ya vyuo 99 vilivyoidhinishwa kutoa mafunzo ya famasi ngazi ya stashahada na shahada, vyuo 30 sawa na asilimia 33.3 vilikaguliwa kwa lengo la kufuatilia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Pwani na Dar es Salaam.

**373. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Baraza **limesajili majeng**o **403 ya kutolea huduma ya dawa**, ambapo kati ya hayo, famasi za ndani ya Hospitali ni 06, famasi za

jumla za wasioagiza dawa nje ya nchi 40, rejareja 304, maghala ya kutunzia dawa 06, na famasi za jumla na rejareja ni 47 na kufanya jumla ya majengo ya famasi yaliyosajiliwa mpaka sasa kufikia 3,763. Aidha, majengo 76 ya famasi yamefutiwa usajili/kibali cha biashara kutokana na kutoendelea kutoa huduma hizo katika kipindi hiki na kufanya idadi ya majengo yanayotoa huduma hadi sasa kubakia 3,238. Jumla ya majengo ya famasi yaliyosajiliwa katika kipindi cha kufikia Machi 2024 ni sawa na asilimia 79 ikilinganishwa na idadi ya majengo yaliyosajiliwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kwa upande wa maduka ya dawa muhimu, vibali vipya vyenye nembo za utambuzi 3,264 vimetolewa na kufikia jumla ya maduka 19,679 yanayotambulika kote nchini.

**374. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki, Baraza limefanya **kaguzi za maduka** yanayotoa huduma za dawa katika mikoa tisa (9) ya Singida, Iringa, Mara, Geita, Tabora, Arusha, Kilimanjaro, Lindi na Dar es
Salaam, ambapo jumla ya maduka 978 yalikaguliwana maduka 235 yalichukuliwa hatua mbalimbali kutokana na makosa kama ifuatavyo; maduka 73 kukosa vibali, maduka 68 kukosa wahudumu wenye sifa za kutoa huduma na 94 kutoa huduma zisizo za kifamasia.

**375. Mheshimiwa Spika,** Baraza limefanya **ukaguzi wa huduma za dawa katika Hospitali sita (6)** za Rufaa za Mikoa ya Geita, Singida, Ruvuma, Mawenzi, Tabora, Amana na vituo tisa (09) vya kufundishia watarajali ambavyo ni Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Taasisi ya Mifupa (MOI), Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Amana, CCBRT, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Aga Khan, Mawenzi pamoja na Kitete ili kuimarisha utendaji wa wanataaluma.

**376. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeratibu **mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD)** ambapo jumla ya wanataaluma 9097 sawa na asilimia 70.1 ya wanataaluma wa dawa 12,975 walishiriki mafunzo hayo. Aidha, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya moduli saba (7) zimepata ithibati na kufikia jumla ya moduli 35 za mafunzo endelevu.

**377. Mheshimiwa Spika,** Baraza limepokea **mashauri 55 ya kinidhamu** dhidi ya wanataaluma waliokiuka maadili ya kitaaluma katika maeneo yao ya kazi. Malalamiko 17 sawa na asilimia 30.9 yalithibitika na kuchukuliwa hatua kupitia kamati ya nidhamu. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na wanataaluma 09 wametakiwa kurudia mafunzo ya utarajali kwa muda wa mwaka mmoja (01), wanataaluma 3 wamepewa onyo, wanataaluma wawili (02) waliruhusiwa kuendelea na hatua za usajili kamili na wanataaluma watatu (03) hawakutokea kwenye kikao cha kamati ya nidhamu kutokana na sababu mbalimbali, hivyo mashauri yao yatasikilizwa kwenye kikao kinachofuata.

**Baraza la Wataalam wa Radiolojia**

**378. Mheshimiwa Spika,** Baraza limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza lilipitia **maombi ya usajili wa wataalam wa Radiolojia** kwa kada mbalimbali na kufanya usajili wa matazamio, kamili, muda, uandikishaji na uorodheshaji kwa wataalam waliokidhi vigezo. Katika kipindi hiki **jumla ya wataalam 344 walisajiliwa,** kuorodheshwa, na kuandikishwa na hivyo kufanya jumla ya wataalam ambao wameshasajiliwa na Baraza tangu kuanza usajili mwaka 2011 kufikia 1,840. Aidha, katika kipindi hiki jumla ya wataalam 810 kati ya wataalam 1,400 walihuisha leseni zao sawa na asilimia 58 ya waliotegemewa kuhuisha leseni kwa mwaka 2023/24.

**379. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kusimamia watarajali wa kada za Radiolojia nchini ambapo jumla ya **watarajali 49 walipewa mafunzo** juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili na kupangiwa vituo vya utarajali. Aidha, mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa usajili (HPRS) yameendelea kutolewa kwa wataalam wa Radiolojia nchini. Jumla ya wataalam 1,450 kati ya 1,840 sawa na asilimia 78 wameweza kutumia mfumo wa kujisajili na kuhuisha leseni. Pia, jumla ya wahitimu 49 wa ngazi ya shahada wameweza kuchagua vituo vya utarajali kwa njia ya mfumo tajwa.

**380. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza lilitoa **mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili kwa wahitimu 300 wa shahada, na stashahada katika fani za Radiolojia nchin**i. Aidha, katika kipindi cha maadhimisho ya mgunduzi wa mionzi (Rountigen Day) Baraza lilishiriki kuandaa mafunzo endelevu kwa Watalaamu 450 juu ya sheria, kanuni, utaalamu (professionalism), miiko na maadili na huduma kwa mteja.

**381. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza lilipokea jumla ya **mashauri matatu (3) ya uvunjifu wa miiko na maadili** ya taaluma. Mashauri yote yapo katika hatua za uchunguzi, yatakapokamilika hatua stahiki zitatolewa kulingana na sheria, kanuni, miongozo ya miiko na maadili ya taaluma.

**Baraza la wataalam wa Macho (Optometria)**

**382.** Baraza la Wataalam wa Optometria limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria ya Optometria ya Mwaka 2007 na kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka. Jukumu kuu la Baraza ni usimamizi na udhibiti wa wataalam wa kada ya optometria, kliniki za optometria, wasambazaji wa vifaa na miwani na kuhakikisha kliniki zote zinazotoa huduma za optometria zinasajiliwa na kupatiwa leseni.

**383. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wataalam 48 **wamesajiliwa** katika kipindi hiki sawa na asilimia 120 ya wataalam 40 waliokusudiwa na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa usajili wa kudumu kufikia 416. Aidha, Baraza linaendelea na utaratibu wa kusajili wataalam wake kwa njia ya mfumo wa kielektroniki, ambapo wataalam wote 416 wamesajiliwa kupitia mfumo huo. Vilevile, Baraza lilifanya **usimamizi shirikishi kwenye kliniki na vituo vya kutolea huduma za optometria** katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma ambapo jumla ya vituo 39 vilikaguliwa ambapo vituo 16 vilikutwa na changamoto mbalimbali. Kati ya vituo hivyo, baadhi vilishauriwa namna bora ya kuendesha huduma za optometria na vingine vilichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Baraza.

**384.** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya wataalam 152 walipatiwa elimu kuhusu **mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD)** ya fani ya optometria katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Baraza lilifanikiwa kufanya kikao na wataalam wa Optometria na wamiliki wa vituo vinavyotoa huduma za optometria kutoka jiji la Dodoma. Jumla ya Wataalam 20 walikumbushwa juu ya kuzingatia maadili, kutoa huduma bora (customer care), Sheria ya optometria, matumizi ya Mfumo wa usajili wa wataalam (HPRS) na Mfumo wa kielektroniki wa kusajili vituo vya kutolea huduma ya afya (HFRS) ili kuongeza ufanisi na kuboresha huduma za macho jijini Dodoma.

**Baraza la Wataalam wa Maabara ya Afya**

**385. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Wataalam wa Maabara limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Jukumu kuu la baraza ni kuhakikisha wataalam wa maabara ya afya wamesajiliwa, wameandikishwa, pamoja na kufuata miiko na maadili ya taaluma ya Maabara. Aidha, jukumu lingine la Baraza ni kuhakikisha usimamizi wa utekelezaji wa mitaala ya mafunzo ya maabara ya afya.

**386.** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya **wataalam 1,267 wapya wa maabara wamesajiliwa** na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia **15,123**. Aidha katika kipindi hiki, wataalam 2,047 wamehuisha leseni zao. Idadi hii ni ongezeko la asilimia 8.4 kati ya Wataalam 3,314 waliosajiliwa kipindi hiki, Wataalam waliopewa usajili wa kudumu ni 1,812 (FRP), usajili wa awali (PRP) ni 1,267 na usajili wa kuorodheshwa ni 235 (ERP). Katika kipindi hiki, Baraza liliweza kutoa leseni kwa wapimaji wa VVU wasio wataalam wa maabara 1,271 na kufanya jumla ya wapimaji waliopewa leseni na Baraza kufikia 13,478.

**387. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilisimamia **mitihani ya usajili** kwa ngazi zote (Astashahada, Stashahada na Shahada) ambapo jumla ya maombi 1,604, yalipokelewa ikilinganishwa na maombi 1,544 mwaka 2022/23 kati yao wataalam wa Astashahada walikuwa 165; Stashahada walikuwa 1,115, na Shahada walikuwa

324. Ufaulu wa jumla ulikuwa asilimia 89.6 na 89.0 kwa mtihani wa nadharia na vitendo mtawalia ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 54.3 mwaka 2022/23. Baraza limeongeza kituo kimoja cha mafunzo ya utarajali na kufanya jumla ya vituo vinavyotambuliwa na Baraza kuwa 24. Kituo kilichoongezeka ni cha Hospitali ya Peramiho baada ya Baraza kufanya ukaguzi katika vituo vitatu (3) vya Hospitali za Nkinga – Tabora, Peramiho – Ruvuma na CCBRT-Dar es salam. Aidha, kwa kipindi hiki jumla ya watarajali 375 wamepata usajili wa muda ambapo wanatarajiwa kufanya mitihani ya usajili wa kudumu baada ya kumaliza mafunzo yao ya utarajali.

**388. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Baraza lilifanikisha kuwapatia wataalam wa Maabara 1,558 alama za **mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD).** Aidha, taasisi nane (8) mpya zimeidhinishwa kuwa watoaji wa mafunzo endelevu (CPD Provider) na kufikisha taasisi 10 zinazotoa mafunzo. Vilevile, Baraza limekamilisha kuweka moduli za CPD katika mfumo wa usajili wa wataalam (HPRS) ili kuwawezesha wataalam wengi zaidi kupata mafunzo hayo kwa urahisi.

**389. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Baraza **lilifuatilia ukiukwaji wa maadili** ambapo jumla ya mashauri sita (6) yalifunguliwa. Shauri moja (1) lilihusisha ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma kwa mtaalam ambapo hatua za uchunguzi zinaendelea. Mashauri matano (5) yalihusisha kughushi vyeti vya taaluma na usajili. Mashauri hayo yamewasilishwa kwenye mamlaka za uchunguzi wa makosa ya jinai kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

**Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira**

**390. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Afya Mazingira lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na. 20. The Environmental Health Practitioners (Registration) Act, 2007 na linatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa taratibu na Kanuni za jumla za Usajili "The Environmental Health Practitioners (General) Regulations, 2011" (GN 388 ya 2011) kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Baraza ni kusajili

Wataalam wa Afya Mazingira ili kulinda na kusimamia nidhamu na Maadili katika taaluma ya Afya Mazingira.

**391. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 idadi ya **wataalam wapya waliosajiliwa** na Baraza la Afya Mazingira ni 382 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa kufikia 4,467 ikilinganishwa na wataalam 397 waliosajiliwa kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kati ya wataalam 4,467 waliosajiliwa, wenye usajili kamili (Full Registration) ni 1,898 usajili wa kuorodheshwa (Enrolment Registration) ni 1,988 na sajili wa kuandikishwa (Enlisting Registration) ni 581. Aidha, Baraza linaendelea na utaratibu wa kusajili wataalam kwa njia ya kielektroniki (hprs.moh.go.tz) ambapo jumla ya wataalam 3,637 wamesajiliwa kupitia mfumo huo.

**392. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeratibu **mafunzo ya utarajali** ambapo kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya watarajali 167 wanaendelea na mafunzo na 109 wamehitimu. Aidha, ufuatiliaji wa usajili, uhuishaji wa leseni na watarajali umefanyika katika mikoa nane (8) ya Mbeya, Morogoro, Singida, Kigoma, Dar es Salaam, Songwe, Njombe na Tanga. Pia ufuatiliaji umefanyika katika vyuo vya Afya Mazingira Mpwapwa, MUHAS, Muheza na Kagemu kwa lengo la kuelimisha juu ya masuala ya usajili na uhuishaji wa leseni, kusambaza leseni za wataalam na kufuatilia watarajali wanaoendelea na mafunzo.

**393. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea kutekeleza jukumu lake la **kusimamia nidhamu na maadili** katika taaluma ya Afya Mazingira ambapo kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Baraza limewabaini wataalam 13 kutoka katika mikoa nane (8) ambao hawajasajiliwa kabisa na hatua za kinidhamu dhidi yao zinaendelea kuchukuliwa kwa kuzingatia Sheria ya Baraza.

**Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala**

**394. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala ni chombo cha kisheria kilichoundwa kwa mujibu wa Sheria Namba 23 ya Mwaka 2002 yenye lengo la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza shughuli za Tiba Asili na Tiba Mbadala nchini. Baraza

limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kwa kuzingatia mpango kazi na bajeti ya mwaka husika.

**395. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya wataalam (waganga na wasaidizi wa Tiba Asili na tiba mbadala na wauza dawa za asili) 5,354 **wamesajiliwa,** sawa na asilimia 118.9 ya lengo la kusajili wataalam 4,500 kwa mwaka, na kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza hadi sasa kufikia 51,593**.** Kati ya wataalam 5,354 waliosajiliwa, wataalam 4,994 walipatiwa usajili wa awali na 360 walipatiwa usajili wa kudumu. Aidha, Baraza lilisajili dawa asili kundi la pili ambapo hadi Machi 2024 **Baraza limesajili jumla ya dawa asili 19** na kufanya jumla ya dawa asili zilizosajiliwa hadi sasa kufikia 112. Pia, Baraza limesajili vituo vya Tiba Asili 225 na kufanya jumla ya vituo 1,600**.** Vilevile, Baraza limeendelea na utaratibu wa kusajili wataalam wake na vituo vya kutolea huduma kwa njia ya mfumo wa kielektroniki (HPRS) ambapo jumla ya wataalam 289 wamesajiliwa.

**396. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilitekeleza mkakati wa kusajili watalaam wa Tiba Asili na tiba mbadala kwa utaratibu wa usajili wa papo kwa papo kwa wataalam wa Tiba Asili na vituo vya kutolea huduma katika mikoa ya Katavi na Rukwa. Utekelezaji huu ni mojawapo ya mkakati wa Baraza wa kuongeza kasi ya usajili wa watalaamu, kupunguza changamoto ya wataalam wengi kufanya kazi bila kuwa na leseni na kupunguza malalamiko ya ucheleweshwaji wa kupata leseni uliokuwepo kutokana na sababu mbalimbali. Katika zoezi hilo, watalaam 1,237 walisajiliwa katika mikoa hiyo. Aidha, katika kipindi hiki, Baraza lilitumia fursa ya kushiriki kwenye Maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba, Nanenane na Wiki ya Tiba Asili ya Mwafrika kuhamasisha na kutoa elimu kwa wananchi ambapo waganga wa Tiba Asili 935 walisajiliwa.

**397. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Baraza **lilikagua vituo 85** vilivyopo Manispaa ya Kinondoni (41), Ilala (15), Temeke (3), Ubungo (20) na Kigamboni (6). Aidha, Katika kuhakikisha kuwa dawa za Tiba Asili zinazosajiliwa na Baraza zinazingatia vigezo muhimu, Sekretarieti ya Baraza ilifanya

ukaguzi wa maeneo ya kutengenezea dawa kwa maombi ya usajili wa dawa yaliyotumwa kabla ya dawa hizo hazijapelekwa kwenye kikao cha kamati kujadiliwa. Ukaguzi huo ulifanyika katika maeneo 15 katika mikoa ya Tabora, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam.

**398. Mheshimiwa Spika,** Baraza limeendelea **kutoa mafunzo kwa watalaamu wa Tiba Asili** kuhusu sheria, kanuni, miongozo na taratibu mbalimbali ili kuendeleza Tiba Asili nchini. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 watoa huduma za Tiba Asili na tiba mbadala 108 wamejengewa uwezo katika utekelezaji wa kazi za usimamizi na utoaji wa huduma za Tiba Asili na tiba mbadala. Aidha, Baraza limeendelea kushirikiana na Baraza la Tiba Asili na Mbadala Zanzibar kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

**399. Mheshimiwa Spika,** Baraza lilifanya Kikao cha Baraza na viongozi wa vyama 19 vya Waganga wa Tiba Asili na tiba mbadala kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na uendeshaji mzuri wa shughuli za Tiba Asili na tiba mbadala nchini. Kikao hicho kiliweka maazimio ya kuboresha huduma za Tiba Asili nchini na kuondoa migongano kati ya Baraza na viongozi wa vyama vya waganga wa Tiba Asili na tiba mbadala. Aidha, katika kuhakikisha masuala ya weledi na miiko ya maadili yanazingatiwa, Baraza lilitoa onyo na tozo kwa vyombo vya habari viwili kwa kukiuka taratibu za matangazo ya tiba asili.

**Bodi ya Maabara Binafsi za Afya**

**400. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ni Chombo kilichoanzishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1997 Sura 136 ya kuratibu huduma za maabara binafsi za Afya. Bodi hii ina jukumu la kusajili, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma bora za maabara binafsi hapa nchini zinatolewa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za Afya (Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali pamoja na Maabara zote zinazojitegemea) kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyowekwa.

**401. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi Julai hadi Machi 2024 idadi ya vituo **vilivyosajiliwa** na Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ni 238

hii inapelekea jumla ya Maabara Binafsi nchini kufikia 4,093. Kati ya hizo maabara zinazojitegemea ni 1,410 na zilizojishikiza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ni 2,683 ikilinganishwa na mwaka 2022/23 ambapo Bodi ilikuwa na jumla ya Maabara Binafsi 3,212 zilizosajiliwa na maabara zinazojitegemea zilikuwa 1,593 wakati zilizojishikiza kwenye vituo vya kutolea huduma za afya zilikuwa 1,619.

**402. Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 Bodi imefanikiwa kufanya ufuatiliaji wa huduma na kutoa elimu ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayotumika katika usimamizi na uendeshaji wa huduma za vipimo kwa wamiliki wa maabara binafsi za afya katika kanda tatu (3) uliohusisha mikoa nane (8) ambapo jumla ya Maabara 742 zilikaguliwa ikilinganishwa na maabara 528 katika kanda tatu (3) zilizohusisha mikoa saba (7) mwaka 2022/23.

**403. Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya kaguzi hizo yanaonesha maabara kuzingatia vigezo vya mfumo wa udhibiti ubora ambapo uhakiki wa ubora wa ndani wa vipimo (IQC) uliongezeka kutoka asilimia 21 hadi 55 na matengenezo kinga ya mashine yalipanda kutoka asilimia 40 hadi 45. Hata hivyo, ilibainika kuwa asilimia 55 ya vituo vilikuwa na watumishi wenye sifa ikilinganishwa na asilimia 74 mwaka 2022/23. Vilevile, kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, idadi ya maabara zisizosajiliwa ilikuwa 110 kati ya 742 zilizokaguliwa sawa na asilimia 15 ikilinganishwa na maabara 170 kati ya 679 sawa na asilimia 25 mwaka 2022/23.

**404. Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mapungufu yaliyobainika, ofisi ya Msajili ilichukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya ubora wa huduma za maabara, matumizi ya mfumo wa usajili wa vituo vya afya (HFRS) na sheria na kanuni za uendeshaji wa maabara binafsi za afya na kuzingatia matengenezo kinga kwa mashine zote za maabara. Hatua nyingine zilizochukuliwa zilihusisha kusitisha huduma za maabara binafsi kwa muda wa miezi 3 hadi 6 kabla ya kuzifutia usajili. Hali kadhalika maabara 90 zilizokuwa na usajili zilipewa onyo na 20 zilizokuwa zinaendeshwa bila kusajiliwa zilifungiwa na kupewa utaratibu wa kujisajili.

**Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi**

**405. Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi iliyoanzishwa kwa Sheria Na. 26 ya Mwaka 1991 ina jukumu la msingi la kusajili na kusimamia vituo vyote vya afya binafsi. Hadi kufikia Machi 2024, **Bodi ilikuwa imesajili** jumla ya vituo 3,242 kati ya vituo hivyo vituo vinavyofanya kazi ni 3,111 vilivyofungwa moja kwa moja ni vituo 15 na vituo 116 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Aidha katika vituo vinavyofanya kazi kuna Hospitali 209, vituo vya afya 295, zahanati 1,818, kliniki 374, polyclinics 375, kliniki za kusafisha damu 22 na vituo vya uchunguzi 18.

**406. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 jumla ya **maombi 166** ya vituo binafsi yaliwasilishwa; maombi 148 yalikuwa maombi ya vituo vipya, maombi 11 yalikuwa ya vituo vinavyoomba kupandishwa daraja, na vituo sita (6) viliwasilisha maombi mengineyo. Aidha, vituo 70 sawa na asilimia 42 vilikidhi vigezo vya kusajiliwa, vituo 80 sawa na asilimia 48 vilikuwa na mapungufu mbalimbali yaliyohitaji kuboreshwa na vituo 16 sawa na asilimia 10 havikukidhi vigezo.

**407. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, jumla ya vituo vya huduma 164 vilisajiliwa, hii ikijumuisha maombi yaliyokuwa yamewasilishwa kabla ya kipindi cha Julai 2023, kati ya vituo hivyo kulikuwa na Kliniki 35, Polyclinics 28, Dialysis clinics 1, Hospitali ngazi ya Mkoa 1, ngazi ya Wilaya 2, vituo vya afya 4 na Zahanati 93. Aidha, jumla ya mashirika 67 yalileta maombi ya kuidhinishwa kusimamia huduma za afya ambapo mashirika 52 sawa na asilimia 78 yamekidhi vigezo, mashirika 14 sawa na asilimia 21 yalikuwa na mapungufu yanayohitaji marekebisho na shirika 1 sawa na asilimia 1 halikukidhi vigezo.

**408. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu na kuhakikisha huduma zinaboreshwa Bodi ilifanya **ukaguzi wa vituo** vya kutolea huduma za afya binafsi katika mikoa ya Songwe, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Manyara na Dar es Salaam. Jumla ya vituo 272 vilikaguliwa ambapo jumla ya vituo 24 vilisitishwa kutoa huduma kutokana na mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na

kutokuwa na usajili, uhaba mkubwa wa watumishi, miundombinu chakavu na kutozingatia miongozo ya kukinga na kuzuia maambukizi.

## E. VIPAUMBELE VYA WIZARA YA AFYA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**409. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2024/25 Wizara imejiwekea vipaumbele vifuatavyo ili kuboresha huduma za afya nchini:-

(a) Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa;
(b) Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Taifa;
(c) Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini;
(d) Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga;
(e) Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;
(f) Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini;
(g) Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;
(h) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za magonjwa ya kuambukiza, magonjwa
(i) yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko;
(j) Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu; na
(k) Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya.

**410. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2024/25, Wizara imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 1,311,837,466,000** kutekeleza

**vipaumbele 10** kwa kutumia **afua (intervention) 89** kama ifuatavyo:-

i. **Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ambapo kiasi cha Shilingi 117,611,588,304.00 kimetengwa zitakazotekeleza afua zifuatazo:**

(a) Kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa kuwafikia watoto (surviving infants) 3,117,564 wenye umri chini ya miaka miwili (2), wasichana 871,429 wenye umri wa miaka tisa (9) na wajawazito 3,298,437 (Shilingi 115,369,238,904.00);

(b) Kutekeleza afua za lishe ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhimiza unyonyeshaji na ulishaji sahihi wa watoto, elimu ya lishe kwa jamii na kuimarisha Mpango wa kuongeza virutubishi kwenye vyakula ambapo ununuzi na usimikaji wa mashine 300 za kuongeza virutubishi (Dozifiers) utafanyika (Shilingi 1,607,700,000.00);

(c) Kuimarisha utekelezaji wa afua za usafi na afya mazingira katika jamii, Mipakani, taasisi za umma na binafsi ikiwemo kutekeleza kampeni ya mtu ni afya awamu ya pili (Shilingi 634,649,400.00);

(d) Kufanya ufuatiliaji wa magonjwa ya mlipuko;

(e) Kutekeleza Kampeni ya Elimu ya Afya Jumuishi mashuleni, sehemu za kazi na maeneo ya umma; na

(f) Kuendeleza utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii (Shilingi 1,000,000,000.00).

ii. **Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote ambapo jumla ya Shilingi 219,010,767,716.00 zimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Kununua, kutunza na kusambaza dawa na bidhaa nyinginezo katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya (Shilingi 200,000,000,000.00);

(b) Kuimarisha upatikanaji wa damu salama (Shilingi 3,503,771,816.00);

(c) Kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini (Shilingi 8,596,534,400.00);
(d) Kuimarisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA katika vituo vya kutolea huduma ili kuboresha ufanisi, kuimarisha udhibiti na kupunguza gharama katika utoaji wa huduma za afya (Shilingi 2,000,000,000.00);
(e) Kuimarisha ubora wa huduma za Uuguzi na Ukunga katika ngazi zote za kutolea huduma kwa vituo vya umma na binafsi (Shilingi 4,910,461,500.00);
(f) Kuimarisha usimamizi na uhakiki wa ubora wa huduma za afya katika vituo vya umma na binafsi kwa kuunganisha Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi (PHAB) na Bodi ya Maabara Binafsi za Afya (PHLB) ili kuwa na chombo kimoja cha usajili na usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini;
(g) Kuimarisha uongozi na usimamizi wa utoaji huduma za afya katika ngazi zote kwa kufanya mapitio ya muundo, majukumu na ujuzi wa wajumbe wa Kamati za Uendeshaji Afya Mikoa, Halmashauri na Hospitali (RHMT, CHMT na HMT) ili kuongeza uwajibikaji na ufanisi wa utoaji wa huduma za afya; na
(h) Kuwajengea uwezo wananchi kuhusu ushiriki wa jamii katika upatikanaji wa huduma bora za afya.

iii. **Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ambapo kiasi cha Shilingi 6,000,000,000.00 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Kufanya mapitio ya mkakati wa upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za Afya;
(b) Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote nchini ikiwemo mfumo wa utambuzi wa wanufaika pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa Bima ya Afya;
(c) Kuanza mchakato wa kuanzisha Chombo cha Kitaifa cha Udhibiti wa bei za huduma za afya katika ngazi zote;

(d) Kuimarisha uhai na ustahimilivu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;
(e) Kuimarisha ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika utoaji wa huduma za afya nchini; na
(f) Kutafuta na kuratibu upatikanaji wa fedha za afya kutoka kwa wadau wa maendeleo.

iv. **Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ambapo kiasi cha Shilingi 17,189,250,000.00 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Kununua na kusambaza dawa muhimu za uzazi salama (Magnesium sulphate, Oxytocin, FeFo na SP) pamoja na dawa za uzazi wa mpango, dawa kinga za minyoo, dawa za kuongeza damu, dawa za Malaria, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi;
(b) Kuimarisha upatikanaji wa dawa bila malipo kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ikiwemo dawa za kutibu nimonia na kuharisha;
(c) Kujenga, kukarabati na ununuzi wa vifaa tiba vya wodi 100 maalum za watoto wachanga (Neonatal Care Unit - NCU) wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu.
(d) Kuwajengea uwezo wataalam wa afya ili kutoa huduma bora za watoto wachanga na uzazi ili kuhakikisha wajawazito wanapata huduma zenye heshima, staha na utu;
(e) Kuelimisha na kuhamasisha jamii hususan kinamama wajawazito kuwahi kuhudhuria kliniki ndani ya miezi mitatu ya mwanzo ya ujauzito pamoja na kuwawezesha kutambua huduma stahiki zinazopaswa kutolewa kwa wajawazito. Huduma hizo ni pamoja na kupima uzito, kimo cha mimba, mapigo ya moyo wa mtoto, mlalo na kitangulizi cha mtoto, Shinikizo la damu (BP), wingi wa damu, Gurupu la damu, mkojo, Malaria, VVU, Kaswende, Homa ya Ini(Hepatitis B)pamoja na Ultrasound ambapo inapatikana;
(f) Kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya mama na mtoto Dodoma;
(g) Kuongeza vituo vipya 300 vinavyotoa huduma rafiki kwa vijana;

(h) Kuongeza vituo vipya 100 vinavyotoa huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na kununua mashine 30 za upasuaji mdogo kwenye mlango wa kizazi ambazo zitasambazwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 28 na mbili za kanda. Aidha, mashine 300 za kutibu mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi zitanunuliwa na kusambazwa katika Hospitali za Halmashauri na vituo vya afya vinavyotoa huduma za uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi;

(i) Kuongeza vituo 10 katika ngazi ya Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa ajili ya huduma jumuishi za manusura wa ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto (One Stop Centre); na

(j) Kusimamia upatikanaji wa huduma bora na salama za afya ya uzazi mama na mtoto ikiwemo kufanya uhakiki na kaguzi za mara kwa mara katika vituo vya kutolea huduma.

v. **Kuimarisha upatikanaji wa wataalam katika Sekta ya Afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kiasi cha Shilingi 74,000,000,000 kimetengwa kuteleza afua zifuatazo:-**

(a) Kuendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa wataalam wa ngazi ya ubingwa na ubingwa bobezi 1,300 (wataalam wapya 600, wataalam wanaoendelea 700) na kufadhili mafunzo ya kada za kati za kimkakati (Shilingi 9,000,000,000.00);

(b) Kutoa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya vya umma (Shilingi 10,000,000,000.00);

(c) Kusimamia ubora wa mafunzo kwenye vyuo vya afya ngazi ya kati vya umma na sekta binafsi;

(d) Kuendelea kuimarisha mfumo wa usimamizi wa vyuo vya afya ngazi ya kati hususan uratibu wa mitihani;

(e) Kugharamia mafunzo kwa vitendo ya watarajali wa kada mbalimbali za afya (Shilingi 54,000,000,000.00);

(f) Kujenga na kukarabati miundombinu ya vyuo vya mafunzo ya Afya vya umma (Shilingi 1,000,000,000.00); na

(g) Kuanzisha kozi mpya ili kukidhi mahitaji ya sasa ya Sekta ya Afya.

vi. **Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi nchini ambapo kiasi cha Shilingi 89,858,609,000.00 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Kuendelea kutoa huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali maalum, Kanda na Mikoa pamoja na kuanzisha huduma mpya kulingana na mahitaji ikiwemo kuanza hatua za awali za kuanzisha huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa kutumia Artificial Intelligence – Robbot katika Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Upandikizaji wa figo Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando; na iii. Upandikizaji wa ujauzito katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma.

(b) Kuwekeza katika vifaa tiba vitakavyowezesha utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ikiwemo ununuzi wa Mitambo ya kupima na kutibu moyo bila kufungua kifua (Cathlab) mbili (2) kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya na Chato na mtambo kwa ajili ya uchunguzi na Tiba ya Saratani (LINAC) kwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando;

(c) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu katika Hospitali 6 za Rufaa za Kanda za Chato, Mtwara, Mbeya, KCMC, Bugando, Benjamin Mkapa, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi Kigoma na Hospitali 28 za rufaa za mikoa;

(d) Kuendeleza ujenzi wa kituo cha matibabu ya Saratani tawi la Taasisi ya Saratani Ocean Road – Mbeya;

(e) Kuanzisha tawi la Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete Kanda ya Ziwa (JKCI- Chato),

(f) Kuanza hatua za awali za maandalizi ya Taasisi ya Sayansi ya Tiba ya Magonjwa ya ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu ili kuimarisha huduma za upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu nchini;

(g) Kugharamia huduma za matibabu ya ubingwa bobezi ndani ya nchi hususan kupandikiza figo, kupandikiza uloto, kupandikiza vifaa vya usikivu kwa watoto na kufanya upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu ili

kuwasaidia wananchi wasio na uwezo sambamba na kuwajengea uwezo wataalam wa ndani kutoa huduma hizo kwa umahiri zaidi;

(h) Kuanzisha Kituo cha Umahiri cha Upandikizaji Uloto na Magonjwa ya Damu cha Afrika Mashariki katika Hospitali ya Benjamin Mkapa;

(i) Kuhakikisha Hospitali na taasisi za ubingwa bobezi zinatekeleza mpango wa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa wataalam wao ili kuwaongezea ujuzi na weledi wa kutoa huduma za ubingwa bobezi;

(j) Kuimarisha utoaji wa huduma za mkoba na tembezi za ubingwa na ubingwa bobezi katika ngazi ya msingi ili kuwafikia wananchi wengi zaidi;

(k) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika Hospitali zilizoteuliwa ili ziweze kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kupitia Tiba Mtandao (Telemedicine) ndani na nje ya nchi;

(l) Kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wagonjwa kutoka nje ya nchi (Tiba Utalii);

(m) Kuendelea kufanya huduma mkoba za Kimataifa kwenye nchi jirani zinazoizunguka Tanzania (International Medical Camps); na

(n) Kuimarisha na kuongeza wigo wa ushirikiano na Taasisi/Hospitali za kimataifa zinazotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ikiwemo kupeleka wataalam katika Hospitali hizo na kufanya kambi za pamoja za matibabu.

vii. **Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala ambapo kiasi cha Shilingi 1,500,000,000.00 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Kuanza utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Tiba Asili na Tiba Mbadala;

(b) Kuendeleza huduma za Tiba Asili ikiwemo mashamba ya miti dawa katika mikoa mbalimbali likiwemo shamba la Mzenga B Kisarawe;

(c) Kununua ardhi na kufanya usanifu wa ujenzi wa Hospitali maalum ya kitaifa ya kutoa huduma jumuishi za Tiba Asili na Tiba Mbadala;

(d) Kuongeza Hospitali zinazotoa huduma jumuishi za Tiba Asili kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa saba (7) hadi kumi na nne (14);
(e) Kuendeleza tafiti za Tiba Asili na kuhamasisha uzalishaji wa dawa za Tiba Asili viwandani kupitia ubia kati ya Sekta ya umma na Sekta binafsi;
(f) Usajili wa dawa, watoa huduma, vituo vya Tiba Asili na tiba mbadala; na
(g) Kuendeleza mafunzo ya wataalam wa Tiba Asili na tiba mbadala.

viii. **Kuimarisha udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza, Magonjwa Yasiyoambukiza, Magonjwa ya Mlipuko na Huduma za Afya za Dharura ambapo kiasi cha Shilingi 84,864,241,569.00 kimetengwa kutekeleza afua zifuatazo:-**

(a) Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria kwa kununua na kusambaza vyandarua vyenye dawa kwa jamii, kununua vitendanishi na dawa ili kuwezesha ugunduzi na matibabu ya ugonjwa wa Malaria;
(b) Utekelezaji wa Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma kwa kununua vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na dawa;
(c) Utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, Homa ya Ini na magonjwa ya ngono nchini kwa kununua vitendanishi vya kupima magonjwa hayo pamoja na dawa kinga na dawa za kufubaza VVU;
(d) Kutoa elimu kwa umma kuhusu vichochezi na visababishi vya magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo tabia bwete, uzito uliokithiri, matumizi ya sukari, chumvi, na mafuta kupita kiasi pamoja na kuelimisha kuhusu athari za matumizi ya tumbaku na unywaji wa pombe kupita kiasi;
(e) Kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza katika ngazi ya afya ya msingi ili kuweza kuyatambua mapema na kuanzisha kliniki;
(f) Kuimarisha upatikanaji wa dawa za kutibu magonjwa yasiyoambukiza;

(g) Kuimarisha Mfumo wa Kitaifa wa Uratibu na Usimamizi wa Afua za Afya ya Jamii ikiwemo kuanzisha Taasisi ya Taifa ya Afya ya Jamii;

(h) Kuendelea kuimarisha timu za wataalam wa dharura (Rapid Response Teams) wa ngazi ya Taifa, Mikoa na Halmashauri ili kujiandaa na kukabiliana na dharura za afya na magonjwa ya milipuko ndani na nje ya nchi pale inakapohitajika;

(i) Kuimarisha usimamizi wa vituo vya Operesheni ya matukio ya Dharura (PHEOCs) vilivyoanzishwa katika Mikoa 16 katika uratibu wa dharura za afya na milipuko ya magonjwa;

(j) Kukamilisha miundombinu kwa ajili ya vituo vya uratibu wa magari ya wagonjwa (ambulance dispatch centers) ikiwemo Mfumo wa uendeshaji ufuatiliaji na uratibu wa magari ya wagonjwa (ambulance dispatch system);

(k) Kutoa mafunzo kwa watoa huduma za magari ya wagonjwa (paramedics) kwa kushirikiana na Vyuo vya kati na Vyuo Vikuu nchini; na

(l) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa vitendo kwa watoa huduma za EMD, watoa huduma za ambulance, Polisi na makundi maalum ya kujitolea katika jamii ikiwemo bodaboda kupitia kituo maalum cha mafunzo cha Hospitali ya Taifa Muhimbili, Benjamin Mkapa, Mbeya, Bugando na KCMC.

ix. **Kuimarisha huduma za Afya ya Akili, huduma za utengamao na Tiba Shufaa hususan kwa Watoto, Wazee na Wenye Ulemavu kiasi cha Shilingi 9,318,528,988.00 kimetengwa;**

(a) Kutoa elimu kwa umma kuhusu vihatarishi vya afya ya akili na namna ya kukabiliana navyo;

(b) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya ya akili katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Halmashauri;

(c) Kuimarisha upatikanaji wa wataalam wa afya ya akili katika ngazi zote;

(d) Kuimarisha upatikanaji wa dawa za afya ya akili;

(e) Kuanzisha huduma za afya ya akili kwa njia ya mtandao;

(f) Kuimarisha uratibu wa huduma, tafiti na mafunzo kuhusu afya ya akili kwa kukamilisha uanzishwaji wa taasisi ya taifa ya akili.
(g) Kuimarisha utambuzi wa mapema wa watoto wenye ulemavu;
(h) Kuanzisha huduma tatu za utengamao (Fiziotherapia, Tiba Kazi (occupational therapy), Matamshi na Lugha (Speech and language therapy) katika Hospitali za Rufaa za Mikoa 10;
(i) Kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za utengamao katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na kuendeleza utoaji wa huduma za utengamao kuanzisha kituo cha umahiri cha huduma za utengamao;
(j) Ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba vya kutolea huduma za utengamao pamoja na vifaa saidizi;
(k) Kuimarisha upatikanaji wa Wataalam wa utengamao na tiba shufaa kwa kuwajengea uwezo watalaam waliopo na kuibua wataalam wapya;
(l) Kuimarisha huduma za utengamao kwenye ngazi ya msingi; na
(m) Kuratibu uanzishwaji wa Klabu za Afya za Wazee katika ngazi ya Halmashauri.

x. **Kusimamia Tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti mbalimbali za afya ambapo kiasi cha Shilingi 3,508,968,000.00 kwa ajili ya kutekeleza afua zifuatazo;**
(a) Tafiti za magonjwa yasiyoyakuambukiza ikiwemo Saratani,
(b) Ufuatiliaji wa usugu wa vimelea dhidi ya dawa,
(c) Utafiti juu ya changamoto ya Afya ya Akili,
(d) Utafiti juu ya matumizi ya Energy Drink,
(e) Utafiti kuhusu Nguvu za Kiume; na
(f) Utafiti kuhusu dawa za Tiba Asili.

## F. SHUKRANI

**411. Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta nyingine zinazosaidia kuchangia katika

uboreshaji na utoaji wa huduma za Afya nchini. Hivyo basi, nitumie wasaa huu kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Ireland, Uswisi, Korea Kusini na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNFPA na UNICEF kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususan Afya ya Msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za Marekani, Uingereza, Ujerumani Ufaransa China, Cuba, India, Italia, Japan, Misri, Sweden na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi mbalimbali inayotekelelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

**412. Mheshimiwa Spika,** Nayashukuru pia mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano walioutoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNAIDS, UNDP, UNFPA, UNICEF, UN-Women, WHO na IAEA); Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU); IMF, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); GAVI; Global Fund; PEPFAR; CDC; USAID; DFID; KOICA; PMI; Susan Buffet Thompson Foundation; Abbott Fund; EED; Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF); GIZ; KfW; Bill and Melinda Gates Foundation; Good Samaritan Foundation (GSF); HelpAge International; John Snow Incorporation (JSI); JICA; Save the Children; World Vision; Path; Pathfinder; KOFIH; Walter REED; Jhpiego; Delloite na Taasisi mbalimbali za kifedha nchini.

**413. Mheshimiwa Spika,** Pia niwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na mashirika yasiyo ya kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin Mkapa Foundation, AGOTA, Aga Khan Foundation, APHFTA, AMREF, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Counsenuth, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, AFRICARE, Msalaba Mwekundu, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, MeLSAT, PASADA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, TPRI, Tanzania Surgical Assosciation (TSA), Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS,

TUNAJALI, Tanzania Midwife Association, TDA, TAYOA, TISS, TEC, UMATI, USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, Kivulini, WiLDAF, TCRF na FSDT.

**414. Mheshimiwa Spika,** Navishukuru Vyuo Vikuu vyote vinavyoshirikiana na Sekta ya Afya ikiwemo Chuo Kikuu Dar es Salaam, Chuo Kikuu Muhimbili, Chuo Kikuu Sokoine, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu Dodoma, Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hurbert Kairuki, Chuo Kikuu IMTU, Chuo Kikuu Tumaini, Chuo Kikuu St. Augustine, Chuo Kikuu CUHAS, Chuo Kikuu Sebastian Kolowa, Chuo Kikuu St. John, Chuo Kikuu Aga Khan, Chuo Kikuu Morogoro Muslim, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu Huria pamoja na Vyuo vyote vilivyo chini ya Wizara ya Afya kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya.

**415. Mheshimiwa Spika,** Kipekee nipende kutoa shukran zangu kutoka kwa viongozi na watumishi wa Wizara ya Afya kwa ushirikiano wao mkubwa. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel (Mb), Naibu Waziri wa Afya. Aidha, naomba kuwashukuru Dkt. John Jingu, Katibu Mkuu na Dkt. Grace Magembe, Naibu Katibu Mkuu na Prof. Tumain Nagu, Mganga Mkuu wa Serikali. Vilevile, nawashukuru, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vya Wizara. Nichukue fursa hii pia kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda ambao ni Prof. Mohamed Janabi (Hospitali ya Taifa Muhimbili), Prof. Abel Makubi (Taasisi ya Mifupa MOI), Dkt. Peter Kisenge (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), Dkt. Julius Mwaiselage, (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), Dkt. Leonard Subi (Hospitali ya Kibong'oto), Dkt. Paul Lawala (Hospitali ya Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda Dkt. Godlove Mbwanji (Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), Dkt. Alphonce Chandika (Hospitali ya Benjamin Mkapa), Dkt. Brian Mawalla (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), Dkt. George Msigati (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara), Dkt. Fabian Massaga (Hospitali ya Bugando), Prof. Geleard Masenga (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC) na Bi. Brenda Msangi (Hospitali ya Rufaa ya Kanda CCBRT).

**416. Mheshimiwa Spika,** Naomba pia kuwashukuru Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambao ni Bw. Mavere Tukai (MSD), Bw. Benard Konga (NHIF), Bw. Adam Fimbo (TMDA), Prof. Aboud Said (NIMR), Dkt. Fidelis Mafuniko (Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali), pamoja na Wasajili wa Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma. Vilevile nawashukuru
Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo vilivyo chini ya Wizara na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika ya Dini, Mashirika ya Kujitolea na Mashirika Binafsi. Natoa shukrani kwa Sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao.

**417. Mheshimiwa Spika,** Nichukue fursa hii pia kuishukuru Familia yangu, kwa uvumilivu wao na kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, napenda kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Tanga Mjini kwa kuendelea kuniamini, kuniunga mkono na kushirikiana nami kikamilifu katika kuijenga Tanga yetu ili kupata maendeleo zaidi katika nyanja zote za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Naahidi kuwa nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo letu.

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025

**418. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25 Wizara na Taasisi zilizo chini yake imekadiria kukusanya kiasi cha Shilingi 756,866,060,248. Kati ya fedha hizo, Shilingi 70,828,500,189.69 zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani Makao Makuu ya Wizara, Shilingi 134,171,499,810.31 zinatarajiwa kukusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa, Shilingi 551,866,060,248.00 zinatarajiwa kukusanywa kutoka katika Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara. Makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na makadirio ya Shilingi 677,621,168,390.95 kwa mwaka 2023/24.

**Matumizi ya Kawaida**

**419. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 632,267,220,000** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na Asilimia 48 ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha Shilingi 484,935,496,000 ni kwa ajili ya Mishahara ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake, na kiasi cha Shilingi 147,331,724,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

**420. Mheshimiwa Spika,** Wizara imepanga kutumia **Shilingi 679,570,246,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 52 ya bajeti tengwa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni Shilingi 416,258,609,000 na fedha za nje ni
Shilingi 263,311,637,000

**421. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni **Shilingi 1,311,837,466,000** ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea.

| Na | Fungu | Matumizi ya Kawaida | Miradi ya Maendeleo | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Fungu 52 | **632,267,220,000.00** | **679,570,246,000.00** | **1,311,837,466,000.00** |

**422. Mheshimiwa Spika,** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti za Wizara ya Afya www.moh.go.tz.

**423. Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.

## VIAMBATISHO

**KIAMBATISHO NA. 1.** MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAKUSANYO HALISI KUTOKA MAKAO MAKUU YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024.

| Na | Idara/Taasisi | Makusanyo kwa Mwaka 2023/24 | Makusanyo kufikia Machi 2024 | Asilimia | Makadirio kwa mwaka 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bodi ya Usajili Hospitali Binafsi | 985,787,225.00 | 789,612,500.00 | 80 | 985,787,225.00 |
| 2 | Bodi ya Maabara Binafsi za Afya. | 827,646,250.00 | 680,084,000.00 | 82 | 900,000,000.00 |
| 3 | Baraza la Wataalam wa Maabara | 715,000,000.00 | 621,322,150.00 | 87 | 715,000,000.00 |
| 4 | Baraza la Mazingira | 269,490,000.00 | 79,110,030.00 | 29 | 269,490,000.00 |
| 5 | Baraza la Radiolojia | 116,075,600.00 | 95,944,900.00 | 83 | 116,075,600.00 |
| 6 | Baraza la Optometri | 248,805,000.00 | 71,115,000.00 | 29 | 248,805,000.00 |
| 7 | Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala | 784,392,000.00 | 274,020,750.00 | 35 | 784,392,000.00 |
| | **Jumla - Bodi Mabaraza** | **3,947,196,075.00** | **2,611,209,330.00** | **66** | **4,019,549,825.00** |
| | **Kinga** | | | | |
| 1 | Vituo vya Afya Mipakani | 2,000,000,000.00 | 1,110,779,316.00 | 56 | 2,000,000,000.00 |
| 2 | Elimu ya Afya kwa Umma | 2,000,000,000.00 | 192,100,200.00 | 10 | 1,000,000,000.00 |
| | **Jumla – Kinga** | **4,000,000,000.00** | **1,302,879,516.00** | **33** | **3,000,000,000.00** |
| | **Tiba** | | | | |
| 1 | Maabara ya Taifa | 15,000,000,000.00 | 148,976,500.00 | 1 | 1,139,300,000.00 |
| 2 | Hospitali Afya ya Akili | 2,522,100,000.00 | 1,442,510,875.47 | 57 | 1,600,000,000.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mirembe na Taasisi ya Isanga | | | | |
| 3 | Hospitali ya Kibong'oto | 1,300,000,000.00 | 993,493,444.00 | 76 | 1,300,000,000.00 |
| 4 | Hospitali ya Kanda Mbeya | 32,000,000,000.00 | 26,343,484,446.00 | 82 | 35,218,952,000.00 |
| 5 | Hospitali ya Kanda Chato | 3,000,000,000.00 | 1,540,580,686.00 | 51 | 3,000,000,000.00 |
| 6 | Hospitali ya Kar Mtwara | 1,800,000,000.00 | 2,165,072,376.00 | 120 | 4,363,940,000.00 |
| | **Jumla Tiba** | **5,622,100,000.00** | **32,634,118,327.47** | **59** | **46,622,192,000.00** |
| | **Mafunzo na Maendeleo ya Wataalam** | | | | |
| 1 | Ada, usajili wa wanafunzi na ada za mitihani na kurejeshwa kwa fedha za umma | 24,845,479,102.00 | 16,562,852,716.68 | 67 | 17,186,758,365.00 |
| | **Jumla – mafunzo** | **24,845,479,102.00** | **16,562,852,716.68** | **67** | **17,186,758,365.00** |
| | **Jumla Makao Makuu** | **8,414,775,177.00** | **53,111,059,890.15** | **60** | **70,828,500,189.69** |

**KIAMBATISHO NA. 2.** MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAKUSANYO HALISI KUTOKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

| Na | Hospitali | Makadirio 2023/2024 | Makusanyo kufikia Machi 2024 | Asilimia | Makadirio kwa mwaka 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Dodoma | 10,752,600,000.00 | 10,209,763,329.40 | 95 | 12,139,670,000.00 |
| 2 | Bombo | 5,127,136,910.00 | 5,922,298,241.57 | 116 | 7,914,712,591.80 |
| 3 | Amana | 5,650,000,000.00 | 5,815,851,323.00 | 103 | 7,500,000,000.00 |
| 4 | Sekou Toure | 6,600,000,000.00 | 6,144,867,502.78 | 93 | 7,240,063,842.90 |
| 5 | Temeke | 5,992,625,083.00 | 7,112,191,228.35 | 119 | 7,678,389,784.03 |
| 6 | Mt. Meru | 7,976,000,000.00 | 8,028,706,395.76 | 101 | 9,172,000,000.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 7 | Iringa | 5,827,370,988.00 | 5,228,448,346.88 | 90 | 6,581,546,528.00 |
| 8 | Bukoba | 3,759,000,000.00 | 3,055,536,917.00 | 81 | 5,677,800,862.80 |
| 9 | Mwananyamala | 6,018,967,859.00 | 4,781,377,428.46 | 79 | 7,071,588,792.00 |
| 10 | Mawenzi | 4,437,195,418.00 | 3,886,682,438.15 | 88 | 4,570,311,280.54 |
| 11 | Morogoro | 4,032,708,429.00 | 4,281,333,290.40 | 106 | 4,500,000,000.00 |
| 12 | Singida | 3,834,000,000.00 | 2,971,966,013.00 | 78 | 3,834,000,000.00 |
| 13 | Mbeya | 2,842,863,212.00 | 2,763,983,598.00 | 97 | 3,704,408,952.00 |
| 14 | Musoma | 3,037,536,782.00 | 3,459,838,819.94 | 114 | 4,000,000,000.00 |
| 15 | Tumbi | 3,639,624,904.00 | 3,230,745,978.03 | 89 | 3,672,000,000.00 |
| 16 | Sumbawanga | 1,600,000,000.00 | 2,337,912,080.00 | 146 | 2,924,352,270.00 |
| 17 | Songea | 3,491,396,532.00 | 2,294,005,577.24 | 66 | 3,665,966,358.60 |
| 18 | Maweni | 4,918,846,825.00 | 3,805,457,055.30 | 77 | 5,295,704,240.00 |
| 19 | Sokoine | 1,768,584,256.00 | 1,115,470,882.35 | 63 | 1,506,813,910.64 |
| 20 | Ligula | 1,905,909,184.00 | 2,344,587,518.47 | 123 | 2,647,883,986.00 |
| 21 | Kitete | 3,727,646,368.00 | 3,057,587,784.00 | 82 | 3,600,000,000.00 |
| 22 | Songwe | 1,985,000,000.00 | 1,216,419,496.98 | 61 | 2,500,000,000.00 |
| 23 | Geita | 2,200,000,000.00 | 1,881,438,936.00 | 86 | 3,600,000,000.00 |
| 24 | Shinyanga | 3,116,134,998.00 | 2,223,116,702.30 | 71 | 3,271,941,747.00 |
| 25 | Manyara | 1,994,077,075.00 | 2,769,201,509.48 | 139 | 3,507,344,664.00 |
| 26 | Katavi | 2,700,000,000.00 | 1,808,460,633.50 | 67 | 3,330,000,000.00 |
| 27 | Njombe | 1,300,000,000.00 | 1,736,213,017.87 | 134 | 1,365,000,000.00 |
| 28 | Simiyu | 1,350,000,000.00 | 1,963,462,770.14 | 145 | 1,700,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **111,585,224,823.00** | **105,446,924,814.35** | **94** | **134,171,499,810.31** |

**KIAMBATISHO NA. 3. MAKADIRIO YA MAKUSANYO NA MAKUSANYO HALISI KUTOKA KATIKA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024**

| Na | Idara/Taasisi | Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka 2023/24 | Makusanyo kufikia Machi 2024 | Asilimia | Makadirio kwa mwaka 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) | 35,043,618,882.00 | 35,105,642,120.00 | 100 | 51,076,251,188.00 |
| 2 | Hospitali ya Taifa Muhimbili | 85,200,000,000.00 | 72,314,411,445.00 | 85 | 98,703,000,000.00 |
| 3 | Hospitali ya Mloganzila | 24,897,181,507.00 | 23,271,041,846.05 | 93 | 34,212,842,400.00 |
| 4 | Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) | 40,800,000,000.00 | 30,278,793,764.00 | 74 | 45,803,150,862.00 |
| 5 | Taasisi ya Saratani Ocean Road | 17,300,000,000.00 | 14,864,446,308.04 | 86 | 19,000,000,000.00 |
| 6 | Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH) | 40,530,050,000.00 | 27,438,561,133.00 | 68 | 46,609,557,500.00 |
| 7 | Baraza la Uuguzi na Ukunga | 4,701,445,000.00 | 2,071,495,451.00 | 44 | 4,910,461,500.00 |
| 8 | Baraza la Famasi | 5,151,300,005.00 | 3,581,527,557.00 | 70 | 5,500,411,930.00 |
| 9 | Hospitali ya Bugando | 69,682,150,196.00 | 43,965,413,357.40 | 63 | 74,862,462,133.00 |
| 10 | Kilimanjaro Christian Medical Center (KCMC) | 37,064,930,806.00 | 30,430,097,878.00 | 82 | 37,064,930,806.00 |
| 11 | Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) | 39,347,777,926.00 | 33,772,337,478.83 | 86 | 41,330,000,000.00 |
| 12 | Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | 44,567,029,460.00 | 29,808,435,040.90 | 67 | 52,070,301,632.00 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 13 | Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu-NIMR | 8,528,618,833.00 | 4,485,781,272.45 | 53 | 10,425,049,774.58 |
| 14 | Baraza la Madaktari | 3,861,158,697.95 | 4,233,776,000.00 | 110 | 4,581,876,188.00 |
| 15 | Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC) | 570,000,000.00 | 332,881,853.00 | 58 | 598,500,000.00 |
| 16 | Comprehensive Community Based Rehabilitation in Tanzania (CCBRT) | 20,375,907,078.00 | 14,216,283,977.00 | 70 | 25,117,264,334.00 |
| | **Jumla Taasisi** | **477,621,168,390.95** | **370,170,926,481.67** | **78** | **51,866,060,248.00** |

## KIAMBATISHO NA. 4 DAWA ZA TIBA ASILI ZILIZOSAJILIWA

| S/N | JINA LA KIBIASHARA | NA. YA USAJILI | FOMU YA DAWA | MUONEKANO KATIKA SOKO | ALIESAJILI | MTENGENEZAJI | TAREHE YA KUSAJILIWA | MAGONJWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | UJANA | TZ17TM 0001 | Urojo | kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Namdeo Shastri | SHASTRI HERBAL LTD P.O BOX 7021 ARUSHA | 2017 | Uchovu wa mwili na Kuimarisha kinga asili ya mwili, kuimarisha uwezo wa kufanya mapenzi kwa wanaume(Ng uvu za kiume) |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2 | COLLOIDAL SILVER | TZ17TM0 002 | Clear solution | Ombre bottle with 250ml | Bi. Elizabeth Lema | CORNWELLL QUALITY TOOLS & CHEMICALS INTERNATIONAL LTD P.O BOX 78158 DAR ES SALAAM | 2017 | kinga ya mwili, vidonda vya tumbo, mafua na UTI |
| 3 | IH-MYOON | TZ 17TM 0003 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 100 | Bi. Elizabeth Lema | CORNWELLL QUALITY TOOLS & CHEMICALS INTERNATIONAL LTD P.O BOX 78158 DAR ES SALAAM. | 2017 | kisukari |
| 4 | SUDHI | TZ 17TM 0004 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Namdeo Shastri | SHASTRI HERBAL LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 2017 | Kukosa choo/kuvimbiwa. Kupunguza uzito, mzio(muwasho) wa ngozi |
| 5 | APAMOL | TZ 17TM 0005 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Namdeo Shastri | SHASTRI HERBAL LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 2017 | Uvimbe kwenye mfumo wa uzazi kwa akinamama. Kuziba mirija ya akina mama, maumivu wakati wa hedhi. |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | VATARY HERBAL | TZ 17TM 0006 | kimiminika | Kopo jeupe mdomo mpana lenye mil 250 | Bw. Namdeo Shastri | SHASTRI HERBAL LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 2017 | Baridi yabisi (gout). Chamgamoto ya moto, kikohozi kikavu |
| 7 | 4A9 | TZ 17TM 0007 | unga | Kopo la kahawia mdomo mpana lenye gramu 100 | Bw. Twaribu Msigwa | HEALING AFRICA GOOD TRUST, P.O BOX 11324, DAR ES SALAAM | 01 Oktober 2018 | Kuimalisha kinga ya mwili, Ugonjwa wa kisukari |
| 8 | LIFE | TZ17TM 0008 | unga | Nyloni nyeupe yenye unga gramu 20 ndani ya box dogo la njano | Bw. Joseph Buberwa | JKBS INTRNATIONAL. CO .LTD P.O. BOX 32284 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Shinikizo la juu la damu, kisukari, ganzi |
| 9 | MUSHANA | TZ17TM 0009 | unga | Nyloni nyeupe yenye unga gramu 20 ndani ya box dogo la bluu | Bw. Joseph Buberwa | JKBS INTRNATIONAL. CO .LTD P.O. BOX 32284 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Malaria |
| 10 | JOY | TZ17TM 0010 | Unga | Nyloni nyeupe yenye unga gramu 20 ndani ya box dogo la kijani | Bw. Joseph Buberwa | JKBS INTRNATIONAL. CO .LTD. P.O BOX 32284 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Tatizo la kuvurugika kwa mzunguko wa siku za hedhi. Tatizo la kutoshika mimba wanawake, tatizo la mirija ya |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | uzazi ya mwamke |
| 11 | DETOXCER | TZ 17TM 0011 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 100 | Bw. Luhamba Lusumo | STAR OF JERUSALEM & HEALTH FOODS CLINICS. P.O BOX 1572 MWANZA. | 01 Oktoba 2018 | Vidonda vya tumbo. Maumivu ya tumbo. Kuondoa gesi tumboni. |
| 12 | BILLYD FOMULA POWER | TZ 17TM 0012 | unga | Nyloni nyeupe yenye unga gramu 20 ndani ya box dogo la kahawia | Bw. Danny Kyauka | D. BILLY POWER CO. LTD P.O.BOX 14760 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Matatizo ya figo |
| 13 | JC | TZ17TM 0013 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 80 | Bw. John Lupimo | LUPIMO SANITARIUM CLINIC P.O. BOX 33799 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Tatizo la kupata haja ndogo kwa shida kwa wanaume (Tezi dume). Matatizo ya upungufu wa mbegu za kiume. Magonjwa ya zinaa |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 14 | FIWEMU | TZ17TM 0014 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 80 | Bw. John Lupimo | LUPIMO SANITARIUM CLINIC. P.O. BOX 33799 DAR ES SALAAM | 01 Oktoba 2018 | Matatizo ya kutopata ujauzito kwa wanawake. Kupunguza maumivu wakati wa hedhi, magonjwa ya zinaa |
| 15 | RN | TZ 17TM 0015 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 100 | Bw. Vanence Jackson | EDEN HERBAL SHOP. P.O.BOX 420 KAHAMA TANZANIA | 01 Novemba 2019 | Vidonda vya tumbo. Maumivu ya tumbo. Kuondoa gesi tumboni. |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 16 | LOW OXYGE | TZ 17TM 0016 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Rashid Sungura | KHAIRA HERBAL CLINIC P.O.BOX 2259 MWANZA | 01 Novemba 2019 | Inazibua mkojo kwa wanaume (tezi dume). Pumu, inaondoa lehemu iliyozidi |
| 17 | SINDU | TZ 17TM 0017 | urojo | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 400 | Bw. Anandi Shastry | SHASTRI HERBS LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 01 Novemba 2019 | Maumivu kwenye viungo vya miguu (gout). Kuvimba kwa tezi za koromeo. Tatizo la figo. |
| 18 | MEDICA | TZ 17TM 0018 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 100 | Bw. Anandi Shastry | SHASTRI HERBS LTD. P.O.BOX 7021 ARUSHA | 01 Novemba 2019 | Maambukizi kwenye njia |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | ya mkojo, ugonjwa wa baridi yabisi(arhtritis). Kisukari |
| 19 | JIKO LA SHAMBA | TZ 17TM 0019 | Kimiminika | chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye milillita 500 | Bw. Mustafa makame Ali | P.O.BOX 1861 ZANZIBAR MUSTAFA MAKAME ALI | 01 Novemba 2019 | Maradhi ya ngozi na mfumo wa mkojo, maradhi ya mishipa |
| 20 | SIGWA ONE. | TZ 17TM 0020 | Unga | Kopo dogo jeupe mdomo mpana lenye gramu 10 | Bw. Simoni Rusigwa | SIGWA HERBAL CLINICP.O BOX 68123 DAR ES SALAAM | 01 Novemba 2019 | Maumivu chini ya kitovu, mgongo na kiuno, Tatizo la ugumba a hedhi isiyo |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | bora |
| 21 | AVIROX 1-9 | TZ 17TM 0021 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Othman K. Shem | PASEKO, O & P. CO. LTD. P. O. BOX 6799 TABATA DAR ES SALAAM | 15 julai 2020 | Vimbe katika mwili (Anti-arthritis/rheumatoid), maumivu ya viungo, |
| | | | | | | | | maambukizi kwenye mfumo wa mkojo. |
| 22 | AVIBA 1-21 | TZ 17TM 0022 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 250 | Bw. Othman K. Shem | PASEKO, O & P. CO. LTD . P.O.BOX 6799 TABATA DARA ES SALAAM | 15 julai 2020 | Maambukizi kwenye mfumo wa mkojo, magonjwa ya zinaa na fangasi, magonjwa ya zinaa |
| 23 | MTINJETINJE | TZ 17TM 0023 | unga | Kopo dogo jeupe mdomo mpana lenye gramu 20 | Bw. Agostino Ditti | NTUZU HERBS, MBAGALA - DAR ES SALAAM | 1-Nov-19 | Kisukari |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 24 | MAJINJ ASI | TZ 17TM 0024 | Unga | Kopo dogo jeupe mdomo mpana lenye gramu 20 | Bw. Agostino Ditti | NTUZU HERBS MBAGALA DAR ES SALAAM | 01 Novemb a 2019 | Matatizo ya nguvu za kiume |
| 25 | UZIMA HERBAL DROP | TZ 17TM 0025 | Mafuta Tete | Chupa ndogo nyeupe mdomo finyu yenye Mililita 10 | Bw. Leonard Nsalazu | UZIMA FOOD PRODUCTS THE UDSM P.O.BOX 350060 DAR ES SALAAM. | 15 Julai 2020 | Shinikizo la damu, mfumo wa upumuaji, maambukizi kwenye kinywa. |
| 26 | COVID OL | TZ 17TM 0026 | kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwemba m ba yenye Mililita 500 | Prof. Hamisi Masanja Malebo | TANZANIA INDUSTRIAL RESEARCH AND DEVELOPME NT ORGANIZATI ON (TIRDO),P.O. BO X 23235 DAR ES SALAAM | 15 Julai 2020 | Mafua makali, mafua makali Pumu |
| 27 | HENSHA | TZ 17TM 0027 | unga | Kopo dogo jeupe mdomo mpana lenye gramu 200 | Bw. Emanuel D. Maduhu | NYASOSI TRADITIONAL CLINIC MAGOMENI – DAR ES SALAAM | 15 julai 2020 | Kisukari na nguvu za kiume |
| 28 | DURAKI | TZ 17 TM 0028 | Urojo | kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 500 | Bw. Khalfani Kayoka | DETUTI FOOD ORODUCTS P.O.BOX 687350 DAR EA SALAAM | 15 Julai 2020 | Kuongeza kinga ya mwili, upungufu wa damu, urutubishaji mayai kwa wanawake |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 29 | AL SAHARI | TZ 17 TM0029 | kimiminika | chupa nyeupe mdomo mwembamba ba yenye millilita 500 | Bi. Saumu Karama | SAUMU KARAMA HERBALMEDICIN E P.O.BOX 7210 DAR ES SALAAM | 15 julai 2020 | uvimbe kwenye kizazi, uvimbe kwenye mirija ya uzai, saratani za kizazi |
| 30 | MFYASA | TZ 17TM 0030 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 95 | Bw. Maximillian Iyana | IFAKARA HERBAL CLINIC TANDALE-DAR ES SALAAM | 15 Julai 2020 | Matatizo ya mfumo uzazi kwa wanawake |
| 31 | M4 | TZ 17TM 31 | unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 95 | Bw. Maximillian Iyana | IFAKARA HERBAL CLINIC TANDALE-DAR ES SALAAM | 15 Julai 2020 | Kupunguza uzito, Maumivu ya mwili |
| 32 | COIS ONE | TZ 17 TM 0032 | kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba ba yenye Mililita 200 | Bw. John Lupimo | LUPIMO SANITARIUM CLINIC .P,O.BOX 33799 DAR ES SALAAM. | 15 julai 2020 | Mafua makali yanayosababi shwa na virusi, pumu, saratani |
| 33 | FITERAWA | TZ 17TM 0033 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba ba yenye Mililita 1000 | Bi. Rahabu E. Rubago | RAHABU ULCERS HERBAL CLINIC.P.O.BOX. 1572 DAR ES SALAAM. | 15 julai 2020 | Vidonda vya tumbo |
| 34 | BUPIJI | TZ 17TM 0034 | Matone ya mafuta tete | Chupa ndogo nyeupe mdomo mwembamba ba yenye Mililita 15 | Bw. George M. Buchafwe | STAR NATURAL PRODUCTS LTD P.O. BOX 45667 DAR ES SALAAM | 1st Febuari 2021 | mafua makali, homa kubanwa na mafua, pumu |
| 35 | MWALAKA | TZ 17TM 0035 | Unga | | Mkurugenzi Mtendaji | ALTERNATIVE INTERNATIONAL MEDICINES LTD. | 1st Febuari 2021 | mafua makali/flue, kifua kubana |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | P.O.BOX 20283 DAR ES SALAAM. | | |
| 36 | ALLIUM | TZ 17TM 0036 | capsules | kopo jeupe mdomo mpana lenye kapsuli 60 | Bi. Elizzabeth Lema | CORNWELL QUALITY TOOL & CHEMICALS INTERNATIONAL LTD. P.O. BOX 78158 DAR ES SALAAM, | 31st january 2021 | lower chplestrol, Periphral arterial disease handering of arteries(arthe rosclensis) |
| 37 | CURCUMIN | TZ 17TM 0037 | capsules | Kopo jeupe mdomo mpana lenye kapsuli 60 | Bi. Elizzabeth Lema | CORNWELLL QUALITY TOOLS & CHEMICALS INTERNATIONAL LTD. P.O.BOX. 78158 DAR ES SALAAM | 31st january 2021 | Arthritis. Boost immune sysytem, Fight agaist tumour |
| 38 | PRUCAN | TZ 17TM 0038 | capsule | Kopo jeupe mdomo mpana lenye kapsuli 100 | Mkurugenzi Mtendaji | INSTITUTE OF TRADITIONAL MEDICINE, P.O.BOX 65001 DAR ES SALAAM | 31st january 2021 | Uvimbe wa tezi dume daraja i&ii |
| 39 | FIVISIA | TZ 17TM 0039 | unga | Kimfuko cha plastic chenye gramu 30 | Mkurugenzi Mtendaji | INSTITUTE OF TRADITIONAL MEDICINE, P.O.BOX 65001 DAR ES SALAAM | 31st Januari 2021 | malaria |
| 40 | T & G DECOCTION | TZ 17TM 0040 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye Mililita 250 | Bonifasi L. Msambure | BONIFASI LAURENT MSAMBURE, P.O. BOX 45728 DAR ES SALAAM | 31st Januari 2021 | Maumivu ya meno, maumivunyafizi |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 41 | IMMUNEGENTZ | TZ 17TM 0041 | syrup | Chupa ya kahawia mdomo mwembamba yenye Mililita 100 | Dr. Michael Magoti | IMMUNEGEN TZ GLOBAL LIMITED , P.O.BOX 25333 DAR ES SALAAM | 1st Februari 2021 | kuimarisha kinga ya mwili, |
| 42 | NOVIRUSA | TZ 17TM 0042 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 50 | Walter E. Macha | MACHA HERBALIST CLINIC.P. O BOX 20950 DAR ES SALAAM | 31st Januari 2021 | Hormonal inbalance, prostate Hyperplasia, Potency restoration |
| 43 | IMMUNO BOOSTER | TZ 17TM 0043 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 500 | Riziki S. Nkya | NATURAL THERAPY RESEARCH LTD.P.O. BOX 32284 DAR ES SALAAM | 1st Februari 2021 | kinga ya mwili, mafua, kupumua kwa shida |
| 44 | VITAL DEFENCE | TZ 17 TM 0044 | kimiminika | Chupa yenye mdomo mwembaba lenye mililita 500 | Riziki .s. Nkya | NATIONAL THERAPY RESEARCH LTD P.O. BOX 32284 DAR ES SALAAM | 1st Febuari 2021 | kinga ya mwili, mafua , kupumua kwa shida |
| 45 | AL -JAWFA | TZ 17TM 0045 | unga | kopo nyeupe mdomo mpana lenye gram 450 | mkuegenzi mtendaji | AMARISON CONSULTANTAN CY LTD, P.O.BOX 65007 DAR ES SALAAM | 31st january 2021 | Kisukari |
| 46 | NIMRCAF | TZ 17TM 0048 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 500 | NIMR | NATIONAL INSTITUTE FOR MEDICAL RESEARCH 3BARAKA OBAMA DRIVE - DSM | 1st Februari 2021 | Mafua makali, kifua kubana |
| 47 | PLANET | TZ 17TM 0049 | Kimiminika | Chupa ndogo transpare | Dr. Yusufu Ramadh | Dr. YUSUFU RAMADHANI NZUGUNI- | 1st Februari 2021 | Mafua makali, kifua kubana |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | nt yenye 10ml | ani | DODOMA | | |
| 48 | MTI HAKI MTEMI | TZ 17TM 0050 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 50 | Bw. Ishila Msoma Itenya | TABORA IGUNGA - NKINGA | 1 Machi 2021 | Magonjwa ya zinaa, saratani(hatua 1),homa ya mafua |
| 49 | COVOTANXA | 17 TM 0051 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 500 | Dr. Bundala | DR. BUNDALA DAR ES SALAAM | 1st Februari 2021 | Mafua makali kifua kubana |
| 50 | BAYCARO | 17 TM 0052 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye mil. 50 na 300 | Bw. Raphael Mbakizaki | BEYCARO.CO.LTD, P.O BOX 21499 DAR ES SALAAM | 01 Machi 2021 | Mfumo wa upumuaji, Kuyeyusha damu, Kikohozi kikavu |
| 51 | COVPLUS | TZ17TM 0053 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 250 | Bw. Shabani Omari Sheklindi | SHEKILINDI COMPANY LTD. P.O BOX 138 LUSHOTO - TANGA | 1 Machi 2021 | Magonjwa ya mfumo wa upumuaji, Maambukizi ya njia ya mkojo, Kuongeza hamu ya kula na kinga mwilini |
| 52 | SHENGENA | TZ17TM 0054 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembam ba yenye Mililita 250 | Bw. Stanley John Mbwambo | SHENGENA MOUNT – FOREST HERBAL CLINIC, P.O BOX 31 KILIMANJAR | 01 Machi 2021, | Maambukizi kwenye mfumo wa upumuajiuvim be kwenye, Uvimbe kwenye mishipa ya damu, Uvimbe kwenye mishipa ya damu |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 53 | KWANDU | TZ17TM 0055 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 200 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTD, P.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Kwa ajili ya uzazi wa mpango kwa wanawake, Maradhi ya ngozi na mfumo wa mkojo |
| 54 | IGULA | TZ17TM 0056 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 200 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTD, P.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Uvimbe wa tezi dume |
| 55 | ISHUMI | TZ17TM 0057 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 200 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTD, P.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Enhance fertility Kuzibua mirija ya uzazi, Maambukizi kwenye njia za uzazi |
| 56 | KALEGA | TZ17TM 0058 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye Mililita 100 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTDP.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Husaidia kuacha pombe, Madawa ya kulevya |
| 57 | MTIMA | TZ17TM 0059 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye Mililita 500 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTDP.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Matatizo ya neva, Shinikizo la damu, Homa |
| 58 | YOGYA | TZ17TM 0060 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye Mililita 500 | Bw. Ansibert Gozbert Mashasi | ANSIMAX INTERNATIONAL . CO.LTDP.O BOX 2247 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Kuondoa mawe kwenye figo |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 59 | GOSHEN | TZ17TM 0061 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamba yenye Mililita 500 | Bw. Michael Medard | CORMIL INTERNATIONAL, DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Maambukizi kwenye njia ya hewa, Kuimarisha kinga ya mwili, Shinikizo la damu |
| 60 | FUKIZA UDANOL | TZ17TM 0062 | Mafuta tete | Chupa ndogo nyeupe mdomo finyu yenye Mililita 10, 15 na 20 | Dr. C. A Mgina | UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM, P.O BOX 45728 DAR ES SALAAM | 1 FEBRUARI 2021 | Matatizo ya upumuaji, mafua, Kikohozi |
| 61 | NIMREGENIN | TZ17TM 0063 | Kimiminika | Chupa ndogo ya kahawia iliyokolea mdomo mwembamba yenye mililita 100 | Mkurugenzi - NIMR | NATIONAL INSTITUTE FOR MEDICAL RESEARCH 3BARAKA OBAMA DRIVE - DSM | 17 MAI 2021 | Saratani (hatua 1&2) |
| 62 | PERSIVIN | TZ17TM 0064 | Kimiminika | Chupa ndogo ya kahawia iliyokolea mdomo mwembamba yenye mililita 100 | Mkurugenzi - NIMR | NATIONAL INSTITUTE FOR MEDICAL RESEARCH 3BARAKA OBAMA DRIVE - DSM | 17 MAI 2021 | Kuvimba kwa tezi dume |
| 63 | RONA MIXTURE | TZ17TM 0065 | Kimiminika | Chupa ndogo ya kahawia iliyokolea mdomo mwembamba yenye mililita 100 | Mkurugenzi - ITM | INSTITUTE OF TRADITIONAL MEDICINE P.O.BOX 65001 DAR ES SALAAM 5 | 17 MAI 2021 | Matatizo ya upumuaji, mafua, Kikohozi |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 64 | INKORORA HERB | TZ17TM 0066 | Unga | Kopo jeupe lenye 50gm | Ferb Cosmass | INKOROLA HERB , DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Matatizo ya mfumo wa upumuaji, kuongeza nguvu za kiume , fungus |
| 65 | MNYANYAPORI | TZ17TM 0067 | Unga | Kopo jeupe mdomo mpana lenye gramu 100 | Bw. Peter Adam Mayunga | P.O BOX 166 MOROGORO | 17 MAI 2021 | Typoid, Maambukizi kwenye mfumo wa mkojo |
| 66 | AFRICOV | TZ 17TM 0068 | Kimiminika | Chupa ya kahawia mdomo mwembamb a yenye mililita 500 | Bw. Ramkhan A. Mohamed | RAMADHAN MOHAMED P.O BOX 4909 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Matatizo ya upumuaji, mafuaKikohozi |
| 67 | TANZAX | TZ 17TM 0069 | Kimiminika | Chupa nyeupe mdomo mwembamb ba yenye Mililita 250 na 500 | Joseph Buberwa Kankola | JKBRS INTERNATIONAL CO. LTD, P.O BOX 32284 DAR ES SALAAM | 17 MAI 2021 | Matatizo ya upumuaji , mafua, Kikohozi, Mwanamke kutokupata ujauzito |
| 69 | COVIBADAWA | TZ 17TM 0071 | Kimiminika | Kopo jeupe mdomo wembamba lenye120 ml | Dr Never Daudi Zekaya | GRACEOUS HERBAL HEALTH CARE , C/O PLANT BIODEFENDERS, P.O BOX 6464 MOSHI | Januari 2022 | Kukohoa, Pumu, Magonjwa ya tumbo |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 70 | NDAMBILE RELIEF DROPS | TZ 17TM 0072 | kimiminika | Chupa ndogo nyeupe yenye mdomo mwembamba 20 mls | Juma Ndambile Ntinginya | JUMA NDAMBILE NTINGINYA P.O.BOX 582222, DAR ES SALAAM | Januari 2022 | Vidonda vya kooni, Mafua, Meno |
| 71 | COVIFORMULA | TZ 17TM 0073 | Unga | Kopo dogo jeupe lenye mdomo mpana | Elizabeth Hazael Lema | CORNWELL QUALITY TOOL & CHEMICALS INTERNATIONAL LTD. P.O. BOX 78158 DAR ES SALAAM, www.cornwelltanzania.com | Januari 2022 | Kuongeza kinga ya mwili, Magonjwa ya mfumo wa upumuaji |
| 72 | PUMAX | TZ 17TM 0074 | | Chupa ndefu yenye mdomo mwembamba ya ujazo wa 200ml | Margreth P. Mhame | VANAPCO, P.O. BOX 6038, DAR ES SALAAM | Januari 2022 | Vidonda vya tumbo, Vidonda vya kinywani, Uvimbe kwenye kizazi |
| 73 | PEPTIN | TZ 17TM 0075 | | Chupa ndefu yenye mdomo mwembamba ya ujazo wa 200ml | Margreth P. Mhame | VANAPCO, P.O. BOX 6038, DAR ES SALAAM | Januari 2022 | Vidonda vya tumbo, Vidonda vya kinywani, Uvimbe kwenye kizazi |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 74 | BUHERI | TZ 17TM 0076 | Unga | Kopo kubwa jeupe lenye mdomo mpana na kipakiti cha plastiki ndani. | John Raphael Nyika | NM – AIST COLLABORATIO N WITH TANHELSO P.O. BOX 447 ARUSHA | Januari 2022 | Homa kali ya mfumo wa upumuaji, Magonjwa ya moyo, kisukari |
| 75 | NUSA 3PLUS | TZ 17TM 0077 | Mafuta | Chupa ndogo yenye mdomo mwembamba | John Raphael Nyika | NM – AIST COLLABORATIO N WITH TANHELSO P.O. BOX 447 ARUSHA | Januari 2022 | Homa kali na mfumo wa upumuaji, pumu, kuondoa nyama za pua ( Nasal polyps) |
| 76 | CAHO GITU | TZ 17TM 0078 | Kimiminika | Chupa ndefu nyembamba yenye mdomo mwembmba | Mary Joshua Mushi | SUPER VITAMIN PLANTS COMPANY P.O.BOX SINZA DAR ES SALAAM | Januari 2022 | Matatizo ya mfumo wa upumuaji, mafua, kuongeza kinga mwili |
| 77 | MADUNDA OILI | TZ17TM 0 047 | Mafuta mepesi | Chupa nyeupe ya 100ml | EMILY MADUNDA | MADUNDA HERBAL CLINIC MOROGORO - TANZANIA | 1ST JULY 2022 | |
| 78 | DANTAHIZA | TZ17TM0079 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya 100ml | ITM - MUHAS | TAASISI YA MADAWA ASILI - MUHAS, S.L.P 65001, DAR ES SALAAM | | Anti asthmatic, anti allergy |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 79 | GASTRIA | TZ17TM0080 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya 100ml | ITM - MUHAS | TASISI YA MADAWA ASILI - MUHAS, S.L.P 65001, DAR ES SALAAM | | stomache ulcers , stomachache |
| 80 | LIVALIN | TZ17TM0081 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya 100ml | ITM - MUHAS | TASISI YA MADAWA ASILI - MUHAS, S.L.P 65001, DAR ES SALAAM | | hepatitis C |
| 81 | CARE SPIRADUL | TZ17TM0046 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya 250 & 500ml | NEVER ZEKAYA MWAMBEELA | GRACIOUS HERBAL HEALTH CARE P.O BOX 6464, MOSHI. | 1ST JULY 2022 | |
| 82 | GENESIS | TZ17TM0082 | CAPSULS | Chupa nyeupe ya 78 caps | DENNIS LUCAS SHIJA | D. S HEALTH LIMITED P.O.BOX 11385 DAR ES SALAAM | 08TH NOVEMBER 2022 | Kuimarisha kinga ya mwili |
| 83 | GILGAL | TZ17TM0083 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya 500ml | CHRISTOPHER MLAGA MKAMA | NYOTA YA MASHARIKI KLINIKI P.O.BOX 14625 ARUSHA - TANZANIA | 1ST DECEMBER 2022 | |
| 84 | KIFUA SYRUP | TZ17TM0084 | SYRUP | Chupa nyeupe ya 100ml | FRANSCIS MUSHI | MAPONEO GROUP ARUSHA P.O.BOX 1044 | 1ST JANUARY 2023 | |
| 85 | NUNGUBASHIDE | TZ17TM0085 | Unga | Kopo jeupe la 250gm | NKOLA THOMAS GWISU | NGIKA HERBS CLINIC P.O.BOX 13700 DAR ES SALAAM | 1ST JANUARY 2023 | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 86 | KAZOLINE | TZ17TM0 086 | Unga | kibox cha kijani cha 45gm | MWESIGA KAZOBA JOHN | KAZOBA INTERNATIONAL . CO. LTD P.O.BOX 13700 DAR ES SALAAM | 1ST JANUARY 2023 | |
| 87 | LAVENDA | TZ17TM0 087 | Unga | Kopo jeupe la 200gm | SABINA KILONGO | KILONGO SANITARIUM CLINIC P.O.BOX 3846 KYELA - MBEYA | 1ST JANUARY 2023 | Maumivu ya viungo vya mwili, Vidonda vya tumbo, kuimarisha kinga ya mwili |
| 88 | BEE GINGER EXTRACT | TZ17TM0 088 | SYRUP | Chupa nyeupe ya 100ml | RAJABU IDDI AMIRI | EMARA SERVICES P.O.BOX 21263 DAR ES SALAAM. | 1ST JANUARY 2023 | |
| 89 | EKIZIMBE | TZ17TM0 089 | Unga | Kopo jeupe la 250gm | SALIM MIPAWA PETER KISANDU | P.O.BOX 21263 DAR ES SALAAM. | 1ST JANUARY 2023 | maumivu ya tumbo, matatizo ya hedhi, uvimbe kwenye kizazi |
| 90 | MUBEEZI HERBAL SOL. | TZ17TM0 090 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya750ml | NAMYALO LEVINATA ANNA | NALONGO MUSANA LTD MISSENYI-KAGERA. | 1ST JANUARY 2023 | Relief from Menstrual cramps, Pelvic pain |
| 91 | RP HERBAL LIQUID | TZ17TM0 091 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya750ml | NAMYALO LEVINATA ANNA | NALONGO MUSANA LTD MISSENYI-KAGERA. | 1ST JANUARY 2023 | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 92 | AK HERBAL SOL. | TZ17TM0092 | Kimiminika | Chupa nyeupe ya750ml | NAMYALO LEVINATA ANNA | NALONGO MUSANA LTD MISSENYI-KAGERA. | 1ST JANUARY 2023 | Peptic ulcers |
| 93 | NTUNDWA | TZ17TM0093 | Unga | Kopo jeeupe la 100gm | EMMANUEL D. MADUHU | NYANSOSI TRADITIONAL CLINIC MAGOMENI DSM | 1ST JANUARY 2023 | Tezi dume , Bawasiri, Matatizo ya uzazi kwa wanawake |
| 94 | NSHISHI | TZ17TM0094 | Unga | Kopo jeeupe la 100gm | EMMANUEL D. MADUHU | NYANSOSI TRADITIONAL CLINIC MAGOMENI DSM | 1ST JANUARY 2023 | Miguu kuwaka moto na kufaganzi, Ngiri, maambukizi kwenye njia ya mkojo |
| 95 | MYUNGAYUNGA | TZ17TM0095 | Unga | Kopo jeeupe la 200gm | | MWENDA POLE HERBAL CLINIC | 1ST JANUARY 2023 | Matatizo ya uzazi kwa wanaume, kifafa, maambukizi kwenye njia ya mkojo |
| 96 | NCHISANO | TZ17TM0096 | Unga | Kopo jeeupe la 200gm | | SHEIKH SHARIF MWINJUMA CLINIC | 1ST JANUARY 2023 | Matatizo ya uzazi kwa wanawake, maralia, ngiri kwa wanaume |
| 97 | MONJO | TZ17TM0097 | Unga | Kopo jeeupe la 100gm | | PEACE HERBALIST CLINIC, S.L.P 547 NJOMBE | 1ST JANUARY 2023 | Matatizo ya moyo, matatizo ya mifupa, matatizo ya mfumo |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | wa chakula |
| 98 | SWAVI | TZ17TM00098 | Unga | kopo jeupe la 250gm | NAMDEO SHASTRY | SHASTRY HERBAL LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 1ST NOVEMBER 2023 | Vdonda vya tumbo, Kiungulia, Bawasili. |
| 99 | RASADI | TZ17TM000099 | Kimiminika | Chupa nyeupe yenye 500mls | NAMDEO SHASTRY | SHASTRY HERBAL LTD P.O.BOX 7021 ARUSHA | 1ST NOVEMBER 2023 | Presha ya kupanda, Moyo kutanuka, |
| | | | | | | | | Kupooza. |
| 100 | MAS-ASILI IMMUNE BOOSTER | TZ17TM00100 | Unga | Bahasha laini yenye 300gm | M&CZ LIMITED | M&CZ LIMITED P.O.BOX 38 IFAKARA | 1ST NOVEMBER 2023 | Husaidia kupandisha kinga ya mwili kupamba na na virusi,kansa ya uzazi, kansa ya koo |
| 101 | PKM-ASILI IMMUNE TONIC | TZ17TM00101 | Unga | Bahasha laini yenye 300gm | M&CZ LIMITED | M&CZ LIMITED P.O.BOX 38 IFAKARA | 1ST NOVEMBER 2023 | Kusisha kiwango cha sukari mwilini, Kutibu mawe ya figo na kibofu, |
| 102 | BURN CARE | TZ17TM00102 | Unga | Kopo jeupe la 50gm | ZACHARIA LAZARO BIHOLE | WET WELL HERBAL CLINIC P.O.BOX 11514,DAR ES SALAAM | 1ST NOVEMBER 2023 | Dawa ya vidonda vya moto, Kisukari, na Vidonda sugu. |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 103 | MBOGO | TZ17TM0 0103 | Unga | Kopo jeupe la 150gm | DAVID MAGINA KILALA | NSONG'WA TRADITIONAL CLINIC P.O BOX 6768 KILIMANJARO | 1ST NOVEMBER 2023 | Kusaidia viungo visisagane katika maungio(Arthr itis), Kusaidia kuondoa maumivu makali kwenye mifupa. |
| 104 | NSONG'WA | TZ17TM0 0104 | Unga | Kopo jeupe la 150gm | DAVID MAGINA | NSONG'WA TRADITIONAL CLINIC P.O 1ST NOVEMBER 2023 | | |
| | | | | | KILALA | BOX 6768 KILIMANJARO | | |
| 105 | MBASA | TZ17TM0 0105 | Unga | Kopo jeupe la 150gm | DAVID MAGINA | NSONG'WA TRADITIONAL CLINIC P.O 1ST NOVEMBER 2023 | | |
| | | | | | KILALA | BOX 6768 KILIMANJARO | | |
| 106 | NGUMBO | TZ17TM0 0106 | Unga | Kopo jeupe la 150gm | DAVID MAGINA | NSONG'WA TRADITIONAL CLINIC P.O 1ST NOVEMBER 2023 | | |
| | | | | | KILALA | BOX 6768 KILIMANJARO | | |
| 107 | LONZWE | TZ17TM0 0107 | Unga | Kopo jeupe la 150gm | DAVID MAGINA | NSONG'WA TRADITIONAL CLINIC P.O 1ST NOVEMBER 2023 | | |
| | | | | | KILALA | BOX 6768 KILIMANJARO | | |
| | | | | Kopo jeupe lenye | | IPHYTOLS TANZANIA CO | | |

**KIAMBATISHO NA. 5:** IDADI YA WAGONJWA WALIOPATA MSAMAHA NA GHARAMA YA MSAMAHA KATIKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA KWA KIPINDI CHA JULAI 2023 HADI MACHI 2024

| Na. | Hospitali | Idadi ya Wagonjwa Waliopata Msamaha | Gharama za Msamaha |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Amana | 23,150 | 143,271,603 |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga -Bombo | 13,088 | 182,245,524 |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera - Bukoba | 47,089 | 153,440,855 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma | 26,825 | 615,153,230 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita | 664 | 22,914,350 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | 759 | 11,327,400 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi | 73,798 | 2,548,636 |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora -Kitete | 16,713 | 139,933,093 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara -Ligula | 316 | 2,214,200 |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara | 2,284 | 145,641,342 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma -Maweni | 15,731 | 118,929,505 |
| 12 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro -Mawenzi | 1136 | 69,461,922 |
| 13 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | 401 | 14,002,634 |
| 14 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro | 9713 | 112,771,942 |
| 15 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa | 3,543 | 80,880,910 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Arusha -MountMeru | | |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara -Musoma | 6,476 | 214,933,140 |
| 17 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Mwananyamala | 14,202 | 105,478,830 |
| 18 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe | 453 | 9,127,524 |
| 19 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza-Sekou Toure | 13,314 | 264,005,050 |
| 20 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga | 2,729 | 48,228,573 |
| 21 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu | 175 | 11,755,747 |
| 22 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida | 6,413 | 195,947,860 |
| 23 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi -Sokoine | 221 | 5,322,800 |
| 24 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma -Songea | 3,745 | 28,476,850 |
| 25 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | 5,071 | 95,397,990 |
| 26 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa -Sumbawanga | 558 | 8,704,649 |
| 27 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Temeke | 13,907 | 106,401,215 |
| 28 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani -Tumbi | 525 | 12,268,856 |
| | **JUMLA** | **302,999** | **2,920,786,230** |

**KIAMBATISHO NA. 6:** HALI YA UTOAJI WA HUDUMA MUHIMU 14 ZA KIBINGWA KATIKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA.

| No | Hospital | Zinazohitajika | Machi 2023 | | Machi 2024 | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Zilizopo | % | Zilizopo | % |
| 1 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - | 14 | 11 | 79 | 11 | 79 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Amana | | | | | |
| 2 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga -Bombo | 14 | 11 | 79 | 10 | 71 |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera -Bukoba | 14 | 9 | 64 | 8 | 57 |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma | 14 | 10 | 71 | 10 | 71 |
| 5 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita | 14 | 3 | 21 | 7 | 50 |
| 6 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa | 14 | 7 | 50 | 8 | 57 |
| 7 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi | 14 | 4 | 29 | 3 | 21 |
| 8 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora -Kitete | 14 | 3 | 21 | 5 | 36 |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara -Ligula | 14 | 5 | 36 | 5 | 36 |
| 10 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara | 14 | 5 | 36 | 5 | 36 |
| 11 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma -Maweni | 14 | 6 | 43 | 7 | 50 |
| 12 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro - Mawenzi | 14 | 6 | 43 | 8 | 57 |
| 13 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | 14 | 6 | 43 | 5 | 36 |
| 14 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro | 14 | 8 | 57 | 9 | 64 |
| 15 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Arusha -Mount Meru | 14 | 9 | 64 | 10 | 71 |
| 16 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara | 14 | 4 | 29 | 6 | 43 |
| 17 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa- Mwananyamala | 14 | 9 | 64 | 10 | 71 |
| 18 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe | 14 | 3 | 21 | 6 | 43 |
| 19 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa | 14 | 6 | 43 | 8 | 57 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Mwanza-Sekou Toure | | | | | |
| 20 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga | 14 | 4 | 29 | 4 | 29 |
| 21 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu | 14 | 3 | 21 | 4 | 29 |
| 22 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida | 14 | 8 | 57 | 8 | 57 |
| 23 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi -Sokoine | 14 | 4 | 29 | 4 | 29 |
| 24 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma -Songea | 14 | 5 | 36 | 7 | 50 |
| 25 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | 14 | 3 | 21 | 6 | 43 |
| 26 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Rukwa - Sumbawanga | 14 | 3 | 21 | 5 | 36 |
| 27 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa - Temeke | 14 | 12 | 86 | 11 | 79 |
| 28 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani -Tumbi | 14 | 9 | 64 | 11 | 79 |

**KIAMBATISHO NA. 7:** HALI YA MADAKTARI BINGWA KATIKA HOSPITALI ZA RUFAA ZA MIKOA.

| No | Hospital | Physician | Pediatric | OBGY | General Surgeon | Orthopaedic Surgeon | Radiologist | EMD Specialist | Anaesthesiologist | ENT Surgeon | Ophthalmologist | Oncologist | Urologist | Haematologist | Dermatologist | Psychiatrist | Dental Specialist | Gastroenterologist | Nephrologist | TOTAL |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AMANA | 3 | 4 | 4 | 2 | 2 | 3 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | **26** |
| 2 | BOMBO | 2 | 2 | 4 | 2 | 4 | 2 | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **21** |
| 3 | BUKOBA | 1 | 2 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **12** |
| 4 | DODOMA | 2 | 4 | 4 | 4 | 4 | 3 | 0 | 0 | 1 | 5 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | **30** |

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | GEITA | 1 | 2 | 4 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **11** |
| 6 | IRINGA | 1 | 3 | 4 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **14** |
| 7 | KATAVI | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **5** |
| 8 | KITETE | 1 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **8** |
| 9 | LIGULA | 0 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **5** |
| 10 | MANYARA | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **7** |
| 11 | MAWENI | 1 | 2 | 3 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **11** |
| 12 | MAWENZI | 1 | 2 | 1 | 1 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **12** |
| 13 | MBEYA | 0 | 2 | 3 | 3 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **10** |
| 14 | MOROGORO | 3 | 2 | 3 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | **14** |
| 15 | MT.MERU | 2 | 2 | 4 | 3 | 2 | 1 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | **21** |
| 16 | MUSOMA | 1 | 1 | 2 | 3 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **9** |
| 17 | MWANANYAMALA | 2 | 5 | 5 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | **21** |
| 18 | NJOMBE | 1 | 1 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **6** |
| 19 | SEKOUTOURE | 3 | 2 | 4 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | **17** |
| 20 | SHINYANGA | 1 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **5** |
| 21 | SIMIYU | 0 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **6** |
| 22 | SINGIDA | 2 | 1 | 4 | 3 | 1 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **14** |
| 23 | SOKOINE | 0 | 0 | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **7** |
| 24 | SONGEA | 1 | 1 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **9** |
| 25 | SONGWE | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | **8** |
| 26 | SUMBAWANGA | 1 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **7** |
| 27 | TEMEKE | 3 | 3 | 6 | 1 | 3 | 5 | 0 | 1 | 2 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | **30** |
| 28 | TUMBI | 1 | 3 | 3 | 4 | 2 | 1 | 2 | 2 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | **2** |

| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | **3** |
| | **TOTAL** | **35** | **54** | **79** | **53** | **27** | **28** | **14** | **6** | **22** | **23** | **1** | **4** | **3** | **2** | **7** | **7** | **2** | **2** | **369** |

**KIAMBATISHO NA. 8.** UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**(a) Miradi ya ujenzi inayoendelea kutekelezwa katika Hospitali ya Taifa, Maalum, Kanda, Mikoa na Vyuo vya Afya**

| **Na.** | **Namba ya Mradi** | **Jina la Mradi** | **Kazi zitakazotekelezwa** | **Gharama za Mradi** | **Fedha zilizotolewa tangu Mradi uanze** | **Hatua ya Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5487 | Hospitali ya Taifa Muhimbili (Upanga) | Ujenzi wa Jengo la Wodi Maalum (Private wards) Phase II | 26,000,000,000.00 | 5,900,412,405.51 | Ujenzi umefikia 95%- Phase I Frame ambapo ni hatua ya umwagaji wa zege ya "roof beam" |
| 2 | 5427 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) | Ujenzi wa Jengo la huduma za tiba - Mionzi kwa matibabu ya magonjwa ya Saratani (Radiotherapy) | 5,029,721,695.00 | 2,000,000,000.00 | Ujenzi umefikia 71% hatua ya ukamilishaji (Finishing) |
| 3 | 5428 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kati - Benjamini Mkapa | Ujenzi wa Jengo la huduma za tiba - Mionzi kwa matibabu ya magonjwa ya Saratani (Radiotherapy) | 30,421,863,042.69 | 7,941,657,575.39 | Ujenzi umefikia 28% usukaji nondo za "Bunker" |

| Na. | Namba ya Mradi | Jina la Mradi | Kazi zitakazotekelezwa | Gharama za Mradi | Fedha zilizotolewa tangu Mradi uanze | Hatua ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 4 | 5424 | Hospitali Maalum ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto | Ujenzi wa jengo la Maabara ya Kisasa- BSL3-Phase II(Mradi uko kwenye DLP) | 10,443,607,808.00 | 9,472,699,735.00 | Mradi umekamilika kwa 100% na jengo limeanza kutumika |
| 5 | | | Ujenzi wa jengo la Radiolojia | 3,100,000,000.00 | 2,523,634,202.11 | Ujenzi umefikia 48% Maandalizi ya kupauwa |
| 6 | 5422 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za juu - Mbeya | Ujenzi wa jengo kwa ajili ya Huduma za uzazi (Maternity Complex) unaofanyika eneo la Meta. | 12,392,191,914.99 | 12,392,191,914.99 | Mradi umekamilika kwa 99% na jengo limeanza kutumika |
| 7 | 5408 | Hospitali ya Rufaa ya Kanda- Burigi- Chato | Awamu ya pili: Ujenzi wa Jengo la Wodi za wagonjwa,"External work" na jengo Radiologia. | 18,547,638,481.98 | 9,756,138,647.49 | Ujenzi wa wodi 82%, "External works" asilimia 100 na Radiolojia asilimia 100 linatoa huduma |
| | | | Ujenzi wa majengo ya Hospitali: (CSSD, Mortuary na Laundry) | 3,773,414,711.45 | 1,509,365,884.56 | Ujenzi wa CSSD, Mortuary, Laundry, Waitingbay na Walkway umefikia 15% |
| 8 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa - Njombe | Ujenzi wa jengo la OPD, Jengo la Afya ya uzazi (Maternity), Upasuaji & Mifupa na wodi, laundry na Incinerator na nyumba tano za watumishi | 27,478,274,300.00 | 22,192,716,800.00 | Mradi umekamilika kwa 100% na jengo limeanza kutumika |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Simiyu | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi (Maternity block) | 7,179,859,632.00 | 6,760,689,988.00 | Ujenzi umefikia 96% hatua ya ukamilishaji |
| 10 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Manyara | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa Nje (OPD), EMD, ICU na ukamilishaji wa jengo la Damu salama | 4,145,712,834.26 | 2,145,712,834.26 | Ujenzi umefikia 68% ya ufungaji wa mifumo mbalimbali |
| 11 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa- Mbeya | Ujenzi wa jengo la upasuaji (theatre, ICU & CSSD) | 5,413,493,180.24 | 5,339,493,180.24 | Ujenzi umefikia 99% ya utekelezaji. |
| 12 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa- Maweni | Ujenzi wa Jengo la OPD-Awamu ya kwanza | 3,590,000,000.00 | 2,690,000,000.00 | Awamu ya kwanza ya ujenzi imefikia 98%. |

| **Na.** | **Namba ya Mradi** | **Jina la Mradi** | **Kazi zitakazotekelezwa** | **Gharama za Mradi** | **Fedha zilizotolewa tangu Mradi uanze** | **Hatua ya Utekelezaji** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,318,243,549.59 | 1,073,589,299.67 | Ujenzi umekamilika kwa 87% |
| 13 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Sokoine | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) | 3,700,000,000.00 | 3,099,000,000.00 | Ujenzi awamu ya pili umefikia 82% ukamilishaji. |
| 14 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Songea | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) | 3,700,000,000.00 | 2,778,338,430.00 | Ujenzi umefikia 75% hatua ya finishing sakafu ya kwanza |
| 15 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Ligula | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa nje (OPD)-Awamu ya Kwanza | 2,700,000,000.00 | 2,226,495,947.00 | Ujenzi umefikia 85% kwa sakafu ya nchini. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 16 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Kitete | Ujenzi wa Jengo laAfya ya mama na mtoto | 4,700,000,000.00 | 3,578,147,591.50 | Ujenzi umefikia 65% awmu ya pili ikiwa yakwanza imekamilika. |
| 17 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Singida | Ujenzi wa Jengo la "Covid-19 Containment Centre" (Wards, Theatres, Pharmacy, Laboratory & ICU) | 20,297,252,638.33 | 6,021,614,224.00 | Ujenzi umefikia asilimia 31% hatua ya kumwaga zege ya sakafu ya "Compatiment" ya pili. |
| 18 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa- Mara | Ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere (Wing C)-Phase IV | 23,855,073,959.00 | 17,873,865,608.85 | Ujenzi umefikia 98% kwa bawa C na linatoa huduma, bawa B. 85 na A ni 45 hatua ya ukamailishaji |
| | | | Ujenzi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere (Wing A)-Phase V | 19,660,423,987.21 | 0 | Mkataba umeshasainiwa na mkandarasi kwasasa anangoja kukabidhiwa eneo la mradi |
| 19 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Kisopwa | Ujenzi wa Kituo cha Umahiri kwa ajili ya matibabu ya magonjwa hatarishi na Milipuko | 2,900,000,000.00 | 1,015,000,000.00 | Ujenzi umefikia 53% hatua ya umaliziaji |
| 20 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Songwe | Ujenzi wa Jengo la Huduma za Afya ya Mama na Mtoto (Maternity block) | 9,745,114,617.00 | 6,791,684,252.78 | Ujenzi umefikia 60% hatua ya upauwaji |
| **Na.** | **Namba ya Mradi** | **Jina la Mradi** | **Kazi zitakazotekelezwa** | **Gharama za Mradi** | **Fedha zilizotolewa tangu Mradi uanze** | **Hatua ya Utekelezaji** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 21 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa-Katavi | Ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa-pamoja na ujenzi wa jengo la mama na mtoto Wing B | 17,950,000,000.00 | 9,260,000,000.00 | Ujenzi kwa bawa "B" ni 98% linatumika, ambapo bawa "A" umefikia asilimia 30 ikiwa ikiwa miundombinu ya nje imekamilika. |
| 22 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Ruf aa-Mawenzi | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya uzazi (Maternity block) | 7,423,559,565.00 | 12,609,352,188.81 | Ujenzi umefikia 86% sakafu ya chini na ya kwanza zinatoa huduma. |
| 23 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa Sekoutour e-Mwanza | Ujenzi wa jengo la Huduma za Afya ya Mama na Mtoto (Ghorofa sita) | 13,916,811,290.29 | 11,153,760,650.51 | Ujenzi umefikia 95% jengo linatoa huduma |
| 24 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Ruf aaRukwa | Ukamilishaji wa ujenzi wa Jengo la Damu Salama | 1,173,653,873.06 | 1,162,242,441.95 | Ujenzi umekamilika kwa 65% |
| 25 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Ruf aaBombo - Tanga RRH | Ujenzi wa Jengo la Damu Salama na kitengo cha utengenezaji wa Maji tiba-Awamu I | 668,495,465.20 | 426,000,000.00 | Ujenzi umekamilika kwa 20% |
| 26 | 5411 | Uimarishaji wa Hospitali za Rufaa Geita | Ujenzi wa Jengo la Afya ya Mama na Mtoto (Maternity Wing) | 13,213,606,303.00 | 4,160,642,442.00 | Ujenzi umefikia 45% hatua Finishing kwa jengo na kazi za nje (Walkway na Dewatts) |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 27 | | Chuo ch Uuguzi n UkungaNachingwea | Ujenzi wa Jengo la madarasa na maabara | 1,609,838,617.79 | 58,000,000.00 | Ujenzi umefikia 27% hatua ya Umwagaji zege wa sakafu ya kwanza |
| 28 | | Chuo ch Afya-Mpwapwa | Ukarabati wa jengo la utawala,maktaba na ukumbi | 353,325,040.00 | 0 | Ukarabati umefikia 30% hatua ya uezekaji |
| 29 | | Wizara y Afya | Ujenzi wa Jengo la ofisi za Wizara ya Afya | 23,346,618,260.38 | 20,002,820,027.04 | Ujenzi umefikia 86% hatua ya finishing |
| **JUMLA KUU** | | | | **342,030,659,409.4** | **193,915,266,671.66** | |

## (b) Miradi iliyo katika hatua za awali

| Na | Jina la Mradi | Kazi zitakazotekelezwa | Hatua za utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Taasisi ya Mifupa -MOI | Ujenzi wa Jengo la OPD | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi |
| 2 | Taasisi ya Saratani ya Ocean Road | Ujenzi wa Kituo cha Mionzi kwa ajili ya matibabu ya Saratani Mbeya | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi |
| 3 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kilimanjaro Mawenzi | Ujenzi wa Jengo la wodi na Jengo la kuhifadhia maiti | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 4 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza -Sekou -Toure | Ujenzi Jengo la huduma Jumuishi | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi |
| 5 | Hospitali Maalum ya | Ujenzi wa miundombinu ya | Hatua ya Usanifu wa michoro |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mama na Mtoto - Dodoma | Hospitali Maalum ya huduma ya afya ya mama na mtoto. | |
| 6 | Hospitali Mpya ya Kanda ya Kusini-Mtwara | Ujenzi wa miundombinu wa awamu ya pili (jengo la huduma za afya ya Mama na Mtoto Mchanga( Maternity Complex), kufulia, kichomea taka na nyumba za watumishi) | Hatua ya Usanifu wa michoro |
| 7 | Hospitali Mpya ya Kanda ya Magharibi-Kigoma | Ujenzi wa miundombinu ya Hospitali ya Kanda | Hatua ya Usanifu wa michoro |
| 8 | Hospitali teule ya rufaa ya kibingwa hadhi ya mkoa –Ukerewe | Ujenzi wa Jengo la kutoa huduma za kibingwa | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi |
| 9 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya | Ujenzi wa Jengo la OPD | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 10 | CEDHA | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 11 | Chuo cha Afya-Kibondo | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 12 | Chuo cha Afya-Muheza | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 13 | Chuo cha Afya-Tukuyu | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 14 | Chuo cha Afya-Same | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 15 | Chuo cha Afya-Sumbawanga | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 16 | Chuo cha Afya-Mbozi | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 17 | Chuo cha Afya-Geita | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 18 | Chuo cha Afya-Maswa | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 19 | Chuo cha Afya-Kahama | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 20 | Chuo cha Afya-Mbulu | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 21 | Chuo cha Afya-Mpwapwa | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 22 | Chuo cha Afya-Rombo | Ujenzi wa miundombinu ya Chuo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 23 | Kituo cha Umahiri wa magonjwa hatarishi na Mlipuko-Kagera | Ujenzi wa miundombinu ya kituo | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 24 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi | Ujenzi wa minudombinu ya Damu salama | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 25 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa | Ujenzi wa minudombinu ya | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa Shinyanga | Damu salama | Elekezi |
| 26 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma | Ujenzi wa minudombinu ya Damu salama | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 27 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara | Ujenzi wa minudombinu ya Damu salama | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 28 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida | Ujenzi wa minudombinu ya Damu salama | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 29 | Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe | Ujenzi wa minudombinu ya Damu salama | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 30 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Geita | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 31 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Simiyu | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 32 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Tabora | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 33 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Dodoma | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 34 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Singida | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 35 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Manyara | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 36 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Songwe | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 37 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Pwani | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 38 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa waRuvuma | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 39 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Iringa | Ukarabati wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 40 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Kigoma | Ukarabati wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 41 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Mbeya | Ukarabati wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 42 | Hospitali yaya Rufaa Mikoa wa Mtwara | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 43 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa ya Rukwa | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 44 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa wa Mara | Ujenzi wa wodi ya Watoto wachanga (NCU) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 45 | ya Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Tanga | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya Mama na Mtoto Mchanga( Maternity Complex) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 46 | ya Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Morogoro | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya Mama na Mtoto Mchanga( Maternity Complex) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 47 | ya Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Kagera | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya Mama na Mtoto Mchanga( Maternity Complex) | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri Elekezi |
| 48 | Hospitali yaya Rufaa Mkoa | Ujenzi wa jengo la huduma za afya ya | Hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mshauri |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa Shinyanga | Mama na Mtoto Mchanga( Maternity Complex) | Elekezi |

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Ahsante sana pia Mheshimiwa Waziri.

Sasa nimwite Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI aje awasilishe maoni ya Kamati yake.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati kuhusu makadirio na mapato ya matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu kama zifuatazo: -

(a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi;

(b) Sehemua ya Pili ni Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(c) Sehemu ya Tatu ni Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi mitatu ilitembelewa na kukaguliwa katika mikoa ya Mwanza na Geita. Lengo lilikuwa ni kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa miradi hiyo na kupima endapo utekelezaji wake utaweza kuyafikia malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, katika miradi iliyokaguliwa, miradi miwili imepokea fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji na mradi mmoja wa ununuzi wa vifaatiba vya matibabu ya ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando haukupokea fedha yoyote hadi kufikia mwezi Machi, 2024.

Mheshimiwa Spika, yatokanayo na ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka 2023/2024. Kufuatia ukaguzi wa miradi hiyo, kamati ilibaini mambo yafuatayo;

(a) Fedha za miradi kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(b) Fedha kutolewa kwa kiwango kidogo chini ya asilimia 50% hadi kufikia mwezi Machi, 2024;

(c) Ufinyu wa maeneo ya Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza – Sekou Toure ikilinganishwa na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kujengwa kwa ajili ya kuboresha huduma za Afya;

(d) Uhaba wa rasilimaliwatu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Rufaa za Kanda ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando.

(e) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* kukataa baadhi ya madai ya fedha za malipo ya huduma za matibabu. Mfano, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando kwa mwezi Oktoba hadi Disemba, 2023 madai yaliyokataliwa ni shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 20% ya madai yote yaliyowasilishwa kwa miezi hiyo mitatu na

(f) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuchelewesha fedha za malipo ya huduma za matibabu kwa vituo vya kutolea huduma za Afya. Mfano Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato inadai kiasi cha shilingi 377,503,452 na kipindi cha kuanzia Disemba hadi Machi, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa ya Bugando inadai kiasi cha shilingi bilioni 12.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla imebainika kuwa mwenendo wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo si wa kuridhisha ikilinganishwa na muda uliobaki wa miezi miwili tu kwa mwaka wa fedha wa utekelezaji wa miradi hiyo kwisha. Hali hii itasababisha miradi kutokukamilika ndani ya muda uliopangwa na kutokuyafikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora zilizokusudiwa. Vilevile kusababisha mabadiliko katika gharama za utekelezaji wa miradi hiyo endapo haitatekelezwa ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Afya ilikadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 677.6 kutoka katika vyanzo mbalimbali vilivyobainishwa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 imekusanywa 62% ya lengo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hali ya makusanyo ni ya kuridhisha isipokuwa upande wa Makao Makuu ya Wizara ambapo imekusanya 42% tu ya lengo kiasi ambacho ni kidogo kulinganisha na muda uliobaki. Ni imani ya Kamati kuwa, hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha mwezi Juni, 2024 kiasi chote cha makusanyo kitafikiwa kama ilivyokadiriwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2023/2024. Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.2. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2024 hali ya utolewaji wa fedha hususan kwa ajili ya miradi ya maendeleo si ya kuridhisha kwani fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimetolewa kwa 35% na fedha za nje zimetolewa 30% kwa kielelezo ambacho tumekiambatanisha, kielelezo namba mbili.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa utoaji wa fedha, si wa kuridhisha kwani unachelewesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni muhimu sana Serikali kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Uchambuzi wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya mwaka 2024/2025. Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2024/2025 ni shilingi bilioni 556.8. Mchanganuo unaonekana katika kielelezo namba tatu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2024/2025 ambapo imeongezeka shilingi bilioni 79 sawa na ongezeko la 12% ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2023/2024. Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Katika mwaka huu Bajeti Kuu ya Serikali ni shilingi bilioni 49.3 ambapo fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) ni shilingi trilioni 1.3 sawa na 2.6% ya Bajeti ya Taifa. Kielelezo namba nne kinaonyesha mchanganuo wa fedha zilizoombwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la fedha zinazoombwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025 ni shilingi bilioni 76 ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia sita ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa mwaka 2023/2024. Hata hivyo ongezeko hilo lipo katika fedha za matumizi ya kawaida ambapo zimeongezeka kwa asilimia 25.7 ukilinganisha na mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la fedha za matumizi ya kawaida linahusu mishahara ya watumishi ambayo imeongezeka kwa asilimia 37. Aidha fedha za matumizi mengineyo zimepungua kwa asilimia 0.9 na fedha za miradi ya maendeleo zimepungua kwa asilima saba ambapo fedha za ndani zimepungua kwa asilimia tatu na fedha za nje zimepungua kwa asilimia 12.8.

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione haja ya kuongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuongeza kasi ya kuboresha sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bohari ya Kuu ya Dawa *(MSD)*. Uchambuzi wa Kamati umebaini changamoto ya mtaji wa Bohari Kuu ya Dawa ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 ombi la mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya. Mtaji unaoombwa ni shilingi bilioni 561.5 kwa mchanganuo kuwa, shilingi bilioni 204 zinahitajika kuwezesha ununuzi wa bidhaa za afya, shilingi bilioni 66.9 kwa ajili ya ujenzi wa maghala, shilingi bilioni 100.46 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na shilingi bilioni 191 kwa ajili ya malipo ya madeni ya washitiri na vituo vya kutolea huduma.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana kwa Serikali kutoa mtaji unaoombwa kwani ikiwa kiasi hiki cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF);* kumekuwepo na changamoto inayokabili uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, hali inayosababisha mvutano

na kusuasua kwa ushirikiano kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* na sekta binafsi ya afya. Baadhi ya sababu za changamoto hizo ni: -

(a) Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura Namba 395 kutokutambua uwepo wa sekta binafsi ya afya kama mnufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;

(b) Kutoruhusu vituo binafsi vya kutolea huduma za afya kutumia mfumo wa kuchangia huduma za afya *(co-payment)* kwa wanufaika wa *NHIF*, ilhali mfumo huo unaruhusiwa kwa vituo vya kutolea huduma vya umma tu;

(c) Kukosekana kwa chombo huru na cha kudumu kinachoratibu na kusimamia bei za huduma za afya;

(d) Kutokuzingatiwa kwa maoni ya wadau wa sekta ya afya kuhusu kitita kipya cha bei za huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, kufuatia changamoto hizo, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kutafuta ufumbuzi kwa haraka ili wananchi ambao ni wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya waweze kuendelea kupata huduma za afya bora katika vituo vya kutolea huduma za afya wanavyopendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi; Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha kwa kiwango kikubwa uwekezaji katika utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini ikiwemo huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi zinazotolewa katika hospitali za rufaa za mikoa, kanda na hospitali maalumu za kitaifa. Huduma hizo za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi zinajumuisha uanzishaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu zinazolenga kusaidia na kuokoa maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, uanzishaji wa huduma hii unawarahisishia wananchi wenye mahitaji kupata huduma hii ndani ya nchi

ambapo gharama si kubwa ukilinganisha na gharama za kupata matibabu hayo nje ya nchi. Aidha, upatikanaji wa huduma hii unachangia kuongeza mapato ndani ya nchi kwa kuwa gharama za matibabu ambazo zingelipwa nje ya nchi sasa zitabaki ndani ya nchi. Vilevile uanzishwaji wa huduma hii unachochea tiba utalii ambapo watu kutoka nchi nyingine hutembelea nchi kwa lengo la kupata matibabu jambo linalochangia kukua kwa tiba utalii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu na faida za utolewaji wa huduma hizi nchini, ni muhimu sasa Serikali iimarishe na iweke mazingira mazuri ya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa kuhakikisha kunakuwepo na sheria zinazosimamia utoaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe za viungo vya mwili wa binadamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa; azma ya Serikali kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 ni kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini. Kamati imebaini kuwepo kwa maendeleo makubwa yaliyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Afya ambapo sekta binafsi imewekeza kwa kiwango kikubwa kwa kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa ambazo vimechochea upatikanaji wa bidhaa za dawa nchini.

Mheshimiwa Spika, licha ya Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za dawa nchini bado kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri uzalishaji wa bidhaa hizo na uwekezaji kwa ujumla. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

(a) Bohari Kuu ya Dawa kuchelewa malipo ya fedha kwa wazalishaji wa bidhaa hizo za dawa;

(b) Kuwepo kwa mamlaka nyingi za udhibiti wa bidhaa za dawa na malighafi za kutengeneza bidhaa za dawa, kwa mfano, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba *(TMDA)*,

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania *(TAEC),* Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Bodi ya Sukari Tanzania, Shirika la Viwango *Tanzania (TBS)* na Wakala wa Vipimo na wengineo;

(c) Uwepo wa utitiri wa kodi wakati wa uingizaji wa malighafi za uzalishaji bidhaa za dawa na baada ya kuzalisha bidhaa za dawa;

(d) Kukosekana kwa masoko ya uhakika ndani ya nchi kutokana na ushindani mkubwa wa bidhaa za dawa kutoka nje ya nchi ambapo bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini. Mfano bidhaa za dawa kutoka India na China; na

(e) Kukosekana kwa nishati ya umeme ya uhakika viwandani jambo linalosababisha shughuli za uzalishaji kusimama kwa masaa kadhaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kulinda wawekezaji wa ndani na kuboresha mazingira ambayo yatawavutia wawekezaji wengi zaidi ndani ya nchi, ni vema Serikali kutafuta ufumbuzi kwa haraka na kutatua changamoto zote zinazowakabili wawekezaji hao ili kuweza kuimarisha zaidi uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za dawa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sasa maoni na ushauri Kamati. Baada ya uchambuzi wa bajeti kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2023/2024; Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, uhaba wa rasilimali watu; Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya afya nchini iendelee kutoa vibali vya ajira vinavyokidhi mahitaji halisi ya hospitali na taasisi zote za afya ili kuwa na wataalam wa kutosha na kufanikisha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa maeneo katika hospitali za rufaa za mikoa; Serikali ipanue maeneo ya hospitali za rufaa za mikoa kwa ajili ya kuongeza miundombinu mipya katika hospitali hizo ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya na kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa huduma za afya hospitalini; ili kuboresha huduma za afya hospitalini, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Serikali iboreshe vitengo vya huduma kwa wateja *(customer care services)* katika hospitali zote nchini; na

(b) Serikali iboreshe vitengo vya TEHAMA katika hospitali zote nchini ili kuimarisha matumizi ya mifumo inayorahisisha utoaji wa huduma za afya kama vile mfumo wa malipo na mifumo ya taarifa za matibabu ya wagonjwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na changamoto ya uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*; ili kuboresha utendaji Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, pamoja na kuondoa mvutano uliopo baina ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na sekta binafsi ya afya, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ianze mchakato wa kurekebisha Sheria ya *NHIF,* Sura Namba 395 ili kuitambua sekta binafsi ya afya ambayo ni mdau muhimu sana katika sekta hii ya afya;

b) Serikali ilipe madeni yote inayodaiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ili kutokukwamisha shughuli za uendeshaji wa mfuko huo;

c) Serikali ianzishe chombo huru mahsusi na cha kudumu kitakachoratibu na kusimamia bei za huduma za afya *(Health Services Pricing Board)* ambacho kitajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi;

d) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)* iwezeshwe kisheria kwa kuwekewa kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za bima ya afya nchini;

e) Vituo binafsi vya kutolea huduma za afya viruhusiwe kuwa na utaratibu wa mgonjwa kuchangia huduma *(co-payment)* ambapo wamiliki wa kadi za *NHIF* watatakiwa kulipa kwa pesa taslimu gharama zinazozidi kiwango cha kitita kinachochangiwa na *NHIF*;

f) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uimarishe mifumo ya TEHAMA ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo na kudhibiti udanganyifu;

g) Tathmini ya kina iendelee kufanyika kuhusu kitita kipya cha bei za huduma za afya na kuhakikisha kitita kipya kinazingatia maoni na makubaliano ya wadau wote wa sekta ya afya kutoka sekta ya umma na binafsi;

h) *NHIF* ianzishe kamati ya wataalam ambao watakuwa wanapitia malalamiko ya kitaaluma yanayowasilishwa na vituo vya kutolea huduma au wataalam kuhusu bima ya afya *(Technical/Expert Review Committee)*; Vilevile Kamati hii ishughulikie madai yanayokataliwa kulipwa *(rejection)* kwa vituo vya kutolea huduma za Afya ili kupunguza malalamiko ya watoa huduma;

i) Serikali iunde Kamati maalum ya kitaalamu ya kupitisha na kutoa mwongozo wa aina za dawa, vifaa tiba na teknolojia ya tiba *(Health Technology Assessment Committee)* zinazotakiwa kutumika katika utoaji wa huduma za Afya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya tathmini ya vyanzo na viwango vya fedha kwa ajili ya mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa malipo ya fedha ya huduma za afya kutoka kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulipe kwa wakati madeni au madai ya fedha za watoa huduma za afya kwa vituo vya kutolea huduma za afya vinavyoudai mfuko huo, ili kutokukwamisha utoaji wa huduma bora za Afya katika vituo hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa mtaji Bohari Kuu ya Dawa; Serikali itoe mtaji wa shilingi bilioni 561.5 kwa Bohari Kuu ya Dawa ili kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya, kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za afya kwa kujenga maghala ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uimarishaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa; ili uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa uweze kuleta tija kwa watanzania, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* ilipe kwa wakati fedha inazodaiwa na viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za dawa;

b) Serikali itoe msamaha wa kodi kwa malighafi zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kuzalisha dawa au bidhaa za dawa;

c) Serikali iongeze kodi kwa bidhaa za dawa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinazalishwa na viwanda vya ndani; na

d) Serikali ihakikishe kwamba kunakuwa na upatikanaji wa nishati (umeme) ya uhakika hasa kwenye maeneo ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu; Serikali ikamilishe utungaji wa sheria ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe za viungo vya binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hii kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya; Serikali iunde bodi moja ya usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Hatua hii itaweka ulazima wa vituo vya kutolea huduma za afya vinavyomilikiwa na Serikali kusajiliwa na kukidhi vigezo kabla ya kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubia kati ya Serikali na sekta binafsi katika huduma za afya *(Public Private Partnership)*; Serikali iimarishe usimamizi na ifanye mapitio ya mikataba ya utoaji wa huduma za afya baina yake na taasisi zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za afya ili kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina yake na taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha kwa kusema, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb) – Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb) – Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaotupa katika Kamati yetu. Ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Profesa Tumaini Joseph Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI

pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, (Mb) – Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu haya. Pia, nichukue fursa hii kumtakia kila la kheri katika nafasi anayogombea kule ambapo anagombea *WHO* katika nafasi ambayo ni kubwa. Ninaomba basi zile baraka ulizokuwanazo Mheshimiwa Spika basi umtemee cheche Mheshimiwa Ndugulile ili aweze kupata ushindi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuwashukuru wajumbe wote wa kamati. Napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kiasi cha shilingi 1,311,837,466,000.00 kama ilivyoombwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha
2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu (3) zifuatazo: -

(a) **Sehemu ya Kwanza** - Utangulizi;

(b) **Sehemua ya Pili** - Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(c) **Sehemu ya Tatu** - Maoni na Ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 2.1 Mambo Yaliyozingatiwa Wakati wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuliwezesha Bunge kufuatilia Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na kushauri ipasavyo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuzingatia mambo makuu matatu (3) ambayo ni: -

(i) Taarifa ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya uliotolewa Mwaka wa Fedha 2023/2024;
(ii) Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na
(iii) Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla, uchambuzi huu ulilenga kuliwezesha Bunge kujiridhisha na utekelezaji wa mipango na mwenendo wa matumizi ikilinganishwa na madhumuni ya Bunge kuidhinisha bajeti husika.

***2.2 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2023/2024***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ilitembelea na kukagua utekelezaji wa baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara ya Afya.

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya Miradi mitatu (3) ilitembelewa na kukaguliwa katika Mkoa wa Mwanza na Geita lengo likiwa ni kujiridhisha na mwenendo wa utekelezaji wa Miradi hiyo na kupima endapo utekelezaji wake utaweza kuyafikia malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa wananchi. Miradi hiyo ni pamoja na ununuzi wa vifaa tiba vya matibabu ya ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando; Ujenzi wa wodi ya huduma za Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza - Sekou Toure; na Ujenzi wa jengo la Kuhifadhia Maiti *(Mortuary),* jengo la kusubiria Miili ya Marehemu *(Waiting Area)*, jengo la kufulia *(Laundry)*, jengo la Jenereta *(Power House)*, jengo la kutakasia vifaa tiba *(Central Sterelization Supply Department)* na njia inayounganisha majengo hayo *(Walkway)* katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Chato.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulijulisha Bunge kuwa, katika miradi hiyo iliyokaguliwa, miradi miwili (2) imepokea fedha kwa ajili ya kuanza utekelezaji na mradi mmoja (1) wa ununuzi wa vifaa tiba vya matibabu ya ugonjwa wa saratani katika Hospitali ya Kanda ya Ziwa - Bugando haukupokea fedha yoyote hadi kufikia mwezi Machi, 2024 hivyo kuchelewa kuanza kwa mradi huo ambao ulitegemewa kuboresha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za matibabu ya ugonjwa wa saratani katika maeneo ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya jirani.

### 2.2.1 Yatokanayo na Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia ukaguzi wa miradi hiyo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

(a) Fedha za miradi kutolewa kwa kuchelewa licha ya mwaka wa fedha kuelekea ukingoni;

(b) Fedha kutolewa kwa kiwango kidogo chini ya asilimia 50 hadi kufikia mwezi Machi, 2024;

(c) Ufinyu wa maeneo ya Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza – Sekou Toure ikilinganishwa na mahitaji ya miundombinu inayotakiwa kujengwa kwa ajili ya kuboresha huduma za Afya;

(d) Uhaba wa rasilimali watu katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Rufaa za Kanda ikiwemo Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Bugando.

(e) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kukataa baadhi ya madai ya fedha za malipo ya huduma za matibabu. Mfano, katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando kwa mwezi Oktoba hadi Disemba, 2023 madai yaliyokataliwa ni **shilingi 2,411,013,905.00** sawa na **asilimia 20** ya madai yote yaliyowasilishwa kwa miezi hiyo mitatu.

(f) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuchelewesha fedha za malipo ya huduma za matibabu kwa vituo vya kutolea huduma za Afya. Mfano Katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Machi, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato inadai kiasi cha **Shilingi 377,503,452.00** na kipindi cha kuanzia Disemba hadi Machi, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando inadai kiasi cha Shilingi Bilioni 12.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla imebainika kuwa mwenendo wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo si wa kuridhisha

ikilinganishwa na muda uliobaki wa miezi miwili tu kwa mwaka wa fedha wa utekelezaji wa miradi hiyo kuisha. Hali hii itasababisha miradi kutokukamilika ndani ya muda uliopangwa na kutokuyafikia matarajio ya wananchi ya kupata huduma bora zilizokusudiwa. Vile vile kusababisha mabadiliko katika gharama za utekelezaji wa miradi hiyo endapo haitatekelezwa ndani ya muda uliopangwa.

### 2.3 Utekelezaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati Mwaka 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu Bajeti ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kamati ilitoa Ushauri katika maeneo Kumi na Nane (18). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi, Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na ushauri mwingine bado unaendelea kutekelezwa. Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu, Kamati inaendelea kuyasisitiza katika Taarifa hii.

### 2.4 Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa Kamati wa Fungu 52 makadirio ya Wizara yalikuwa ni kukusanya maduhuli ya **Shilingi 677,621,168,391.00** kutoka katika vyanzo mbalimbali vilivyobainishwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2024 jumla ya **Shilingi 420,085,359,638.86** zilikusanywa sawa na **asilimia 62** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Imebainika kuwa katika vyanzo vya maduhuli vilivyobainishwa na Wizara, chanzo cha hospitali za Kanda, Maalum, Taifa, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara ndicho kinachangia kwa kiasi kikubwa ikiwa ni mchango wa **Shilingi 477,621,168,391.00** ikilinganishwa na vyanzo vingine vilivyobainishwa. Aidha, hadi mwezi Februari, 2024 chanzo hicho kimekusanya **Shilingi 302,377,528,252.25** sawa na **asilimia 63** ya lengo la chanzo hicho. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganuo wa makusanyo ya maduhuli.

**Kielelezo NA. 1: Hali ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Kipindi cha Mwaka 2023/2024**

| NA | CHANZO CHA MAKUSANYO | KIASI KILICHOIDHINISHWA KUKUSANYWA | KIASI KILICHOKUSANYWA | ASILIMIA (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makao Makuu ya Wizara | 88,414,775,177.00 | 36,762,671,134.51 | 42 |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 111,585,224,823.00 | 80,945,160,252.25 | 73 |
| 3. | Taasisi zilizo chini ya Wizara | 477,621,168,390.95 | 302,377,528,252.25 | 63 |
| **JUMLA** | | **677,621,168,390.95** | **420,085,359,638.86** | **62** |

***Chanzo: Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti (Fungu 52) kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Februari 2024***

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla hali ya makusanyo ni ya kuridhisha isipokuwa kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara ambapo kiwango cha makusanyo kipo chini kwani makusanyo yake ni **asilimia 42** ilhali ilipaswa kuwa imekusanya angalau **asilimia 66** mpaka mwezi Februari 2024.


**Mheshimiwa Spika,** Ni imani ya Kamati kuwa, hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha mwezi Juni, 2024 mapato yaliyoidhinishwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2023/2024 yatakuwa yamekusanywa kwa ukamilifu wake.

**2.5 Hali ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2023/2024**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Bajeti ya mwaka wa Fedha 2022/2023, Wizara ya Afya (Fungu 52) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,235,316,516,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 502,951,909,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 41** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 732,364,607,000.00** ambazo ni sawa na **asilimia 59** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2024 hali ya utolewaji wa fedha hususan kwa ajili ya miradi ya maendeleo sio ya kuridhisha kwani fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimetolewa kwa **asilimia 35** na fedha za nje zimetolewa **asilimia 30** tu. Kielelezo kifuatacho kinaonesha fedha zilizoidhinishwa na kiasi kilichotolewa.

**Kielelezo NA. 2: Mchanganuo wa Fedha zilizoidhinishwa na Fedha zilizopokelewa kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Februari, 2024**




| | MATUMIZI MENGINEYO (OC) | MISHAHARA | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
|---|---|---|---|---|
| FEDHA ZILIZOIDHINISHWA | 148,609,423,000.0 | 354,342,486,000.0 | 430,298,000,000.0 | 302,066,607,000.0 |
| FEDHA ZILIZOTOLEWA | 78,737,405,012.74 | 243,610,981,791.69 | 148,705,735,116.4 | 90,425,316,208.13 |
| ASILIMIA | 53 | 69 | 35 | 30 |

FEDHA ZILIZOIDHINISHWA FEDHA ZILIZOTOLEWA ASILIMIA

***Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Afya, Machi 2024***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwenendo huu wa utoaji wa fedha, ni dhahiri kuwa kutakuwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo jambo ambalo linachelewesha maendeleo kwa wananchi. Ni muhimu sana Serikali kuhakikisha fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge zinatolewa kabla ya

mwaka wa fedha 2023/2024 kuisha ili kufikia malengo ya utekelezaji wa kila mradi uliokusudiwa.

## 2.6 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umezingatia miongozo mbalimbali kama vile Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka Mmoja (2024/25), Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya (HSSP-V 2021-2026) na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's 2030).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo: -

### 2.6.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Makadirio ya makusanyo ya maduhuli ya Wizara ya Afya katika mwaka wa fedha 2024/2025 ni **Shilingi 756,866,060,248.00**. Kielelezo kifuatacho kinaonesha mchanganuo wa makadirio ya makusanyo kutoka katika kila chanzo.

**Kielelezo NA. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli Fungu 52 kwa Mwaka 2024/2025**

| CHANZO CHA MAKUSANYO | KIASI |
|---|---|
| Makao Makuu ya Wizara | 70,828,500,189.69 |
| Hospitali za Rufaa za Mikoa | 134,171,499,810.31 |
| Taasisi,Hospitali za Taifa, Maalum na Kanda | 551,866,060,248.00 |
| **JUMLA** | **756,866,060,248.00** |

***Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2024/2025 ambapo zimeongezeka **Shilingi 79,244,891,857.00** sawa na ongezeko la **asilimia 12** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2023/2024. Aidha, kwa upande wa makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka Makao Makuu ya Wizara kuna upungufu wa **asilimia 20,** makadirio ya makusanyo ya maduhuli kutoka hospitali za rufaa za Mikoa yameongezeka kwa **asilimia 20** na makadirio ya makusanyo ya Taasisi yameongezeka kwa **asilimia 16** ukilinganisha na makadirio ya makusanyo ya mwaka 2023/2024.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza Wizara ya Afya kuendelea kusimamia makusanyo, na pia Serikali kuhakikisha inakuwa na mifumo imara ya ukusanyaji wa maduhuli ili kuzuia uvujaji wa mapato.

### 2.6.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2024/2025 Bajeti Kuu ya Serikali ni **Shilingi Bilioni 49,345.7** ambapo fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Wizara ya Afya (Fungu 52) ni **Shilingi 1,311,837,466,000.00** sawa na **asilimia 2.6** ya Bajeti ya Taifa. Kati ya fedha zinazoombwa kwa ajili ya Wizara ya Afya **Shilingi 632,267,220,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 679,570,246,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa ajili ya Wizara ya Afya unaonekana katika kielelezo namba 4.

**Kielelezo NA. 4: Fedha zinazoombwa kuidhinishwa kwa Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**





***Chanzo: Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati umebaini ongezeko la fedha zinazoombwa kwa ajili ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2024/2025. Fedha zilizoongezeka ni **Shilingi 76,520,950,000.00** ambazo ni sawa na ongezeko la **asilimia 6** ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa mwaka 2023/2024. Hata hivyo, ongezeko hilo lipo katika Fedha za Matumizi ya Kawaida ambazo zimeongezeka kwa **asilimia 25.7** ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Ongezeko la Fedha za Matumizi ya Kawaida linahusu Mishahara ya Watumishi ambayo imeongezeka kwa **asilimia 37.** Aidha, Fedha za Matumizi Mengineyo zimepungua kwa **asilimia 0.9** na Fedha za Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **asilima 7** ambapo fedha za ndani zimepungua kwa **asilimia 3** na fedha za nje zimepungua kwa **asilimia 12.8.**

**Kielelezo NA. 5: Ulinganisho wa Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025**




**Chanzo:** ***Randama ya Wizara ya Afya ya Mwaka 2024/2025***

**Mheshimiwa Spika,** Ni rai ya Kamati kuwa, Serikali ione haja ya kuongeza kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya ili kuongeza kasi ya kuboresha Sekta hii muhimu inayogusa maisha ya kila Mtanzania. Aidha, fedha zote zitolewe kwa wakati ili kutimiza malengo yaliyowekwa kwa mwaka wa fedha husika.

### 2.6.3 Bohari Kuu ya Dawa (MSD)

**Mheshimiwa Spika**, Bohari Kuu ya Dawa imekasimiwa majukumu ya msingi ambayo ni Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za Afya kwenda kwenye vituo vya umma vya kutolea huduma za Afya na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya. Katika uchambuzi wa Taarifa ya Utendaji ya Bohari ya Kuu ya Dawa, Kamati imebaini changamoto ya mtaji, ambapo katika mwaka wa fedha 2022/23, ombi la mtaji liliwasilishwa kupitia Wizara ya Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Mtaji unaoombwa ni **Shilingi bilioni 561.5** kwa mchanganuo kuwa, **Shilingi bilioni 204** zinahitajika kuwezesha ununuzi wa bidhaa za Afya, **Shilingi bilioni 66.9** kwa ajili ya ujenzi wa Maghala, **Shilingi bilioni 100.46** kwa ajili ya ujenzi wa Viwanda na **Shilingi bilioni 191** kwa ajili ya malipo ya madeni ya washitiri na vituo vya kutolea huduma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, ikiwa kiasi hiki cha mtaji kitapatikana kitaiwezesha Bohari Kuu ya Dawa kununua mahitaji yote ya bidhaa za Afya bila kusubiri fedha za vituo vya kutolea huduma za Afya. Hivyo, ipo haja ya Serikali kutoa mtaji kwa Bohari Kuu ya Dawa ili kuleta ufanisi.

### 2.6.4 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**Mheshimiwa Spika**, Katika utekelezaji wa shughuli za Kamati imebainika uwepo wa changamoto inayokabili uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Changamoto hiyo imesababisha mvutano na kusuasua kwa ushirikiano kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Sekta Binafsi ya Afya. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto hizo zinasababishwa na mambo yafuatayo; -

a. Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura Namba 395 kutokutambua uwepo wa Sekta binafsi ya Afya kama mnufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;

b. Kutoruhusu vituo binafsi vya kutolea huduma za Afya kutumia mfumo wa kuchangia huduma za Afya *(Copayment)* kwa wanufaika wa NHIF, wakati mfumo huo unaruhusiwa kwa vituo vya kutolea huduma vya umma tu;

c. Kukosekana kwa chombo huru na cha kudumu kinachoratibu na kusimamia bei za huduma za Afya;

d. Kutokuzingatiwa kwa maoni ya Wadau wa Sekta ya Afya kuhusu kitita kipya cha bei za huduma za Afya.

**Mheshimiwa Spika**, Kufuatia changamoto hizo, Kamati inaona ipo haja ya Serikali kutafuta ufumbuzi kwa haraka ili wananchi ambao ni wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) waweze kuendelea kupata huduma za Afya bora katika vituo vya kutolea huduma za Afya wanavyopendelea.

### 2.6.5 Huduma za Matibabu ya Kibingwa na Ubingwa Bobezi

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Wizara ya Afya imeendelea kuimarisha kwa kiwango kikubwa uwekezaji katika utoaji na upatikanaji wa huduma za Afya nchini ikiwemo huduma za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa bobezi zinazotolewa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali maalumu za Kitaifa. Huduma hizo za matibabu ya Kibingwa na Ubingwa bobezi zinajumuisha uanzishaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu zinazolenga kusaidia na kuokoa maisha ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Uanzishaji wa huduma hii unawarahisishia wananchi wenye mahitaji kupata huduma hii ndani ya nchi ambapo gharama si kubwa ukilinganisha na gharama za kupata matibabu hayo nje ya nchi kama ilivyokuwa awali. Aidha, upatikanaji wa huduma hii utachangia kuongeza mapato ndani ya nchi kwa kuwa gharama za matibabu ambazo zingelipwa nje ya nchi sasa zitabaki ndani ya nchi. Vilevile, uanzishwaji wa huduma hii unachochea tiba utalii ambapo watu kutoka nchi nyingine hutembelea nchini kwa lengo la kupata matibabu jambo linalochangia kukua kwa tiba utalii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia umuhimu na faida za utolewaji wa huduma hizi nchini, ni muhimu sasa Serikali iimarishe na iweke mazingira mazuri ya utoaji na upatikanaji wa huduma kwa kuhakikisha kunakuwepo na Sheria zinazosimamia utoaji wa huduma ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa chembechembe na viungo vya mwili wa binadamu.

**2.6.6 Uwekezaji wa Viwanda vya Kuzalisha Bidhaa za Dawa**

**Mheshimiwa Spika,** Azma ya Serikali Kama ilivyotamkwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2020 – 2025 ni kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji/sekta binafsi kujenga viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba nchini. Kamati imebaini kuwepo kwa maendeleo makubwa yaliyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Afya ambapo sekta binafsi imewekeza kwa kiwango kikubwa kwa kuanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa ambavyo vimechochea upatikanaji wa bidhaa za dawa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya Serikali kuendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za dawa nchini bado kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazoathiri uzalishaji wa bidhaa hizo na uwekezaji kwa ujumla. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo; -

a) Bohari Kuu ya Dawa kuchelewesha malipo ya fedha kwa wazalishaji wa bidhaa za dawa;
b) Kuwepo kwa Mamlaka nyingi za udhibiti wa bidhaa za dawa na malighafi za kutengeneza bidhaa za dawa, kwa Mfano, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba TMDA, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania-TAEC,
Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa SerikaliGCLA, Bodi ya Sukari Tanzania-SBT, Shirika la Viwango Tanzania-TBS na Wakala wa Vipimo-WMA;
c) Uwepo wa utitiri wa kodi wakati wa uingizaji wa malighafi za kuzalisha bidhaa za dawa na baada ya kuzalisha bidhaa za dawa;
d) Kukosekana kwa masoko ya uhakika ndani ya nchi kutokana na ushindani mkubwa wa bidhaa za dawa kutoka nje ya nchi ambapo bidhaa hizo huuzwa kwa bei ya chini. Mfano bidhaa za dawa kutoka India na China; na
e) Kukosekana kwa nishati (umeme) ya uhakika viwandani jambo linalosababisha shughuli za uzalishaji kusimama kwa saa kadhaa.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuendelea kulinda wawekezaji wa ndani na kuboresha mazingira ambayo yatavutia wawekezaji wengi

zaidi, ni vema Serikali kutafuta ufumbuzi kwa haraka na kutatua changamoto zote zinazowakabili wawekezaji hao ili kuweza kuimarisha zaidi uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za dawa nchini.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/2025 kwa Wizara ya Afya (Fungu 52), sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara hii.

### 3.1 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2023/2024

Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza na kukamilisha miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2023/2024.

### 3.2 Uhaba wa Rasilimali Watu

Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya afya nchini iendelee kutoa vibali vya Ajira vinavyokidhi mahitaji halisi ya Hospitali na Taasisi zote za Afya ili kuwa na wataalam wa kutosha na kufanikisha upatikanaji na utoaji wa huduma bora za Afya.

### 3.3 Ufinyu wa Maeneo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa

Serikali ipanue maeneo ya Hospitali za Rufaa za Mikoa kwa ajili ya kuongeza miundombinu mipya katika Hospitali hizo ili kuimarisha utoaji wa huduma za Afya na kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi wanaohitaji huduma katika maeneo hayo.

### 3.4 Uboreshaji wa Huduma za Afya Hospitalini

Ili kuboresha huduma za Afya Hospitalini, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iboreshe vitengo vya huduma kwa wateja *(Customer Care Services)* katika Hospitali zote nchini; na

b) Serikali iboreshe vitengo vya TEHAMA katika Hospitali zote nchini ili kuimarisha matumizi ya Mifumo inayorahisha utoaji wa huduma za Afya kama vile Mifumo ya malipo na Mifumo ya taarifa za matibabu ya wagonjwa.

**3.5 Changamoto ya Uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

Ili kuboresha utendaji Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) pamoja na kuondoa mvutano uliopo baina ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Sekta Binafsi ya Afya, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali ianze mchakato wa kurekebisha Sheria ya NHIF, Sura Namba 395 ili kuitambua Sekta Binafsi ya Afya ambayo ni mdau muhimu wa Afya;

b) Serikali ilipe madeni yote inayodaiwa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kutokukwamisha shughuli za uendeshaji wa Mfuko huo;

c) Serikali ianzishe chombo huru mahsusi na cha kudumu kitakachoratibu na kusimamia bei za huduma za Afya *(Health Services Pricing Board)* ambacho kitajumuisha wajumbe kutoka sekta ya umma na sekta binafsi;

d) Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) iwezeshwe kisheria kwa kuwekewa Kanuni chini ya Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuipa mamlaka ya kudhibiti utoaji wa huduma za Bima ya Afya nchini;

e) Vituo binafsi vya kutolea huduma za Afya viruhusiwe kuwa na utaratibu wa mgonjwa kuchangia huduma *(co-payment)* ambapo wamiliki wa kadi za NHIF watatakiwa kulipa kwa pesa taslimu gharama zinazozidi kiwango cha kitita kinachochangiwa na NHIF;

f) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya uimarishe mifumo ya TEHAMA ili kukabiliana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo na kudhibiti udanganyifu;

g) Tathmini ya kina iendelee kufanyika kuhusu kitita kipya cha bei za huduma za Afya na kuhakikisha kitita kipya kinazingatia maoni na makubaliano ya Wadau wote wa Sekta ya Afya kutoka sekta ya umma na binafsi;

h) NHIF ianzishe Kamati ya wataalam ambao watakuwa wanapitia malalamiko ya kitaaluma yanayowasilishwa na vituo vya kutolea huduma au wataalam kuhusu Bima ya Afya *(Technical/Expert Review Committee)*; Vilevile Kamati hii ishughulikie madai yanayokataliwa kulipwa *(rejection)* kwa vituo vya kutolea huduma za Afya ili kupunguza malalamiko ya watoa huduma;

i) Serikali iunde Kamati maalum ya kitaalamu ya kupitisha na kutoa mwongozo wa aina za dawa, vifaa tiba na teknolojia za tiba *(Health Technology Assessment Committee)* zinazotakiwa kutumika katika utoaji wa huduma za Afya.

**3.6 Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote**

Kamati inaendelea kusisitiza kwamba, Serikali ikamilishe mchakato wa kufanya tathmini ya vyanzo na viwango vya fedha kwa ajili ya mfuko wa kugharamia watu wasio na uwezo kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

**3.7 Ucheleweshaji wa Malipo ya Fedha za Huduma za Afya kutoka kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ulipe kwa wakati madai ya fedha za huduma za Afya kwa vituo vya kutolea huduma za Afya vinavyoudai Mfuko huo ili kutokukwamisha utoaji wa huduma bora za Afya katika vituo hivyo.

**3.8 Ukosefu wa Mtaji Bohari Kuu ya Dawa (MSD)**

Serikali itoe mtaji wa **Shilingi bilioni 561.5** kwa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ili kuboresha upatikanaji wa bidhaa za Afya,

kusaidia uwekezaji kwenye viwanda na kuongeza uwezo wa kuhifadhi bidhaa za Afya kwa kujenga maghala ya kutosha.

**3.9 Uimarishaji wa Viwanda vya kuzalisha Bidhaa za Dawa**

Ili uwekezaji wa viwanda vya kuzalisha bidhaa za dawa uweze kuleta tija kwa watanzania, Kamati inashauri yafuatayo; -

a) Bohari Kuu ya Dawa (MSD) ilipe kwa wakati fedha inazodaiwa na viwanda vya uzalishaji wa bidhaa za dawa;
b) Serikali itoe msamaha wa kodi kwa malighafi zinazoingizwa nchini kwa ajili ya kuzalisha bidhaa za dawa;
c) Serikali iongeze kodi kwa bidhaa za dawa zinazotoka nje ya nchi ambazo zinazalishwa na viwanda vya ndani; na
d) Serikali ihakikishe upatikanaji wa nishati (umeme) ya uhakika hasa kwenye maeneo ya viwanda.

**3.10 Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe na Viungo vya Mwili wa Binadamu**

Serikali ikamilishe Utungaji wa Sheria ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa chembechembe na viungo vya binadamu ili kuweka namna nzuri ya utoaji wa huduma hii kwa wananchi.

**3.11 Usajili wa Vituo vya kutolea huduma za Afya**

Serikali iunde bodi moja ya usajili wa vituo vya kutolea huduma za Afya nchini. Hatua hii itaweka ulazima wa vituo vya kutolea huduma za Afya vinavyomilikiwa na Serikali kusajiliwa na kukidhi vigezo kabla ya kuanza kutoa huduma.

**3.12 Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika huduma za Afya *(Public Private Partnership – PPP)***

Serikali iimarishe usimamizi na ifanye mapitio ya mikataba ya utoaji wa huduma za Afya baina yake na Taasisi zisizo za kiserikali zinazotoa huduma za Afya ili kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina yake na Taasisi hizo.

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu. Vilevile, napenda kukupongeza kwa namna unavyoliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa. Aidha, namshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Utekelezaji mzuri wa majukumu yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee nawashukuru sana Mheshimiwa Ummy Ally Mwalimu (Mb)-Waziri wa Afya pamoja na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel (Mb)-Naibu Waziri wa Afya kwa ushirikiano wanaoipa Kamati wakati wote. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu, Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Maghembe na Mganga Mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Joseph Nagu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano mkubwa ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati inapotekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kipekee nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI pamoja na Mheshimiwa Dkt. Faustin Engelbert Ndugulile, (Mb)-Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa wakati wote wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Wajumbe hawa wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina wa masuala mbalimbali ambayo yamesaidia sana katika uandishi wa Taarifa hii. Nawapongeza sana na naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mb - **M/MKITI**
3. Mhe. Aysharose Ndogholi Mattembe, Mb Mjumbe
4. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb “
5. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb “
6. Mhe. Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mb “
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb “

8. Mhe. Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb "
9. Mhe. Elibariki Emmanuel Kingu, Mb "
10. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb "
11. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb "
12. Mhe. Hassan Seleman Mtenga, Mb "
13. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb "
14. Mhe. Juliana Daniel Shonza, Mb "
15. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb "
16. Mhe. Mohamed Lujuo Monni, Mb "
17. Mhe. Mrisho Mashaka Gambo, Mb "
18. Mhe. Seif Salum Seif, Mb "
19. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb "
20. Mhe. Zubeida Khamis Shaib, Mb "
21. Mhe. Agness Mathew Marwa, Mb "
22. Mhe. Jacquiline Andrew Kainja, Mb "

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge Ndugu. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vyema na kuhakikisha shughuli zote za Kamati zinatekelezwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika, Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya (Fungu 52) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kiasi cha Shilingi 1,311,837,466,000.00 kama yalivyoombwa na mtoa hoja.**

**Mheshimiwa Spika, Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.**

Stanslaus H. Nyongo (Mb),
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI**
13 Mei, 2024

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuwasilisha maoni hayo ya Kamati, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni wengine walioingia hapa ndani, nasubiri orodha ya wageni nikiletewa hapa nitawatangaza; lakini sasa tuendelee na utaratibu wetu. Baada ya kumsikia Mwenyekiti na kumsikia Mheshimiwa Waziri wako Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii. Wapo Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii. Majina ya wageni yamefika sasa nitawatangaza.

Wapo wageni wengine wa Waziri wa Afya Mheshimiwa Ummy Mwalimu, hawa ni Kamati ya *Odo Ummy Cup* wakiongozwa na Mwenyekiti wapo ndugu Abdalah Mapikipiki, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo viongozi kutoka Chama cha Wataalam wa Maabara wakiongozwa na Yahaya Munung'a ambaye ni Rais wa Chama cha Melsat, karibuni sana.

Taasisi ya *Lukiza Autism* wakiongozwa na Hilda Nkabe mwanzilishi na mtendaji wa taasisi hiyo, waganga wafawidhi hospitali za rufaa za mikoa; yuko wapi anayetoka Mbeya hapo, hebu simama, eeh lazima, anafanya kazi nzuri sana. Hao wengine ndio hawajapata hiyo fursa, ndiyo muhimu sana. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Madaktari Bingwa wanaotoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi katika mikoa na halmashauri wakiongozwa na Dkt. Caroline Damiani. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mabalozi wa Afua za mazoezi katika kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambikiza wakiongozwa na ndugu Selemani Mathew. Wadau wa Maendeleo ya Wizara ya Afya, karibuni sana Bungeni.

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo, wanafunzi 50 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari Kikombo ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge baada ya tangazo hilo na kwa maneno aliyosema Dkt. Kunti hapa, maana leo humu ndani kila

mtu ni dakatari. Kwa maneno ya Dkt. Kunti, Dkt Mbwanji hebu simama kidogo watu wengine hawakuji. Jamani huyu ndiyo Mkurugenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu kusini, anafanya kazi nzuri sana. Sasa, siyo kwamba wengine hawafanyi kazi nzuri, wote wanafanya kazi nzuri lakini kwa sababu huyu anafanya huku ambako nafanya naye kwa karibu, kwa hiyo, naona kazi yake kwa haraka zaidi. Kwa hivyo, yeye anatoa ushirikiano mzuri sana kwa Mganga wetu Mkuu wa…ndiyo Hospitali zote hizo ziko Mbeya Mjini, tuko vizuri.

Waheshimiwa Wabunge wachangiaji ambao wameomba nafasi za kuchangia asubuhi hii tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, atafuatiwa na Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, ajiandae.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini katika sekta ya afya. Nipongeze sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa kwa sababu kuna vigezo ambavyo tunavitumia kuangalia ubora wa huduma za afya na niseme tu kwamba Tanzania tuko vizuri, ukiangalia katika suala la chanjo tuko zaidi ya asilimia 95, ukiangalia maambukizi ya UKIMWI, *TB* na Malaria nayo yameshuka kwa kiwango kikubwa, vifo vya akina mama vimepungua kutoka 556 kwa vizazi hai 100,000 mpaka 104, haya ni mafanikio makubwa sana, pia tumeona vifo vya Watoto chini ya miaka mitano navyo vimepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile mapinduzi makubwa katika huduma za kibingwa, tumeona kwamba sasa hivi Watanzania wengi waliokuwa wanakwenda kupata matibabu ya nje ya nchi, sasa hivi kwa kiwango kikubwa matibabu yanapatikana hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili sasa hivi dunia inaongelea suala la afya kwa wananchi wote *(Universal Health Coverage)* na *Universal Health Coverage* ina maeneo makubwa matatu:-

(i) Inaangalia wigo wa utoaji wa huduma *(Access)*

(ii) Inaangalia suala la ubora wa huduma

(iii) Uwezo wa wananchi kuhgharamia matibabu.

Mheshimiwa Spika, katika hili napenda tena kuipongeza Serikali kwa uwekezaji mkubwa wa kuongeza wigo wa utoaji wa huduma za afya. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wameonesha kwa kiasi kikubwa kwamba, tumeweza kuongeza vituo vingi vya utoaji wa huduma za afya. Sambamba na hilo, tumeweza kuanzisha Sheria ya Bima ya Afya kwa wananchi wote ambalo ni jambo kubwa sana. Jambo la mwisho ambalo ni la kufanyia kazi ni suala la kuboresha hizi huduma za afya ili lile jambo lote liweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, mimi leo nitatoa ushauri tu na nitajikita katika baadhi ya maeneo ambayo nafikiri ni vizuri twende tukayawekee msisitizo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni suala la Bima ya Afya, tumepitisha Sheria lakini mimi nilitaka nishauri. Pamoja na ushauri wa Kamati ambao mimi ninauunga mkono kwa asilimia 100, nilitaka kuongeza ushauri mwingine wa ziada;

(i) Kabla hatuja-*rollout* Bima ya Afya kwa wananchi wote ni muhimu sana tukawekeza katika elimu kwa jamii ili wananchi waelewe nini maana ya bima. Wengine tunahisi kwamba Bima ni hela ambayo umeiweka wewe ukiugua, wanaanza kutafuta kadi ya bima na kutaka kuchangia pale ambapo amekwishaugua. Kwa hiyo, hiyo elimu tuitoe kwenye jamii waielewe ili tuweze kuhamasisha wananchi waweze kujitokeza;

(ii) Nataka nishauri kwamba, wakati wa utekelezaji tufanye kwa awamu ili sasa tukae tupime na tuangalie utekelezaji. Halafu tunakwenda ka awamu tunaweza tukaifanya kwa makundi ama kuangalia

kwa mikoa, mtakaa mtaangalia ni jinsi gani ya kuweza kufanya hivyo. lakini yale mengine ambayo yalikuwa yameshauriwa na Kamati ninayaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo sikuona limeongelewa na mimi nitaendelea kulisema ni suala la lishe na usalama wa chakula. Bado kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba taasisi inayosimamia masuala ya lishe na ukizingatia tatizo kubwa la udumavu na lishe iliyopitiliza nchini, bado kuna umuhimu wa kuwa na chombo chini ya Wizara ya Afya ambacho kitasimamia masuala ya lishe, inawezekana lisiwe Shirika lakini inaweza ikawa mamlaka, taasisi iliyoko chini ya Wizara ya Afya.. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili bado tunaendelea kusisitiza umuhimu wa jukumu la usalama na ubora wa chakula kuwa chini ya Wizara ya Afya badala ya kuwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, ni jambo ambalo Serikali muendelee kulifanyia kazi ili jambo hili liweze kurudishwa kwenye maeneo ambayo ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo nilitaka nichangie, Mheshimiwa Waziri ameongea hapa, ongezeko kubwa la magonjwa yasiyoambukiza na mimi hili Waheshimiwa Wabunge nitaomba mtuelewe kidogo. Mheshimiwa Waziri ametoa takwimu ya idadi ya wagonjwa ambao wanakwenda hospitalini, mimi nataka tuliangalie katika sura nyingine; endapo wagonjwa hawa wengi ambao wanakwenda hospitalini ni wagonjwa wa magonjwa ambayo yasiyoambukiza, maana yake ni kwamba sisi kama nchi sasa hivi tuna *crisis*. Kwa sababu tumeweza kufanya kazi kubwa ya kudhibiti magonjwa ambayo ni ya kuambukiza na mtu ambaye anaumwa Malaria ukimtibu leo hutomuona tena kwenye mfumo. Lakini mtu mwenye kisukari, presha, ugonjwa wa figo, huyu mtu akiingia katika mfumo wa afya ni mgonjwa wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu sasa tukajaribu kuangalia afya yetu, badala ya kuwa ni afya ya tiba iwe ni afya

ya kinga zaidi kuliko afya ya tiba. Kwa hiyo, nashukuru mwelekeio huo Wizara mmeanza kuuona na mimi nawapongezeni sana. Sasa nini tunahitaji kukifanya? Ukiangalia mtiririko afya ina misingi mikubwa minne; kuna elimu ya afya *(Health promotion),* elimu ya afya ya kinga *(Health prevention),* tiba na Kuna huduma za *rehabilitation* (huduma za utengamao).

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu kama nchi tumekuwa tukiwekeza sana kwenye afya ya tiba, sasa kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba tunawakinga zaidi na kutoa elimu zaidi ya kuhakikisha kwamba Watanzania hawaendi hospitalini, hiyo ndiyo itakuwa mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kukiongezea ni kwamba, tumeanzisha sasa programu ya magonjwa yasiyoambukiza, tunafanya vizuri. Hata hivyo, huduma hizi hazijashuka katika afya ngazi ya msingi, Mheshimiwa Waziri, umetoka kusema asilimia zaidi ya 73 ya wagonjwa wanaonwa katika ngazi ya msingi. Kule katika afya ya msingi mnatakiwa kuhakikisha kwamba *BP machine* zinapatikana, vipimia sukari vinapatikana na tunawajengea uwezo wale watoa huduma katika ngazi ya msingi kuweza kuwabaini wagonjwa wa magonjwa yasiyoambukiza na kuanza kupata matibabu ya awali.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna mgonjwa anatoka Kigamboni anakwenda Muhimbili kliniki kupata dawa. Kwa hiyo, hili nadhani ni muhimu sana tukashusha huduma hizi katika ngazi ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele imegonga nimalizie kwa haraka haraka. Jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuishauri Wizara ni kwamba, sekta imepanuka sana na kuna kada nyingi. Mheshimiwa Waziri umetoka kuongea kwamba kuna suala la wataalam tibalishe, umeongelea suala la manesi wa afya ya akili, kuna watu ambao kazi yao ni *perfusionist*, *intensivist*, hawa watu siyo madakatari, siyo wafamasia na wengine siyo wataalamu wa afya ya kinywa. Kuna umuhimu sasa kuwa na kada maalum na tukatengeneza muundo ambao utaweza kukaa na ku-accommodate watu hawa wote.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nilitaka kuligusia ni kwamba, sasa hivi tunafanya kazi nzuri sana ya kuhakikisha tunafanya upandikizaji wa viungo. Hata hivyo, tunahitaji tuwe na Sheria ya uvunaji, utunzaji na upandikizaji wa viungo vya binadamu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa kwa sababu tunafikia mwisho, kabla sijagongewa kengele, tuna tatizo kubwa sana la usugu wa madawa, sasa hivi dawa zinauzwa holela sana, *typhoid* zinatibiwa kiholela sana, *UTI* zinatibiwa kiholela sana na *P2* sasa hivi zinakuwa kama *Panadol*. Sasa, ni muhimu sana kuhakikisha tunaweka mifumo ya kudhibiti matumizi ya dawa *especially antibiotic* ambapo sasa hivi tumekuwa na hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, *otherwise* naipongeza sana Wizara kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kufanya, ni kazi nzuri na kwa kweli *indicator* zetu ni za kusifika katika Bara la Afrika na Dunia. Kwa hiyo, nataka kuipongeza Wizara ya Afya kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nimeletewa taarifa hapa kwamba, hawa Madaktari bingwa wanaotoa huduma za Kibingwa na ubingwa bobezi katika mikoa na Halmashauri akiongozwa na Dkt. Caroline Damian ndiyo ninyi wenye makoti meupe? Hebu msimame.

Sawa, sasa nimeletewa taarifa za ziada kwamba hawa wanazunguka nchi nzima kwa ajili ya kutoa zile huduma zinazohitajika kwenye kila Halmashauri ama Hospitali ya Mkoa, kama ni upasuaji au vipimo wanafanya, kwa hiyo, tunawashukuru sana kwa kazi nzuri. Pamoja na hayo nimeambiwa kwa ujumla wao wanaitwa Madaktari wa Dkt. Samia, kwa hiyo, ahsanteni sana kwa kazi nzuri tunawashukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimekwishamtaja Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mheshimiwa Esther Lukago Midimu ajiandae. Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, yupo au ametoka kidogo? Haya Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, atafuatiwa na Mheshimiwa

Esther Lukago Midimu, Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila, ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya. Pia, nimshukuru kwa wakati huu kuwa mzima na sasa nimesimama katika Bunge hili Tukufu kuzungumzia suala la Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru Mheshimiwa Ummy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri wake. Viongozi wetu hawa wanafanya kazi kubwa. pia, kama alivyozungumza hapo Mheshimiwa Ummy kwamba Naibu Waziri wake na ana imani kweli, ni kweli ana imani n ani mchapakazi. Vilevile, anapopewa kazi huwa anaifanya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ninaendelea kuzungumza suala langu la kuwajengea uwezo wagonjwa wa Saratani wa hii nchi nzima nikizungumzia kuanzia hapa Tanzania hadi visiwani. Kuna ugonjwa huu wa saratani umeenea sana, kama tunavyozungumza ugonjwa wa saratani ukiugundua mapema basi unapoa mapema. Lakini ugonjwa wa saratani ukikaa mpaka ukaja ukagundulika kwamba wewe una ugonjwa wa saratani, mwisho wa habari unakwenda na maji.

Mheshimiwa Spika, kuna hii nadhia iliyojitokeza sasa hivi kwa upande wetu wa Zanzibar, kuna suala la mgonjwa wa saratani akionekana ili kuletwa *Ocean Road* basi ataanzia kwanza hospitali ya Muhimbili. Sasa hivi ni lazima kuna kigezo cha barua kutoka Zanzibar ije huku Tanzania Bara ipokelewe ndipo aweze kutibiwa yule mgonjwa.

Mheshimiwa Spika, mgonjwa yule anayetoka Zanzibar kuja huku, kuna wengine hawana barua, pia hili suala halijatambulika kwa dhati kwamba, mgonjwa wa saratani kutoka Zanzibar basi awe na barua, maana wengine wanatoka kule vijijini moja kwa moja kuja Bara, wale wanakuwa hawana barua. Pia, kama takuwan a Barua ataambiwa kuwa barua ile imekwisha-*expire*. Sasa mgonjwa yule anakaa hatibiwi na anakuwa anaumia.

Mheshimiwa Spika, mpaka ianze *process* mpya kutoka pale iende Zanzibar halafu ndipo ile barua itumike ili mgonjwa yule atibiwe. Kweli yule mgonjwa atapona? Haponi. Kwa hiyo, naomba Mawaziri wangu wa Afya hili suala mlichukulie uzito kwamba, mgonjwa akitoka kule Zanzibar kuja kutibiwa huku Bara basi mumchukulie kuwa huyu mgonjwa ni dhaifu, hana Kitu, mumtibu ili awe mzima.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mollel, alikuja mgonjwa na ukaitwa ukaja *Ocean Road* na ukawaambia madaktari kwamba yule mgonjwa wamtibu. Kama siyo wewe huyu mgonjwa angefariki, nakushukuru sana kwa jitihada yako hii uliyoichukua mpaka mgonjwa yule akatibiwa na kufikia kurudi nyumbani lakini baadaye mgonjwa alifariki *Inna Lillahi wa Inna Ilayhi Raji'un*. Mwenyezi Mungu hakumhitaji sana, ndiyo yale niyoyasema, ulikwenda na ukawaambia wamtibu yule mgonjwa bila matatizo yoyote. Kwa bahati nzuri yule mgonjwa ni mheshimiwa ukamwambia kwamba, wewe ukitaka kutibiwa haraka jilipue. Haya Mheshimiwa ajilipue? Asiyekuwa Mheshimiwa si ndiyo atadhalilika huyo? Anakuwa hapati matibabu tena atadhalilika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mawazirio wangu nyote wawili Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Mollel, nawaomba hili suala lichukuliwe kwa kina ili liwezekane na lifanyiwe kazi kwa hawa wagonjwa wetu wa saratani kutoka Zanzibar kuja huku Tanzania.

Mheshimiwa Spika, suala langu la pili nalizungumzia, kuna hawa madaktari wanaokuwepo kule mahospitalini, hatutaki hili ninalosema sitaki kwamba wale madaktari wasiende kula kwa sababu hii ndiyo afya ya akili inamuingia, kama hakula huyu mgonjwa atakuwa hana afya ya akili. Lakini akienda kula akijua kwamba huku nina wagonjwa wamenisimamia na wanataka kutibiwa, kuliko kujisahau kwenda kunywa chai masaa mawili huku anasubiriwa na mgonjwa aje kumtibu, daktari bado anakunywa chai, chai gani hiyo?

Mheshimiwa Spika, anywe chai robo saa na ajue kuwa huku ninatakiwa nirudi niende nikatibu wagonjwa na hili suala lipo na mlichukulie hatua. Mnafanya kazi nzuri sana, Mheshimiwa Ummy,

hotuba yako umeitoa kwa kina na haina mjadala, hotuba nzuri na ina mambo kadhaa ambayo inatutetea mpaka sisi wagonjwa wa sukari tulioko humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mgonjwa sukari unaambiwa asifurahi, asishereke sana, pale pale inapanda sukari na tayari ugonjwa umekwishamuingia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ummy, nakuomba hili suala mlizingatie kwa kina hawa madaktari wetu wanywe chai kwa kiasi ili warudi waje wahudumie wagonjwa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala langu la tatu ninalozungumzia ni kuhusu Mjamzito na mwenza wake, hili suala bado liko nyuma. “Mume wangu nimekwishakuwa mjamzito nataka unipeleke hospitali niende nikapime, anakwambia wewe nenda tu mimi nitakuja baadaye. Au mwingine anasema amimi nahusika na nini mambo hayo ya kwamba wewe nikuchukue uende ukapime mimi nikusubiri pale? Hapana, mimi unanipotezea muda wangu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala nakuomba Mheshimiwa Waziri, ni lazima hawa watu wapatiwe mafunzo, hasa wanaume, kwa maana wao ndiyo wanaofanya kile kitendo mpaka mtu akabeba ile mimba. Ni kwa nini hataki kuchanganyika na mwenzie wakaenda kule wakapima pamoja? Kwa nini hataki kuchanganyika na mwenziwe wakaenda zao hospitali akamsubiri mkewe akajifungua? Yeye akamchukua mtoto akambeba, kwa nini hawataki? Mheshimiwa Ummy suala hili lipo kwa hiyo, lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa na mambo yangu haya matatu muhimu niliyotaka kukwambia. Mheshimiwa Waziri ninakusifu sana pamoja na Naibu Waziri wako mnafanya kazi kubwa usiku na mchana. Hakuna mfano wa kiasi cha hii kazi mnayoifanya Tanzania nzima, mpaka Zanzibar mnakuja kutusaidia, kule Mnazi Mmoja. Kiko Kitengo maalum, hawa watoto wangu waliokuja hapa hawa wanakuja mpaka Zanzibar kutufahamisha kuhusu masuala haya. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili suala mlipe uzito wa kulichukua, ili hawa wanaume wafuatane na wake zao wanapokuwa wajawazito waende wakapime. Sina mjadala, naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso ajiandae.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa naanza kukupongeza, unafanya kazi nzuri sana, unatulea vizuri sana, wewe ni Spika wa kiwango. Una mapenzi makubwa na Wabunge wako hata sisi wote tunakupenda. Nawaomba Wana-Mbeya wakurudishe tena Bungeni, ili tuje tukupatie tena Uspika. Umeiheshimisha Mbeya na Tanzania nzima umeiheshimisha, wewe ni Rais wa *IPU*, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni, ninampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya. Mnafanya kazi nzuri. Mheshimiwa Ummy, hotuba yako imesheheni matumaini ya Watanzania, ninaomba uisimamie mtani wangu nina imani wewe ni mchapakazi. Mheshimiwa Ummy umekutana na misukosuko ya kila aina, iliingia ebola ukaidhibiti, dengua ukaidhibiti, ikaingia *corona,* sisi tulikuwa tunaogopa, lakini wewe ulikuwa unaenda kuona wagonjwa. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuipongeza Serikali kwa kupunguza vifo vya mama na watoto kwa 80%. Hongera Mheshimiwa Rais umefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha Hospitali ya Muhimbili, inafanya upasuaji wa kichwa, upasuaji wa moyo, upandikizaji wa figo na upandikizaji wa uroto, hata wagonjwa kutoka nje ya nchi wanakuja kutibiwa hapa. Mheshimiwa Rais umefanya kazi nzuri, umewapunguzia Watanzania gharama za kwenda nje, ubarikiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuboresha Hospitali ya Bugando. Kama unakumbuka Wabunge wa Kanda ya Ziwa tulisimama hapa tukaiomba Serikali iboreshe hospitali ya Bugando, wagonjwa wa kansa watibiwe pale kwa vile wagonjwa wengi wanatoka Kanda ya Ziwa. Mheshimiwa Rais alisikia kilio chetu, hospitali imeshaboreshwa, wagonjwa wanapata matibabu mapema katika hospitali ya Bugando. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naendelea kushukuru kwa kuunda timu ya kufanya utafiti, ili kujua ugonjwa wa kansa unasababishwa na nini Kanda ya Ziwa. Naipongeza Serikali kwa kuimarisha upatikanaji wa dawa kutoka asilimia 58 mpaka asilimia 79. Mheshimiwa Rais umefanya kazi nzuri sana, sasa hivi dawa zinapatikana kwenye hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naenda Mkoani kwangu Simiyu. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha za kujenga hospitali ya mkoa, namshukuru sana. Pia, ametupatia zaidi ya shilingi bilioni saba, kwa ajili ya kujenga majengo manne. Jengo la Mama na Mtoto, Jengo la Mochwari, Jengo la Kusafishia Vifaa na Jengo la Kufulia. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Simiyu haina wodi za kulaza wagonjwa. Juzi nilisimama hapa nikauliza swali, Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu vizuri kwamba, Serikali imetenga shilingi bilioni mbili za ujenzi wa wodi katika Hospitali ya Mkoa wa Simiyu. Naiomba Serikali ipeleke mapema zile pesa, ili tukaweze kujenga wodi za kulaza wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, hospitali yetu ya mkoa haina uzio. Mwaka jana nilisimama hapa nikasema hospitali haina uzio, hospitali ikikosa uzio ni hatari sana, hata utoroshwaji wa dawa na kuibiwa vifaa tiba inakuwa ni rahisi sana. Vilevile tuna upungufu wa watumishi katika hospitali yetu ya Mkoa wa Simiyu. Watumishi waliopo ni 231, upungufu ni watumishi 437. *Specialist* waliopo ni wa nne tu, upungufu ni *specialist* 21. Upungufu wa wauguzi 102, waliopo ni 97. Kuna upungufu wa madaktari 27 pamoja na

wafamasia 12. Tunaiomba Serikali ituletee madaktari wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapohapo ninawapongeza madaktari wote nchi nzima, wanafanya kazi nzuri, wanaokoa maisha yetu. Ninawapongeza Madaktari wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wanaozunguka nchi nzima kututibu. Ninawashukuru sana, wanaokoa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaendelea hospitali ya Mkoa. Tuna kipimo kikubwa cha *CT scan*. Mpiga picha yupo, lakini mtaalam wa kusoma yale majibu hayupo, majibu yanapelekwa Mwanza ndiyo yarudi Simiyu. Tunaomba mtaalam wa kusoma majibu ya kipimo cha *CT scan*.

Mheshimiwa Spika, tuna Hospitali Teule ya Somanda, Bariadi Mjini. Hospitali hiyo hata mwaka jana nilisimama hapa nikasema majengo yamechakaa, ni hospitali ya muda mrefu, ilipandishwa hadhi ikawa hospitali ya mkoa. Mheshimiwa Ummy ni msikivu sana ametupatia shilingi milioni 900 na hiyo hospitali inafanyiwa ukarabati sasa hivi. Kama haitoshi tukaletewa shilingi milioni 900 nyingine tukajenga jengo la maabara, jengo la *theatre* na jengo la *OPD*. Mheshimiwa Ummy mtani wangu, hiyo hospitali haina jengo la dharura, nakuomba sana utupatie pesa tuweze kujenga. Mgonjwa akija amezidiwa anachanganywa na wagonjwa wa kawaida, sasa mgonjwa wa kawaida akimuona mgonjwa aliyezidiwa na yeye presha inapanda. Tunaomba utupatie pesa, ili tuweze kujenga jengo la dharula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, hospitali hiyo ina Madaktari wanne tu. Tunaomba utupatie Madaktari Bingwa kama ulivyosema kwamba, hata Simiyu wanahitajika Madaktari Bingwa. Mheshimiwa Ummy, tunaomba Daktari Bingwa *(Specialist)* wa Wanawake na Watoto, tunakushukuru kwa jitihada zako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imetuahidi muda mrefu kutujengea kiwanda cha vifaa-tiba katika Mkoa wa Simiyu. Mpaka sasa hakuna kinachoendelea. Tunaiomba Serikali itenge fedha, iipatie bohari ya dawa, ili iweze kujenga kiwanda cha

vifaa-tiba katika Mkoa wa Simiyu kwa sababu, uzalishaji wa pamba mwingi unatoka Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nimtie moyo Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mama yetu kipenzi unapendwa, narudia tena, unapendwa na wananchi wako. Mheshimiwa Rais chapa kazi, hata sisi Wabunge wako wote tunakupenda, wawe Wabunge wa CCM, wawe Wabunge wa upinzani. Siyo kwamba, tunakupenda kwa vile wewe ni mwanamke tu, Mheshimiwa Rais tunakupenda kwa vile unafanya kazi nzuri. Kura utakazozipata ni za mafuriko, haijawahi tokea; tunakushukuru kwa kufanya kazi kubwa, jina lako litaandikwa kwa wino wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana Mheshimiwa Rais ajengewe mnara kwa vile amefanya kazi nzuri haijawahi kutokea na ni mwanamke wa kwanza kuwa Rais, *East Africa*. Hongera sana Mheshimiwa Rais, Mungu akubariki, tuko pamoja na wewe, tuko bega kwa bega, tutachapa kazi. Sisi wanawake tunaringia mama yetu, Mama Mary Chatanda na Mama Shomari, wanafanya kazi nzuri sana, UWT kwa ujumla inafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mary Chatanda amezunguka nchi nzima pamoja na timu yake, anachapa kazi. Hongera sana Mama Chatanda na timu yako, Mungu akubariki sana mama yangu, ahsante. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Gerald Mwandabila atafuatiwa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kutia mchango wangu katika Wizara hii muhimu, kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu la Tanzania. Tunatambua Wizara ya Afya ni Wizara ambayo kwa kweli, Watanzania tunaitegemea sana kwa sababu, tunajua tukiwa na afya nzuri ndipo tunaweza tukafanya kazi nyingi za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi naungana na wenzangu ambao wameendelea kukupa pongezi nyingi kama kiongozi wetu mkuu wa Bunge kwa namna ambavyo umekuwa ukiendelea kufanya kazi kwa weledi mkubwa. Sisi kama watu wa kutoka Nyanda za Juu Kusini tunajivunia sana wewe kwa sababu, unatuwakilisha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha naendelea kuwapongeza Wizara ya Afya kwa namna ambavyo wamekuwa wakiendelea kumuakilisha Mheshimiwa Rais vizuri. Mheshimiwa Ummy na Mheshimiwa Mollel wanafanya kazi nzuri kwa kweli, tunajisikia faraja wanapokuwa wanatusikiliza tunapopeleka maombi yetu kwao. Kwa hili kwa kweli, wanamtendea haki Mheshimiwa Rais, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na mchango ambao nimekusudia, naomba niwasilishe maombi yangu maalum kwa Mheshimiwa Waziri, kwa ajili ya watu wangu wa Mkoa wa Songwe. Namuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie tuweze kupata fedha za kujenga Kituo cha Afya Kamsamba. Hiki ni kituo cha muhimu ambacho kinahudumia watu wengi, kimechoka na kwa kweli, kinahitaji maboresho ya kina, ukitupatia fedha utakuwa ametusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naomba niwasilishe ombi langu kwa watu wa Kata ya Chilulumo, Wilaya ya Momba, wamesema wanaomba Mheshimiwa Waziri uwapatie kituo cha afya, zahanati imekuwa haiwezi kuwatosheleza kwa sasa, kata ni kubwa. Pia, niweze kukuomba kipekee kabisa, pale Kata ya Makambini sisi tuliomba kituo cha afya, lakini ajabu na kweli zinakuja fedha, kwa ajili ya kuweka kambi maalum ya magonjwa ya mlipuko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mji wa Tunduma, pale Kata ya Makambini, ni katikati kabisa ya mji ambapo kuna watu wengi. Sasa, kinapojengwa kituo cha magonjwa ya mlipuko sisi kama wana-Tunduma tunaona siyo sehemu sahihi ya kujenga kambi ya magonjwa ya mlipuko. Ombi letu lilikuwa ni kituo cha afya au zahanati, kama ikishindikana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba pabadilishwe, badala ya kutujengea hiyo kambi ya magonjwa ya mlipuko mtusaidie tupate kituo cha afya na kambi ya magonjwa ya mlipuko ipelekwe sehemu ambayo iko *isolated* na jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, tunamuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata fedha ya kumalizia maboma haya kwa sababu, yamekaa muda mrefu. Kuna Zahanati ya Sampanda, Ileje, kuna zahanati ya Shiwinga, Mbozi, Mheshimiwa Waziri tusaidie, tunajua ukitupatia shilingi milioni 50, zitakuwa zimetusogeza na vituo hivi vitaanza kufanya kazi. Sina mashaka na wewe dada yangu Mheshimiwa Ummy katika utekelezaji wa ahadi mbalimbali ambazo unakuwa umezitoa kwetu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kutuma maombi yangu hayo kwa Mheshimiwa Waziri, naomba nijikite kwenye mchango ambao nimeudhamiria kwa leo. Tunafahamu kabisa Wizara ya Afya imekuwa na mkakati kabambe wa kujenga vituo vya afya vingi sana kwenye maeneo yetu. Sisi wana-Songwe ni mashahidi wa kuona vituo vya afya ambavyo vimejengwa na kituo kimojawapo naweza kusema ni Mkulwe. Pia, tumeboreshewa Kituo cha Afya Tunduma, Kata ya Mwakakati kuna vituo vinajengwa, kiukweli tunaona viko vingi. Hoja yangu inakuja wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vituo hivi vinajengwa vinakamilika, lakini vinachelewa kutumika kwa wakati. Tunomba Mheshimiwa Waziri, kama ataweza, atusaidie kuhamasisha au kufanya mkakati wa ziada hivi vituo vinavyokuwa vimejengwa, basi vifunguliwe na vianze kufanya kazi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, nataka niongelee kitu kimoja kuhusiana na utoaji wa dawa, vifaatiba na vitendanishi kwenye

maeneo yetu. Tunajua kabisa zahanati ndio eneo ambalo mwananchi kwa haraka anaweza akafika. Ndio tunaona hapa kwenye utoaji wa dawa, upatikanaji wa dawa kwenye zahanati, bado upo chini. Tunawapongeza kwa sababu wametoka kwenye 52% wamekuja kwenye 71%. Tunajaribu kuwaza ni wapi ambapo wanakuwa wanafeli kwa sababu, fedha wanazopeleka *MSD* ni nyingi.

Mheshimiwa Spika, kulingana na Ripoti ya *CAG* ambayo imetoka hivi karibuni ineonesha kwamba, Serikali za Mitaa zililipa shilingi bilioni 3.05 kwa *MSD*. Vitendanishi na vifaatiba vilivyopelekwa vilikuwa ni vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.78. Kwa hiyo, unaweza ukaona kuna *gap* la hela ambayo inakuwa ina-*hang* haijulikani iko wapi. Mimi naamini kama kweli, vifaa vingekuwa vinapelekwa kulingana na thamani ya fedha zinazolipwa *MSD* hili *gap* lisingekuwepo. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kufuatilia fedha zetu, ili Serikali za Mitaa zinapokuwa zinaenda *MSD* ziweze kulipwa kwa thamani ya vifaa vile ambavyo tunakuwa tumevihitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine hapo hapo tunaona kwamba, Serikali ilitoa ruzuku ya kutupatia vifaatiba na dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 11.91. Ruzuku hii haikuweza kutumika ambapo *MSD* walipeleka vifaa venye thamani ya shilingi bilioni 3.6. Sasa, sisi kama wananchi tunaona dhamira ya Serikali kwa wananchi wake ni njema kwa kutoa hela karibu shilingi bilioni 12, halafu *MSD* hawatuletei hivyo vifaa. Sasa tunashindwa kuelewa kwamba, hii ni dhamira ya wazi ya *MSD* kutuumiza wananchi au ni fedha hazikwenda, zimeishia *somewhere?*

Mheshimiwa Spika, tunashindwa kuelewa. Hili pia, natamani Mheshimiwa Waziri atusaidie kuwafuatilia hawa watu. Fedha za ruzuku zinapotoka zije zifanye kazi husika kwa wakati husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niongee kwenye kipengele cha masuala ya dawa za kulevya. Katika bajeti ya mwaka jana niliomba kwamba, waweze kuweka waratibu wa dawa za Kulevya katika ngazi za halmashauri. Tuna waratibu wa

malaria, *TB* na ukoma; sasa nashindwa kuelewa kwamba, ukoma unaweza ukawa na nguvu kuliko dawa za kulevya? Jinsi ambavyo watoto wetu wanaharibika kwa kiwango hicho? Kwa hiyo, natamani pia, Mheshimiwa Waziri aweze kuliona hili kwa uzito wake, atupatie waratibu wa dawa za kulevya kwenye ngazi za halmashauri, ili waweze kufuatilia haya mambo kwa ukaribu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, *okay* nashukuru ila naomba Suala la *TFNC* walitazame kwa uzuri. Ni bodi ambayo kama maafisa lishe tunaihitaji sana, ahsante na naunga hoja...

**SPIKA:** Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, tutamalizia na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji. Awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuleta fedha nyingi za maendeleo kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Mkoa wa Katavi umepewa fedha za maendeleo kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi. Mheshimiwa Rais ametoa fedha ambazo zimeifanya sasa Hospitali ya Mkoa ianze kufanya kazi, lakini zipo changamoto ambazo zipo kwenye Hospitali ya Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, hospitali hii haina *fence* na bado majengo ambayo yamejengwa hayajakamilika yote. Nilikuwa naiomba Serikali iweze kukamilisha ujenzi wa hospitali ili iweze kutoa huduma kwa wananchi ambao wana matumaini makubwa kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Rais ametoa fedha za kujenga Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika. Mheshimiwa Waziri alishafika kwenye eneo hilo na analifahamu vizuri. Serikali

imejenga majengo mazuri sana na watumishi ambao wapo ni wachache sana. Naiomba Wizara isaidie sana kuleta watumishi wa kada hii ya afya. Kwa Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika tuna upungufu wa watumishi zaidi ya 200, wanahitajika. Tuna idadi ndogo mno; hospitali ya wilaya inatoa huduma utafikiri ni kituo cha afya. Pamoja na kuleta vifaa vya matibabu ambavyo vipo pale lakini bado idadi ya watumishi ambao tulikuwa tunahitaji Serikali iwalete ili waweze kutoa huduma hiyo ya afya ni chache.

Mheshimiwa Spika, tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada ambazo amezifanya yeye pamoja na Naibu Waziri wake, ambapo mmekuwa mkifika mara kwa mara kwenye Wilaya ya Tanganyika na kuangalia changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, tuna vituo vya afya 10 ambavyo havina watumishi kwenye Wilaya ya Tanganyika na tunavyo vituo vya afya vitano ambavyo vimekamilika: Kituo cha Afya cha Ikola, Kituo cha Afya cha Katuma, Kituo cha Afya cha Ipwaga, Kituo cha Afya cha Sibwesa, Kituo cha Afya cha Mnyagala na Kituo cha Afya cha Bulamata. Watumishi wanatolewa kwenye hospitali ya wilaya wanapelekwa kwenye kituo cha afya, unakuta kituo cha afya kina watumishi wawili tu.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri jitihada ambazo amezifanya za kuleta vituo vya afya kwenye maeneo hayo ziende sambamba na kupeleka rasilimali watu ambao wanaweza kwenda kutoa huduma ya afya. Tunaipongeza Wizara kwa mpango mkakati wa kupeleka huduma za afya kupitia timu ya madaktari. Tumepokea madaktari waliokuja kutoa huduma za afya kwenye Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika ambao wametoa huduma nzuri mno, tunaipongeza Serikali. Madaktari hawa wametoa huduma ambayo kimsingi imewasaidia sana wananchi. Madaktari wanajituma na wanafanya kazi nzuri; wanashirikiana na watumishi waliopo kwenye hospitali hiyo ya wilaya na wanatoa huduma kwa watu wa ngazi ya chini. Kiukweli mmeiheshimisha Serikali na wananchi wanapongeza sana jitihada ambazo zimetolewa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la ukosefu wa *X-ray* kwenye Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika. Huduma hii ni muhimu na inapaswa irejeshwe. Tuliletewa *X-Ray* ya kwanza ikawa imekosa watumishi ambao walishindwa kuifanyia kazi. Baadaye ikaonekana kwamba ile ilikuwa haina uwezo wa kufanya kazi kwenye maeneo yale. Tukaomba *X-ray* mpya mpaka sasa bado haijafika. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuleta hivyo vifaa ambavyo vitafanya kurahisisha shughuli za utoaji huduma kwenye maeneo ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, tatizo la bima; Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika inatoa bima kwenye vijiji nane na Mheshimiwa Waziri anakumbuka akiwa Waziri wa TAMISEMI alishuhudia akitoa hundi ambayo ilikuwa inalipa huduma hiyo ya afya kupitia vijiji hivyo nane ambao wanapata fedha za uhifadhi wa mazingira. Kwa bahati mbaya sana fedha zilizolipwa na huduma inayotolewa ni vitu viwili tofauti sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri afuatilie jambo hili. Tumelipa fedha kwenye *CHF* lakini hakuna huduma inayotolewa hakuna. Kati ya fedha zilizotolewa zaidi ya shilingi milioni 150 waliopata huduma ni watu wachache sana ambao wametumia shilingi milioni 20 tu. Naiomba Serikali ifuatilie kuhakikisha malipo yanayolipwa na wananchi yaende sambamba na huduma ambayo wanapaswa kuipata kupitia huduma walioilipia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za dhati kwa Serikali kwa kuleta *ambulance*. Tumepata *ambulance* mbili ambazo zimekuwa zikitoa huduma lakini nimkumbushe Mheshimiwa Waziri Ummy alituahidi kutupa *ambulance* nyingine ya tatu kwa kulingana na jografia iliyopo kwenye Wilaya ya Tanganyika. Tumeenda naye Eneo la Karema alitoa huduma nzuri na alituahidi kutupa *ambulance*.

Mheshimiwa Spika, pia tumeenda na Naibu Waziri kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Tanganyika. Sisi tuna uhitaji wa *ambulance* zaidi ya tatu lakini tumepata mbili kupitia Ofisi ya TAMISEMI. Mheshimiwa Waziri nikukumbushe zaidi ile *ambulance* ya tatu utusaidie ili tuipeleke ule Ukanda wa Ziwa ikawasaidie wananchi wanaoishi kwenye maeneo yale na wewe ulifika

kwenye eneo husika. Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa jitihada ambazo umezifanya pamoja na timu yako kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii ya Afya na nianze kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa alioufanya katika sekta ya afya. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maeneo kama matatu ya kuchangia na la nne kama muda utatosha. Kwanza, watoa huduma wa sekta ya afya hapa nchini wengi wanajitahidi kufanya huduma hiyo kwa ubora kulingana na mazingira ambayo wanakutana nayo. Kuanzia hospitali zetu za rufaa mpaka hospitali za chini kabisa kwa maana ya zahanati. Pamoja na kazi kubwa wanayoifanya lakini wako baadhi ambao utoaji wao wa huduma kwa kweli hauridhishi na kwa nini hauridhishi? Wako baadhi ambao mgonjwa anapofika anahitaji huduma hata ile kauli tu ya mapokeo inakuwa siyo nzuri. Nakumbuka Mheshimiwa Ummy uliwahi kusema hili utalisimamia vizuri sana. Ninaimani hapo bado inahitajika kuweka nguvu kubwa kusimamia. Haya sasa yanasababisha wanakosa umakini katika utoaji wa huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana leo unasikia mgonjwa alikuwa hahitaji kuwekewa damu anawekewa damu mgojwa anapoteza maisha. Huku ni kukosa umakini lakini unakuta labda mgonjwa alikuwa hahitaji dawa *X* anapoewa dawa nyingine. Labda mgonjwa alishajenga usugu kwenye dawa *X* anapewa dawa *Y*, ni kwa nini? Ni kwa sababu ya baadhi ya watoa huduma katika nchi hii hawafanyi kazi hii kwa uaminifu. Vilevile, wanafanya kazi hiyo kwa kukosa umakini lakini inawezekana ni mazingira, lakini wakati mwingine inawezekana ni mzaha tu yanatokea haya ambayo leo tunayasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi huko kwenye mitandao ya kijamii nako kumeibuka madaktari wengi sana. Ukisoma mtu ametoka hospitali anaeleza kabisa; "Nimetoka hospitali nimeonana na daktari nimeambiwa hili." Lakini bado anarudi mtandaoni kwenda kuomba tena ushauri. Unajiuliza hivi kuna nini? Maana yake ama haya mawasiliano kati ya daktari na mgonjwa hayako sawasawa ama huyu mgonjwa hajaridhika na maelezo ya daktari kwa sababu ya mapokeo ya daktari anarudi mtandaoni kwenda kuomba ushauri mwingine. Yaani ukisoma kwenye mitandao kuna *crisis* kubwa sana ya watu kwenda kutafuta huduma nyingine kwenye mitandao ilihali ametoka kwa daktari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ipo kazi kubwa sana ya baadhi ya watoa huduma wetu kufanya kazi zao kwa ufanisi kumridhisha mgonjwa, kumsikiliza, kujua mgonjwa huyu anahitaji nini? Labda anahitaji dawa hii na anahitaji kufanya hivi ili akitoka pale asirudi tena mtandaoni kwa sababu mwisho wa siku sasa kama anarudi mtandaoni maana yake kule ataambiwa kitu kingine ataacha kufuata ule ushauri wa daktari. Ndiyo tunaendelea kupata changamoto kubwa. Kama ndiyo hizo dawa ambazo zinatumika hovyo hovyo zitaendelea kutumika na kuendelea kutengeneza wagonjwa zaidi na zaidi wa magonjwa yasiyotibika kwa kiwango kikubwa *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine nataka kuuliza inawezekana hawa watoa huduma ama hawapati *course* za mara kwa mara? Kwa hiyo inawezekana ukomo wake wa kumhudumia mgonjwa

uko kwa kiwango fulani ndiyo maana mgonjwa anakimbilia mtandaoni, lakini je, anapata *course* za mara kwa mara? Anaji-*upgrade* kulingana na uhalisia wa dunia ya leo? Ninyi wataalamu mnajua si mnasema sijui *bacteria* huyu amegeuka amekuwa hivi kwa hiyo mgonjwa huyu atahitaji hii. Mimi siyo mtaalamu sijui lakini mnajua au *virus* hawa hawahitaji dawa hii, sasa kwa sababu tumemtibu labda na dawa *X* kulingana na *bacteria* alionao labda atahitaji dawa *Y*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inawezekana pia madaktari hawapati hizo *course* au hawaji-*up grade* ili waweze kuendana na hali halisi ya sasa ndiyo maana mwananchi au mgonjwa anaweza kukimbilia kwenye mitandao ya kijamii. Kwa hiyo, upo umuhimu na haja kubwa sana ya mawasiliano kati ya mtoa huduma na mgonjwa yaendelee kuimarishwa, yaendelee kuwa ya kisasa na yahakikishe mgonjwa anapata kile ambacho anakistahili kulingana na kile ambacho anaumwa.

Mheshimiwa Spika, kingine, nimemsikia Mheshimiwa Waziri hapa amesema vizuri sana kuongezeka kwa vifaa tiba kwa wingi katika hospitali zetu kwa ujumla wake. Yeye ameeleza kwa *level* yake kwa maana ya hospitali za kanda, hospitali za rufaa na hata huko TAMISEMI nako kuna vifaa vingi ambavyo vimeongezeka, lakini kuongezeka kwa vifaa ni hatua moja, hatua nyingine ni matumizi sahihi ya vifaa husika. Hatua ya tatu ni matengenezo ya vifaa husika kama vikipata hitilafu.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia katika maeneo mengi *X-ray* ikiharibika inachukua wiki, wiki mbili au wiki tatu mpaka matengenezo yafanyike, wananchi wanakosa huduma. Hii pia ni changamoto kubwa sana. Sasa hizi juhudi Mheshimiwa Rais alizoziweka za kununua hivi vifaa hazitaweza kuzaa matunda kama haya mambo hayataweza kwenda sambamba. Tumenunua vifaa tunahitaji wataalamu wa kuhakikisha vifaa vinatumika. Sijui *CT-scan,* sijui *X-ray* na vyote ambavyo mmevitaja lakini pale ambapo kinaharibika kitengenezwe kwa wakati uleule ili kuhakikisha mgonjwa anapoenda kupata huduma basi asianze tena kuambiwa kwamba *X-ray* haifanyi kazi njoo wiki ijayo, njoo mwezi ujao, nenda hospitali nyingine au nenda mkoa mwingine

akapate huduma hiyo; tutakuwa hatujawasaidia Watanzania. Inatakiwa pia tuone namna gani ya kuhakikisha kwamba mgonjwa anapata huduma kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, pamoja na kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma hapa nchini kama Mheshimiwa Waziri alivyoongea hapa, kuongezea vituo kwa maana ya majengo ni jambo moja na upatikanaji wa dawa ni jambo lingine lakini upatikanaji wa watumishi wa kutosha kuhakikisha huduma inatolewa ndilo la msingi. Mwananchi ukimwambia umeongeza vituo 1,000 au 2,000 vya kutolea huduma hakuelewi, kama akienda pale anakuta hakuna daktari, hakuna nesi, hakuna sijui cha kupimia damu na hakuna vitu vyo ambavyo vinatakiwa itakuwa haina maana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni lazima haya mambo yaende sambamba. Yaani wakati mwingine tujenge vituo kulingana na idadi na kuhakikisha tunapata watumishi. Kituo kinakuwa *full equipped* kwa vitu vyote kwa maana ya vifaa, watumishi (wataalamu na wasiokuwa wataalamu) na vyote ambavyo vinahitajika kuifanya kweli iwe ni hospitali kwelikweli na iwe hospitali ambayo imekamilika.

Mheshimiwa Spika, lingine kuna changamoto kubwa sana ya wanawake wengi ndani ya nchi hii kutamani kupata ujauzito na watu wamekuwa na shida kubwa sana ya kutokushika ujauzito. Tumesikia Muhimbili wameanzisha huduma za kupandikiza. Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa hilo lakini ipo haja ya kupanua huduma hii kwenda mpaka mikoani kwa sababu changamoto na uhitaji ni mkubwa. Hatujui shida ni nini. *May* be labda ni *life style* au ni vitu gani au ni vichocheo vya *hormones* na vitu vinginevyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wewe kama mwanamke ambaye unajua mwanamke ambaye hajapata mtoto alivyo na changamoto kwenye jamii yake. Jinsi jamii, familia na mume anavyomtazama naomba ulisimamie hilo. Tuwasaidie wanawake ambao wanatafuta watoto. Hivi vituo kama ni vya kupoandikiza visambazwe kwenye mikoa na huduma iwafikie wanawake wote nchini ambao wanahitaji kupata matibabu haya.

Mheshimiwa Spika, kingine nataka niulize maswali mawili. Kwanza, kwenye Hotuba ya Kamati imeelezwa upungufu wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo. Mpaka Julai imetolewa 35% tu. Ni ndogo sana kwenye sekta muhimu sana ya afya. Serikali iko hapa, tunaamini mpaka Julai fedha hizi zitatolewa kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Spika, swali dogo la mwisho, madaktari hawa wa ubobezi wanafanya kazi kubwa sana kuzunguka nchi nzima. Je, zoezi hili litaendelea kwa muda gani? Ili huduma hii iendelee kutolewa, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagongwa, ahsante sana.

Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, awali ya yote kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kutukutanisha hapa tukiwa na afya njema. Sambamba na hilo naishukuru Serikali kupitia Wizara kwa kuelekeza macho yake na msisitizo mkubwa katika Wizara ya Afya. Mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Afya na Mambo ya UKIMWI nimeshuhudia katika maeneo tofauti ambayo Kamati imefanya ziara, uwekezaji mkubwa wa vifaa tiba pamoja na madawa na wataalamu mbalimbali. Kwa hiyo ni shukrani kubwa kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyosemwa hapa magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza, hili tunaweza kuita ni janga la dunia na Tanzania ikiwemo ndani yake. Kwa kweli janga hili linaula mfuko mkubwa wa Serikali katika matibabu yake. Kwa mfano magonjwa sugu ya kupumua, magonjwa ya saratani, kisukari na magonjwa mfano wa hayo yanaua takribani watu wasiopungua milioni 40 kwa dunia nzima kwa kila mwaka na Tanzania nayo imeathirika katika tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kila vifo 10 vya wagonjwa vifo saba vinatokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kwa hiyo, ni wito wangu kwa Serikali kama ilivyokuwa malaria, UKIMWI na magonjwa mengine yamefunguliwa mifuko mbalimbali ili kuweza kutibu basi na maradhi haya lazima nayo yafunguliwe mfuko wake ili iweze kurahisisha matibabu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hapo wataalam wetu wafanye utafiti wa kuweza kujua visababishi vya maradhi haya kama saratani kwa mfano, unajua wataalam wetu wako kazini lakini bado hawajatoka na maamuzi thabiti ambayo yanaeleza ni kitu gani ambacho kinasababisha saratani na magonjwa kama hayo. Kwa hiyo, tunatoa wito, kwa kweli utafiti uendelee kufanywa ili tuweze kujua.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji mmoja hapa alizungumza kwamba nini kinasababisha Kanda ya Ziwa lakini kwa taarifa ambazo Wajumbe wa Kamati tunazo tunajua Kanda ya Kaskazini inaongoza katika tatizo hili la saratani.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, nije katika Bohari Kuu ya Dawa, *MSD*. Moja kati ya majukumu ya *MSD* ni kuzalisha, ununuzi wa madawa, utunzaji na usambazaji, hiyo ndiyo kazi yake kubwa ambayo kwa kweli ina wajibu wa kufanya hivyo pamoja na kusambaza katika vituo vya Serikali pamoja na binafsi. Ni muda mrefu Kamati yetu imekuwa ikitoa maoni hapa katika Bunge lako Tukufu na katika vikao vyetu vya Kamati mbalimbali tumetoa wito lazima Bohari Kuu ya Dawa iongezewe mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtaji iliyonao ni mdogo na ndiyo maana wanakuwa na maghala madogo ambayo hayakidhi mahitaji ya kupeleka madawa na kuhifadhiwa katika Kanda. Leo kwa mfano, baadhi ya Kanda ambapo wanapeleka dawa hizo, hospitali chache tu za Halmashauri zikichukua utakuta zile dawa muhimu zimeisha, ni kwa sababu ya ufinyu wa maghala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata lile ghala kubwa lililoko pale Dar es Salaam ni ghala la kukodi ambalo kila mwaka linai-*cost* au linagharimu *MSD* siyo chini ya shilingi bilioni mbili. Sasa fikiria miaka

mitano tu watakuwa wanalipa shilingi ngapi? Sasa ni muhimu kupewa mtaji huu na wamekuwa wakiomba mtaji usiopungua shilingi bilioni 561.5. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ya Fedha iipe ili kuweza kufanya majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika Mamlaka ya Dawa na Vifaatiba, *TMDA*. *TMDA* nayo majukumu yake makubwa ni kuhakiki ubora na usalama wa madawa, vifaatiba pamoja na vitendanishi. Kwa hiyo, kwa kweli taasisi hii ya *TMDA* inafanya kazi, ina vifaatiba vya kisasa, vya kileo kabisa, ina maabara nzuri yenye vifaa vingi vya kisasa na inatambulika duniani. Hawa ni watu muhimu sana katika kusimamia afya za jamii. Uingizaji wa madawa holela, unaweza kuingiza madawa holela kama hawapo hawa, wakachunguza wakakamatwa, pia uingizwaji wa vifaa ambavyo havikidhi viwango na mambo kama haya itakuwa ni shida.

Mheshimiwa Spika, shida waliyonayo hawa ni ukosefu wa watumishi, wanao watumishi wa kudumu na watumishi wa mkataba ambao wako siku nyingi lakini mpaka leo hawajaajiriwa kwa sababu ya kukosa vibali vya kuweza kuwaajiri. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa Wizara inayohusika ya Utawala Bora na Utumishi watakapopeleka maombi yao basi wayashughulikie. Hizi ni taasisi muhimu sana, zinahitaji kuwa na watumishi wa kutosha katika maeneo mengi ili kuweza kudhibiti hali kama hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije katika taasisi ya mifupa ya *MOI*, nayo inafanya kazi nzuri, tumewatembelea pale wanavyo vifaa vya kutosha, vifaa vya kisasa lakini wameelemewa sana na ndugu zetu wa bodaboda na ajali zao. Ukienda pale utakuta wodi nzima wamejaa vijana hawa wa bodaboda waliopata ajali. Siwasemi bodaboda kwa ubaya kwa sababu ni vijana ambao wamejiajiri wenyewe, wanatoa huduma mahali ambapo hata huduma za daladala hazifiki lakini kutokana na kuwa pengine hawana taaluma, uzoefu, maelekezo mara nyingi wanapata ajali kubwa na kimbilio lao ni *MOI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, asilimia 70 ya bodaboda hawa huwa hawana bima wala hawana uwezo wa kulipia gharama, kwa hiyo

mzigo mkubwa unawaangukia *MOI* na hivyo zile *resources* ndogo walizonazo inabidi wazitumie kwa ajili ya kuweza kuwahudumia. Kwa hiyo, ni muhimu Serikali ikalitazama hilo, Wizara ya Mambo ya Ndani ikaandaa mtaala maalum wa kuweza kuwaelimisha hawa ili kuwaelekeza namna ya kutumia vyombo vyao, namna ya kuweza kuvi-*handle* pamoja na kuweza kuepusha ajali ambazo siyo za lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa hapa, hata Kamati yetu imesisitiza, Sheria ya Uvunaji, Utunzaji na Upandikizaji wa Chembechembe na Viungo vya Mwili wa Binadamu. Sasa hivi hospitali zetu kwa kuwatumia mabingwa na mabingwa wabobezi wanafanya shughuli hizi lakini sheria mahsusi bado haijatungwa. Kwa hiyo, tunaomba mchakato wa sheria ufanye kazi, tupitishe sheria hapa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali, wadau wa dini mbalimbali pamoja na watu wa haki za binadamu kuona namna gani tunaweza kufanya huduma hii ili wananchi wetu waweze kupata huduma hii na kuendeleza maisha yao. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. KHALIFA MOHAMED ISSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.*(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu yetu ya kwanza ya kukutana leo. Wabunge ambao tutaanza nao wakati wa michango mchana ni Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi na wengine wataendelea kutajwa kadri muda utakavyokwenda.

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la *Engender Health* na *Marie Stopes* Tanzania pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya

Afya - *NHIF*, watatoa huduma ya upimaji wa afya kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watumishi wa Bunge katika kituo chetu cha afya kilichopo kwenye jengo la Utawala *Annex*. Zoezi hili linaanza leo tarehe 13 Mei, 2024 na litaendelea hadi tarehe 24 Mei, 2024. Upimaji huo utahusu magonjwa yafuatayo:

Magonjwa ya moyo, magonjwa ya wanawake ikiwa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na matiti na ushauri nasaha. Kuna wakati tuliambiwa ushauri na nasaha ni kitu hicho hicho haya, ushauri nasaha na nasihi ya uzazi wa mpango, magonjwa ya mifupa na mgongo na magonjwa ya afya ya akili na saikolojia.

Waheshimiwa Wabunge, katika haya yote, kila mmoja aende kwenye lile linalomuhusu. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, zoezi hili linashirikisha Madaktari Bingwa kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Magonjwa ya Moyo, *JKCI*, *Ocean Road* na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma - *General*. Waheshimiwa Wabunge, tutakutana huko, kila mtu kwenye eneo lake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri, Madakatari, sijui niwaite Madaktari au sijui wanaitwa nini lakini aliowazungumzia Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa kweli wako wengi na wanawachanganya wananchi. Kwa mfano, hapa niliposikia mimi kwamba Madaktari wanaenda kunywa chai kwa muda mrefu nikashangaa, kwa sababu kuna Madaktari wanatuambia tule mlo mmoja, sasa sijaua kama ule mlo mmoja ndiyo hiyo chai wanayoenda kunywa au wao wanakula mara nyingi ila sisi raia ndiyo tunywe chai tu au tule mlo mmoja! Sasa haya yote kwa kweli wananchi wanatuchanganya kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kama wapo ambao ni kama mimi ambaye sielewi hiyo taaluma halafu nimejifanya, basi kuwe na namna ya wananchi kufahamu ili wajue wachukue ushauri wa nani ambao ni wa kitaalam na ushauri wa Tulia ambaye siyo mtaalam wa tiba na yeye anazungumza kuhusu lishe, sasa kila mtu anatuchanganya, mwishoni tunashindwa kuelewa sasa kama

kazi tunazofanya tule au tukae tu na njaa tunywe maji sasa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri nadhani hayo utayatazama na wataalam wako, kwa kweli jamii inachanganyikiwa imsikilize nani kwa sababu wasemaji wamekuwa wengi mno.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.09 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tulikuwa tunatafuta majina ya wachangiaji wa jioni, yameshapatikana. Tunaanza na Mheshimiwa Ikupa, ajiandae Mheshimiwa Shigongo.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa fursa hii. Awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya neema ya uzima na uhai. Pia, natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyomsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais kutimiza malengo yake kwenye Sekta hii ya

Afya, Mheshimiwa Waziri hongera pamoja na timu yako yote ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia nafasi hii, kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri lakini pia kulingana na uhalisia wa maeneo tunayotoka, ninaomba kuipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anayeongoza Serikali ya Chama changu cha Mapinduzi, kwa mageuzi makubwa ambayo yanaendelea kufanyika kwenye Sekta hii ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache miongoni mwa mengi, ya kuishukuru Serikali kama ifuatavyo. Ninaishukuru Serikali kwa ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya kwenye maeneo mbalimbali ndani ya nchi yetu. Ninaishukuru Serikali kwa kuongeza vitanda vya kulaza kama ambavyo Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesema. Pia, ninaishukuru sana Serikali kwa kupunguza vifo vya watoto na kuboresha ama maboresho makubwa ambayo yamefanyika kwenye eneo la huduma ya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaishukuru sana Serikali kwa kuongeza watumishi kwenye eneo hili la afya pamoja na vifaa mbalimbali zikiwemo *CT – Scan* pamoja na *MRI*. Mambo ni mengi ambayo yamefanyika na Serikali yetu, na bado yanaendelea kufanyika. Hivyo, ninaendelea tena kuishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imeendelea kutoa huduma za utengamao kwa watoto wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma hii ni muhimu sana kwa sababu, inapunguza athari za ulemavu ama kuuondoa kabisa na hivyo inapelekea kwamba mtoto ambaye angekuwa mlemavu, kupitia huduma hii ya utengamao, basi mtoto huyu ule ulemavu unamuepuka ama unampungua si sawa na ambavyo asingekuwa amepata huduma hii ya utengamao. Kwa hiyo ninaishukuru sana Serikali kwa hili pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukurani hizo na pongezi kwa Serikali, nina maombi yafuatayo. Ninaiomba Serikali

ione namna bora ya kutoa huduma za matibabu kwa kundi la watu wenye ulemavu wakati tunasubiri mchakato wa Huduma ya Afya kwa Wote kukamilika. Kwa nini? Ninatambua utaratibu uliopo sasa hivi kwamba mtu mwenye ulemavu asiyekuwa na uwezo wa kugharamia gharama za matibabu, anapatiwa barua ya utambulisho mahali anapotokea, halafu akifika hospitali anakutana na Afisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu hauna matokeo chanya kwa kundi la watu wenye ulemavu. Nikitolea mfano, mimi nikiwa Mheshimiwa Mbunge wa kundi hili napata simu nyingi ambazo wanalalamikia utaratibu huu kwamba huwa hauwasaidii. Mfano mzuri ni wiki iliyopita, kuna mtu mwenye ulemavu wa viungo alipata ajali akavunjika tena miguu yote miwili, akafanyiwa operesheni nyingi nyingi tu kama tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwa na barua ya utambulisho ya kumtambulisha lakini alikutana pia na Afisa Ustawi wa Jamii kwenye hospitali husika ila bado hakupata ule msamaha wa matibabu. Kwa hiyo ninaiomba Serikali, ione namna bora ya kuweka utaratibu mzuri ambao kweli utatoa unafuu kwa kundi hili la watu wenye ulemavu wasiokuwa na uwezo wa kugharamia huduma za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu lingine kwa Serikali, ninaishukuru kwamba baadhi ya hospitali ambazo ni chache sana, imetenga vyumba vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu. Naiomba Serikali, iendelee kutenga vyumba hivi vya kujifungulia wanawake wenye ulemavu kama ambavyo nimekuwa nikisema. Wanawake wakati wa kujifungua wanahitaji usiri, lakini kundi la watu wenye ulemavu linahitaji usiri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni hilo kwamba vyumba hivi viwepo karibia kwenye kila hospitali, mwanamke mwenye ulemavu anapokuwa anahitaji kujifungua, basi aweze kupata huduma hii. Ninaomba kuipongeza Hospitali ya Benjamin William Mkapa, ambayo imetenga chumba hiki. Ni chumba kizuri na wanawake wenye ulemavu wanakitumia na wanafurahia huduma mahali hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba kuipongeza *CCBRT*. Huduma hii pale *CCBRT* ni nzuri sana kwa wanawake wenye ulemavu. Chumba kiko kizuri na huduma ni nzuri, wanawake wenye ulemavu wanafurahia mazingira mazuri ya kujifungua *CCBRT*. Pia, naipongeza Hospitali hii kwa huduma nyingine ambazo zinatolewa mahali hapa chini ya Mkurugenzi Brenda ambaye tuko naye mahali hapa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninaomba kuiomba Serikali inapokuwa inanunua vitanda, iweze kuangalia kujumuisha vitanda ambavyo ni; nakosa neno zuri la Kiswahili; sijui ni vitanda vinavyorekebishika, vile *adjustable beds*. Kwamba iweze kununua vitanda hivi si tu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, lakini kuna wazee, kuna wagongwa ambao inakuwa ni ngumu sana anapofika hospitali amezidiwa anumwa hoihoi, aanze kuwekewa ubao, apande pale juu mpaka afikie kile kitanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hivi vitanda ni muhimu sana si tu kwa kundi la watu wenye ulemavu, isipokuwa ni kwa watu wote hasa ukiangalia wazee pamoja na wagonjwa wale ambao wanakuwa wamezidiwa sana. Ninaomba pia kuiomba Serikali kwa habari ya upatikanaji wa mafuta ya watu wenye ualbino. *KCMC* imekuwa ikitoa mafuta haya bure lakini sasa hivi *KCMC* haitoi tena mafuta haya vile inavyotakiwa kwa sababu wanakosa malighafi za kutengenezea mafuta haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali mwaka jana ilitoa shilingi 60,000,000 na *KCMC* wakaweza kutengeneza mafuta chupa 2,200 lakini kwa mujibu wa Sensa, mafuta haya hayatoshi. Ninamuomba Mheshimiwa Rais, Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aone namna ya kuongeza bajeti ya utengenezwaji wa mafuta haya pale *KCMC* walau hata nusu ya mahitaji kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kumalizia, ninaomba Serikali pia ione namna ya kununua zile *Cryoguns Machines*. Mashine hizi ni muhimu sana, mara nyingi zinatumika kwa watu wenye ualbino, lakini pia si tu kwa watu wenye ualbino, hata kwa mtu yeyote ambaye ana *cancer* inayokuwa inaanza. Mashine hii

inakuwa inamsaidia mtu ambaye ana *cancer* inayoanza, anapopuliziwa ile hewa, *cancer* ile inadhibitiwa kwenye hatua za awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naiomba Serikali iweze kutenga fedha za kuweza kununua mashine hizi kwa sababu ni muhimu si tu kwa kundi la watu wenye ualbino, isipokuwa ni kwa watu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda wangu bado upo, ninaomba kuongeza ombi lingine kwa Serikali na ombi hili si lingine, ni kuhusiana na viungo bandia. Viungo hivi vimekuwa vikipatikana kwa bei kubwa na hii ni kutokana na kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa, muda wako ume…

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo, wajiandae Mheshimiwa Aysharose Mattembe na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwanza kwa kunga mkono hoja kabla sijaendelea. Baada ya hapo, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri dada yangu Mheshimiwa Ummy na Naibu wake ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mollel kwa kazi kubwa wanayoifanya. Sina mashaka na uwezo wa dada yangu Mheshimiwa Ummy, kazi aliyoifanya mwanzo, akarudi tena Wizara ya Afya kwa mara ya pili, nina uhakika anafanya kazi nzuri sana, nakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo ambayo imefanya jimboni kwangu. Vituo vya afya vimejengwa karibu vinne lakini bado zahanati za kutosha. Jambo moja nataka kuiomba Serikali, ni watumishi wa afya hawatoshi. Najua hili liko TAMISEMI lakini naomba kulizungumza hapa Mheshimiwa Waziri wa Afya ananisikia. Tunahitaji watumishi, watumishi hawatoshi kwa hiyo

tunahitaji watumishi wa kutosha Buchosa ili tuweze kupambana na magonjwa yanayosumbua watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia ugonjwa wa homa ya ini. Ugonjwa wa homa ya ini nimeanza kuuzungumzia tangu nimeingia Bungeni, naomba kuendelea tena na mapambano yangu haya ambayo sitachoka kuyasema mpaka siku mambo yatakapobadilika. Kumbukumbu zangu ni kwamba ugonjwa huu upo na tangu nimeanza kuuongelea mara ya kwanza, *prevalence rate* (uwepo wa ugonjwa huu kwenye jamii yetu) ulikuwa ni 4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Ripoti ya Mheshimiwa Waziri leo, anasema ni 4% bado lakini ziko ripoti zinasema uwepo wa homa ya ini kwenye jamii yetu ni 6% na baadhi ya maeneo 7%. Hii inaashiria kwamba ugonjwa huu upo na ni ugonjwa hatari, unaendelea kuchukua maisha ya Watanzania. Lazima ugonjwa huu uondoke kwenye jamii yetu na inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kuondoa kabisa homa ya ini kwenye jamii yetu. Mara ya mwisho nilizungumza, narudia tena leo, njia pekee ambazo Misri na Taiwan wametumia, ni mambo makubwa kama matatu hivi. Jambo la kwanza ni elimu kwa jamii. Wanachukua muda mrefu sana kuelimisha jamii, matangazo, habari mbalimbali kwenye redio ili watu waweze kuuelewa ugonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi hawauelewi ugonjwa huu, wengi hawauelewi. Inawezekana hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawaelewi vizuri kama jamii iliyoko nje. Huu ni ugonjwa hatari, umechukua maisha ya watu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nataka kuzungumzia suala la chanjo, chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini. Chanjo ipo na Serikali yangu inachanja, naomba kuishukuru sana. Mimi nataka kuja na wazo litakalofanya ugonjwa huu tuweze kuwachanja watu wote uweze kutokomea kabisa na usiwepo kabisa katika nchi yetu. Ndiyo ndugu zetu wa Egypt na Taiwan wamefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafanyaje, ili uweze kufikia lengo la jamii yako iwe imekingwa dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini, wao wataalamu wanaita *herd immunity*, unatakiwa uchanje 90% ya watu wako. Sasa kwa Tanzania, tuna watu 60,000,000, 90% ya kwetu sisi ni watu 54,000,000. Ukiwachanja watu 54,000,000, wale 6,000,000 hata usipowachanja watakuwa na kinga, watakuwa na *herd immunity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uwezo wa kuwachanja watu wote hawa 54,000,000 tunao? Ndiyo shida yetu. Sensa ya mwaka 2002 inaonesha kwamba Tanzania, vijana chini ya umri wa miaka 25 ni 70%. Asilimia 70 ya Watanzania wote ni 42,000,000, na hii ni vijana chini ya umri wa miaka 25. Mwaka 2001, nchi yetu ilianza kuwachanja watu wake kwa kuwachanja watoto wote wanaozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwachanja watoto wote wanaozaliwa maana yake ni kwamba, watoto wote waliozaliwa 2000 mpaka leo 2024, miaka 24 wote wamekwishachanjwa, 42,000,000. 42,000,000 ukitoa kwenye 54,000,000, wanabaki 12,000,000 peke yake ambao hawajachanjwa. Kazi yetu sisi ni kuchanja watu 12,000,000. Je, hatuna uwezo wa kuchanja watu 12,000,000? Ukipiga hesabu, kama hatuna uwezo huo, yako mashirika ambayo yanatoa fedha kwa ajili ya kuchanja watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni *GAVI (Global Alliance for Vaccination and Immunization)* na ya pili ni *CDAF*. *CDAF* ni *Center for Disease Analysis Foundation*; hawa wananunua chanjo kwa bei nafuu kwa ajili ya nchi masikini. Tukifanya hivyo, tutawachanja watu wetu wote na ninahakika kabisa ugonjwa huu utaweka kutokomea, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kusema kitu kimoja. Kwa nini sisi tunashindwa kuchanja watu wetu? Kama hatuna fedha, tufanye nilichokisema hapa watu wachanjwe tuokoe maisha ya watu. Tukiokoa maisha ya mtu mmoja, ni faida kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nimesoma kwenye Ripoti ya Mheshimiwa Waziri hapa, wamesema matumizi ya *antibiotics* yameongezeka kutoka 62% mpaka 80%, zaidi hata ya kiwango cha Shirika la Afya Duniani ambayo ni 30%. Kwa nini imezidi? Imezidi kwa sababu kuna dawa nyingi *fake*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kumalizia kwa kusema hivi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Shigongo, kengele ya pili hiyo.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia, sekunde moja tu. Kuna dawa…

**NAIBU SPIKA:** Umeshamaliza sekunde moja.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wa dawa wanaingiza dawa *fake* kwa sababu gani? Kwa sababu huku hawapati faida. Wanaenda ku-*negotiate* na wale watu wenye viwanda wapunguziwe *potency* ya dawa ili dawa iwe bei rahisi, wakija hapa wauze kwa bei ndogo. Matokeo yake dawa hazitibu, haziui wadudu, watu wetu wanazidi kufa. Mheshimiwa Waziri chukua hatua, nenda kakague kwenye bohari za watu, ukikuta mtu ana dawa chukua hatua kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Shigongo unaruhusiwa kumuandikia Mheshimiwa Waziri hoja za ziada. Mheshimiwa Aysharose, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu inayogusa maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mungu kwa baraka na rehema zake na kwa kuendelea kunijalia afya njema. Natumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa wa miundombinu pamoja na vifaatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI. Maeneo mbalimbali tuliyofanya ziara, tumejionea uwekezaji mkubwa. Tumeona miundombinu ya hospitali pamoja na vituo vya afya na zahanati lakini pia na uwekezaji mkubwa katika vifaatiba. Mheshimiwa Rais, tunakupongeza sana, tunakutakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanawake wa Mkoa wa Singida wamenituma nikufikishie salamu Mheshimiwa Rais, wanakupenda sana, wako bega kwa bega na wewe katika azma yako ya kuwaletea wananchi maendeleo. Pia, wanakuahidi ifikapo 2025, wanasimama na wewe na watakupa ushindi wa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, ninaomba kujielekeza katika Hospitali yangu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida. Hospitali hii inasuasua katika ujenzi wake. Hospitali nyingine za mikoa mingine zimeshakamilika lakini ujenzi wa Hospitali yangu bado haujakamilika na ujenzi wake umeanza toka mwaka 2014. Leo ni takribani miaka 11 tunaizungumzia hospitali hii. Naomba sana Serikali, Hospitali hii iweze kukamilika majengo yake lakini na jengo la ghorofa nne ambalo ni jengo tengefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine huwa najiuliza, hivi wananchi wa Mkoa wa Singida ni wakimbizi? Mheshimiwa Ummy wewe ni shahidi, umeshafika katika ile Hospitali lakini pia kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mollel umefika pale. Ile Hospitali haikamiliki, ni kwa nini haikamiliki? Mimi leo hii nakusudia kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Hospitali hii, wananchi wa Mkoa wa Singida wanateseka sana kwenda umbali mrefu, kwenda mikoa mingine kwa ajili ya kupata huduma za kibingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali hii ndiyo mkombozi wa wananchi wa Mkoa wa Singida kupata huduma za kibingwa hivyo naomba ikamilike. Pia, Hospitali hii inakabiliwa na uhaba wa watumishi. Tunahitaji watumishi 290 ili sasa Hospitali hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi. Pia, inakabiliwa na uhaba wa vifaatiba. Naomba sana Hospitali hii iangaliwe kwa jicho la pekee kwa kuwa imeachwa kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na wahudumu ngazi ya jamii. Niipongeze sana Serikali kwa namna ambavyo imeendelea kuajiri wahudumu wa afya katika ngazi ya jamii, ninawapongeza sana lakini niiombe iharakishe mchakato huu kwa sababu wahudumu hawa wanasaidia sana jamii. Wanawasaidia akina mama wajawazito kujua siku zao za kujifungua, pia wanawasaidia akina mama wajawazito wasiweze kujifungulia nyumbani au kujifungua njiani. Vilevile, wanawasaidia akina mama wajazito kuweza kutambua vidokezo hatari na kuwasaidia kwa haraka kupata matibabu. Hivyo basi, niombe sana mchakato huu uharakishwe na Mkoa wangu wa Singida pia upate wahudumu hawa afya ngazi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia, nimefurahishwa sana na Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa maana kwamba kipaumbele cha kwanza cha Wizara ni kutoa huduma za kinga. Hivyo basi, Dada yangu Mheshimiwa Ummy ninakuomba jambo hili sasa tujikite kwa miguu miwili, ili sasa tuweke kinga zaidi badala ya tiba. Kwa sababu tunaona kabisa mrundikano mkubwa katika hospitali zetu na ni kwa sababu hatujasisitiza jambo hili la kinga tumejikita zaidi katika tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo, ninatumaini kwamba tutaweza kupunguza hata mzigo kwa madaktari wetu, lakini tutaipunguzia Serikali yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mattembe kengele ya pili hiyo.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** …tutaipunguzia Serikali yetu mzigo wa fedha nyingi kuwekeza katika vifaa tiba pamoja na wataalamu…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mattembe, kengele yako ya pili…

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, jiandae Mheshimiwa Mafuwe, jiandie Mheshimiwa Mariam Kisangi.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu sana, kwa kweli bila afya hakuna kitakachofanyika. Niwashukuru sana Waziri wa Afya, Naibu wake, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana. Mambo yanaimarika sana na tunaona uwekezaji mkubwa ambao Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameufanya katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati ninayashuhudia haya kwa sababu nimeyaona kwa macho. Tumetembea katika hospitali mbalimbali za rufaa za kikanda lakini na za mikoa, kwa kweli uwekezaji uliofanyika ni mkubwa sana. Hata ukianza kuelezea kwa mambo makubwa ambayo yanafanyika dakika zangu zitaisha sijamaliza, kwa sababu mahali ambapo tumetembelea, mfano katika Hospitali ya Sekou-Toure Mwanza sasa hivi wanatoa huduma ya *dialysis*. Mwanzo wote walikuwa wanategemea Hospitali ya Bugando kwa kweli ni uwekezaji mkubwa sana ambao unafanyika. Niwapongeze sana Wizara ya Afya kwa kuwa wasikivu na watendaji wote wanafanya kazi kwa bidiii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna uwekezaji ambao kwa sisi Watanzania ambao hatujapata fursa ya kutembelea hizi hospitali hatuwezi tukashuhudia, tukasema kwamba kweli kuna uwekezaji, lakini kwa watu ambao wamebahatika kutembelea Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mloganzila, Benjamini Mkapa, Taasisi ya *MOI*

na Taasisi ya Jakaya Kikwete kwa kweli kuna uwekezaji mkubwa sana umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda *MOI* pale kuna mashine ambayo mimi mwenyewe pamoja na kwamba nipo katika hii *field* nilikuwa sijawahi kufikiria kwamba inaweza ikawepo hapa Tanzania. Mashine hii inaitwa *Hyperbaric Oxygen Machine*, mashine hii inarahisisha sana watu wenye majereha makubwa, wenye vidonda vikubwa kuingia katika ile mashine ya kuweza kupata *oxygen* kwa asilimia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwa sisi ambao sasa hivi ni *age go*. Ukihitaji unaweza kwenda pale, ukaingia kwenye ile mashine, ukapata *oxygen* yako kwa 100% na hatimaye ngozi yako ika-*regrow*. Kwa kweli ni uwekezaji mkubwa mkubwa mkubwa sana, hii yote ni juhudi kubwa za Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata ukienda Mloganzila kumekuwa na utamaduni sasa hivi wanawake wengi tunapenda kuendelea kuwa warembo. Hakuna anayetaka kuzeeka jamani, tunapenda tuendelee kuonekana na mwonekano ambao labda Mwenyezi Mungu hakutuumba nao, huduma hizi Tanzania zinapatikana. Kwa kweli ni uwekezaji mkubwa sana. Kwa hiyo ninaomba sana sana pamoja na uwekezaji mkubwa ambao unafanyika, Wizara na Serikali mwendelee kutoa fedha kwa wakati katika hospitali zetu ambazo kimsingi ni asilimia chache sana ambazo zinakwenda. Mpaka Februari ni 49% mpaka 50% ya fedha ambazo zimekwenda kwenye hospitali zetu ninaomba sana tujitahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna changamoto, nitaongelea kwenye suala zima la Bima ya Afya. Changamoto ambayo inatokea kwenye Bima ya Afya hasa katika vituo vyetu, nitaongelea katika Hospitali za Mkoa wa Shinyanga. Mwananchi anapokwenda na Bima ya Afya kuna baadhi ya wagonjwa wananyanyapaliwa *simply because* ana Bima ya Afya siyo hospitali zote kuna baadhi ya watumishi wanafanya hivyo, lakini anaandikiwa kipimo cha *typhoid fever* anaambiwa alipe shilingi

10,000 haipo kwenye Bima ya Afya, lakini kuna mwingine amekwenda katika hospitali hizi za kanda kaandikiwa kipimo cha *CT scan* anaambiwa achangie *reagent*, sasa nini maana ya Bima ya Afya? Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri unafanya kazi kubwa sana, kuna watu ambao wanasababisha Bima ya Afya ionekane siyo rafiki kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe kwa sababu ya kutokuwa na uadilifu au kama kuna miongozo ambayo imetokea basi naomba mtujulishe sisi wawakilishi wao wa Bunge tuweze kuwaelimisha wananchi wetu. Kwamba ukienda kupima *CT scan* kuna *reagent* ambayo utalipia, kwamba ukienda kupima *typhoid fever* unatakiwa uwe na shilingi 10,000, lakini kazi kubwa inayofanyika Sheria ya Bima kwa Wote imekwisha kusainiwa. Kama bima hii ya sasa hivi haifanyi kazi vizuri, hiyo bima nyingine itakuwaje? Wananchi watakuwa na imani ya kujiunga na bima kwa wote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, wanafanya kazi kubwa sana mambo madogo madogo ambayo yanatokea *site* tunaomba myarekebishe ili tuweze kuendelea…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava, ahsante…

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe, jiandae Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii nyeti, nianze na Bima ya Afya. Hivi karibuni kumekuwa na malalamiko mengi kwenye utoaji wa huduma eneo la Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niombe sana Mheshimiwa Waziri wewe umekuwa mtu mahiri sana kwenye kusimamia sekta hii. Usikubali jambo hili likakuondelea heshima yako, tunakuomba sana sana jitahidi u-*control* jambo hili. Ziliondolewa baadhi ya dawa kwenye vifurushi, leo tumeambiwa hapa dawa 178 zimerejeshwa lakini bado bei haijarejeshwa, haijahuwishwa. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri rejesha, huisha bei kama ilivyokuwa awali, huduma hii ya Bima ya Afya irejee kama ilivyokuwa awali ili tutengenezee *departure* nzuri ya kuelekea kwenye Bima ya Afya kwa Wote. Tukienda namna hii tutakuwa na wasiwasi wa kuingia kwenye Bima ya Afya kwa Wote, hili lilikuwa ombi langu namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, kumekuwa na uhaba wa dawa hasa dawa za tezi dume na dawa za kansa ya kizazi. Ushauri wangu, tuombe Serikali iweke ruzuku in *advance* muagize kwa *bulk,* hizi dawa ambazo Watanzania wengi wanazihitaji ili sasa zinapohitajika watu waweze kuzinunua zikiwa kwenye *stock* ya Serikali. Tukisema tufanye kama biashara Watanzania wengi watapoteza uhai kwa sababu hii ni huduma haiwezi kuwa biashara, ombi langu la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, huduma ya kusafisha figo, hili limekuwa ni tatizo Mheshimiwa Waziri na tumekuwa tukikusumbua wewe mwenyewe mara kwa mara kwamba kuna wananchi ambao wana tatizo hili la kusafisha figo kwa wiki mara mbili mara tatu na wanaenda na shilingi 250,000. Hii ni ngumu sana kwa wananchi kuweza kumudu. Nikuombe sana mfanye *study* wenzetu wa Zanzibar wamefanyaje wakaweza kupata huduma hii bure kwa wananchi? Hili ni eneo muhimu sana la kuwekeza maana tunapoteza watu wengi na ikizingatiwa ugonjwa huu sasa unaenda kwa kasi umeingia mpaka kwa vijana. Kwa hiyo nikuombe sana Mheshimiwa Waziri uzingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninaomba sana chonde chonde Mheshimiwa Waziri. Tazameni namna mpya ya kuanzisha Taasisi ya Lishe Nchini ili iweze kutoa mwongozo, ili iweze ku-*centralized* elimu ya lishe nchi hii. Leo kumekuwa na walimu wengi, kumekuwa na *theory* nyingi zinazofundisha mambo ya

afya kila mtu anasema la kwake. Mimi niombe kwa kuwa Mwalimu Nyerere alianzisha hii Taasisi ya Lishe ili ku-*centralized* elimu. Tangu Jumapili nimejipa kazi ya kusoma kwenye mitandao wanaotoa elimu ya afya. Ukichukua ugonjwa mmoja, ukichukua walimu kumi, walimu tisa wanazungumza vitu viwili tofauti. Sasa tunawapotosha wananchi lakini pia tunaangalia muktadha, tunawaelimisha watu wa aina gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nampongeza Daktari Janabi anajitahidi sana kutufundisha, lakini wakati mwingine nikimsikiliza, ninajiuliza sana.  Sina *authority* ya kum-*question* daktari lakini ninajiuliza anazungumza na Watu wa Dar es Salaam? Anazungumza na wachimbaji wa madini? Anazungumza na wale wanaobeba mizigo pale Kariakoo? Kwa sababu kwa ulaji ule Mheshimiwa Waziri wale vijana wa Kariakoo wanabeba kilo 70, kilo 100 halafu uwaambie wale punje mbili, jamani si tutakuwa na nchi ambayo hatuna uwezo wa kubeba hata kilo 30? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ninachokifahamu mwili wa binadamu unahitaji *certain calories* kwenye kila *activity* anayofanya. Sasa wote tukila vile vimboga vimboga vya mjini vile, kweli watu wataenda kuchimba madini? Tutakuwa na uwezo hata wa kubeba kilo 50? Leo tumuulize Dkt. Janabi anaweza kumbebeshe mtu kilo 30 kwa chakula anachotumbia? Hawatabeba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naiba Spika, tunahitaji vijana wale *as per calories* wanazozihitaji kulingana na *activity* yake. Kwa hiyo ushauri wangu kwake ni kwamba a-*set* mazingira ya utoaji wa elimu kulingana na aina ya watu anaowahutubia, vinginevyo tutakuwa na Taifa la wakondefu na tutashindwa kazi ili hali tunahitaji kufanya kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba jambo lingine hii Taasisi ya Lishe ikiundwa ifanye kazi ya kudhibiti dawa. Leo duniani watu hawatumii mabomu tu, wanatumia vyakula kufanya watu wako kuwa wadumavu, wanatumia chakula watu wako kuwa mazezeta, wanatumia chakula watu wako kutokuwa na uwezo wa kufikiri, hiyo ndiyo silaha nyingine ya kisayansi. Sasa nani

anadhibiti vyakula vinavyoingia nchini? Viko Wizara gani? kwa taaluma ipi? Kwa uwezo upi? Kwa vipimo vipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninaomba sana sana Taasisi hii ikiundwa ijengewe uwezo iweze ku-*control* aina ya ulaji tunao kula, ni sambamba na utoaji wa elimu kuanzia ngazi ya chini kabisa. Mtoto anaundwa kuanzia ili miezi 1,000, anakula chakula gani? Nani anakisimamia ili tupate watu *smart* wa kuweza kusimamia nchi yetu? Vinginevyo itakuwa ni vita hiyo tutakuwa na watu huku, uwezo wa kufikiri mdogo kwa sababu ya aina ya chakula wanachokula. Ni sambamba na huko shuleni, watoto wetu shuleni nani anaye-*control* kwa kiwango gani kwamba watoto wetu wanakula kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze kuomba, nimepata vituo vingi sana kule zaidi ya vitano…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Mafuwe …

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** …kule Hai lakini niombe sana Serikali inisaidie kufanya…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe ahsante…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kuunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi, jiandae Mheshimiwa Nahodha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza napenda kumpongeza Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya katika nchi yetu ya kufanya maboresho makubwa sana katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumza Waheshimiwa Wabunge wengi hapa ndani na wamezungumza mambo ya kweli kila kanda imefanya maboresho makubwa sana katika sekta ya afya. Katika Bunge lililopita kwenye kipindi hiki cha bajeti nilisimama hapa, niliongea sana kuhusiana na Hospitali ya Muhimbili na Mloganzila lakini leo nasimama hapa kama Mkazi wa Dar es Salaam kutoa pongezi zangu za dhati sana kwa Wizara ya Afya. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wenu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Muhimbili imefanya maboresho makubwa sana katika utoaji wa huduma. Kwa kweli huduma zinatolewa vizuri sana na yale ambayo niliyaongea kwa nini mnawafukuza ndugu wa wagonjwa wodini? Mnawakimbiza hovyo hovyo sasa hayapo. Ndugu wa wagonjwa wamewekewa makochi ya kukaa, wanakaa huku wakiuguza wagonjwa wao ni jambo kubwa katika nchi yetu na jambo la kihistoria sana, sasa kweli Tanzania inaelekea kuwa kama India.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda niongee machache kuhusiana na Hospitali yetu ya *Ocean Road.* Hospitali yetu ya *Ocean Road,* hospitali ya kansa ina wagonjwa wengi sana lakini kuna changamoto, kumejengwa jengo kubwa sana pale la maabara lakini wagonjwa wanakwenda pale wanawekwa kwenye *list* ya kufanyiwa vipimo kama vile vya *bone scan* na vingine lakini wanakosa dawa. Ukiwauliza dawa hiyo inakuwaje? Wanasema sijui mshitiri au mfumo unaelekeza hivi na hivi. Mbona mambo hayo zamani hayakuwepo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kuboresha mifumo ndiyo watu wanakosa na huduma yenyewe kabisa hii inakuwaje? Mheshimiwa Rais wetu ame-*invest* pale kwenye lile jengo la kupimia, siyo la kawaida, lakini utakuta hata watumishi wa pale hawafanyi kazi kwa sababu hizo dawa hazipo. Wao wanakaa, wanawapigia watu simu zao wenyewe wakati wanaoleta dawa (*agent)* hawajazitoa *airport* kuleta pale. Sasa hii ni shida, niiombe Serikali iangalie upya mfumo huu wa watu ambao wanaleta dawa au tunawaagiza dawa, wanatuwekea foleni na watu wanashindwa kupata huduma ile inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye hospitali za mikoa. Hospitali zetu za mikoa Amana, Temeke, Mwananyamala na Ubungo zote hizi ni hospitali ambazo zinafanya huduma, lakini hospitali zetu zilikuwa na majengo yale ya zamani, majengo yale yamepauliwa na mabati mpaka yanaweka kutu. Niombe Serikali ije na mpango basi wa kuhakikisha sasa wanapandisha zile wodi moja moja kwenda juu. Mabadiliko sasa hivi Mji wa Temeke hauwezi kupata nafasi tena ya kusema utaongeza jengo, wabomoe, waanze kwenda na jengo moja moja kwenda juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye hospitali zetu za mikoa kuna changamoto. Mtu anaweza akaandikiwa kipimo leo, akikaa, baada ya siku tatu alishindwa labda kupata kipimo hicho baada ya hizo siku anaondolewa kwenye mfumo akija aanze kulipa upya, hilo ni tatizo. Niombe Serikali iangalie huu mfumo inakuaje unamfuta mtu ambaye aliambiwa leo atolewe damu lakini haikuwezekana kutolewa damu, akija baada ya siku alipe tena hiyo inakuwa shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine katika hospitali zetu za mikoa ni ada ya kumwona daktari ni shilingi 20,000. Sasa jambo hili linawapa shida sana watu, gharama za matibabu zinakuwa kubwa. Mwanachi anakwambia, ukienda Alexia Kongowe unamwona daktari kwa shilingi 7,000 lakini ukija Temeke unamwona kwa shilingi 20,000. Sasa hapo anashindwa kuelewa inakuwaje? Japokuwa hospitali ile ni ya ngazi ya mkoa lakini waangalie kuna watu wengine wanapata majeraha ya dharura akiwa anatembea maeneo ya Temeke. Lazima aje katika Hospitali ya Temeke, Mwananyamala au Amana hawezi akarudi tena Mbagala akaandikishe kwenye zahanati kisha apewe rufaa ya kuja Temeke, lazima utahitaji huduma ya hapo kwa hapo Temeke au Mwananyamala au Amana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa waangalie huduma hiyo ya kumwona daktari shilingi 20,000 wakati *private* ni shilingi 7,000, hiyo haiwezekani lazima twende nao. Kweli tumefanya maboresho na mimi nakubaliana kabisa maboresho yaliyofanyika ni makubwa, vimenunuliwa vipimo vingi na vikubwa lakini tuangalie sasa changamoto kubwa ni gharama za matibabu tunafanyaje?

Pamoja na Bima ya Afya tumepitisha sheria wakati haijaanza tutumie utaratibu gani ili kuwasaidia wananchi wetu waweze kupata huduma stahiki kutokana hali yao ya kimaisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ongezeko la magonjwa. Kwa kweli kumekuwa na ongezeko kubwa sana la magonjwa. Ukienda kwenye vipimo japokuwa siri ya mgonjwa wanaijua wenyewe lakini mnapokaa pale kwenye *group* kila mtu anasema heee! Mimi nimeambiwa nina kansa, mimi nina kansa, mimi kansa, mimi kansa. Lazima Serikali itenge fedha kufanya tafiti hii kansa inayoendelea namna hii kama malaria kweli na matibabu yake yalivyo makubwa, Kweli tutafika vizuri? Lazima tufanye utafiti ongezeko la magonjwa ni makubwa sana sana sana. Ukikaa hapa huwezi kuyaona nenda hospitali. Ukifika hospitalini akina mama wana kansa za vizazi, akina baba wana kansa za tezi dume lakini bado kuna kansa nyingine za utumbo, pamoja na kansa ya koo na yanazuka magonjwa ya kila aina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna tatizo la figo. Hospitali zetu za mikoa bado hazijakuwa na uwezo wa kuweka vyumba vya kutoa huduma ya *dialysis*. Tuombe Serikali iangalie kwa msingi ule ule wa kupandisha majengo juu ili tuweze kupata huduma hizi za *dialysis* katika hospitali zetu za mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tena nimpongeze kwa kweli Dkt. Janabi umetufanyia kazi nzuri pale Muhimbili Mloganzila kwa kazi ile…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja 100%. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Janabi anasema tupunguze uzito. Mheshimiwa Shamsi Nahodha, jiandae Mheshimiwa Shonza.

**MHE. SHAMSI VUAI NAHODHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe mchango wangu kwa kusema jambo moja, miaka 100 iliyopita Mwanasayansi maarufu Thomas Edson aliwahi kusema "Madaktari wa Karne ya 21 watatibu kwa kutumia tibalishe badala ya kutumia dawa za kemikali"

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa tibalishe pamoja na tibaasili, ndio maana Baba wa Taifa Mwaka 1970 aliunda Idara Maalum ya Tibalishe katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la Mwalimu lilikuwa ni kutayarisha watalam wa tibaasili na tibalishe, ili watumike sambamba na wataalam wa tiba ya kimagharibi. Kwa bahati mbaya sana, ndoto na wazo la Baba wa Taifa halikufanikiwa kama alivyotarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo basi, naomba nipendekeze mambo mawili; la kwanza, Chuo Kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili, kishirikiane na Chuo Kikuu cha Sokoine, ili wafanye utafiti wa tiba asili na tibalishe, ili tupate ufumbuzi wa kudumu kwa magonjwa, hasa magonjwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa pili, nashauri Wizara ya Afya iweke mkazo mkubwa sana katika elimu yak inga na matumizi ya tibalishe, ili tukabiliane na matatizo hasa magonjwa sugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa tunatengeneza kizazi chenye vijana na watoto wenye matatizo makubwa sana ya afya kutokana na utumiaji wa chakula cha wanga kilichopita kiasi, matumizi ya sukari, matumizi ya chumvi kupita kiasi na mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri wakati sasa umefika kwa Madaktari wa Kitanzania wafundishwe umuhimu wa kutumia tibalishe katika matibabu, badala ya kuelekeza nguvu zao katika matumizi ya dawa za kemikali. Kwa bahati mbaya sana wazungu ambao ndiyo waliotuletea dawa za kemikali, hivi sasa wanatoka taratibu taratibu kwenye matumizi ya dwa za kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano Chuo Kikuu Maarufu cha Havard, hivi karibuni kimeanza mafunzo maalum ya

tibalishe, ili kitumike katika matibabu badala ya kuelekeza nguvu kwenye matumizi ya dawa za kemikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu basi Wizara ya Afya nayo itafanya hima kadiri inavyowezekana katika kipindi kifupi kijacho. Chuo kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili pamoja na vyuo vikuu vingine vya tiba hapa nchini, vianze kutoa mafunzo maalumu ya tibalishe kwa ajili ya madaktari na wataalam wengine wa afya, ili tuanze kupunguza taratibu matumizi ya dawa za kemikali na tuelekeze nguvu zetu katika matumizi ya tibalishe katika kuwatibu wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja na nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shonza, jiandae Mheshimiwa Jacqueline Kainja.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kwa kupata nafasi, ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya. Sote tunafahamu kwamba, Wizara hii ni kubwa na Wizara ambayo ina changamoto nyingi, lakini wanasema mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Mheshimiwa Ummy anafanya kazi kubwa sana. Tumeshuhudia namna ambayo anavyopambana usiku na mchana kushughuluikia changamoto katika sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi kubwa ambayo Wizara inafanya, lakini kama hawapewi fedha za kutosha hususan Fedha za Miradi ya Maendeleo, itakuwa ni kazi bure. Tumeeleza kwenye Taarifa yetu ya Kamati kwamba, mpaka kufikia Mwezi Machi bado inaonesha mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha. Kwa hiyo, kwa sababu tumebakiza miezi miwili kuweza kumaliza Mwaka huu wa Fedha, nipende kuomba Serikali iweze kutoa fedha zote ambazo zimebaki ili ile

miradi ambayo imepangwa kuweza kutekelezwa kwenye Mwaka huu wa Fedha iweze kukamilika, kwa kuwa tunaenda kupitisha Bajeti ya Mwaka 2024/2025, niombe pia Serikali iweze kuhakikisha kwamba, katika bajeti ijayo fedha zote zinatolewa kwa wakati, ili kuweza kutimiza lile lengo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha kwamba, watanzania wanapata huduma bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mambo ambayo Rais wetu atakumbukwa, mojawapo ni kusogeza huduma karibu na wananchi, hususan Wananchi wa Vijijini. Vilevile, Mheshimiwa Rais wetu amefanya kazi kubwa sana, ameboresha huduma za kibingwa na bingwa bobezi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati, tumetembelea maeneo mengi, tumeenda pale Muhimbili, *MOI, JKCI, Ocean Road,* Bugando na maeneo mengine. Maeneo yote haya tumeona namna gani Mheshimiwa Rais amefanya uwekezaji mkubwa hasa katika kununua vifaa vya kisasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi natoka kwenye Mkoa wangu wa Songwe, Mkoa wa Songwe ndani ya miaka mitatu ya Mheshimiwa Rais, tumepata Hospitali ya Wilaya ya Songwe, Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma, Hospitali ya Wilaya ya Momba, maboresho makubwa yamefanyika kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ileje, pia Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe imekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii ni kubwa sana. Amezungumza Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kwamba, tayari sasa Serikali imeshaboresha miundombinu kwa maana ya kujenga majengo ya kisasa, vilevile, kuweza kununua vifaatiba vya kisasa. Kazi kubwa iliyobaki ni kuweza kuboresha huduma na ili tuweze kuboresha huduma ni lazima tuhakikishe kwamba, tunayo ikama ya kutosha ya watumishi katika ngazi zote za afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tuna changamoto kubwa ya upungufu wa watumishi katika nchi yetu. Ukisoma takwimu mahitaji ni 219,061 waliopo sasa hivi ni 126,925 sawa na 58% tu. Changamoto hii ni kubwa hata katika Mkoa wangu wa Songwe, tumepata vituo vya afya vya kutosha lakini

changamoto kubwa ni watumishi. Tuna vituo vya afya ukienda pale Chapwa au Chipaka na Chiwezi vimekamilika lakini bado havijafunguliwa kutokana na kwamba, hatuna wataalam wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali kama ambavyo Mheshimiwa Rais anavyofanya miaka yote, tunaomba Serikali iendelee kutoa vibali vya ajira hususan katika sekta hii ya afya, vilevile, waweze kutukumbuka katika Mkoa wangu wa Songwe, Mkoa ambao ni mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize pia kwa kuznungumzia changamoto moja, nizungumzie kuhusiana na na Sera ya Afya. Sera ya Afya ya Mwaka 2007, imesema wazi kwamba huduma za mama na mtoto ni bure na Serikali ilivyokuwa ikileta hiyo sera haikuleta kwa bahati mbaya, Ilileta hiyo sera kwa sababu ilijua kwamba, ni lazima tuweze kumlinda mama pamoja na mtoto. Ni wazi kwamba, kwenye baadhi ya maeneo mengi sera hiyo haitekelezeki ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano kwenye Hospitali yetu ya Mkoa wa Songwe, sasa hivi mwanamke akienda kujifungua pale analipa kati ya shilingi 120,000 na 140,000. Hata akienda na vifaa vyake, vile vifaa vinakataliwa analazimishwa kwamba anunue vifaa pale pale hospitali na kwa hili nimpongeze sana *RMO* wetu wa Mkoa, kwa sababu tayari ameshalifanyia kazi, ameshamwajibisha mtumishi mmoja ambaye ndiye alikuwa anahusika kwenye kuwauzia vifaa na kuwalazimisha wakinamama waache vifaa vyao, wanunue vifaa vipya pale hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni changamoto kubwa na siyo mpya hata kwenye Hospitali yetu ya Wilaya ya Mbozi, nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja, akalifanyia kazi na changamoto hiyo kwenye Hopsitali ya Wilaya ya Mbozi imesiha. Kwa hiyo, imebaki kwenye Hospitali yetu ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe tunafahamu huenda kwa mazingira yaliyopo sasa hivi ikawa sera hii haitekelezeki.

Tunajua kabisa kwamba tunaenda sasa hivi kwenye bima ya afya kwa wote. Mimi nimuombe dada yangu Mheshimiwa Ummy, wewe ni mwanamke ni mchapakazi unafanya kazi nzuri sana. Sisi tunaomba tu, kama sera hii sasa hivi haiendani na mazingira ya sasa hivi, mimi niombe sera hii iletwe hapa Bungeni ibadilishwe, ili angalau mwanamke anapokwenda kujifungua ajue kabisa kwamba anahitaji kuwa na fedha anahitaji kuchangia kuchangia. Kuliko mwanamke anatoka nyumbani, anajua kwamba huduma ni bure, anafika hospitali anaambiwa kwamba achangie, hii ni changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuamini Mheshimiwa Ummy hili ni jambo dogo sana kwako ambalo lipo ndani ya uwezo wako. Mimi niombe kwa sababu tunajua azma ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba anapunguza vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Shonza. Mheshimiwa Jacqueline. Ajiandae Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi na kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Afya, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya kwa kuleta maendeleo katika sekta hii na Wizara nzima ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi zote hizo za kumpatia Mheshimiwa Rais ni pamoja na kazi kubwa anazozifanya zinazoonekana kwa kusambaza huduma za afya hususan kwa wananchi ambao wana matatizo ya ugonjwa wa moyo ambao kwa hivi sasa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato wanaweza kupata huduma hizo, lakini vilevile huduma za kansa, Hospitali ya Bugando wanatoa huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa ni mmoja wa Wanakamati wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI tumeweza kutembelea

na tumejionea namna gani Wizara hii inafanya kazi na imepanua wigo mkubwa zaidi kwa wananchi kuweza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niweze kumpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya pamoja na Naibu wake kwa bajeti nzuri na kwa kazi wazozifanya, wamekuwa ni Mawaziri ambao wapo *site* muda wote, wanasikiliza ushauri wa Kamati na wanasikiliza ushauri wa Wabunge wenzao. Lakini vilevile niwapongeze watendaji wetu kuanziaa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Naibu Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali, Mfamasia wa Serikali na watendaji wote wa Wizara hii ya Afya, hususan watendaji wetu kuanzia ngazi ya zahanati mpaka Hospitali ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pamoja na pongezi zote hizo kuishauri Serikali kwa maana ya maboresho katika Wizara hii na moja kwa moja nilikuwa naomba lichukuliwe kwa upana sana jambo ambalo natamani kulishauri hapa, nalo ni suala la Kurugenzi ya Huduma ya Dawa na Vifaa Tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri mlichukulie kwa upana jambo hili kwa sababu moja; kwa nini naomba kuwe na Kurugenzi ya Huduma ya Dawa na Vifaa Tiba. Ni kwa sababu tayari tumekuwa na kurugenzi nyingi ndani ya Wizara hii ambazo zinafanya kazi vizuri na tija inaonekana, lakini Kurugenzi hii ya Huduma ya Dawa na Vifaa Tiba ikipatikana tunaweza tukaboresha zaidi kada hii ya *pharmacy* kwa maana ya kwamba kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu kada hii au idara hii ya *pharmacy* kwenye suala zima la mapato ya hospitali ndio idara ambayo inaingiza mapato kuanzia asilimia 48 mpaka 50 na 60, kuanzia ngazi za zahanati mpaka Taifa, lakini haina kurugenzi ya idara hii kwa sababu wanakosa kwenda kuingia kwenye vikao vikubwa kama Bodi ya Hospitali hawapo, *management executive* hawapo, kwa hiyo, wao wanaingia kwenye vikao vya hospitali. Nani anayewasemea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunapeleka pesa nyingi kwenye idara hii, tunashindwaje kuitengenezea kurugenzi yake ikiwa kama Kurugenzi ya Maabara na Mionzi wanayo, lakini vilevile kuna Kurugenzi ya Madaktari, kuna Kurugenzi ya Manesi, kuna Kurugenzi ya *Surgical*, yaani hii *pharmacy* ina shida gani mpaka mnashindwa kama Wizara kuona ina haja ya msingi ya kuweka kurugenzi yake, kwa sababu pesa wanazalisha ni nyingi na bajeti ni nyingi ambayo inaenda kwenye idara hii ya *pharmacy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile tumekuwa na hoja ya kusema kwamba kuna Mfamasia Mkuu wa Serikali, lakini Mfamasia Mkuu wa Serikali hana Kurugenzi ambayo ni wasaidizi wake, lazima tumtengee kurugenzi kuanzia mkoani, Hospitali zote za Kanda ziwe na kurugenzi ili waweze kuwa wanaingia kwenye vikao nani anayewaongelea hawa, kada kubwa kama hii ambayo inapeleka pesa nyingi, inaingiza mapato mengi kwenye hospitali, shida ni nini? Mnataka kuidogosha hii fani kwa sababu zipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba muweze kuajiri wataalam wapo wengi na muweze kuwaingiza kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya, hospitali zote waweze kupatikana. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma. Jiandae Mheshimiwa Neema.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake. Kwa kweli umefanya kazi kubwa kwenye nchi hii, mimi nimekaa Tanga, naenedelea kuwaomba

Wanatanga, wasije wakaipoteza hiyo bahati. Hata kama wanakupiga majungu, alama uliyoiweka kwenye nchi hii naona kama wanapoteza muda, ni bora wakakuunga mkono ili uweze kuendelea kuitumikia Tanga yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na rafiki yangu Janabi. Kwa kweli tunamuheshimu sana Janabi. Ni mtu anaheshimika sana pengine labda hajielewi kama profesa, maneno anayoyatamka mtakuja kujaza watu wana utapiamlo kwenye hospitali, kweli. Maana yake watu wanaona vitu vinavyozungumzwa na mtu tunayemuheshimu sana kaka yetu Janabi, wanafuata hayo maelezo. Sasa hivi nikuulize unataka mtu ale kijiko kimoja kama alivyosema mwenzangu, sisi tunaamka saa kumi na moja kwenda shambani tunakunywa uji saa saba, halafu tunapiga *free* mpaka jioni kwenda kula nyumbani. Sasa unaniambia ninywe kijiko kimoja cha uji, nitalimaje ndugu zangu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba sana Profesa Janabi, masomo yako ukiwa unaeleza hebu waeleze wale watu wa Dar es Salaam, Arusha mjini mjini, wanaokula chipsi hawana kazi nzito, hasa wale wanaoshinda ofisini, nyie Wabunge lakini mtu tuko *field* shambani, hapana Profesa hapo itabidi niku-*challenge* maana mimi ni Daktari mwenzio, itabidi ushike *break* kidogo kwenye hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, suala la kadi za kliniki. Umesema vizuri sana Mheshimiwa Ummy, sasa, hakuna tena kuuza kadi za kliniki, umetengeneza vitabu. Hebu toa na waraka na sisi Wabunge utupatie, maana mnaandika vitu haviuzwi unakuta hospitali havipo, halafu mpiga debe ni yule aliyeko hospitali nenda pale. Sasa hii inatuchanganya kwa kweli, naomba utoe waraka kabla Bunge halijaisha na sisi Wabunge twende na huo waraka ili tuweze kukusaidia kuzungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu. Mimi huwa nafanya tafiti zangu kulingana na elimu yangu. Chanjo ni nyingi sana, na nimejaribu kujiuliza mbona zinafumuka ghafla na chanjo hizi

zinafanywa na wafadhili. Tusipoangalia tumekataa suala la ushoga humu ndani, tutakuja kuwa na mashoga waliopandikizwa ushoga bila sisi kujijua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumze tulisema hapa kwa mfano, hebu leo mjaribu kutembea tu huko mashuleni na wapi. Angalieni watoto wetu, mtoto ana miaka saba, nane maziwa yamelala karibu yanafika tumboni, kibaya zaidi mpaka watoto wa kiume sasa hivi wana maziwa. Mimi nasema ukweli labda kama nyie hamtembei mkaona hayo mambo. Hata mimi nina watoto lakini najiuliza mbona sisi mtu kuota maziwa alikuwa anaota ana miaka kumi na kitu. Miaka saba, nane anavaa sidilia, sasa, utafiti ukoje? Kwa sababu kwanza nyinyi wenyewe kwenye Wizara yako Mheshimiwa Ummy, hamfanyi utafiti. Tunapiga kerere hamfanyi utafiti, *NIMR* ina bajeti gani inafanyaje utafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nenda *SUA* nimepita juzi. Mimi huwa najaribu *whisky* kidogo, *bar* zote pale ni za maprofesa wa Chuo cha *SUA*. Badala ya kulima mashamba muuze *products* Kariakoo, mmefungua *bar*, sasa hivi vitu mnafika mahali nani atatufanyia utafiti? Hivi ni kweli wazungu watoke Ulaya waje watuthamini sisi kutufanyia utafiti, vitu vya kula tumboni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna kuku wa siku saba, siku 21 mnakula kuku kwenye kikaango imekaangwa, paja linalingana na mkono, mnataka utafiti wa *design* gani? (tushtuke kwa *design* gani?) Zamani sisi tunakua matikiti maji kazi yake ni kumwagilia, leo matikiti maji yana dozi za sindano, jamani huu ni utafiti wa *SUA* kweli? Nendeni huko kwenye vijiji vyetu tunapokaa kule. Utanisamehe sana kwa sababu naelimisha jamii. Leo utakuta mashirika ya kigeni yanazunguka kutahiri vijana, kuchoma saratani ya shingo ya kizazi. Ukienda kwao wazungu kutahiri siyo muhimu, tunataka tushtuliwe namna gani jamani? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mnapata hizi saratani, kila siku mnafanya uchunguzi. Ninakuomba sana, kama tumekosea kwenye utafiti ni bora watu wetu wa ndani wakafanye utafiti, tule vitu vilivyofanyiwa utafiti na watu wetu kwa sababu,

wala hamuwezi kupingana na mimi. Juzi-juzi hapa tumekunywa dawa za kikohozi, miaka miwili tunakunywa, wamekuja kuibuka ndiyo mnakimbilia kuzitoa kwenye maduka; watu tumeshakunywa tunaunguza maini kwa hiyo, kila siku tunaugua matumbo na vitu vingine. Ninakuomba sana Mheshimiwa Ummy, kama tulikosea kuweka pesa nyingi kwenye utafiti, basi wawezeshe *NIMRI* wafanye. Hata huko *SUA* zungumzeni lugha moja, Profesa kazi yake ni utafiti, siyo kuuza baa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni, mimi ninatoka kijijini, tulipitisha sheria humu juu ya pesa ya kuwaongezea madaktari wanapoamshwa usiku kunapokuwa na wagonjwa, hamleti hela. Sisi wengine tunatoka maeneo ambayo ukimpigia daktari kwamba, kuna dharura anapishana na fisi kama sita, halafu anakuja huku anatoka mfuto. Watu tunadai shilingi milioni 15 unaleta shilingi milioni nne, kesho ukimuamsha ataamka kweli? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri haya mambo tuliyapitisha. Ni bora uyasimamie watu wetu kule vijijini wapate hizo pesa ziweze kuwasaidia. Ninakupa mfano tu kwa *Geita DC; Geita DC*…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa. Mheshimiwa Musukuma, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka nimpe Mchangiaji Taarifa, hasa alipokuwa anazungumza kuhusiana na tafiti dhidi ya pombe. Ninaungana naye kwa sababu, sasa hivi kuna pombe ambazo zipo mtaani zinaitwa *Cooker*, nyingine Roboti, nyingine Shing’waa, zinateketeza kizazi chetu kwa magonjwa ya ini na wengine wakinywa wanakufa hapohapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wangekuwa wamefanya utafiti hizi pombe zingezuiwa zisiuzwe mtaani, lakini zinauzwa.

Ukiona mtu ameshikilia ka-*energy*, ujue ameweka *Cooker*, *Robot*, *Shing'waa* na Ching'waa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sibishani na dada yangu kwa sababu, ni mteja wa hivyo vitu. Kwa hiyo, ni kitu amekifanyia utafiti. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dada yangu Mheshimiwa Esther Matiko amezungumza suala zuri sana na hili siyo la kufanyia mzaha. Nendeni mkakae bandarini leo, angalia *spirit* zinavyoingia Tanzania halafu uliza zinakouzwa. Leo hakuna pombe *original* humo, zimening'inia pombe *fake*, halafu watu mnaanza kuwatolea vifurushi vya kwenye *NHIF* kwa sababu, ninyi mmekosa udhibiti tunakunywa majitu matakataka. Watu wanaweka majani ya chai, watu wanaweka mpaka rangi za viatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jamani hii nchi kwa kweli, kama tumekosa watafiti na udhibiti. Kuna *TBS,* kuna nani, vimepita wapi hivi vitu? Nendeni mkaone makontena mangapi yanapita kila siku? Yanaenda wapi ikiwa viwanda vinaagiza vyenyewe? Hawa watu wapo wana viwanda viko sebuleni watu wanatengeneza pombe wanauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukipita mtaani ukitupa chupa ya *Heineken* inanunuliwa, ukitupa ya *Whisky* inanunuliwa. Unajiuliza zinaenda wapi? Mnahitaji kupata *degree*? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Musukuma, ahsante.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema. Jiandae Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Iddi Kassim jiandae. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia kwenye Bajeti ya Wizara ya Afya. Kwanza kabisa, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Ummy Mwalimu pamoja na Naibu Waziri Dkt. Mollel na viongozi wote kwa kazi kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na muda nitakwenda moja kwa moja kwenye maeneo ninayotaka kuchangia. Eneo la kwanza ni kuhusuiana na lishe. Nimefurahi katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba, lishe ni moja ya maeneo yake ya kipaumbele, lakini jambo ambalo ninapenda kumwomba sana Mheshimiwa Waziri ni waende wakaangalie upya umuhimu wa Taasisi yetu ya Chakula na Lishe *(TFNC)* kwa sababu, bado Taifa letu lina changamoto kubwa ya masuala ya udumavu, utapiamlo pamoja na lishe kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapahapa ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri arejee Taarifa ya Tafiti ya Hali ya Lishe Nchini ya Mwaka 2018 ambapo waliahidi wataanza kuwashauri wadau wa maendeleo miradi ya lishe iende kwenye maeneo yote ambayo yana uhitaji, lakini hayafikiwi. Hivi karibuni, Mwezi wa Nne, umeziduliwa mradi mpya wa lishe na imechaguliwa mikoa mitano yenye hali kubwa ya udumavu, lakini Mkoa wa Kagera haujachaguliwa, ilhali ndiyo mkoa ambao unaongoza kwa idadi halisi ya watoto wenye udumavu. Kwa hiyo, ninamuomba sana Mshehimiwa Waziri ahakikishe kile ambacho aliahidi kwamba, Serikali itafanya kufikia uwiano wa miradi ya wadau wa maendeleo kinafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Tunafahamu jiografia ya Mkoa wa Kagera na changamoto za milipuko ya magonjwa mbalimbali, ni muhimu sana na jambo hili nimeshaliomba hapa Bungeni, tunahitaji Serikali ijenge Kituo cha Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko Mkoani Kagera, ili kuhakikisha kwamba, jitihada za Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, za kuimarisha afya nchini zinafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, isiwe tu pale ambapo kuna mlipuko wa magonjwa kama ilivyotokea …, basi

wadau wa maendeleo wote wanakuja Kagera na hali ikitulia wanaondoka. Mheshimiwa Waziri ninaomba utakapokuja kuhitimisha utueleze ni lini Kituo hiki cha Kudhibiti Magonjwa ya Mlipuko kitajengwa Mkoani Kagera kwa sababu, mara kadhaa nimeshaomba hapa Bungeni na ukaahidi hata kwenye bajeti iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni, ninaipongeza sana Serikali, nimeona imetangaza ajira kwa ajili ya *CHW* (Wauguzi wa Afya Ngazi ya Jamii). Ninashukuru kati ya wilaya ambazo zimepata pia, ni pamoja na Wilaya ya Bukoba Mjini, lakini Serikali imeweka kigezo kwamba, ili mtu apate ajira ile ni lazima awe na kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo sawasawa kwa sababu, watu wamekuwa wakijitolea kwa zaidi ya miaka minne bila kutakiwa kuwa na hiki kigezo. Natolea mfano pale Bukoba Mjini, sisi tumekutana na *CHW* 71, kati ya hao 71, 37 wana Darasa la saba peke yake, lakini wamekuwa wanafanya kazi hii kwa zaidi ya miaka minne. Leo tu kwa sababu imetokea ajira, basi *CHW* wale wanakuwa hawafai kwa sababu hawa kigezo cha kidato cha nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha atupatie ufafanuzi wa hiki kigezo cha lazima kuwa na kidato cha nne wakati *CHW* wamekuwa wakifanya kazi hii wakiwa hawatakiwi kuwa na hicho kidato cha nne. Hii itasaidia sana kuongeza motisha na kuondoa unyanyapaa kwa kigezo tu cha hawana kidato cha nne, wakati walikuwa wakifanya hiyo kazi hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kwa harakaharaka, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amehakikisha zaidi ya halmashauri 100 zimepata *dentist chair* (viti vya kufanya upasuaji wa kinywa na meno), lakini ninatumia fursa hii kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba sana Waziri utoe maelekezo. Pale kwenye hospitali yetu, Kituo cha Afya cha Zamzam, Bukoba Mjini, tumepokea hiki kiti *(cha dentist chair)* toka

Mwezi wa Tisa mwaka jana, mpaka leo kipo tu kwenye maboksi. Mheshimiwa Waziri utafika wakati vitu vitaanza kupotea *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Bukoba Mjini, Hospitali ya Mkoa tu ndiyo ina kiti hiki, *(cha dentist chair),* kwa maana ya kufanya upasuaji wa kinywa na meno, wakati Mheshimiwa Rais amepambana mmepata fedha. Gharama ya kiti hiki ni zaidi ya shilingi milioni 140, ninaomba utoe maelekezo, ili wahusika wafike kwenye Kituo cha Afya cha Zamzam waweze kufunga kiti hicho *(*cha *dentist chair)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitimisha kwa hoja yangu ya siku zote, suala la *TFDA*. Tumesikia Wabunge wengi wakichangia, na hata kwenye bajeti pia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, jambo la magonjwa mbalimbali ambayo yanaongezeka kwa kasi, *cancer* ya koo, *cancer* ya utumbo na magonjwa mengine mengi kama figo na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuendelea kuweka suala la udhibiti wa chakula *(food safety)* chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Huu ni mwaka wa nne sasa, kila mwaka Mheshimiwa Waziri anatuambia suala hili limefika mwisho, lakini mbona halifiki mwisho? Mheshimiwa Waziri, unasema na unatueleza mara nyingi mzigo mkubwa ambao *NHIF* inao kwa kutibu magojwa haya yasiyoambukiza, lakini magonjwa mengi yanatokana na uholela wa kuingiza vyakula nchini, yanachangiwa na kutokuwa na udhibiti imara wa usalama wa chakula *(food safety)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani kote, *best practice* ni masuala ya usalama wa chakula *(food safety)* yanapaswa kuwa chini ya Wizara ya Afya. Mheshimiwa Waziri, wewe ni mmoja kati ya Mawaziri wabobezi mnaosifika sana Barani Afrika, usiache hili suala liendelee kuwa doa kwako. Hata hivyo, Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alishatuambia hapa Bungeni Wizara ya Afya mfanye kazi pia ya kudhibiti magonjwa na siyo tu kutibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tutawezaje kudhibiti magonjwa kama jambo la usalama wa chakula *(food safety)*

tunaendelea kuliacha kuwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara? Suala la afya ya binadamu na maisha ya binadamu siyo suala la kuangalia maokoto na tozo zinazopatikana. Ni suala la uhai na hivyo ninaomba utakapohitimisha utupatie maelezo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina. Jiandae Mheshimiwa Kassim Iddi.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa nafasi. Pia, ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana madaktari, wauguzi na wataalamu wote wa Sekta ya Afya kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuokoa Maisha ya wananchi wetu, lakini wapo wa Tiba Asili na Tiba Mbadala ambao na wenyewe wanafanya kazi kubwa sana ya kuokoa maisha ya wagonjwa wetu. Nao tunawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri. Bila kuwasahau viongozi wetu wa dini zote kwa maombi na dua wanazozifanya kwa wagonjwa wetu, hatimaye mambo yanakuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengi Waziri ameyazungumza, hasa haya mambo 10 ambayo ni mageuzi makubwa ndani ya miaka mitatu ya kusisimua ambayo mimi ninaipongeza Wizara ya Afya na Mheshimiwa Rais kwa mageuzi hayo makubwa yaliyofanyika kwenye sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tumefanya mambo mengi mazuri, kwa mfano udhibiti na usimamizi wa vifaa tiba, ukoje? Vifaa vyetu vinafanya kazi? Taarifa zinaonesha kuwa, asilimia 14 ya vifaa vyetu vyote pamoja na mitambo tiba ambayo ipo

kwenye maeneo ya kutolea huduma haitoi huduma, imewekwa tu, wamei-*park*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo changamoto nyingi, moja ni hili la usimamizi ambapo, vifaa vya kitabibu vinaingizwa nchini bila kukaguliwa. Taarifa ya *TMDA Post Market Surveillance Report* ya Mwaka 2022/2023 inadhihirisha wazi kwamba, mashine na mitambo ya kitabibu inayoingia nchini, asilimia 28 inaingia bila ukaguzi. Sasa, kama mitambo inaingia bila ukaguzi na mitambo mingine ni hatari, yenye mionzi, halafu wananchi wetu wanaenda kuhudumiwa kwenye mitambo ile ambayo haikukaguliwa, ambayo haikuthibitishwa ubora wake. Ni nini tunategemea katika huduma pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Nibu Spika, moja, mgonjwa anaweza akatibiwa, anaweza akafanyiwa uchunguzi yakapatikana matokeo ya uchunguzi ambayo si ya ugonjwa ule anaougua na akatibiwa matibabu yasiyostahili. Sasa asilimia 28 ya mitambo yetu inaingia bila kukaguliwa hapa nchini. Ni jambo ambalo limeruhusuwaje? *TMDA* wameliruhusu vipi jambo hili? Waziri wa Afya ameliruhusu vipi jambo hili kufanyika hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, vifaa hivi vya kitabibu vimekuwa viki-*operate* bila mwongozo. Asilimia 61.3 inaonekana mitambo yetu hii inapokwenda kule kwenye matumizi inafanya kazi bila kufuata mwongozo, zile *COPs*. Matokeo yake ni mitambo hii inaharibika mara kwa mara, mitambo hii haifanyi kazi mara kwa mara na kuleta ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni utunzaji usioridhisha wa hivi vifaa na mitambo ya tiba ambapo utunzaji wake siyo mzuri. Asilimia 72 ya vifaa katika meneo yetu havifanyiwi matengenezo kwa wakati na matokeo yake haiwezi kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi changamoto hizi, tumenunua vifaa na mitambo ya tiba kwa fedha nyingi za Watanzania, ili ziweze kutoa huduma, lakini matokeo yake hazisimamiwi kikamilifu. Matokeo yake badala ya kwenda kutatua matatizo ya

afya tuliyonayo, yanaenda kutengeneza matatizo mengine ya kiafya. Sasa, jambo hili linaruhusiwaje kutokea? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni upatikanaji wa dawa na huduma za afya. Tumeelezwa hapa kwenye taarifa kwamba, *MSD* imeshindwa ku-*meet orders* zake kwa asilimia *24*. *Average* ya *MSD* imeshindwa ku-*meet orders* zake kwa asilimia 24 na sababu kubwa ni deni la Serikali ambalo limefikia shilingi bilioni 366. Pia, *NHIF* imeshindwa kulipa *commitments* za wateja wake kutokana na deni kubwa ambalo inaidai Serikali, deni la shilingi bilioni 208. Matokeo yake ni wanaopata huduma kupitia *NHIF* hawapati matibabu kwa sababu, *NHIF* wameshindwa kuwalipa wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeshakatwa pesa miaka mitano, Serikali imeenda kukopa hela mnaenda kuzitumia kwa shughuli zenu, halafu mimi ninaenda kukosa huduma. Wananchi wetu wanahangaika sana, watumishi wetu wanahangaika sana na jambo la Serikali kulipa haya madeni ya *NHIF,* tumesema muda mrefu. Tuseme kwa lugha gani sasa, ili haya mambo yatekelezwe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninadhani kwamba, leo tuoneshe mfano tusipitishe hii bajeti ya huyu Waziri wa Afya ili kwamba, fedha zilizoombwa za *MSD* kiasi cha shilingi bilioni 562 na deni la *NHIF* la shilingi bilioni 208 lilipwe na Serikali. Zaidi ya hapo tusikubali hii bajeti ipite kwa sababu, tutakuwa hatutendi haki kwa wananchi kwa sababu, hawawezi kupata huduma ya afya na badala yake itakuwa ni kuzungushwa tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliseme hili la kufutwa kwa Taasisi ya Chakula Lishe. Tangazo la Waziri Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo la kufuta taasisi nne na kuunganisha nyingine 16, tulishakubaliana hapa kwamba, kwanza ni batili na lipo kinyume cha sheria. Taasisi kama hii ya Lishe sasa hivi imekosa *commitment* kutoka kwa wadau. Tulikuwa tunapata shilingi bilioni nane kila mwaka kwa ajili ya mambo ya lishe, lakini hatutazipata hizi fedha kwa tangazo la Mheshimiwa Prof. Mkumbo kwa sababu, wale

wameshaona kwamba, ninyi hamko *serious* kwa hiyo, fedha zao hawajaweka mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa migogoro kwenye mipango ya Serikali, Waziri Mkuu atoe tamko hapa Bungeni la kufuta hayo maamuzi ya Mheshimiwa Prof. Mkumbo mpaka pale Serikali itakapokuwa imekubaliana na sisi Bunge. Mpaka tutakapokuwa tumekubaliana kwa pamoja kuondoa, ni nini kifutwe na nini kiunganishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Serikali na Kamati wanakiri kwamba, huduma za matibabu ya kibingwa na ubingwa bobezi zilikuwa zikifanyika hapa nchini bila Sheria. Wamekiri hivyo, Kamati imekiri hivyo na Waziri amekiri hivyo. Sasa wamesema Sheria zitungwe, zisitungwe Sheria za kuruhusu kuongeza makalio na matiti kwa sababu, zile haziruhisiwi kwa mujibu wa Sera yetu ya Mwaka 2007. Kwa hiyo, usije ukatumika huu uchochoro wa kusema kwamba, sasa tunatunga Sheria. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi sikuwa na tatizo na zile huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, zile ambazo zinaruhusiwa kwa mujibu wa sera za nchi, sina tatizo nazo, hata zilipo-*operate* bila kuwa na sheria, bila kuwa na mwongozo, bila kuwa na kanuni. Kwa mfano mtu anabadilishiwa figo, mtu anafanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo, mtu anabadilishiwa kiungo kingine chochote, ini na mambo mengine, sikuwa na tatizo hata bila ya sheria, lakini mambo haya ya kuongeza, na imetumika hapa lugha ya kuongeza makalio na matiti, tusiruhusu nchi yetu kuingia kwenye matatizo makubwa ... *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mhesimiwa Mpina.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba dakika moja.

**NAIBU SPIKA:** Mhehimiwa Iddi Kassim Iddi. Jiandae Mheshimiwa Hawa, jiandae Mheshimiwa Festo. *(Makofi)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii leo niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Afya, dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na mimi leo niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya Waziri wa Afya, lakini pia, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika kuboresha Sekta ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ninamshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya na bado mimi ninaendelea kushangaa mpaka leo na ninajiuliza maswali mengi sana. Kwa nini vyuo vikuu vya Tanzania vya Kada ya Afya mpaka leo havijamtunukia Udaktari dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashangaa sana hata baada ya kupitisha bajeti hii kama vyuo hivi havitaenda kukaa na kutafakari kumtunukia Udaktari kwa sababu, elimu anayoifanya dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni *Open University* na anafanya kwa vitendo na mambo yanaenda vizuri. Amepita kwenye misukosuko mingi, Korona na mambo mengine. Ninawaomba wenye mamlaka muone namna ya kumtunukia Udaktari huyu dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, na yeye awe Daktari kama Mheshimiwa Dkt. Mollel. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana kaka yangu hapo Mheshimiwa Dkt. Mollel, Naibu Waziri, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya. Ninarudia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi mingi ya afya ambayo ametupatia kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mhesimiwa Naibu Spika, Jimbo la Msalala Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Sekta ya Afya ameweza kutupatia vituo vya afya vinne na mpaka sasa baadhi ya vituo hivyo vimekamilika. Naanza na Kituo cha Afya cha Isaka kimekamilika, Kituo cha Afya Segese kimekamilika, Kituo cha Afya Mwalugulu kimekamilka, Kituo cha Afya Bulige ambacho Mheshimiwa Dkt.

Mollel ulikuja na chenyewe kimekamilika na bado mmetupatia fedha nyingine ambazo tumeanza ujenzi wa kituo cha afya kingine katika Kata ya Mwanase. Hamjaishia hapo, mmetupatia fedha, kwa ajili ya kumalizia Hospitali yetu ya Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ninaushukuru sana Mgodi wa *Barrick* kwa kuweza kutupatia fedha kuanzisha chuo cha afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naanza na hili la kumuomba dada yangu, Mheshimiwa Waziri Ummy. Sisi Jimbo la Msalala kupitia Mkurugenzi aliyekuwepo kipindi kile, kaka yangu Berege, tulianza mchakato wa ujenzi wa chuo cha afya kwenye Jimbo la Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, chuo hiki tayari tumekikamilisha na kwa sasa hivi kilichobaki ni umaliziaji wa mabweni. Kipo tayari, tumeshakikabidhi kwao, na Mheshimiwa Dkt. Mollel anafahamu. Niombe sasa, tunahitaji kupokea wanafunzi ili chuo hiki kiweze kuanza mapema ili tuondokane na upungufu wa watumishi tulionao kwenye Jimbo la Msalala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Msalala lina upungufu mkubwa sana wa watumishi kwenye kada ya afya. Niombe Mheshimiwa Waziri na niombe sana TAMISEMI watuongezee watumishi, utaona sasa hivi tuna takribani vituo 12 vya afya na tuna hospitali moja kubwa ya wilaya. Sambamba na hilo tayari tumemaliza zahanati 34 kwa mpigo na hivyo jumla ya zahanati tulizo nazo ni 52 kwenye Jimbo la Msalala. Hata hivyo bado tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi wa sekta ya afya. Niendelee kuomba watuletee watumishi wengi wa kada ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nizungumzie habari ya huduma inayotolewa kwenye vituo vyetu vya afya. Ni kweli kabisa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassa ametupatia fedha kwa ajili ya kuimarisha vituo vya afya kwenye maeneo yetu, lakini je, huduma inayotolewa kwenye vituo vya afya na zahanati inaendana na uhalisia? Niombe sana, kumekuwa na matukio mengi kwenye vituo hivi vya afya hasa kwenye usimamizi mzuri

wa kutoa huduma ya afya iliyokuwa bora kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Kituo cha Afya Bugarama. Kituo hiki kimekuwa kikilalamikiwa sana na wananchi kwenye maeneo hayo, wananchi, hasa akina mama wa maeneo hayo wamekuwa wakipoteza maisha katika Kituo cha Afya cha Bugarama. Niombe sana ikiwezekana atume tume yake iende kwenye hiki Kituo cha Afya Bugarama, iende ikachunguze ni sababu zipi ambazo zinapelekea akina mama wajawazito kupoteza maisha kwa wingi kwenye Kituo cha Afya Bugarama, inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tumepeleka vifaa tiba kwenye maeneo hayo ya vituo. Kwenye hiki Kituo cha Afya Bugarama tumepeleka mashine za meno, *X-ray machine* na pia *Ultrasound,* lakini bado hatujapeleka wataalamu wa kwenda kuvitumia. Mimi wakati mwingine huwa najiuliza; hebu nimwombe na nimshauri Mheshimiwa, dada yangu Ummy, kwamba wakati sasa umefika wa kuibadilisha hii sekta ya afya ili ikatoe huduma za kibiashara na si huduma za bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vyote wameshusha huko, wametuletea, wametujengea vituo vya afya, wametuletea vifaa tiba lakini hadi sasa hivi tunavyozungumza vile vifaa tiba vyote vya *X-ray machine*, *ultrasound* na hiyo *dental chair* wameweka stoo kwa sababu hakuna watu. Yanakosekana tu maarifa ya hata kuweza kuajiri watumishi wa kuweza kuvitumia kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Kituo cha Afya Ngaya wametuletea vitanda na vifaa tiba pale lakini tumekosa fedha kidogo za kumalizia *OPD* ili vifaa vile vifungwe na kuanza kutumika; leo vimewekwa stoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana waanze kuwapima ma-*DMO* nama-*in charge* kwenye vituo vyao kwa *performance* yao ya ukusanyaji mapato, utoaji wao wa huduma kwenye maeneo yale ili wananchi wetu waweze ku...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Iddi. Sasa namwita Mheshimiwa Hawa, jiandae Mheshimiwa...

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na sasa nimesimama kuchangia katika Wizara hii ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri na naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya, wamekuwa na ushirikiano mzuri kwetu. Hata pale tunapokuwa na changamoto wamekuwa wakitusikiliza na kuzifanyia kazi zile ambazo zinawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naomba nijielekeze zaidi kwenye suala la maradhi ya figo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili imekuwa ni janga, ni janga ni janga kubwa kwelikweli. Kama Taifa hatutaangalia maradhi haya ya figo kwa Watanzania tutakwenda kuwamaliza Watanzania kwa ugonjwa huu kuliko hata tunavyofikiria. Ugonjwa huu umekuwa mkubwa sana. Mimi nazungumza kwa sababu kama Mbunge nina kesi sita za wagonjwa wa figo *serious* kabisa katika Manispaa yetu ya Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miezi miwili iliyopita kati ya kesi sita, tumempoteza mama wa katibu wangu kwa maradhi ya figo. Pale Tabora tunayo hospitali ya rufaa lakini haina kitengo maalum kwa ajili ya *dialysis*. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, watu wetu wanaangamia kwa kukosa huduma za kufanya *dialysis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza kuna ustaadhi mmoja yupo pale Tabora, Ustaadhi Mtoro, figo zote mbili zimekufa, wananchi tumemchangia mpaka sasa hivi

tunaendelea. Hata hivyo kila siku mkeka wa kuchangia unapungua kwa sababu watu wameshafikia mahali wanachoka kuchangia. Niombe sana, na hili suala nilimwambia Mheshimiwa Naibu Waziri, naamini Mheshimiwa Naibu Waziri analifanyia kazi, wamsaidie huyu Ustaadhi ili aweze kunusuru maisha yake kwa angalau kusafisha hizo figo. Mara tatu kwa siku anatumia shilingi 750,000, kipato ni kidogo hana kipato cha kutosha kuweza kunusuru maisha yake. Nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, niombe sana mbele ya Bunge hili wasaidieni watu hawa, msaidieni Ustaadhi Mtoro ili aweze kuokoa maisha yake, anaumwa sana, figo zote mbili hazifanyi kazi. Kama tusipoangalia huu ugonjwa unakwenda kutuangamiza na unaweza kutumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu na niiombe sana Wizara ya Afya, tunaomba sana katika bajeti ambayo mnapanga, mpange bajeti kubwa kwa ajili ya kuwakinga Watanzania kuliko kutibu Watanzania. Kwa sababu tunachofanya sasa hivi tunatibu zaidi kuliko kuwakinga Watanzania katika kupata haya maradhi...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** ...hususani maradhi yasiyoambukiza...

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimsaidie tu dada yangu mchangiaji tu ili amsaidie Ustaadhi, kwa sababu Ustadhi yuko kule katika jimbo lake na yeye ni Mbunge amkatie tu bima ya afya haya mambo yaendelee yakae vizuri, ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa taarifa hiyo.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bima ya afya haiwezi kufanya *dialysis* popote unapokwenda, na hizo hospitali ni hospitali binafsi, ingekuwa ni hospitali ya Serikali sawa. Lakini hata kwenye hospitali za Serikali punguzeni gharama ili angalau hata sisi Waheshimiwa Wabunge tunaochangia tuweze kuchangia wakati gharama pia zikiwa nafuu; kwa sababu watu ni wengi humchangii mtu mmoja tu, tunachangia watu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana elimu kwa Watanzania kuhusiana na majanga haya ya maradhi yasiyoambukiza itolewe kwa wingi ili Watanzania waweze kuelewa. Wanatoa elimu kwenye *television* na kwenye *redio;* lakini je, ni wangapi wanaangalia *television* ni wangapi wanaosikiliza redio? Tunaomba sana watu wetu waweze kufikiwa, hususani kwenye maeneo ya vijijini, ambako wengi hawana muda wa kuangalia masuala ya *TV* wala kusikiliza redio; ili waweze kupona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia kuhusiana na suala la saratani. Kwanza tuwashukuru Serikali kwa, kweli ni eneo ambalo mnapambana nalo sana. Lakini nimwambie Mheshimiwa Waziri, hili eneo bado ni changamoto kubwa sana. Watanzania wengi mpaka inapofika *cancer stage four* ndipo anakuja kugundua kwamba ana ugonjwa wa saratani. Kama tungekuwa tuna utaratibu maalum kwenye maeneo yetu wa kuwa tunapima afya za hawa akina mama, hususani sisi wanawake ambao tunapata saratani za kizazi nadhani haya maradhi ya *cancer* yangepungua kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo niwashukuru na niwapongeze hata kwa kuanzisha hizi chanjo kwa ajili ya watoto wetu ambao wana miaka tisa mpaka 14, za kuweza kuzuia saratani za shingo za kizazi na matiti. Kwa hiyo niwaombe sana, na bado ninasisitiza kuhusiana na suala la elimu, elimu itolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kumpongeza Profesa Janabi wa hospitali ya Muhimbili kwa kazi kubwa aliyoifanya. Sasa hivi imefika mahali hata mimi binafsi natamani

kwenda Muhimbili kutibiwa, kwa sababu kwanza ukifika pale kwa kweli unapata huduma bora. Tunafahamu kabisa wapo wauguzi ambao wana tabia zao, na tabia siku zote haina dawa. Kwa hiyo unaweza ukaitibu tabia ya mtu ambaye anaweza kurekebishika, lakini kuna wengine hawawezi kurekebishika. Wapo ambao ni watukutu mpaka leo bado hawaelewi, lakini asilimia kubwa sasa hivi ukienda pale Muhimbili unafurahia huduma na unaweza ukapata huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna changamoto kubwa ambayo wanaipata Watanzania wengi wanaopata rufaa kutoka mikoani kwenda Muhimbili. Tungeomba sana wizara iangalie uwezekano angalau wa kuwa na *hostel* kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania ambao wanaleta wagonjwa wao Muhimbili na hawana ndugu pale katika jiji la Dar es salaam, wapate sehemu ya kujihifadhi. Wanalala hovyo, kwa sababu pale hospitalini sasa hivi hakuna hata korido ya mtu kuweza kujihifadhi. Kwa hiyo wanalala hovyo. Unakuta wamelala kwenye vibanda vya chipsi anasubiri asubuhi ifike ili aweze kwenda kumwangalia mgonjwa wake. Kwa hiyo niombe sana... *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** ... angalau watengeneze *hostel* ya watu hata kwa bei rahisi  ya 10,000, 20,000 kwa siku...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wanaweza wakagharamia ili kuweza kusaidia wagonjwa wao ambao wamefikishwa katika hospitali ya Muhimbili. Kwa hiyo niombe sana; na nimpongeze sana Profesa Janabi, kwa sababu sasa hivi hata ukifika pale Muhimbili hakuna vibanda vibanda vya simu, hakuna vibanda vibanda vya chakula, hakuna vibanda vibanda vya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante...

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Hee! *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Kaa na vibanda. Waheshimiwa kwanza tumshukuru Mheshimiwa Rais, kuna mtambo hivi karibuni utafungwa, unaitwa *Positron Emission Tomography*, huu utakuwa una-*detect any warning* za *cancer*. Nafikiri Mheshimiwa Waziri ulisemee hili ili watu wajue Mama, Dkt. Samia anafanya nini kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Festo, halafu jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Jambo la kwanza ninaunga mkono hoja iliyopo mezani ya Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa asilimia 100 kabisa. Nina kila sababu za kuunga mkono kwenye bajeti hii kwa sababu mambo yanafanyika, licha ya ujenzi wa miundombinu lakini pia huduma ya afya jinsi ambavyo inasambazwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mambo machache ya kuzungumza. Jambo la kwanza linahusisha madaktari wanaokwenda mikoani; madaktari wa Dkt. Samia. Hawa ni *mobile doctors* kutoka kwa Mheshimiwa Rais ambao wanazunguka mikoani na kwenye wilaya mbalimbali kwa ajili ya kutibu wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ummy. Katika kipindi chote cha Wizara ya Afya ubunifu huu ambao umefanyika wakati huu wa kuwafikishia huduma za kibingwa wananchi kule waliko sisi ambao tunaamini kwa Mwenyezi Mungu hii ni moja kati ya baraka ambazo anajichotea kwa kuwafikia wazazi wetu kule waliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, madaktari hawa ambao unawakuta wamekaa pale wanatumia muda wao, lakini pili wameonesha uzalendo wa hali ya juu sana kwa kuzunguka mikoani na wilayani na kutumia muda wao kuwasaidia wazazi wetu. Kuna mambo matatu yanajitokeza kutokana na kazi ya kizalendo ambayo wanaifanya watu hawa. Jambo la kwanza,

kwetu sisi Makete wamekuja, wametoa huduma na wanaendelea kutoa huduma. Katika kutoa kwao huduma cha kwanza nilichojifunza ni kushuka kwa gharama za matibabu kwa yale magonjwa ambayo mtu alikuwa anakwenda Muhimbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu alikuwa ana uwezo wa kusafiri kutoka Makete kwenda Muhimbili, kwenda na kurudi ni zaidi ya shilingi laki mbili lakini leo anatumia shilingi 5,000 pale pale Makete kupata huduma hiyo ambayo Mheshimiwa Rais amewafikishia wananchi. Hizi kwetu sisi tunasema kabisa kwamba Mheshimiwa Rais anawatendea haki Watanzania, alikuwa na uwezo kwa jinsi ambavyo amejenga hospitali za rufaa, kwa jinsi ambavyo amepeleka mitambo kama *digital X-rays* pamoja na *CT scan* kwenye mikoa, alikuwa na uwezo wa kuishia hapo lakini Mheshimiwa Rais amewafikia wananchi pale pale walipo, hususani kwenye maeneo ya wilaya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili linalojitokeza kwa huduma ambayo hawa watu wanaitoa ni *capacity building*, wanawajengea uwezo ndugu zetu ambao wapo kule, ambao wamekuwa wakifanya kazi kwenye hospitali hizo kwa muda mrefu. Kwa sababu sekta hii ya afya inakua kila siku, na hivyo kwenda kwao huko hawa madaktari wa Dkt. Samia wamewatengenezea uwezo mkubwa madaktari wetu kwenye hospitali zetu za wilaya namna sekta ya afya inakuwa na kuelimisha. Hiki mnachokifanya Wizara ya Afya hakijawahi kutokea, mnastahili maua yenu. Niwapongeze sana kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge. Niwaombe, kama kuna watu ambao wanapenda... *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi Kingu hapa. Ninaomba nimpe taarifa mchangiaji, kaka yangu, Mheshimiwa Sanga kwamba kitendo hiki cha madaktari hawa wanaozunguka mikoani kimevunja *notion* ya kitaifa na kimataifa, kwamba Tanzania kuwa na *flying doctors* lazima watoke nje. Leo tunashuhudia *flying doctors* wana-*fly* ndani ya nchi yetu kwa kuwasaidia walipa kodi wa Tanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na alichokizungumza Mheshimiwa Kingu. Kwa sababu jambo hili linafanyika kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na niiombe Serikali, kama kuna *incentive* zozote ambazo hawa watu wanastahili kupewa, kama kuna chochote wanatakiwa waongezewe ninawaombea, mimi kwa niaba ya wananchi wa Makete, na Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote tunaomba kama kuna chochote cha kuwasaidia hawa watu wasaidiwe. Hii ni kwa sababu kuna Watanzania wengi walikuwa hawana *access* ya huduma hizi lakini sasa hivi wanazipata huduma pale pale Makete. Mheshimiwa Ummy na Katibu Mkuu wananisikiliza hapa, kwa niaba ya wananchi wa Makete, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Makete lakini pia na viongozi wa Makete tunaomba madaktari warudi lile eneo la Makete kwa sababu wananchi wa Makete walijitokeza kwa wingi lakini muda umekuwa ni mfupi. Tunaomba takribani hata wiki mbili, tatu mkaweke kambi maeneo ya Matamba, Tandala na Lupila ili wananchi wetu waweze kupata huduma. Hili jambo ni la busara, ni la hekima na pia ni la baraka mbele za Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalopenda kulizungumza ni jambo la kiwanda cha dawa, kwa maana ya mipira ya mikono *(gloves)* ambacho kimejengwa pale Idofi Njombe. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais. Kwanza kiwanda hiki kinakwenda kuokoa zaidi ya shilingi bilioni 24 ambazo tulikuwa

tunaagiza *gloves* kutoka nje, saa hivi zinakwenda kuzalishwa Mkoa wa Njombe pale Idofi. Huu ni mkakati mzuri katika sekta ya uchumi kwa ajili ya kuokoa fedha za kigeni kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili tutatengeneza ajira zaidi ya 200 za Watanzania wanaokwenda kwenye kiwanda kile. Tatu kuanza kufanya kazi kwa kiwanda hiki *MSD* inakwenda kutimiza malengo yake kwa zaidi ya asilimia 83.4. Kwa hiyo niiombe Serikali, kwamba kiwanda cha mipira ya mikono *(gloves)* pale Njombe kianze kufanya kazi ili tuokoe fedha za kigeni kwa ajili ya mustakabali mzuri wa Taifa letu, niiombe sana Serikali ilifanye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kuhusiana na bima ya afya kwa wote. Suala la bima ya afya, kwa maana ya *universal healthy insurance* ni jambo zuri, ni jambo ambalo sisi kama Watanzania lazima tuliunge mkono. Suala ni kuiomba Serikali iangalie jinsi ya ku-*finance* hii *project* ili iweze kufanikiwa na Watanzania waanze kupata hii huduma. Dunia nzima imeelekea kwenye *universal healthy insurance*. Ukienda kwenye mataifa ya Jirani kama Rwanda, South Africa na nchi nyingine ambazo tunazizunguka suala la bima kwa wote ni mpango wa dunia, ndiko unakoelekea, kwa hiyo lazima tuiunge mkono na ni lazima tumuunge mkono Mheshimiwa Waziri. Suala ni *financing* ya *project* hii iweze kufanyiwa vizuri na Watanzania tupo tayari kwa ajili la kulifanyia kazi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwenye kazi ambayo anaifanya hususani kwenye sekta ya afya na miradi mingine. Sisi kama wana-Makete tunamuunga mkono, na tumuhakikishie kwamba hakuna kitakachodondoka Makete kwa sababu utekelezaji wa Ilani Makete ni zaidi ya asilimia 90. Kwa hiyo sisi kama wananchi wa Makete tunamuunga mkono na tunapendekeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, Serikali lazima pia iangalie namna gani ya ku-*control*; amezungumza Mheshimiwa Musukuma kuhusu suala la hizi pombe *fake* na *microwaves*. *Microwaves* ukienda kwa watu wa *atomic* wanazitaja kama ni

sehemu ambazo zinasababisha mionzi inayosababisha *cancer;* pia kuna simu *fake*. Serikali lazima iangalie namna ya kudhibiti *microwaves*, na simu *fake* ili kukimbizana na ugonjwa wa *cancer,* kwa sababu umekuwa ni changamoto kubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Waziri na ninamtakia kila la kheri hatuna tatizo na yeye Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, dakika kumi, jiandae Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwa kuwa kiongozi wa mfano na hasa kwa wanawake na watoto wa kike. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Afya kwa umahiri wake, umakini na kuwa mfano katika uchapaji kazi, kwa kweli yeye ni mfano wa kuigwa. Niseme tu Mheshimiwa Ummy amekuwa ni *inspiration* kwa viongozi chipukizi na hasa wanawake. Kwa hiyo nampongeza sana, sana Mheshimiwa Waziri wa Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na yeye kwa kuonesha mfano wa kuwa kiongozi mnyenyekevu, kiongozi mchapa kazi na mwenye nidhamu ya kuweza kumsaidia *boss* wake. Nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Mollel. Niipongeze timu nzima ya wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa upekee nimpongeze Mheshimiwa Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa kwa kudumisha mahusiano ya kikazi kati ya Wizara ya Afya na Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na pia kwa usimamizi wa miradi yote ya afya ambayo ipo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na ile ambayo inaletwa kutoka Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia mambo mbalimbali. Ninaomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tumepokea michango yao, maoni yao, maombi yao na tutayafanyia kazi. Kiupekee ningependa kugusia katika maeneo machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia hitaji la kupata zahanati na vituo vya afya. Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imeweka kipaumbele katika kukamilisha miradi viporo vya Hospitali za Halmashauri, pia katika kuhakikisha kwamba inanunua vifaa na vifaatiba katika zahanati, vituo vya afya na hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo hapa ni kuhakikisha kwamba, huduma za afya msingi zinaimarika. Kwa hiyo, niwaeleze Waheshimiwa Wabunge na ninyi wote ni mashahidi, mnafahamu tangu mpango wa (MMAM) umeanzisha Mpango wa Maendeleo ya Afya Msingi, kumekuwa na ongezeko kubwa la vituo vya kutoa huduma ya afya msingi, kutoka hospitali 77 sasa tuna hospitali 177, lakini kutoka Vituo vya Afya 535 sasa tuna Vituo vya Afya 896, kutoka zahanati 4,554 sasa tunazo zahanati 6,160. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kipaumbele cha Serikali kwa wakati huu ni kuhakikisha vituo vyote hivi vya kutoa huduma ya afya msingi vinatoa huduma iliyo bora. Ndiyo maana Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imetenga bilioni 67.7 kwa ajili ya kuhakikisha inanunua vifaa na vifaatiba ili viende kwenye vituo vyetu hivi vya kutolea huduma ya afya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, zimetumika bilioni 220.3 kwa ajili ya kuhakikisha vifaa na vifaatiba vinapatikana katika vituo vyetu vya kutoa huduma ya afya msingi. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, fedha hizi zilizotengwa katika mwaka wa bajeti 2024/2025 za kwenda kununua vifaa na vifaatiba, zitatumika kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana kwa wakati bila kuchelewesha ili huduma kwa wananchi ziweze kupatika na ziwe zina ubora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejielekeza na inaweka kipaumbele katika kuajiri watumishi wa kada ya afya na ndiyo maana katika mwaka wa fedha 2023/2024, Seriakli imeajiri watumishi katika kada ya afya 8,070. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali inatarajia kuajiri watumishi wa kada ya afya 10,112. Kwa nini? Huu ni mkakati mahsusi wa kuhakikisha kwamba, vituo vya kutolea huduma ya afya msingi vinaimarika na vinatoa huduma iliyo bora kwa watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Serikali imetenga bilioni 43.84, kwa ajili ya miradi viporo ya hospitali za Halmashauri. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali ina nia dhabiti ya kuhakikisha kwamba, huduma za afya msingi zinaimarika na wananchi wanapata huduma iliyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumepokea orodha ya maombi ya Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya vituo vya afya, orodha hiyo niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge Serikali imeipokea. Serikali itahakikisha inatafuta fedha ili vituo hivi vya afya vya kimkakati ambavyo Waheshimiwa Wabunge, mmeainisha vinaweza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia maboma ya zahanati. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tayari Serikali imefanya tathmini na kubaini kwamba, kuna vituo 1,265 ambavyo vinahitaji bilioni 75.9, kwa ajili ya kukamilisha. Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie Serikali itatafuta fedha kuhakikisha inaunga mkono jitihada za wananchi walioanza kujenga maboma. Kwa hiyo, Serikali itahakikisha maboma haya yanakamilika ili huduma za afya ziweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika kipindi hiki cha miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeshapeleka bilioni 88.1 kwa ajili ya ukamilisha wa maboma. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Serikali itaendelea kutafuta fedha kuhakikisha maboma yaliyobakia ambayo

wananchi wametoa nguvu yao kuchangia katika maendeleo ya Taifa hili haipotei bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema machache hayo. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono bajeti hii ya Wizara ya Afya, fedha ziweze kwenda kuwanufaisha Watanzania wenye matarajio makubwa na Serikali ya Mama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Naibu Waziri Afya dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nianze kwa kukushukuru wewe, pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wakati wote mmekuwa mkitushika, wakati wote mmekuwa mkitushauri, wakati wote tumekuwa tukishirikiana pamoja katika masuala yote mazuri mnayoyaona, kwa kweli Bunge hili na ninyi ni sehemu ya haya makubwa yaliyotokea kwenye Wizara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yamesemwa mengi na Waheshimiwa Wabunge, wameeleza matatizo mengi sana, wameeleza mambo mbalimbali ambayo wanategemea yafanyiwe kazi. Mimi niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, sina sababu ya kwenda moja baada ya lingine, kwa sababu ninyi ni mashahidi kwamba, tunae Mheshimiwa Rais ambae ni Rais mahiri hajatuacha pekee yetu, ukitaka kutafakari itafakari Wizara ya Afya, miaka mitano iliyopita pia itafakari miaka mitatu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, uitafakari tulikotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wetu huyu moja, alipokuwa Rais hakutuacha pekee yetu, alitupa Dada yetu Mheshimiwa Ummy Mwalimu wengine wanamwita Odo Ummy Mwalimu na Dada huyu amesema Kaka yangu hapa apewe *PhD*. Mimi nitaka kuwaambia wenzangu, leo niwaambie nisameheni Madaktari wenzangu, ni kazi ngumu kweli kutuongoza sisi Madaktari, lakini Dada huyu amekuja ametulia na sisi tumetulia Madaktari tumeingia kwenye *line* tunatoa pasi nzuri. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dada huyu amepitia misukosuko mingi ukiangalia kuanzia *Corona*, *Marburg* watu wanakimbia *Marburg* yeye anaelekea huko. Amesema Kaka yetu tumpe *PhD*, leo kwa mambo yote mliyoyataja hapa, wakati tunampa Mheshimiwa Dkt. Samia Uprofesa wa *leadership* kwenye kuboresha huduma za afya, huyu Dada anastahili *PhD* kama ambayo kaka uyangu Mheshimiwa Iddi alivyosema. Hata kama watu watasema *PhD* ni ngumu haiwezekani sijui kitu kingine, lakini uwezo wa kusimama kwenye mambo magumu, uwezo wa kusimama kwenye wakati mgumu ambao huwezi kutabiri ni nini kinatokea kesho, yeye anao huo uwezo wa kujitoa mbele kwa ajili ya watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwamabie Kamati ya Siasa ya Tanga ipo hapa na juzi tulipokuwepo kule niliwaambia hii ni lulu siyo ya Tanga tu ni lulu ya Tanzania nzima. Leo mmekuja hapa mmeliona Bunge linavyozungumza nendeni Tanga na mimi leo nitumie nafasi hii kama Msaidizi namba moja wa Mheshimiwa Waziri, niseme huyu ni kiongozi mahiri wananchi wa Tanga siyo lulu tu kwenu, amekuwa lulu kwa watanzania wote, amekuwa lulu ya mafanikio makubwa, akija mtu anasogelea Tanga muulizeni nini amefanya *tangible* cha kutuheshimisha nchi nzima kama alichokifanya Mheshimiwa Ummy Mwalimu kwenye Taifa letu na kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mnakumbuka Mheshimiwa Rais wetu siku anafungua Bunge mara ya kwanza analihutubia, alisimama hapa kukiwa na kilio chenu ninyi Waheshimiwa Wabunge, mnasema akina mama wanakufa 556 kwa mwaka. Mkasema wakina mama 556 kwa mwaka na ninyi mlitegemea mwaka kesho 2025 vifo vya kina mama vishuke viwe 225, lakini *input* aliyoiweka Mheshimiwa Rais wetu na aliyoisimamia Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wetu, leo tumeshuka tofauti na ilivyotegemewa na *WHO,* tofauti na ilivyotegemewa na wenzetu duniani leo tunazungumzia vifo vya akina mama 104 tofauti na mahesabu ya kidunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mmekuja hapa mara ya mwisho aliposimama Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia

Suluhu Hassan, alisimama hapa mkisema Tanzania nzima tunawapoteza Watanzania kwenye eneo la *emergency* kwa sababu ya Watanzania kukosa huduma zile za muhimu za haraka za *emergency* kwa kufuata utaratibu na kupata vifaa vinavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo anasimama hapa Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kulikuwa na *emergency department* saba tu kwenye nchi nzima, kwa kipindi kifupi cha miaka mitatu leo tuna *emergency* 116 kwenye nchi ya Tanzania. Maana yake Mheshimiwa Rais wetu kwa kipindi hiki kifupi tu zimejengwa *emergency departments* 109. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayarudia haya ili tukumbuke vizuri ili haya madogo madogo mnayoyasema mjue kwamba ni madogo mno hayafiki matrilioni aliyoweka Mheshimiwa Rais wetu hapa. Ni mambo madogo ambayo yanahitaji mabilioni kama yamewezekana kufanyika hapa mli-*relax* tuachieni shilingi, tuachieni tupitishe haya mambo kwa sababu haya mambo yanawezekana na njia imeshaoneshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo alipohutubia Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mara ya mwisho hapa, alipohutubia kulikuwa na hospitali mbili tu za Mikoa zenye *CT scan,* leo tumesimama kila Mkoa, kila mahali kuna *CT scan*. Leo tumesimama hapa kila mahali kuna *CT scan.* Tulikuja hapa mara ya mwisho Waheshimiwa Wabunge mlikuwa kila Mbunge, anayesimama anasema Hospitali yetu ya Wilaya haina *X-Ray,* Hospitali yetu ya Wilaya haina *X-Ray,* lakini leo hapa tunasimama ikiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa hii miaka mitatu amenunua *X-Ray 199*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo amesimama Mheshimiwa Mbunge wa Tanganyika hapa hazungumzii kutokuwepo kwa *X-Ray,* anazungumzia *X-Ray* ilikuwepo tena mpya bahati mbaya ikaungua, maana yake anataka apelekewe nyingine au kifaa kitafutwe ili kufanyiwa *repair,* maana yake Mheshimiwa Rais wetu

amefanya kazi kubwa. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, wenzangu kwamba, wala hatuna haja ya kuogopa haya mengine ya kujibu. Mimi ninasema ni madogo madogo mwachieni Mheshimiwa Ummy Mwalimu, wala hatuyapeleki kwa Mheshimiwa Rais, mengine tutaomba hela kwa Mheshimiwa Rais, hayo yanaenda kukamilika wala tusiogope, twendeni tupitishe hiki kitu tukafanya mambo mengine jioni hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakati tunasimama hapa, watu walikuwa hapa, ulikuwa ukipata uvimbe chini ya sakafu ya ubongo kichwa kizima kinabomolewa, vichwa vinabomolewa vya watu. Mlisimama hapa mkisema watu wanakaa muda mrefu wodini, watu wanabomolewa kichwa kizima na wakati mwingine mambo mengine, leo Mheshimiwa Rais wetu huyu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameingiza teknolojia ndani ya nchi hii leo unatibiwa bila kufungua kichwa kwa kupitisha tu vifaa kwenye pua unafika chini ya sakafu ya ubongo unatibiwa unaondoka kwenda kuikuta familia yako. Huyo ndiyo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunazungumza hapa amesema Waziri, wakati wanatoa hotuba, tumeanza Muhimbili ilikuwa Muhimbili kifua kizima zinafunguliwa ndiyo utibiwe moyo, kifua kizima kinatibiwa unakaa wodini miezi mitatu na wewe unaweza kufikiria gharama za familia kukaa pale na muda ambao unaupoteza wa kazi lakini ni maumivu kiasi gani mtu anafunguliwa kifua kizima. Leo Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyesimama miaka mitatu hapa, ameleta kifaa unafunguliwa sentimita mbili mpaka sentimita nne unatibiwa moyo, baada ya siku mbili umeondoka umeenda kukaa na familia yako. Huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ninaendelea kuwaambia Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naendelea kuwakumbusha na kuwaomba kwamba, hapa tusiwe na mjadala mrefu mpeni Waziri mambo yake aende nayo akawafanyie kazi. Hakuna muda wa kupoteza kukaa kujadiliana hapa. Leo mlikaa miaka mitatu hapa ilikuwa kwamba, wagonjwa wa *sickle cell*

ilikuwa ni ugonjwa wa kuishi nao, wengi walikuwa hawakatizi miaka 45 wanakuwa wameshaondoka wameshaaga dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumesimama hapa Mheshimiwa Rais, wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amenunua vifaa, amewezesha Madaktari na leo ndani ya Tanzania watoto wanatibiwa na wanapona wanarudi kwenda kwenye familia zao. Huyo ndiyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, huyo ndiyo Mheshimiwa Rais ninayewaambia tusiogope, kwa sababu Mheshimiwa Rais, huyu haya ambayo mmeyasema tukisha yafikisha mezani kwake anatoa *resources* na mambo yatakwisha. Ninaomba mtuondoe hapa ndani mapema tuondoke zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge, tukitembea kwenye Kamati za Wabunge, mnakumbuka tulikuwa tukienda *Ocen Road* asilimia 80 ya wagonjwa waliokuwa wanakutwa *Ocean Road* ni wale ambao wamekuja na *cancer* ambayo imefika *stage* ambayo haitibiki, ipo *stage* ya nne, ipo *stage* ya mwisho kabisa, huyu mgonjwa anahitaji kupata huduma za *palliative* zile za kungojea ili aage dunia. Asilimia 80 asilimia 20 tu ndiyo walikuwa wanafika *Ocean Road* wakiwa *cancer* ipo kwenye *stage* ambayo inaweza ikafanyika lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais, wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejenga uwezo wenye utaalamu wataalam wetu, lakini amenunua vifaatiba kuanzia taifani mpaka unafika Wilayani na mmesema ninyi wenye hapa leo magonjwa yanagundulika kule chini mapema na ninavyosimama hapa leo asilimia 70 ya wagonjwa na tulienda na Kamati ya Bunge mliona ripoti na mkashangaa ninyi wenyewe, mnaona leo asilimia 70 ya wagonjwa waliopo *Ocean Road* leo ni wale ambao wakitibiwa wanapona kwenda kukaa na familia zao asilimia 30 tu ndiyo wanakuja na *terminal stage* na ninaamini baada ya miaka miwili sasa wagonjwa hawa watakuwa karibia wote wanakuja zikiwa hatua ya mwanzoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninawaambia hivyo, amesema Naibu Spika hapa kwamba Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, amenunua *petty scan,* lakini akanunua kiwanda cha mionzitiba. Kwanza, niwaeleze kitu kimoja ametupeleka, wakati Mheshimiwa Rais wetu ananunua mashine hii *petty scan* na kujenga kiwanda cha kutengeneza cha kuzalisha miozitiba, ni nchi nne tu Barani Afrika zilikuwa na kiwanda hicho, maana yake sisi kwa Afrika sasa ni nchi ya tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jiulizeni moja kile kiwanda cha kuzalisha miozitiba ni gharama kubwa, lakini pia inahitaji utaalam wa hali ya juu sana, lakini wakati huo huo ni kama kinu kingine cha kuzalisha miozi ile mingine ambayo inaleta madhara mengine. Mheshimiwa Rais wetu yupo kwenye nchi tano ambazo leo kupitia hii *petty scan, cancer* inaweza kugundulika kwenye *molecular stage* yaani chini ya *cellular level.* Unaiangalia *cancer* inaonekana *cancer* ambayo inaweza ikatokea miaka 10 ijayo inagundulika leo. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha hilo, sijui kama ninaeleweka wandugu? Wangapi wanamuelewa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema hivi kweli kuna mjadala hapo, yaani kama Mheshimiwa Rais huyu leo wewe unazungumzia zahanati yako, unazungumzia sijui tatizo gani Mheshimiwa Rais huyu amekuja na teknolojia ya kudundua *cancer* itakayotokea miaka 10 ijayo. Ni kwa nini usimwamini hizi zahanati anamalizana nazo mara moja? Twendeni tuendelee na mambo mengine tusipoteze muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tumeambiwa hapa wametibiwa wagonjwa kutoka nje 7,843. Sasa usihesabu tu tumepata *revenue* kutoka nje kiasi gani, lakini jiulize wenzatu walivyo, maana yake teknolojia hii Mheshimiwa Rais, wetu aliyoingiza kwenye nchi yetu, uwezeshaji kwa Madaktari wetu siyo tu kwamba, umetatua matatizo ya Watanzania kwa asilimia 97 ya kwenda nje huu uwekezaji wake umemimina neema mpaka nchi za jirani. Maana yake ametatua matatizo mpaka ya Marais

wenzake ambao walikuwa wanatumia gharama kubwa kupeleka watu wao Ulaya, Marekani na India, leo wanakuja hapa karibu na wanatatuliwa matatizo na bajeti yao ya kupeleka watu nje inakuwa imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake kama huyu Mheshimiwa Rais, anaweza kuwekeza kwenye eneo la afya na akawekeza *impact* ya uwekezaji wake inagusa nchi yake na inagusa nchi zilizotuzunguka, ni kwa nini usimwamini kwenye haya mambo madogo madogo tunayoyazungumzia hapa? Ni kwa nini? *Impact* ikagusa. *(Makofi)*

Mhehsimiwa Naibu Spika, leo wamekuja Zambia, wamekuja wapi na nchi nyingine tulizoea kutumia maneno na nchi nyingine tulizoea kutumia sijui vitu gani kama ndio mfano kwetu. Leo wamesaini mikataba na sisi haki ya Mungu, tunawatibu watu wao. Unamuonaje huyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tunawatibu watu wao. Huyo ndiyo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tusisahau aliyemkabidhi trilioni 6.7, akazisimamia ni Mheshimiwa Ummy Mwalimu na *message* iwafikie watu wa wa Tanga, kwamba wao wamezaa lulu na ni lulu ya Tanzania nzima wailinde, kwa sababu tunaihitaji wakati mwingine wanaletwa Waheshimiwa Wabunge, wakuja kujaza namba. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema rafiki yangu mmoja akazungumzia *hyperbaric oxygen machine,* ile ambayo leo unaingia ndani kama una kidonda kilikuwa kichukue miezi mitatu upone leo ukiingia kwenye hiyo mashine ndani ya wiki mbili kidonda kinakuwa kimepona. Pia kifaa hicho kinaonekana hata ukiwa unaingia unapata ile *pure oxygen* kinachoonekana hata muda wa kuishi nao unafanya nini, kwa sababu seli zako zinaanza kujitengeneza upya na mambo mengine yanatokea, huyo ndiye Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, vifaa hivyo ilizoeleka kutumika na matajiri huko duniani lakini leo kipo pale Muhimbili watanzania tukitumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa fedha pale Muhimbili. Wakina mama mlikuwa mnahangaika hapa masuala ya kubeba mimba lakini ninataka niwaambie hili moja; siyo tu kubeba mimba, leo ukijisikia hautaki kuzaa na mke wako mna wasiwasi mbegu zinaweza zikapotea miaka miwili ijayo mnazitoa leo mbegu yako na ya mke wako zinatunzwa hata kwa miaka kumi pale Muhimbili. Siku mnataka hiyo mimba inabebeshwa mnarudi kuja nyumbani mkiwa na mtoto wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyo ndiye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sijui kama naeleweka hivyo? Yaani unaweza ukawa unawaza kwamba unapitisha umri wa kubeba mtoto lakini uchaguzi umekaribia, sisi tupo tayari kukutunzia mbegu hata ukipitisha umri kuna mambo ya kufanya mambo yakaenda kwa uwezeshaji wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo mambo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yakisimamiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu, yakisimamiwa na Katibu Mkuu wetu Dkt. Jingu, yakisimamiwa na Dkt. Grace Mgembe, yakisimamiwa na *CMO* Dada yangu *Professor* Nagu pamoja na dada yetu akicheza mchezo na kutuongoza vizuri ambaye anatokea Tanga. Kamati ya siasa pelekeni ujumbe, pelekeni kwa kila mtu na uende duniani kwamba huyu ameleta *revolution* kubwa, amemsaidia mama kazi kubwa, Rais wetu amemkabidhi shilingi trilioni 6.7 na leo Wabunge wote mnakubaliana kwamba kazi imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Wabunge nawashukuru kwa kazi kubwa ambayo mmemsaidia Mheshimiwa Rais, mnatusaidia sisi lakini niseme ahsanteni sana, nisingependa kuongea sana niwasumbue. Nina mengi kwa kweli ya kusema ila nitawatosha. Mimi niseme tu nyie mmekuwa njia yetu ya kutusaidia, nyie mmekuwa ni watu wa kutubeba. Yote haya hauwezi kuliacha hili Bunge mafanikio yote lakini nimshukuru dada yangu Mheshimiwa Ummy Mwalimu. Sisi madaktari ni wakorofi,

umetuvumilia sana. Kwa niaba ya madaktari wenzangu na mimi mwenyewe umetuvumilia sana, umetuongoza sana. Ahsante sana dada yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu aliyetuamini na akatuleta na mimi tukawa tunakusaidia. Nimshukuru sana na niwashukuru watu wote ahsanteni sana na Mungu awabariki. Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tupitishe hii kitu tumalizane nayo. Hakuna sababu ya kushikiana shilingi sijui kifungu kimefanya nini, mambo yameisha twendeni nyumbani tukafanye mambo ya msingi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waziri wa Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kutoa ufafanuzi wa hoja zilizoelezwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kwa kutoa maoni na ushauri wa Kamati. Pia, ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni na ushauri ambao mmetupatia. Ninataka katika hatua hii kusema kwamba Wizara inakubaliana na maoni na ushauri wenu na tutatekeleza na kufanyia kazi ushauri ambao mmetupatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu imechangiwa na Wabunge 28, Wabunge 25 wamechangia kwa kuongea na Wabunge watatu wamechangia kwa maandishi. Kama nilivyosema tumepokea maoni na ushauri wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kabisa, mimi na wenzangu tumepokea pongezi za Waheshimiwa Wabunge na mimi ninaomba niseme pongezi hizi anayestahili ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa

Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Rais mwenye maono, ni Rais anayejali utu pamoja na kutaka kutatua kero au changamoto zinazowagusa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata mafanikio makubwa katika Sekta ya Afya kwa sababu tunaye Rais Samia anayetuongoza vizuri. Sisi Sekta ya Afya tumeziona falsafa nne za Mheshimiwa Rais Samia katika Sekta ya Afya: *reconciliation* (mapatano), *rebuild* (kujenga upya), *reforms* (kufanya maboresho), lakini pia *resilience* (kujenga ustahamilivu katika masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo ya kiuchumi, kijamii katika nchi yetu).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema asubuhi na mmemsikia Mheshimiwa Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge kuna baadhi ya watu tukimsifu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wanaona tumezidi. Kwa nini tusimsifu kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata heshima ya kuwa Waziri wa Afya hii leo ni bajeti ya nane ya Wizara ya Afya nawasilisha katika Bunge hili. Nimesafiri dunia sehemu mbalimbali, America, Ulaya, Africa, Tanzania tunakwenda vizuri chini ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Siyo maneno tu ya kusema tunamsifu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anabebwa na namba. Namba zilizothibitishwa na Shirika la Afya Duniani, namba zilizothibitishwa na Taasisi zetu za Utafiti *including National Bureau of Statistic*. Hongera Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na Naibu Waziri na Watumishi wa Sekta ya Afya hatutakuangusha kwa sababu tunafahamu Sekta hii ni pana sana lakini Sekta ya Afya ni *very dynamic*. Inabadilika kila siku kutokana na idadi ya watu. *Dynamics* nyingine pia unazikuta kutokana na mabadiliko ya tabianchi, maradhi, magonjwa pamoja na teknolojia. Ulichokifanya leo Sekta ya Afya baada ya siku mbili miaka mitatu kimebadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba sisi tumepokea haya maoni na ushauri. Kubwa ambalo nimeliona ni suala ambalo limeelezwa pia na Kamati ni upatikanaji wa fedha za mwaka 2023/2024. Kwa ufupi ni kwamba fedha zimetolewa, wakati tunawasilisha bajeti ilikuwa fedha zilizotolewa za miradi ya maendeleo ilikuwa asilimia 38. Zimeongezeka mpaka asilimia 59 *by March* 2024. Kwa hiyo tunakwenda vizuri na tunaamini kabisa fedha zilizobaki zitatoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uhaba wa rasilimali watu, Naibu Waziri TAMISEMI ameeleza vizuri jinsi ambavyo Serikali inaajiri na sisi tutaendelea kuajiri. Nilikuwa ninaangalia takwimu; mwaka 2021/2022 tuliajiri watumishi wa afya 9,392. Sasa ninatoa watumishi wa Sekta nzima; mwaka 2023/2024 ni watumishi wa afya 13,187 na tutaendelea kuajiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala lingine ambalo limezungumzwa na nimefurahi sana Waheshimiwa Wabunge. Bunge hili linakubaliana na sisi kwamba sasa ipo haja kuwekeza kwenye kinga badala ya kusubiri kuwatibu Watanzania wakiwa wagonjwa. Jambo hili tutalifanyia kazi. Nimekusikia kaka yangu Mheshimiwa Shamsi Nahodha na wote ambao mmezungumza masuala ya lishe, masuala ya chanjo, masuala ya kuhamasisha wananchi kuzingatia mtindo bora wa maisha ikiwemo ulaji unaofaa wa vyakula pamoja na kupunguza matumizi ya pombe kupita kiasi pamoja na vihatarishi vingine vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ikiwemo pia kuacha tabia bwete. Suala la kinga tutaendelea kulipa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililozungumzwa ni suala la huduma za utengamao. Tumekusikia mdogo wangu Mheshimiwa Stella Ikupa, kununua vitanda maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu ikiwemo wanawake wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dawa, Kamati na wajumbe waliochangia wametoa ushauri Serikali kuipa mtaji *MSD*. Naomba nitoe habari njema. Kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania Serikali chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu

Hassan imetoa shilingi bilioni 100 kwa ajili ya mtaji wa *MSD*. Nimepata hela hizi kutoka kwa Waziri wa Fedha wiki illiyopita. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu tunakushukuru sana, haijawahi tokea kama nilivyosema hii ni bajeti yangu ya nane kama Waziri wa Afya Serikali kuipa mtaji *MSD* shilingi bilioni 100 na Waziri wa Fedha ameniambia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Afya tunakuongezea. Ameniambia anaangalia kabla ya tarehe 30 Juni anaweza aka-*pump* tena, mabilioni mengine kwenda kuiwezesha *MSD*. Hii ndiyo kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Vitendo zaidi, maneno machache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni ubora wa huduma za afya. Mdogo wangu Mheshimiwa Cecilia Paresso, Dada yangu Mheshimiwa Mwantumu Dau tumekusikia na ndiko tunakoelekea. Ni kweli tumejenga sana, tumenunua vifaatiba sana. Watanzania sasa hawatatupima kwa sababu ya majengo na vifaatiba tulivyovifunga. Watanzania wanataka huduma bora za afya. Kwa hiyo hiki ndiyo kipaumbele chetu, ulikiona baada ya kinga namba mbili nikaweka ubora wa huduma za afya. Tutazingatia weledi na maadili ya watumishi wa afya, nidhamu lakini pia upatikanaji wa dawa pamoja na huduma zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linawezekana. *Professor* Janabi ameibadilisha Muhimbili chini ya muda mfupi kwa sababu ya usimamizi na uongozi. Kwa hiyo sambamba na kununua dawa na kufanya mengine tunakwenda kuimarisha uongozi na usimamizi wa utoaji huduma za afya kuanzia ngazi za chini. Huwa ninashangaa, jambo linatokea Mganga Mkuu wa Mkoa upo wapi? Mganga Mkuu wa Wilaya upo wapi mpaka azungumze Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya, Waziri wa TAMISEMI au Mkurugenzi wa TAMISEMI? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunafanya mapitio ya muundo wa Kamati za Uendeshaji Afya za Mikoa *(Regional Health Management Team)* na *(Council Health Management Team)*. Tunaangalia muundo wao, tutaangalia majukumu yao, tutaangalia na ujuzi wao ili sasa tuweze kuwasimamia kikamilifu na kuweza kuwapima kwa majukumu mahususi ya kusimamia

ubora wa huduma za afya. Mmemuona Mkurugenzi wa Afya, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dkt. Rashid, anapita anaibua mambo. Unajiuliza hii halmashauri, huu mkoa kuna Kamati ya Uendeshaji Afya kweli ya Mkoa na Wilaya hadi haya mambo yanatokea?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutashirikiana na Mheshimiwa Waziri Mchengerwa kuboresha huduma za afya. Kuna suala, ambalo limezungumzwa la madaktari bingwa. Kwa kweli na mimi nitumie fursa hii kuwapongeza madaktari wetu ambao wamejitolea bila malipo kwenda kutoa huduma za ubingwa na ubobezi katika mikoa na halmashauri mbalimbali. Mheshimiwa Festo Sanga umesema vizuri, madaktari hawa bingwa ukiwakuta Muhimbili, ukimkuta *Ocean Road*, ukimkuta *Mbeya Zonal*, ukimkuta Bugando unamlipa hela nyingi kumuona lakini wamekuwa wazalendo. Nilipowaambia tunataka muanze kwenda kwenye halmashauri, wakasema Waziri sisi tupo tayari kwenda na hawalipwi wanamuona mgonjwa kwa gharama ile ile halmashauri ambayo imepanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kumuona daktari Makete ni shilingi 5,000 daktari hao wanapokea shilingi 5,000 na ile hela sio inaingia kwao inaingia kwenye hospitali. Hongereni sana madaktari wetu bingwa. Waheshimiwa Wabunge nataka niwaahidi huu moto wa Mheshimiwa Rais Samia hauzimiki. Tunaendelea na zoezi hili kwenye halmashauri zote na litakuwa zoezi endelevu. Pia, si kwamba wanaenda kutoa huduma tu, wanakwenda pia kuwajengea uwezo madaktari waliopo katika halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumechagua kada tano za kipaumbele. Kuna daktari bingwa wa magonjwa ya ndani ambayo ni mtu wa *internal medicine,* daktari bingwa wa masuala ya uzazi na masuala ya wanawake *(gynecologist),* daktari bingwa wa watoto lakini tumechukuwa daktari bingwa wa huduma za ganzi na usingizi na daktari bingwa wa upasuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumechukua fani tano tumewasambaza katika halmashauri zote. Waheshimiwa

Wabunge naomba tuwape ushirikiano na tuwaunge mkono. Mheshimiwa Festo hata wenye mahitaji mmoja mmoja tutafanya pia, anayehitaji sisi tuta-*facilitate* kuwaleta ili watoe huduma katika majimbo yenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunawashukuru madaktari bingwa waliotoa huduma katika ngazi za hospitali za rufaa za mikoa. Hawa wamefanya kazi nzuri sana, sana na tunawashukuru. Kuna moja ambalo limezungumzwa na kaka yangu Mheshimiwa Musukuma kuhusu kadi za *clinic* kwamba nitoe waraka. Mheshimiwa Musukuma nitatoa waraka kabla hatujaondoka Bungeni. Kadi za *clinic* kwa kina mama wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano haziuzwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana wataalamu wa afya tuzingatie maelekezo ya Serikali. Hapa niunganishe hoja ya Mdogo wangu Mheshimiwa Juliana Shonza kwamba huduma za kina mama wajawazito zinalipishwa. Niseme tunaendelea kusimamia au tutaendelea kusimamia Sera ya Afya inayosema matibabu kwa makundi maalum yakiwemo wajawazito yanapaswa kugharamiwa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia takwimu zangu. Kwa mfano mwaka 2023/2024 tumetumia takribani shilingi bilioni 126 kwa huduma za wakina mama wajawazito. Kwa hiyo tutaendelea kuboresha zaidi lakini kutenga fedha mahususi. Leo kwenye bajeti ambayo mtaipitisha na ninaamini mtaipitisha, tumeweka fedha za kununua dawa za uzazi salama na hizi dawa tutawapa taarifa kwamba dawa hizi hazipaswi kuuzwa, huduma hizi hazipaswi kutolewa kwa gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninataka kulizungumzia ni suala la tafiti za afya. Suala la *NHIF* nimeliweka mwisho kidogo. Hatuwezi kutoa huduma za afya au kufanya maboresho bila kuwa na ushahidi wa kisayansi. Kwa hiyo tutaendelea kuwekeza kwenye tafiti. Bahati mbaya niliposema tumetenga shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kufanya tafiti kinachozunguka ni kwamba Wizara ya Afya wanataka kufanya tafiti ya kuangalia nguvu za kiume tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Watanzania, tafiti katika Sekta ya Afya ni muhimu sana. Zitafanyika tafiti sita ikiwemo ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, dada yangu Mheshimiwa Mariam Kisangi umesema hapa. Tutafanya tafiti kuhusu masuala ya usugu wa vimelea vya dawa. Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza suala hili. Tutafanya tafiti kuhusu ongezeko la magonjwa ya figo, masuala ya tiba asili na masuala ya afya ya akili. Kwa hiyo nguvu za kiume ni jambo dogo katika mambo makubwa ambayo tunakwenda kuyafanyia utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hili moja la *NHIF*. Kwanza lazima tukubali na tukiri kwamba suala la bima ya afya si jambo jepesi. Marekani huko wanagombana kila siku na *Obama Care*. Siasa za *Europe* ni bima ya afya na masuala ya *social security*. Nataka kukiri Tanzania na namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile. Watanzania wanataka kuwa na bima tayari mgonjwa yupo kitandani, hapana. Bima ni suala la kuchangiana, tuchangiane tukiwa hatujaumwa ili wenzetu wakiumwa tuweze kuwagharamikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sisi tutawekeza katika kutoa elimu kuhusu dhana ya bima ya afya na umuhimu wa bima ya afya. Nataka kukiri, ni kweli nimekuwa nikikumbana na misukosuko lakini kwenye hili bima ya afya tutasimama kwenye sheria, kanuni na taratibu za kuendesha bima ya afya. Kama kuna jambo lingine tuzungumze kuanzisha mifuko ya kugharamia wasio na uwezo na hili tumelizungumza Waheshimiwa Wabunge katika Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ile inakwenda kutibu changamoto ya kutatua kero ya upatikanaji wa matibabu au gharama kubwa za matibabu kwa watu wasio na uwezo. Kwa hiyo Kamati imezungumza kwamba Serikali iboreshe uendeshaji wa Mfuko wa Bima ya Afya. Tumepokea ushauri ikiwemo kutambua *private sector*. Tayari Sheria ya Bima ya Afya inatambua *private sector* lakini nikiangalia fedha zinazolipwa na *NHIF* zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022/2023, *NHIF* ilipa shilingi bilioni 743. Kati ya hizo, shilingi bilioni 230 sawa na asilimia 37 zililipwa kwa vituo binafsi, shilingi bilioni 212.4 sawa na asilimia 29 zililipwa kwa vituo vya madhehebu ya dini na shilingi bilioni 250 sawa na asilimia 34 zililipwa kwa vituo vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaona tayari mchango au ushiriki wa Sekta Binafsi katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Jambo lingine Serikali ilipe madeni inayodaiwa na *NHIF*. Tunashukuru madeni haya tayari yameshahakikiwa. Shilingi bilioni 210 na Wizara ya Fedha tayari imeshatuma uthibitisho ikiwemo kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, kwamba tutalipa haya madeni ya *NHIF*. Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Serikali kuanzisha chombo huru mahususi na cha kudumu cha kuratibu bei za huduma za afya, hili nimelisema katika hotuba yangu. Tunalipokea na tutalifanyia kazi. Kuhusu suala *TIRA* kusimamia bima za afya, hili tayari linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niseme, kwamba suala la bima ni suala ambalo kwa kweli tutaendelea kulisimamia kwa kuzingatia maoni ya Kamati na ushauri wa wadau. Pia, nataka niseme, kwamba kuna sehemu tutakubaliana kutokubaliana. Lazima ukweli usemwe, hakuna haja ya kutaka kudanganyana. Kwa sababu kila mtu anaangalia, mimi naweza kufanya hivi. Maana ya bima ni kutomwongezea mzigo mwananchi mwenye bima. Mtu akishakuwa na bima hapaswi tena kuanza kulipia kila kitu na kuchangia changia, hapana. Kwa hiyo, sisi tutaangalia yale ambayo yana tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niseme kwamba mambo mengine yote tumeyapokea. Kuna la wataalam; naomba niliseme; nisipolisema hili madaktari hawatanielewa; ni kuhusu *on call allowance***.** Ni kweli kwamba mwaka jana Serikali ilibadilisha viwango vya posho lakini *on call allowance* haiukuwa imeguswa. Mheshimiwa Musukuma anataka tulifanyie kazi suala hili. Tumeshamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, wanalifanyia kazi. Tunaamini kabisa *on call allowance* kwa

madaktari itaongezwa, posho ya kuchunguza maiti pia itaongezwa pamoja na posho ya *uniform* kwa ajili ya wauguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *TFNC* Lishe, tumelipokea. Naomba, najua Mheshimiwa Neema Lugangira na wengine mmeliongea jambo hili, tutalifanyia kazi pia katika ngazi ya Serikali. Suala la *TMDA, TFDA* na *TBS,* tumepokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalize tena kwa kukushukuru wewe, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote hususan Kamati ya Bunge ya Afya na Masuala ya Ukimwi. Tunawashukuru sana viongozi wakuu wa nchi, Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu. Ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Godwin Mollel. Kwa kweli nataka kusema nina Naibu Waziri mzuri sana ambaye ananisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, namshukuru Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mganga Mkuu wa Serikali, wataalam wote wa afya, bila kusahau waganga wafawidhi wa hospitali zetu za taifa, kanda maalum, na hospitali za rufaa za mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kipekee niwashukuru sana sana wataalam wote wa afya. Wengi ni wazuri; tuna madaktari wazuri, tuna wauguzi wazuri na wafamasia wazuri, lakini wale wachache tutaendelea kuwajibishana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimalize kwa kuwashukuru wapiga kura wangu wa Tanga Mjini. Ninawashukuru sana kwa heshima kubwa ambayo mmenipa ya kuwa Mbunge wenu. Ninafurahi kuiona kamati yangu ya siasa ya wilaya iko pale. Pia, ninayo Kamati ya uendeshaji ya Odo Ummy Cup kwa kuja kuniunga mkono. Mimi naamini kabisa Tanga Mjini ni salama na Odo Ummy. Tanga Mjini itaendelea kuwa salama na Odo Ummy.

Hawawezi kuyumbishwa, ni watu wenye msimamo na uelewa mkubwa sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki**.**

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unatakiwa uombe fedha vilevile. Waheshimiwa, kaeni. Uliomba wakati unasoma bajeti, sasa umalizie hapo.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unajua kwa sababu najua Waheshimiwa Wabunge, wote wanaenda kupitisha bajeti yangu, kwa hiyo, kidogo nikajisahau...

*(Hapa Mhe. Esther N. Matiko alizungumza bila kutumia kipaza sauti)*

**WAZIRI WA AFYA:** Wifi Matiko... *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ambapo kiasi kinachoombwa ni shilingi 1,311,837,466,000 ili tuweze kutekeleza vipaumbele 10 ambavyo tumevibainisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, hapa tuko kwenye mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natam...

**MWENYEKITI:** Ngoja, ngoja, ngoja.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1001 – *Administration Human Resources Management*........................................Sh. 8,195,913,800

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuko kwenye mshahara wa Waziri. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Natambua juhudi mbalimbali zimeelekezwa na Serikali kwenye kuhakikisha wanaboresha na kujenga miundombinu ya hospitali hasa za rufaa za Taifa na kanda, ambazo kwa kweli zimesaidia sana kuweza kuwatibu Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kumeendelea kuwepo na changamoto hasa kwenye kitengo cha utambuzi wa magonjwa kwa maana ya *diagnosis*. *Specifically,* hapa nitaongelea utambuzi wa magonjwa kwa maana ya hatua mbalimbali kwenye matatizo ya *cancer* na ini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tumeendelea kushuhudia kwamba kuna Watanzania ambao wanasafiri kwenda nje ya nchi ambapo wanatumia fedha nyingi sana kwenda kutibiwa kule. Mathalan kuna wanaokwenda India, na baadhi wanaokwenda Uturuki, South Afrika na nchi nyingine mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakiwa Tanzania wanaambiwa labda *cancer* iko katika hatua ya tatu au ya nne lakini wakisafiri kwenda kule wanaambiwa *cancer* iko katika hatua ya kwanza au ya pili. Ambapo wakiwa Tanzania unakuta wameshatumia dawa katika *stage* ya tatu na ya nne. Kwa hiyo, wakiwa kule wanaambiwa ulikuwa katika hatua ya kwanza na ya pili lakini umetumia fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nijue, pamoja na kwamba wamewekeza jitihada kubwa sana, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha inaboresha kitengo hiki cha utambuzi wa magonjwa haya, hasa aidha kwa kuwa na wataalam ambao wanaweza kusoma na kutafsiri vilivyo au kununua vifaa vya kisasa zaidi ili tuweze kupunguza gharama hizi? Akitambulika ana ugonjwa fulani *stage* ya kwanza basi atibiwe kwa *stage* ya kwanza. Asiambiwe ni *stage* ya tatu na ya nne huku anaendelea kuwa... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru dada yangu Mheshimiwa Matiko kwa *observation* nzuri. Ninataka kusema, kwamba hiyo ni miaka fulani iliyopita kidogo; lakini ni ukweli kwamba bado kuna watu wanakwenda, ndiyo maana tumesema imepungua kwa asilimia 97. lakini pia hata hiyo *PET scan* ambayo tunaizungumzia ambayo imekuja sasa hivi, ambayo hata Mheshimiwa Naibu Spika umeuliza

inafanya lini kazi, itaanza mwezi Juni na itasaidia sana kwenye eneo hili. Afya Sholarship ya Mheshimiwa Dkt. Samia pia inaenda kuboresha hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikuhakikishie, ili tusiwakatishe tamaa wataalam wetu, kwamba, wanafanya kazi kubwa sana kulingana na vifaa walivyo navyo kwa sasa kwenye hilo eneo la *cancer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *by June*, watakuwa na uwezo wa kuona mambo makubwa kama ambavyo umetegemea na ninataka kuwaambia, *pet scan* na hicho kiwanda cha mionzi kinaenda kuanza kazi na wataalam wako tayari wameshatayarishwa, nakuhakikishia mambo yataenda kukaa vizuri kama ambavyo umesema wewe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri, isipokuwa tu nitahitaji *commitment* ya Serikali. Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Afya ndiyo ambayo inaratibu taratibu nzima za sera na mafunzo kwa vyuo vya kati, kwa maana ya diploma kwa zile taaluma za kada ya afya. Kumekuwa na sintofahamu kupitia wizara yake Mheshimiwa Waziri Kurugenzi ya mafunzo kutaka kubadilisha mitaala na vigezo vya udahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni ndiyo tunaelekea sasa katika kudahili hao wataalam wetu. Kigezo kimoja wapo ambacho tumekuwa tukikitumia kwa muda mrefu ni kuwa na angalau D ya somo la baiolojia na haijaleta shida yeyote katika hili lakini pia imeongeza soko la ajira na tumeendelea kuongeza wataalam katika ngazi ya kati ya sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka *commitment* ya wizara, kwa nini isisitishe zoezi hili ili wafanye kwanza tathmini ya kutosha kwa kuzingatia uhitaji wa soko la ajira, dira ya maendeleo na kwa kuzingatia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inasema itaongeza wigo wa ajira katika sekta ya afya. Kwa

kutumia kigezo hiki tunaamini kwamba wigo wa wataalam wetu kwenye sekta ya afya, utapanuka zaidi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Kassinge kwa hoja yake nzuri. Ni kweli Wizara inahusika na kuratibu uzalishaji wa wataalam wa kada za kati za afya, maana yake *certificate*, diploma na diploma ya juu. Naomba niseme kwa kiingereza, *certificate, diploma* na *advanced diploma*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuko kwenye mazungumzo kuhusu matumizi ya mitaala ya kada za kati za afya. Wiki iliyopita nilikutana na watu ambao ni wamiliki wa vyuo vya afya na tukakubaliana kwamba, nilisimamisha mchakato wa vigezo vipya vya udahili kutumika hadi kama sheria inavyotaka, wadau wakutane waongee. Tuliwaomba kwamba tumalize leo bajeti na ndani ya wiki hii naamini watakutana na watakubaliana kwenye vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba nitoe angalizo, tunataka si tu kuzalisha wataalam wengi wa afya, Hapana, tunataka kuzalisha wataalam wa afya wenye sifa na ujuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala uliopo ni kwamba, je, tuondoe kigezo cha *D* kwa mtu ambaye anataka kufanya labda kozi ya famasi na masuala mengine? Tutaangalia pia na wenzetu wa wizara ya elimu, ufaulu wa vijana wetu katika mitahani ya *form four* ukoje. Kwa sababu, tusishushe sana tukaja kuwa na wataalam ambao watakosa sifa na vigezo vya kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme, suala la afya si suala la mchezo mchezo. Tunazungumzia maisha ya watu, sisemi kwamba fani nyingine siyo muhimu, lakini ukikosea mtu umeshamuua, huwezi tena kumrudisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wadau wakatutana, watajadili, lakini naomba niseme, tutaangalia kwenye maisha ya wananchi kwanza kabla ya kushusha au kupandisha vigezo vya kada za kati za afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, kwa sababu tunamtambua kama Waziri mchapakazi na Hodari, na kwa kweli ni daktari wa sekta ya afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. Kwa mujibu wa sera ya afya, sera inahitaji wataalam wa afya kuwa na sifa na ujuzi lakini pamekuwa na uvujaji wa mitihani ya wanafunzi wa vyuo vya afya. Naomba ufafanuzi, Serikali ama wizara inafanya mkakati gani mahususi kwa ajili ya kudhibiti jambo hili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana mdogo wangu Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tanga kwa hoja yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli siku za karibuni tumekuwa na uvujaji wa mitihani ya kada za kati za afya ikiwemo mitihani ya wauguzi, wafamasia na wataalam wengine wa afya. Kubwa ambalo tumelifanya, kama Mheshimiwa Husna amefuatilia, tulishafuta. Tukishapata taarifa kwamba mitihani imevuja na tumejiridhisha kwamba mitihani imevuja, tunafuta matokeo hayo na katika hilo tumekuwa wakali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa muda mrefu ni kuimarisha usimamizi wa kada hizi za vyuo vya kati vya afya kwa kuanzisha taasisi au bodi ambayo itakuwa inasimamia mafunzo ya kada za kati za afya. Tumeshaandika andiko la mchakato huo. Tunaamini kabisa kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu tutaweza sasa kuwa na mfumo imara na mzuri ikiwemo pia kuboresha katika masuala ya TEHAMA. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sikusudii kukamata shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu anafanya kazi sana; lakini naomba *commitment* ya Serikali juu ya suala na hoja yangu ambayo nimeitoa kuhusu kurugenzi ya famasi au idara ya huduma ya dawa na vifaa tiba kwa sababu ya msingi. Kwa mfano, huo huo wa Hospitali ya Muhimbuli kwa mwaka Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Idara hii ya Famasi imeingiza bilioni 34 lakini kuna idara ambazo zimetengenezewa kurugenzi zake kama; idara ya vipimo, maabara pamoja na mionzi kwa mwaka huo imeingiza bilioni tisa, kurugenzi ya *nursing* imeingiza bilioni nane, kurugenzi ya *medical services* imeingiza bilioni nane na kuna *surgical services* imeingiza bilioni 19. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona mtiririko huo wa mapato ambao wameingiza hizi idara ambazo mmezitengenezea kurugenzi lakini hii idara ya famasi ambayo nusu ya bajeti ya hospitali inaenda famasi na nusu ya mapato ya hospitali yanatoka famasi. Kwa nini hawaweki kurugenzi yake? Kwa hiyo, naomba maelezo ya kina juu ya suala hilo. Kwa sababu sikusudii kushika shilingi ila nisiporidhika dada yangu, nitashika shilingi. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli namshukuru sana mfamasia Jacqueline Kainja, ana hoja nzuri na anachosema ni kweli, kwamba wafamasia pia ni nguzo muhimu katika utoaji wa huduma za afya. Lakini siyo tu kwa upande wa mapato, mimi ninaangalia pia katika muktadha mzima wa ongezeko la usugu wa vimelea vya dawa. Kwa hiyo ni kweli tunahitaji tuwaingize katika *level* ya menejimenti ili waweze kushiriki pia katika kufanya maamuzi na waweze kushiriki na pia katika masuala ya fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli, ukiangalia mapato ya hospitali zote yanajeneretiwa *(to be generated)* kutoka idara ya

famasi, ndiko kwenye fedha. Kwa hiyo mdogo wangu Jacqueline mimi naomba urudishe shilingi; umesema kwamba hukusudii kuishika, usiishike, haujaichukua, lakini acha nilifanyie kazi hili suala. Kwa sababu katika ngazi ya wizara tayari Mfamasia Mkuu wa Serikali sasa hivi anatambulika kama Mkurugenzi wa Famasi wa idara hiyo. Kwa hiyo, najua sasa, twende sasa kwenye ngazi ya hospitali zote ili iwe ni idara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye, hata ukiangalia wananchi wetu, kero kubwa atakwambia kwamba nimemwona daktari lakini hakuna dawa. Sasa ni lazima tuboreshe hii idara ya famasia, wawepo katika ngazi ya maamuzi ili pia tuweze kutatua kero ya upatikanaji wa dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, fedha hizi nyingi za dawa ambazo tumeziongeza mpaka ngazi ya zahanati, tunazihitaji kwa kweli. Nakubaliana na yeye. Naomba mdogo wangu aridhike kwamba dada yake sijawahi kumwangusha. Nitaifanyia kazi hii hoja, tuweze kurudisha hiyo... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, Kifungu hiki kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaingia kwenye *guillotine*.

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*……..….Sh. 1,882,247,086
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……….……Sh. 2,246,391,500
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 989,716,900
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*.....Sh. 408,104,128
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*…..Sh. 1,276,043,300
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*……………………..Sh. 567,251,800
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………………………Sh. 845,716,500
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*………Sh. 305,940,000
Kifungu 2001 – *Curative Services*……………..………Sh. 514,091,099,648
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*………………Sh. 27,094,582,767

Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division*..............................................Sh. 821,730,000
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*………Sh. 1,321,426,100
Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care Technology Services Unit*…………………….……Sh. 11,800,319,400
Kifungu 3001 – *Preventive Services*…………………Sh. 28,995,899,352
Kifungu 3002 – *Health Quality Assurance Division*…...Sh. 740,816,800
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness Response Unit*……………………………………….Sh. 626,307,300
Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child Health Division*…………………………………….Sh. 1,716,670,500
Kifungu 4002 – *Social Welfare*……………………………………..Sh. 0
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*…Sh. 28,341,043,119

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 52 – Wizara ya Afya**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……..……Sh. 30,390,950,500
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………………………Sh. 205,300,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*…………..………………Sh. 60,000,000
Kifungu 2001 – *Curative Services*…………………..Sh. 150,508,331,211
Kifungu 2003 – *Chief Medical Officer*…………….Sh. 149,950,673,569
Kifungu 2004 – *Nursing and Midwifery Services Division*…………Sh. 0
Kifungu 2005 – *Pharmaceutical Services Unit*…...Sh. 205,088,300,000
Kifungu 2006 – *Diagnostic and Health Care Technology Services Unit*……..…...........………Sh. 1,702,001,816
Kifungu 3001 – *Preventive Services*……………….Sh. 119,556,038,904
Kifungu 3003 – *Health Emergency Preparedness Response Unit*…………………………………….Sh. 1,067,300,000

Kifungu 3004 – *Reproductive, Maternal & Child Health Division*……………………………………Sh. 1,000,000,000
Kifungu 5001 – *Human Resource Development*…Sh. 20,041,350,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshikiwa tukae. Mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Hivyo, naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, kwamba Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Wanaoafiki waseme ndiyo. Wasioafiki waseme siyo. Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bajeti ya Serikali kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hongera sana wewe na Naibu wako na timu yako nzima ya Katibu Mkuu na wataalam wake; madaktari wetu, maprofesa na wauguzi. Kwa kweli wizara yako imebadilika na tunawashukuru sana. Tunawashukuru sana Muhimbili, *JKCI,* Mkapa na maeneo mengine yote. Mabadiliko yapo na tunaona hamasa na michango ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kuileta katika wizara yenu. *(Makofi)*

Kamati ya Siasa Tanga mpo, mmeiona kazi ya Mheshimiwa Waziri wenu. Hebu simameni kidogo kwanza; lakini wajumbe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, Wizara hii sasa Bajeti yake imepitishwa rasmi na Bunge, nendeni mkafanye kazi ya kuokoa maisha ya wananchi. Tunaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna anavyoendelea kuboresha huduma mbalimbali katika Taifa letu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri wa Mifugo anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa anawaalika Waheshimiwa Wabunge wote mtembelee Banda lao la Protein Bungeni, ambapo kuanzia kesho kuna maonesho ambayo yameandaliwa na wizara yake. *(Makofi)*

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.42 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*